Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA SITA - TAREHE 14 JUNI,2010

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 35

### Kupandishwa Hadhi Barabara za Halmashauri ya Hai

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeelemewa sana na wingi wa barabara inazozihudumia na kwa kuwa, barabra za Bomang'ombe-Rundugai-Loliondo-Kikavu Chini hadi *TPC* na ile ya Shirinjoro-Narumu-Lyamungo hadi Makoa zinakidhi vigezo vya kupandishwa daraja na zilishapitishwa kwenye vikao husika kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Mkoani:-

Je, ni lini zoezi la kupandisha hadhi barabara hizo litakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Archt. Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu imepokea maombi mbalimbali ya kupandisha barabara za Wilaya na Mikoa madaraja zikiwemo za Wilaya ya Hai.

Baada ya ya uchambuzi uliofanyika mwaka 2008/2009 Wizara iliorodhesha barabara zilizokidhi vigezo kulingana na sheria mpya ya barabara ya mwaka 2007. Sheria hiyo inaelekeza vigezo vya kupandisha barabara madaraja mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote zilizokidhi vigezo zilipandishwa madaraja na Mikoa yote ilifahamishwa. Maombi yaliyokidhi vigezo kwa mkoa wa Kilimanjaro yalikuwa matatu (3) kati ya maombi ya barabara 18 yaliyokuwa yamewasilishwa.Katika barabara ambazo Mbunge amezitaja hakuna barabara iliyokidhi vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo barabara hizo zilizopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge, zinaendelea kupatiwa fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili ziweze kupitika wakati wote.

Aidha, kwa mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Hai imetenga jumla ya shilingi milioni 136.6 kutoka mfuko wa barabara kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ya kawaida ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuzipandisha hadhi barabara mbalimbali kulingana na umuhimu, vigezo vilivyowekwa na kutegemeana na hali ya kiuchumi ya nchi itakavyoruhusu.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hizi barabara kama anavyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, ni muhimu sana sana kwa ajili ya uchumi katika eneo lile. Kwa upande wa tambarale ndiko mazo mengi yanakolimwa na wale wananchi wa wilaya ya Hai na upande wa milimani ndiko kahawa nyingi inakolimwa ambayo ndiyo inaongezea pato katika uchumi wa nchi yetu.

Kwa hiyo, ningemwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, atashiriki naye kwa sababu anaifahamu vizurijiografia yetu ya wilaya la Hai katika kuishawishi Serikali ili iweze kuitikia kilio changu na ombi langi hili la kuzipandisha hizi barabara daraja ili ziweze kuhudumiwa na Serikali Kuu kwa maana ya *TAN ROADS?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mhehsimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa na ndugu na rafiki yangu Fuya Kimbita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nikiri kwamba hizi barabara anazozizungumzia Mheshimiwa Kimbita, mimi ninazifahamu sana kwa sababu sisi tulikuwa ni sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Kwa hiyo, mara kwa mara tumekuwa tunazizungumzia barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka hapa niseme ukweli kwamba Fuya Kimbita ametumia kipaji chake na nafasi yake yeye kama Archtect kuhakikisha kwamba barabara za Hai zinakuwa nzuri na hivi tunavyozungumza hapa kuna barabara ya Kwa Sadala-

Masama sasa hivi mkandarasi yuko kule kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi ambavyo Mbunge ametumia kipaji chake na kufanyakazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongeze hapo kwamba anayepandisha madaraja hizi barabara amekaa hapa ni Waziri wa Miundombinu ambaye ndiye mwenye dhamana,mimi ameniomba kwamba nitumie nafasi yangu kwa kuielewa wilaya ya Hai niweze kuiomba Serikali na mimi nimo humu basi mimi nitaendelea kuomba na kusaidia ili na hizi barabara nyingine ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama inavyosemwa hapa ni kweli barabara hizi ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, mimi nitafanya hivyo kama alivyoniomba.*(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na pia kwa kumpongeza Mheshimiwa Fuya Kimbita kwa juhudi zake ambazo zinaonekana moja kwa moja, naomba nitoe maelezo ya ziada kwamba, barabara hizi zinapangiwa hadhi kufuatana na Sheria ya Barabara. Kwa hivyo zote zimeanishwa ni vigezo gani ambavyo barabara ikifikiwa inaweza ikapangiwa hadhi fulani. Aidha barabara kuu au barabara ya mkoa ama barabara ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamati Maalum ambayo Serikali imeiunda inayoongozwa na Mwenyekiti wa Mfuko wa Barabara ambayo inatathimini kwa kina barabara zote na kuhakikisha kwamba zinakidhi vile vigezo ambavyo vimewekwa. Sasa zile ambazo hazikupitishwa kama walivyotangaza mwaka jana barabara ambazo zimepanda hadhi ni kwamba, hazikutimiza vigezo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaielekeza Kamati iendelee kuangalia hizi ambazo hazikupitishwa kama walikuwa wamefanya makosa mahali fulani kwenye mchanganuo wao ili ziweze kupangiwa hadhi zinazofaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA.** Nitamuita mmoja tu sasa, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kwa sababu niliishamwita.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, barabara ya Longido-Siha ilikuwa kwenye barabara hizo na katika ushauri Waziri alionipa tumekwishatekeleza.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza sasa kuiweka barabara hiyo ya Longido-Siha katika barabara hizo za kupandishwa hadhi kwa sababu tumetimiza vigezo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile ambazo zimetimiza vigezo Kamati itaniwasilishia hivi karibuni na tutazipandisha hadhi kwa kadri ambavyo itatakiwa. *(Makofi)*

Na. 36

**Ujenzi wa Barabara ya Mbande-Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kujenga barabara ya Mbande hadi Mpwapwa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa, Serikali imekubali kuanza kujenga barabara za Mpwapwa Mjini kwa Kiwango cha lami.

(a) Je, Upembuzi yakinifu wa barabara ya Mbande –Mpwapwa utaanza lini?

(b) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani katika bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami za Mpwapwa Mjini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haijaweza kutenga fedha za kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa, yenye urefu wa kilomita 49.3 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Wakati jitihada za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zinafanyika. Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo yanayostahili barabara hii ili iendelee kupitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami Mpwapwa Mjini kutegemea na uwezo wa Bajeti. Kwa kuwa barabara za Mpwapwa Mjini ni za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwawa ambazo kiutaratibu zinahudumiwa na Bajeti yake inayopitia TAMISEMI; Wizara yangu kutegemea na uwezo wa Bajeti itakuwa tayari kuunga mkono jitihada za Halmashauri ya Mpwapwa katika ujenzi wa barabara zake hizo.

Kwa hivi sasa kutokana na ufinyu wa Bajeti Wizara yangu haijatenga fedha zozote kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa barabara za Mpwapwa Mjini kwa kiwango cha lami.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imefanyakazi nzuri sana ya kujenga daraja la Gulwe baada ya kusombwa na maji wakati wa mafuriko na hivi sasa Serikali

inajenga daraja la Godegode ikishirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Wananchi wa Godegode na wananchi wa wilaya ya Mpwapwa pamoja na *Tanroads.*

(i) Je, sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba pamoja na ufinyu wa Bajeti lakini kwa kuwa upembuzi yakinifu huchukua muda mrefu, iko haja sasa ya kutenga fedha kwa Bajeti ijayo ili upembuzi yakinifu uweze kufanyika kwa ujenzi wa barabara ya lami Mpwapwa hadi Mbade?

(ii) Kwa kuwa Mpwapwa kuna Mamlaka ya Mji Mdogo tunaandaa Mji wa Mpwapwa kuwa Halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, barabara za lami Zinahitajika. Je, kwa Bajeti ijayo Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba iko haja ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Mpwapwa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara hii ya kutoka Mbande-Ng'ambi-Chunyu-Mpwapwa. Kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba Bajeti itakaporuhusu katika mahitaji haya mengi barabara hii tutaipa kipaumbele kwa kwa kuipangia pesa ili angalau upembuzi yakinifu uanze kwa ajili ya kuiandaa barabara hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa hatuna fedha hizo lakini niseme kwamba Bajeti zinazofuatia ikiwezekana ya mwaka huu unaokuja au hiyo inayofuatia tutatenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za Mpwapwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba nirudie tena kwamba, ni barabara za wilaya hivyo, ni jukumu la Halmashauri ya wilaya, lakini tutajitahidi sana pale itakapowezekana kuwaunga mkono wenzetu wa Halmashauri ya Mpwapwa ili waweze kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa utekelezaji wake wa ilani hasa katika shughuli nzima za utengenezaji wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kibaha ni Mji na kwa kuwa Waziri Mkuu alipokuwa Waziri wa TAMISEMI aliahidi kumwona Waziri Mkuu aliyekuweko wakati huo, lakini sasa yeye ndiye Waziri Mkuu kwamba barabara ya kilomita 4 pale Kibaha Mjini ataiwekea Bajeti maalum ili iwe kiwango cha lami wakati Kibaha Mjini ukiacha hiyo barabara kuu hatuna lami.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa kuhusu hizo kilomita nne (4) za Kibaha Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hilo ni swali jipya kabisa, lakini hata hivyo Dr. Kawambwa naomba ujibu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la ziada la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuhakikisha kwamba ndiyo ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa lakini kwa kumheshimu Mheshimiwa Mbunge na bila shaka nasema lile ambalo limeahidiwa nitalifuatilia ili kuhakikisha kwamba kama siyo mwaka ujao wa fedha basi mwaka unaofuatia wa fedha tuweze kutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilitaka tu kumwuliza Mheshimiwa Waziri, barabara ya Uhuru imeishaingizwa katika programu ya Serikali na michoro yake mipya kwa taarifa za wataalam iko tayari.

Je, ni hatua gani sasa Serikali imefikia kukamilisha kuirekebisha barabara hii ambayo ni ya kihistoria katika nchi yetu?

**SPIKA:** Hata hilo ni swali jipya lakini kwa sababu ya uzoefu wa Mheshimiwa Waziri basi jibu tu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile ya Uhuru tumeipandisha hadhi mwaka jana sasa ni barabara ambayo inahudumiwa na *TANROADS* na tayari tumeiweka kwenye mchakato lakini kama nilivyojibu awali tuna tatizo kubwa kwamba, mtandao wetu wa barabara ni mkubwa, barabara zilizopandishwa hadhi mwaka jana peke yake ni zaidi ya kilomita 2000 na katika kilomita unayoijenga ni shilingi bilioni 1 au milioni 1000 kwa hiyo tuna kama Trilioni 2 kwa barabara zote ambazo tumezipandisha hadhi mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ni kubwa lakini changamoto ya Jiji la Dar es Salaam ni kubwa. Barabara ya Uhuru ni barabara ya kihistoria tutaipa umuhimu mkubwa ili tuhakikishe kwamba tunaifanyia kazi mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Na. 37

**Wazee wa Baraza Kutolipwa Posho zao**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kupambana na rushwa kwa nguvu zote; na kwa kuwa bado posho za wazee wa baraza ni ndogo na hazilipwi kwa wakati:-

(a) Je, ni lini wazee wa baraza wataongezewa posho zao?

(b) Je, ni lini tabia ya kuwakopa Wazee wa Baraza itakoma?

(c) Je, kwa kitendo cha kushindwa kuwalipa wazee hao kwa wakati, Serikali haoni kama inajenga na kishawishi cha rushwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na ( c ) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imedhamiria kupambana na rushwa kwa nguvu zote. Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kuwa ukubwa wa mishahara au posho pekee, sio kigezo cha kumzuia mla rushwa mzoefu kuacha kula rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inakusudia kupandisha kiwango cha posho ya Wazee wa Baraza kuanzia mwaka ujao wa fedha. Nitalifafanua zaidi jambo hili katika hotuba yangu ya Bajeti nitakayosoma hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara zote imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha Wazee wa Baraza wanalipwa posho zao kwa wakati kwa kupeleka fedha za posho hizo kwenye Mahakama za wilaya mara zinapopatikana kutoka Hazina. Aidha, nitashukuru sana kama Mheshimiwa Mbunge anaifahamu Mahakama ambayo Wazee wake wa Baraza hawajalipwa posho zao kwa muda mrefu. Nitamwomba atupatie taarifa ya madai hayo, ili utaratibu wa malipo ya wazee hao ufanyike mara moja.

**MHE. ISMAIL J. LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeambiwa nikukumbushe jina langu naitwa Ismail Jussa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ismail Yusuf! *(Kicheko)*

**MHE. ISMAIL J. LADHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jussa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa suala hili la kuchelewa kulipwa Wazee inawezekana ndilo linatokana na kutotekelezwa kwa muda mrefu kwa ahadi ya Serikali ya kuipatia Idara ya Mahakama Bajeti yake ili iweze kuihudumia yenyewe kama inavyofanyika kwa Bunge na kwa sababu hii ya kuipatia Mahakama mfuko ambao utakuwa unajitegemea kutoka Serikalini imekuwa ikitolewa kwa miaka mitano iliyopita hadi kufikia mara ya mwisho kukaririwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe. Namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie lini ahadi hii itatekelezwa ili mahakama zetu kweli ziwe mkono unaojitegemea wa dola kama ilivyo Serikali na Bunge lenyewe?

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ismail Jussa kama ifuatavyo. Suala la Mfuko wa Mahakama Serikali kweli imelikubali, Mheshimiwa Rais alikwishatangaza kukubali kwake kinachohitajika sasa ni utaratibu ambapo itabidi tulete sheria ndani ya Bunge hili kama tulivyoanzisha Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakusudia kufanya hivyo katika Bunge la Mwezi Januari. Labda niongeze tu kuwepo kwa mfuko huu hakuna maana kwamba labda Bajeti itabadilika sana. Bajeti inatokana na Bunge hili hili ila tu wanapata *autonomy* ya kupanga fedha zao wenyewe. Lakini kiwango cha fedha kinatolewa bado na Bunge hili hili na kinategemea uwezo wa Serikali.

Na. 38

**Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe Kukosa Ofisi Zake**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mahakama ya Kisarawe haijapata Ofisi zake yenyewe tangu uhuru na badala yake imeazimwa majengo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya; na kwa kuwa majengo ya Mahakama za Mwanzo wilayani humo yapo katika hali mbaya sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Wilaya majengo ya Mahakama ya Wilaya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati Mahakama hizo hasa zile za Mwanerumango, Chole, Sungwe na Mzenga?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athumani S. Janguo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mahakama ya Wialaya ya Kisarawe haijapata majengo yake yenyewe na bado imeazimwa majengo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Serikali katika mwaka huu wa fedha ina mpango wa kuanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kisarawe.

(b) Serikali ina mpango endelevu wa muda mrefu kwa kukarabati majengo ya Mahakama za Mwanzo kwa awamu kadri Bajeti itakavyoruhusu. Kwa mwaka huu wa fedha mahakama alizozitaja Mbunge hazimo katika mpago huo. Hata hivyo, kwa maoni ya Wizara yangu majengo ya Mahakama za Mwanzo za Mwanerumango na Sungwe yana hali nzuri kidogo ukilinganisha na Mahakama ya Mwanzo Mzenga, ambayo kama fedha zitapatikana itafanyiwa kwanza ukarabati.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri atapokea shukrani za awali kwa ahadi yake kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hizo mbili na kwamba atakubaliana na dua yangu ya kumwomba arudi tena ili ahakikishe kwamba ahadi yake inatimizwa? Swali la pili Mungu apishilie mbali suala la kutokurudi endapo hatarudi atafanya kama nitakavyofanya mimi kumwachia anayemfuatia *handing over notice* kuhakikisha haya yanatekelezwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu kwake kwa dua ambalo ananiombea ili nipate kurudi na naamini wananchi wa Nachingwea nao watafanya kama hivyo tunavyoomba wote. Lakini la pili niseme tu Serikali ni endelevu na wazungu wana msemo wa Serikali *moves on paper*. Kwa hiyo, kama sitarudi na Mungu apishilie mbali kama anavyoomba Mheshimiwa Janguo, basi atakayefuatia atayakuta yapo yataendelea na yeye ataendeleza kadri atakavyoweza.

**NAIBU SPIKA:** Habari ya kuombeana kutokurudi isiwemo humu ndani. (*Kicheko*)

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri Masha alipotembelea Kisiwa cha Ukerewe hivi karibuni katika Kisiwa cha Ukara alisikitika sana kuona hali ya kitu kinachoitwa Mahakama ya Mwanzo na alishangaa sana pamoja na sisi wote kuona kitu hicho hakimu anaweza kukaa humu akahukumu. Je, haoni kwamba hizi habari alizofikishiwa na Waziri Masha zinapaswa kuingizwa haraka katika mkakati wa kujenga mahakama, awamu kwa awamu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri Laurence Masha alipofanya ziada kule Ukara aliona Mahakama ya aina hiyo na akanipigia simu mara moja tukaongea wote pamoja na Mheshimiwa Mongella na wakati ule nimwahidi hivyo hivyo kwamba tutakavyoweza basi katika mwaka huu wa fedha tutaiwekea kipaumbele Mahakama hiyo pamoja na Mahakama ya Bunda. (*Makofi*)

Na. 39

**Nishati Mbadala kwa Matumizi ya Nyumbani**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wananchi wengi bado wanaendelea na tabia ya kukata miti kwa ajili ya kuni na uchomaji mkaa kwa matumizi ya nyumbani:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatafutia wananchi nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Chilolo kwamba kuni na mkaa yaani nishati itokanayo na tungamotaka (*biomass*) ndiyo chanzo kikuu cha nishati majumbani. Hapa Tanzania tungamotaka inachangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati itumikayo kwa matumizi ya majumbani. Sababu za hali hii ni nyingi, na zinafanana kwa nchi nyingi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

Matumizi ya umeme majumbani yanakwazwa na gharama za awali za kuunganisha umeme, kununua majiko ya umeme na vifaa vingine vya umeme ambavyo gharama yake ni kubwa na watu wengi wa mijini na vijijini pale ambapo wanafikiwa na umeme wanashindwa kutumia umeme kwa ajili ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa mpango wa utekelezaji wa kazi zake kila mwaka na katika mpango huu miradi mbalimbali inaainishwa kwa ajili ya utekelezaji. Mfano Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini *(TPDC)* kwa kushikiriana na mwekezaji kutoka nje, imeanzisha mradi wa majaribio ya matumiz ya gesi asili iliyoshindiliwa *(compressed Natural Gas (CNG)* kwenye magari, taasisi mahospitali, mahoteli na majumbani. Kati ya miradi inayoletekelezwa kwa lengo la kuwapatia wananchi nishati mbadala ni pamoja na kuhamasisha wananchi kutumia *biogas* inayoweza kutumika kwa kupikia majumbani pamoja na kuwasha taa.

Aidha, kwa upande mwingine nishati ya umeme itokanayo na mionzi ya jua inaendelezwa nchini kupitia mradi wa Umeme nuru unaofadhiliwa na *UNDP* Mkoani Mwanza na ule unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden chini ya Sida unaotekelezwa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati nyingine kama vile uzalishaji wa vitofali vya tungamotaka (*biomass brequattes*) kwa ajili ya kupikia majumbani. Aidha, Serikali inaendelea kukamilisha utafiti wa *flue gas* zinazotokana na makaa ya mawe ili mkaa huo uweze kutumika kwa ajili ya kupikia majumbani.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba matumizi ya kuni na mkaa kama nishati majumbani yana athari pana sana zinazoonekana moja kwa moja, na zile zisizoonekana moja kwa moja. Athari ya matumizi ya kuni na mkaa ambayo yanaongezeka kila siku kadiri Watanzania wanavyoongezeka ni kwenye mazingira na ushahidi huu ni maeneo ambayo awali yalikuwa ni misitu na sasa ni majangwa, kupungua kwa mvua na viwango vya maji kwenye mabwawa na mito. Kwa hiyo, suala hili ni nyeti na ni mtambuka na Serikali kwa kushirikiana na idara zingine inakamilisha mpango wa matumizi ya nishati mbadala ambayo itaongeza matumizi ya gesi asili majumbani, sambamba na kuhamasisha na kurahisisha matumizi ya nishati mbadala kwa kujenga elimu na ufahamu wa manufaa wananchi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ametoa maelezo mengi sana ya Nishati mbadala ambayo inaweza ikatumika badala ya kuni. Sasa nataka nijue ni kwa kiwango gani Wizara ya Nishati na Madini imeweza kutoa uelewa kwa nishati hii mbadala aliyoielezea kwa wananchi ili wakaweza kuepukana na wakaanza kuondokana taratibu kutumia nishati ya kuni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya nishati mbadala majumbani ni kitu kigeni, ni kitu ambacho kwa nchi nyingi zinazoendelea tunatambua sasa hivi kwamba ni jambo la dharura. Kuna uwekezaji wa makusudi unaotakiwa ufanywe ili nishati mbadala, suala linalogomba siyo suala la ufahamu tu lakini pia suala la uwekezaji wa makusudi kabisa ambao inabidi ufanywe kwa mfano Mkoa wa Dar es Salaam au Jiji la Mwanza au Jiji la Arusha ambalo kwa pamoja Majiji matatu yanatumia kiasi kikubwa sana cha kuni na mkaa ambapo tungeweza kutumia nishati ya mitungi ya gas au kama tulivyosema hapa. Kwa hiyo, suala siyo kama kuna tatizo la ufahamu. Wizara ya Nishati na madini inafanyia kazi suala hilo. Lakini pia naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba hata Wizara ya Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Batilida Burian, wanalifanyia kazi jambo hili. Kwa hiyo, suala siyo ufahamu, suala ni kwamba tunahitaji uwekezaji wa makusudi ambao tunatarajia kuufanya ndani ya Serikali. Lakini pia kwa kushirikisha sekta binafsi ili wananchi wa kawaida wapate matumizi rahisi zaidi ya Nishati mbadala.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kukosekana kwa nishati mbadala kwa muda mrefu kumeendelea kuhatarisha misitu yetu hapa Tanzania, kwa kuwa kiwango cha matumizi ya mkaa kinaongezeka kila siku na kwa kuwa kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema ipo mikakati mikubwa na mipango ya kuhakikisha kwamba tunapata nishati mbadala.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya uliza swali moja tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unajibu swali moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimmiwa Naibu Spika, sijauliza swali.

**NAIBU SPIKA:** Ulikuwa na kwa kuwa nyngi mno zako.

**MHE. MAGLALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa aliyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba yako kwenye vitabu lakini hayako kwenye utekelezaji kwa sababu tunaona matumizi ya mkaa yanaongezeka kila siku hali ambayo ni hatari. Je, Serikali sasa iko tayari kuhakikisha kwamba kwenye bajeti hii ambayo hatujaona mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunawapatia wananchi wetu nishati mbadala iweze kuweka kiwango cha kutosha ili kuhakikisha kwamba mipango hii inatekelezwa ndani ya mwaka huu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda hatukuelewana na Mheshimiwa Sakaya, suala la matumizi ya nishati mbadala

limekuwa linafanyiwa utafiti kwa muda mrefu ili tupate matumizi yanayofaa na ya gharama nafuu na yenye ufanisi wa hali ya juu  majumbani.

Kwa hiyo, Serikali chini ya Wizara ya Nishati na Madini na chini ya Wizara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais nimesema tumekuwa tunalifanyia kazi ili sasa hivi tunalobaki nalo ni kulipatia utekelezaji ndani ya majumbani mwa Watanzania lakini hilo linataka uwekezaji wa  sekta ya umma na sekta binafsi.

**MHE. VEDASTUSI  M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba gharama za mwanzo za kuingiza umeme ndizo zinazosababisha watu wengi wa mijini wanashindwa kuwa na umeme, ningependa kufahamu hivi Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba sasa inapunguza  gharama za mwanzo za uingizaji wa umeme ambayo ni pamoja na kuwaruhusu wananchi waweze kulipa kidogo  kidogo ili wote waweze kuwa na umeme kwa ajili ya kueupuka athari za mazingira?  *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hivi matumizi ya umeme majumbani yanakwazwa na mambo mengi, mojawapo ni hilo la uunganishaji wa umeme. Lakini pia hata matumizi ya vifaa vya umeme vile vifaa vyenyewe kidogo gharama yake ni kubwa  sana.

Lakini gharama za kuunganisha umeme zinalingana na gharama zinazotokana na vifaa na kadhalika. Sasa huwezi kupunguza gharama zile kama vifaa vyenyewe vina gharama kadhaa,  ambavyo vinaifikisha pale.

Tulichosema ambalo tumekuwa tukilisema humu ndani kwa muda mrefu ni kwamba tunazungumza na *TANESCO* ili katika mambo mengi basi yule mtumiaji anapotaka kuunganisha umeme aweze kulipa   kwa  awamu.

Hilo linafanyiwa kazi na matarajio yangu ni kwamba *TANESCO* na Serikali tutakuja na mpango huo hivi karibuni ili kwa maeneo yote watu wanapounganishiwa umeme hili suala la kuunganishiwa umeme tatizo la gharama lisiwe ni tatizo tena.

Na. 40

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Mgandu**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kupeleka umeme Kata ya Mgandu ambayo ina shule tatu za sekondari za Kalekwa, Mitundu na Mgandu,  pamoja na Hospitali ya Mtakatifu  Vincent.

(a)Je, ni lini ujenzi wa miundombinu ya umeme utaanza katika maeneo hayo muhimu?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuchelewesha mradi huo kunaongeza gharama zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni, Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapa Bungeni Julai, 2009 wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, utekelezaji wa mradi umekwishaanza. Shirika la umeme *TANESCO* linakamilisha mkataba na mkandarasi aliyechaguliwa kwa ajili ya ujenzi wa njia za umeme, kampuni ya *Spencon Power LLC*.

Mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Itigi hadi Mgandu lenye urefu wa kilomita 75, ufungaji wa transfoma tatu za kVA50, tatu za kVA100 na mbili za kVA 200 pamoja na ujenzi wa kilomita 13 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4. Inategemewa kuwa ujenzi wa njia za umeme utaanza kabla ya mwisho wa mwezi Julai, 2010. Mradi utakamilika miezi 12 baada ya kuanza utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wowote kila unavyozidi kuchelewa kawaida gharama zake huongezeka. Kuchelewa kuanza kwa ujenzi kumetokana na mchakato wa manunuzi kuwapata wakandarasi hao kuchukua muda mrefu.

Miradi ilikuwa itekelezwe na *TANESCO* yenyewe, hata hivyo, kutokana na *TANESCO* kutokuwa na raslimali za kutosha kutekeleza miradi hiyo kwa wakati mmoja na ikamilike mapema, ilionekana kuwa ni vyema itekelezwe kwa utaratibu wa kuwapata wakandarasi ili kutekeleza miradi hii. Kwa sasa *TANESCO* wanakamilisha mikataba na wakandarasi hawa na baadhi ya wakandarasi wapo kwenye maeneo ya miradi na wamekwishaanza kazi za ujenzi. Hata hivyo, utekelzaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Lwanji, kwa ufuatiliaji wa karibu wa mradi huu, ambao umefanikisha utekelezaji kutoka hatua za awali. Ninamhakikishia kuwa Serikali itatoa taarifa za mara kwa mara za utekelezaji wa miradi ya umeme ili wananchi wafahamu maendeleo na hatua zilizofikiwa. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mradi huu wa kupeleka umeme kutoka Itigi kwenda Mgandu ulikuwa uende sambamba na ule mradi wa kupeleka umeme Kitopeni na kushusha umeme pale Gurungu. Je, ni hatua zipi zimefikiwa kwa miradi hiyo miwili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ambayo tumezungumza tuliyatoa hapa awali tuliwahi kuzungumzia utekelezaji wa miradi hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge na naomba Mheshimiwa

Mbunge tuwasiliane baadaye ili nikupe taarifa ya utekelezaji wa miradi hii iliongezeka ili tujue kwa sasa hivi imefikia hatua gani pamoja na ile miradi ya Mheshimiwa Chiligati ya Manyoni kwenda Kilimatindi. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi linahusu ahadi za kusambaza umeme nchini.

Kwa kuwa muda wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unakaribia mwisho wake na kwa kuwa ahadi nyingi zilizotolewa hususan za kusambaza umeme nchini bado hazijatekelezwa hasa zile za kupeleka umeme katika miji Mikuu ya Kasulu, Kibondo na kuunganisha umeme Mkoa wa Kigoma na Grid ya taifa. Aidha Waziri kwa kutambua kuwa ahadi ni deni. Je, wanadhani deni hili watalipa lini kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Susan Lyimo ufahamu wake wa utekelezaji wa miradi aliokuwa nao ambao umefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi sio kama ule ambao ufahamu ambao tunao sisi wote na wananchi wengine wa Tanzania na pamoja na utekelezaji wa mradi huo wa Kasulu na Kibondo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi huo wa Kasulu na Kibondo ni sehemu ya utekelezaji wa kununua majenereta 17 ambayo yanakwenda kwenye maeneo husika. Utekelezaji wa ahadi hiyo umeshakamilika Kigoma na kesho Mheshimiwa Rais anakwenda kufungua mradi huo wa Kigoma. Hayo ndiyo mambo ya Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ridhaa yako kujibu kile kipande cha pili cha kuunganisha umeme wa *grid* ya Taifa. *Grid* kwa upande wa Kigoma katika masuala ya kiuchumi labda Mheshimiwa Zitto Kabwe angekuwepo angeweza kukusaidia kidogo. Lakini Kigoma kuunganishwa grid inabidi ama tuutoe kule juu Geita ama tuutoe Tabora. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tatizo sio kuunganisha *grid* Kigoma, suala ni kuwapatia Kigoma umeme wa uhakika. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya Kigoma Mjini ni megawati 5 ambazo sasa hivi tunazifikisha megawati nne (4). Tukimaliza na mitambo hii ikiingia kwenye utekelezaji Kigoma watakuwa na megawati kumi (10). Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imetimiza ahadi yake kwa Kigoma na itatimiza ahadi zake maeneo mengine na ndiyo maana wananchi wanaichagua CCM. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona tu nisimame kidogo kuongezea maelezo mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa jambo hili ni kubwa na linagusa Watanzania wa mkoa wa Kigoma ni vizuri tukalipa maelezo sahihi. Kubwa ninachotaka kusema ni kwamba pamoja na Rais anakwenda Kigoma kesho atafanya uzinduzi wa zile jenereta pale Kigoma. Lakini nilitaka vile vile nimwongezee dada yangu kwamba Kibondo na Kasulu ni sehemu vile vile ya utekelezaji wa hiyo miradi. Mkandarasi tayari

yuko pale Kibondo anajenga kile kitako kwa ajili ya jenereta akimaliza pale anakwenda Kasulu anafanya kazi hiyo hiyo. Mkandarasi huyo pia atafanya kazi pale Sumbawanga kwa ajili ya kujenga kitako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hasa ni nini wakati mwingine tunafikiri Bunge hili ndio mwisho wa jukumu la Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa maana ya utekelezaji wa Ilani. Hatujafika mwisho, Bajeti hii ndiyo itatupeleka mwaka wetu wa tano (5). Kwa hiyo, hata kama leo unaona hakuna kinachoendelea Bajeti hii ndiyo inatupeleka tukamilishe baadhi ya miradi ambayo tulikuwa nayo tayari. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya tunaendelea, maana swali moja linafanya watu wajieleze zaidi.

Na. 41

**Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI**

**MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. EMMANUEL J. LUHAHULA)** aliuliza:-

Wakati maambukizi ya virusi vya UKIMWI Wilayani Bukombe yanakadiriwa kuwa 16% kipo kituo kimoja tu cha kupimia maambukizi hayo, wakati Wilaya inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 500,000 kwa ongezeko la asilimia 7.5 (7.5%) kwa mwaka.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha vituo vingine vya kupimia virusi vya UKIMWI katika maeneo ya Masumbwe, Mhongwe, Lulembela (Ikunguigazi) na Uyovu kutokana na wingi wa watu katika maeneo hayo?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje waathirika wanaotumia dawa za kurefusha maisha *ARVs* Wilayani Bukombe, ambao maisha yao ni duni sana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri aliyokuwa amemjibu Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba idadi ya Watanzania inaongezeka kwa wastani wa asilimia 2.9 kwa mwaka.

Ongezeko alilotaja Mheshimiwa Mbunge la 7.5% kwa watu wa Wilaya ya Bukombe ni kubwa sana na Wizara haina taarifa nalo. Serikali itashukuru kama

Mheshimiwa Mbunge atatueleza chanzo cha takwimu hizi ili Wizara iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya awali naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kupanua huduma ya upimaji wa *VVU* kwa kutumia mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na upimaji wa hiari, upimaji kwa watumiaji huduma za afya (*Provider Initiated Counselling and Testing (PICT)*) na vile vile upimaji wa nyumba kwa nyumba (*home based counselling and testing (HBCT*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Bukombe vipo vituo 19 vya ushauri nasaha na upimaji wa Virusi vya UKIMWI. Vituo hivyo ni Hospitali moja ya Wilaya, Vituo vinne (4) vya afya vya Uyovu, Masumbwe, Iboru na Ushirombo. Pia kuna zahanati 14 za Iponya, Ikuzi, Lugunga, Ilolangulu, Bugando, Bwelwa, Bukombe, Lubelo, Nyasato, Ushirika, Iyogelo, Bukandwe, Ikunguigazi na Nyahologo. Pia zinatoa huduma hizo hapo juu.

Aidha, Wizara itaendelea kuongeza vituo hivyo kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi. Sambamba na hilo, Serikali imetoa mafunzo ya ushauri nasaha kwa watoa huduma za afya 226 katika Wilaya ya Bukombe.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kupitia vituo vyake vya kutolea huduma, inaendelea kuwapatia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, *(ARVs)* wagonjwa wote wanaostahili kupata dawa hizo nchi nzima ikiwa ni pamoja na wale wa Wilaya ya Bukombe. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2010, wagonjwa 654,982 walikuwa wameandikishwa na kupata huduma katika vituo 909 vinavyotoa huduma za UKIMWI nchini kote.

Kati ya hao, wagonjwa 337,854 walikuwa wameanzishiwa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI ambapo wagonjwa 4,375 wanatoka Wilaya ya Bukombe (wanaume 1,765, wanawake 2,366 na watoto 244).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itaendelea na mpango maalum wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula vinavyopatikana nchini kwa ajili lishe kwa wale wanaoishi na *VVU.* Pia itafanya utaratibu wa kubadilisha aina hii ya hitaji kutoka kundi la chakula kuwa kundi la dawa ili zipatikane kwa bei nafuu sehemu zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kuwa Waheshimiwa Wabunge wasaidie kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujikinga na maambukizi ya UKIMWI katika kutekeleza dhana ya kinga ni bora na yenye gharama nafuu kuliko tiba.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika Wilaya ya Bukombe yanalingana na ya Wilaya ya Kahama kwa sababu Wilaya hizi mbili ni majirani. Na kwa kuwa idadi ya watu wa Wilaya ya Kahama inakaribia laki tisa wakati huo huo hospitali ya Wilaya ya Kahama ina upungufu mkubwa wa vifaa, watumishi na hata madawa ya kurefusha maisha kwa waathirika. Je, Serikali itaisaidia vipi Hospitali ya Wilaya ya Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kahama kuwa na upungufu wa madawa, vifaa na watumishi. Suala la vifaa na watumishi kama tunapokuwa tunazungumzia hapa wanakuwa wanapelekwa kadri tunavyowatoa katika soko. Kwa hilo bado tunaendelea nalo ili tuweze kuhakikisha kwamba watumishi wanapatikana.

Kuhusu madawa kama anamaanisha *ARVs* utaratibu ni kwamba kila hospitali kulingana na idadi ya waathirika walioko pale wenyewe ndio wanaagiza dawa kutoka *MSD.* Hivyo kama kuna upungufu sisi kama Wizara hatujapata lalamiko la kuona kwamba kuna upungufu wa dawa ambazo katika Hospitali ya Kahama inapatikana.

Lakini ushauri ni kwamba wale wenyewe wa kutoka Hospitali ya Kahama wapeleke idadi ya wagonjwa ambao wanawahudumia na hizi dawa *MSD* zipo. Kwa hiyo, wapeleke idadi sahihi kulingana na mahitaji yao na dawa zitapatikana. Hakuna sababu ya kukosekana dawa za *ARVs* kwa wale ambao wanazihitaji kwa sababu dawa zipo na zinatosheleza.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema anatuomba Wabunge tusaidie kuhamasisha majumbani kwetu kuzuia maambukizi ya UKIMWI na kwa kuwa kutokana na mila, silka na tabia na hata dini ya baadhi ya majimbo ni vigumu Wabunge kwenda hadharani mkawaambia wananchi muvae *condom*. Na kuwa kuna asasi ambazo zinafanya kazi hiyo kwa niaba ya Wabunge ambazo zinajitahidi sana, lakini asasi hizo haziangaliwi vizuri. Na kwa kuwa kuna fedha nyingi *TACAIDS* na kule Zanzibar *AIDS Committee*.

Je, Waziri atasaidia nini kwamba zile asasi ambazo zinasaidia kuhamasisha mitaani maambukizi ya UKIMWI yasiendelee zaidi zitaweza kusaidiwa ili nao ziweze kufanya kazi ambapo hivi sasa zimekaa tu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Nakubali kabisa kwamba kuna mila na desturi ambazo wakati mwingine zinatuzuia sisi kama wawakilishi, lakini kwa kweli sisi ni jukumu letu na sisi kama wawakilishi katika kutoa elimu tunayopewa na sisi pia tuchukue nafasi kubwa ili hata zile mila na desturi hazituruhusu basi tuweze tukaona ni jinsi gani ambavyo tutaifikia jamii. Lakini ni wajibu wetu kwa

hiyo sisi kama Waheshimiwa Wabunge tusiogope hatutanyimwa kura kwa sababu ya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asasi ambazo sio za Kiserikali. *TACAIDS* kwa kushirikiana na Wizara ya Afya huwa inatoa fedha ambazo zinasaidia hizi taasisi ili ziweze kutoa huduma hizo nyingine ambazo zinashindikana. Kinachotakiwa hapa ni zile taasisi zenyewe ziende zikajiorodheshe katika maeneo husika kama ni Halmashauri au katika Wilaya husika halafu fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zile kwa kutambua zile asasi zilizokuwepo pale ndio wanapatiwa hizi fedha.

Kwa hiyo, utaratibu huu upo na umekuwa ukiendelea. Ningemshauri Mheshimiwa Mbunge kama una asasi ambazo unaziona ziko kule nyumbani kwako ambazo pengine hazisaidii basi zifuate utaratibu huu. Mimi ninaamini kabisa kwa kushirikiana na Serikali na *TACAIDS* pamoja na *AIDS Committee* naamini tunaweza tukawasaidia.

Na. 42

**Madhara ya Dawa za Malaria kwa Wagonjwa**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Tanzania bila Malaria inawezekana, lakini dozi ya dawa za matibabu yake huwaletea madhara baadhi ya wagonjwa na kuwafanya kuacha kwenda hospitali kupata matibabu.

Je, Serikali inaondoaje hofu hiyo kwa wagonjwa wa Malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tanzania bila Malaria inawezekana. Wizara ya Afya ilifanya mabadiliko ya Sera ya Tiba ya Malaria hapa nchini mwaka 2006 kutoka dawa ya *SP* kama dawa ya safu ya kwanza na badala yake dawa ya *ALU* (Mseto) ikaidhinishwa kutumika kama dawa ya safu ya kwanza kwa tiba ya Malaria isiyo kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kusitisha matumizi ya dawa ya *SP* uliotokana na matokeo ya utafiti kubainisha kuwa vimelea vya Malaria vilipata usugu dhidi ya dawa ya *SP*. Wizara inapoanzisha matibabu mapya inaifuatilia dawa hiyo kwa

karibu kuhusu uwezo wake wa kutibu lakini vile vile kama inaleta madhara yoyote. Ndivyo inavyofanyika kwa dawa za *ALU*.

Fomu zimesambazwa vituo vyote vinavyotoa dawa hizi na Waganga wanaelekezwa kujaza dalili zozote wanazopata wagonjwa; fomu hizi zenye rangi ya njano na ambazo zimewekwa stempu tayari hutumwa *TFDA* kwa uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Dawa ya mseto *(ALU)* ni salama na haina madhara. Dawa hii ilifanyiwa utafiti wa kutosha hapa nchini na kuratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* katika vituo vyetu vya kutathmini ubora wa dawa (*sentinel sites)* ambavyo ni:-

Mkuzi (Muheza), Ujiji (Kigoma). Nagaga (Masasi), Chamwino (Dodoma), Ipinda (Kyela); Mlandizi (Kibaha), Butimba (Mwanza) na Mlimba (Kilombero).

Utafiti ulihusisha makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo watoto chini ya umri wa miaka mitano na hakuna madhara yoyote yaliyobainishwa. Vile vile tangu kuanza kutumika kwa dawa ya *ALU*, Desemba, 2006 hatujapata taarifa yoyote toka vituo vya huduma ya afya kuonyesha madhara yaliyotokana na dawa hii ya mseto.

Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vipindi vya afya katika luninga, radio, magazeti, vijarida na mikutano ya kitaalam kuhusiana na matumizi sahihi ya dawa ya mseto ili kuwaondolea hofu watumiaji.

Aidha, ningependa kutoa rai kwa Bunge lako Tukufu kwamba tuendelee kuwaelimisha wananchi kuwahi mapema kwenda kwenye vituo vya kutolea tiba, pindi wanapojihisi dalili za ugonjwa wa Malaria.

Aidha, tuwahimize kutumia dawa hizi kwa usahihi na kumaliza tiba kama inavyoshauriwa na wataalam. Pia watoe taarifa katika vituo vyetu wanapopatwa na madhara wakiwa katika tiba ya Malaria ili uchunguzi zaidi uweze kufanyika kubainisha sababu za madhara hayo.

Na. 43

**Mafao ya Wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Shamba la Mpira ya Kihuhwi limekabidhiwa Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* likiwa na wafanyakazi ambao hawakuwa wamelipwa mafao yao:-

Je, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na *NDC* imekabidhiwa pia jukumu la kulipa mafao ya wafanyakazi wa shamba hilo, na itasaidia vipi kuharakisha malipo ya mafao ya wafanyakazi hao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya mpira ya Kihuhwi, lililoko Muheza na Kalunga lililoko Kilombero yalikuwa yanamilikiwa na Kiwanda cha *General Tyre* tangu yaanzishwe mwaka 1978 hadi yaliporudishwa Serikalini mwaka 1994 baada ya Kiwanda cha *General Tyre* kuona kuwa ulimaji wa mpira sio shughuli ya msingi kwao.

Wakati mashamba hayo yanarejeshwa Serikalini na *General Tyre* mafao yote ya wafanyakazi yalilipwa na wafanyakazi wote wakaachishwa kazi. Kuanzia mwaka 1996 hadi 2005 mashamba haya yalikuwa yanakodishwa kwa Makampuni binafsi ili wayaendeshe na ni Makampuni hayo ndiyo yaliajiri wafanyakazi kulingana na mahitaji yao.

Kati ya mwaka 1996 na mwaka 2000 mashamba hayo yalikuwa yamekodishwa kwa Kampuni ya *Merchantile Freighters Ltd.* ya Kenya.

Aidha, kuanzia mwanzoni mwa Januari 2001 hadi mwaka 2005 mashamba hayo yalikodishwa kwa Kampuni ya *Muhsin Jumaan El-Ardhi* ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni yote mawili hayakuwalipa wafanyakazi mishahara wala mafao yao ipasavyo. Kutokana na hali hii wafanyakazi walifungua kesi Mahakamani wakiwashtaki waajiri wao ambao ni Makampuni hayo katika vipindi tofauti na kushinda kesi.

Hata hivyo hawakulipwa kwa vile waajiri hao walikwishaondoka nchini na hakuna mali walizoacha. Kwa kipindi ambacho mashamba hayo yamekuwa chini ya Serikali au Shirika la Umma mishahara na mafao yalikuwa yanalipwa kulingana na makubaliano kati ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu na *NDC* hadi sasa havijakabidhiwa jukumu la kulipa mafao hayo. Badala yake Wizara yangu inafanya jitihada za kuwasaidia wafanyakazi hawa kupata haki zao kutoka kwa waliokuwa waajiri wao, kwa kuwasiliana kwanza na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili ifanye mawasiliano na Serikali za nchi waliko hawa wawekezaji ili Serikali hizo ziwashinikize kulipa.

Pili, tumefanya mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili taratibu za kidiplomasia zikishindikana tuitumie taasisi ya *Interpol* kuwaleta wawekezaji hawa mbele ya vyombo vya sheria vya Kimataifa na hukumu iliyopitishwa itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Eng. Herbert Mntangi, kwa jinsi alivyolishughulikia tatizo hili kwa jitihada kubwa na kwa kipindi kirefu kidogo. Ni matumaini yangu kuwa ataendelea kushirikiana nasi hadi wananchi hao wapate haki yao. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, ya kina na vilevile kwa jinsi ambavyo amefanya jitihada ya kuzishirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuweza kuwapata hao ambao wanadaiwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu na wajibu wa Serikali ni kulinda haki za wananchi pamoja na mali zao. Kwa msingi huo, ningeomba nimwombe Mheshimiwa Waziri afanye jitihada kwa niaba ya Serikali; na je, kama hili litashindikana ataweza kuishawishi Serikali iweze kuchukua jukumu lake hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo la mashamba, kulikuwepo pia na shamba lingine *Kihuwi Sisal Estate* na kuna mgogoro kati ya mipaka ya mashamba hayo mawili dhidi ya wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, wameanza kushughulikia tatizo hilo. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuishirikisha NDC ili nayo ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuondoa tatizo hilo la migogoro ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mntangi kwamba, Wizara yangu imejitahidi kadiri ya uwezo wake, kushirikiana na yeye kuhakikisha kwamba, wananchi hawa wanapata haki yao. Sasa endapo hawa walipaji ambao wanapaswa kulipa hawataweza kufanya hivyo kwa namna yoyote ile, taratibu za Serikali kuchukua jukumu la kuwalipa hao wafanyakazi haziwezi kufanyika bila kupitia hatua mbalimbali; mojawapo ni kuja hapa katika Bunge letu Tukufu na kuomba Bunge liidhinishe fedha za kuwalipa hao ambao wamefanya hivyo. Kwa hiyo ni suala la muda mrefu, lakini nimhakikishie kuwa, tutafanya naye kazi na nina imani kwamba, endapo Wizara hizi mbili zitashirikiana na sisi na yeye mwenyewe, hatutafika kote huko hadi kuleta hapa Bungeni wananchi watapata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda nimkahikikishie kwamba tutaiagiza NDC itoe ushirikiano huo kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaishi kwa amani. Kwanza aman kati yao wenyewe lakini kati ya wananchi wenyewe na wawekezaji wetu kama wa shamba hilo ambalo amesema Mheshimiwa Mntangi.

Na. 44

## Mkoa wa Kigoma Kukabiliana na Changamoto za Biashara ya Kimataifa

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI (K.n.y. MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma unapakana na Nchi za Congo (DRC), Burundi, Zambia na Rwanda kibiashara Kigoma ni mithili ya Dubai katika nchi zetu zote za Maziwa Makubwa:-

(a) Je, Serikali ya Awamu wa Nne ina mkakati gani wa kuusaidia Mkoa wa Kigoma kukabiliana na changamoto za kibiashara ya kimataifa *(boarder trade/transit trade)?*

(b) Chama cha Wafanyabiashara Wilaya ya Kasulu kiliomba Serikali iwasaidie kutoa mafunzo ya biashara za kimataifa, ikiwemo utambuzi wa fursa za biashara na mambo ya forodha; je, kwa nini Serikali imekaa kimya juu ya ombi hilo?

(c) Je, kipo chombo katika Wizara chenye jukumu la kutoa mafunzo hayo; kama kipo kimefanya nini kwa Mkoa wa Kigoma na kama hakipo kwa nini Serikali isifikirie kuanzisha chombo hicho muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mkoa wa Kigoma umepakana na Nchi za Rwanda, Burundi, DRC na Zambia na hutoa huduma mbalimbali za kibiashara kwa nchi hizo. Ili kukabiliana na changamoto za kibiashara ya kimataifa zikiwemo za kibiashara mpakani, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mpango wa miaka minne unaoitwa *Lake Tanganyika Intergrated Development Programme.* Katika Mpango huu, kuna Mradi wa Kuendeleza Uvuvi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Tanganyika, ulioanza kutekelezwa mwaka 2005. Katika Mpango huu, Dola za Kimarekani milioni 7.4 zinatumika katika kuboresha shughuli za uvuvi. Shughuli hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya sehemu ya kukaushia samaki, kujenga masoko matatu ya kisasa vijijini, kujenga vyumba kumi vya baridi na vyumba vingine kumi kwa ajili kutayarishia samaki. Aidha, kiasi kingine cha fedha kitatumika kukarabati barabara katika maeneo ya Mradi. Mpango huu unafadhiliwa na ADP, UNDP DANIDA na FAO, kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, kwa lengo la kuboresha na kuhalalisha Biashara baina ya Tanzania na nchi za jirani. Mpango huu utakuwa ni chachu ya maendeleo katika Mkoa wa Kigoma na utawavutia wawekezaji kuwekeza katika Mkoa huu na kuufanya Mkoa kuchukua nafasi yake katika biashara ya kimataifa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi la wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu la kupatiwa mafunzo ya biashara za kimataifa na utambuzi wa fursa za masoko Wizara yangu iliandaa Semina mwezi Machi na Aprili mwaka 2008 zilizoendeshwa katika Kanda nane za Tanzania Bara pamoja na Zanzibar kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu fursa za masoko zinazopatikana katika nchi mbalimbali. Washiriki wa semina hizo walikuwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Watumishi wa Serikali, Wafanyabiashara, wenye viwanda na asasi zisizo za Serikali. Semina kwa Mikoa ya Ukanda ya Ziwa ilifanyika katika Mkoa wa Dodoma Tarehe 9, April 2008 ambapo jumla kwa washiriki kumi kutoka Mkoa wa Kigoma walihudhuria semina hiyo. Barua kutoka kwa chama cha Wafanyabiashara kutoka Kasulu kuomba kupewa mafunzo ya biashara ya kimataifa bado haijatufikia. Hata hivyo Wizara itawasiliana na uongozi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu ili kuandaa utaratibu wa kwenda kutoa mafunzo hayo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Wizara una Idara zinazoshughulikia utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu fursa za masoko mbalimbali yanayopatikana ndani na nje ya nchi. Idara hizo ni Mtengamani wa Biashara na ile ya Uhamasishaji wa Biashara na Masoko. Aidha, Wizara ina kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano, ambacho husambaza taarifa hizo kupitia njia mbalimbali za TEKNOHAMA ikiwemo tovuti ya Wizara. Idara na Kitengo hicho, ndizo zinazoandaa na kutoa mafunzo ya utambuzi wa fursa za masoko yaliyotolewa tarehe 9 Aprili, 2008 katika Kanda ya Dodoma.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI**: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kigoma ni Mkoa ambao uko pembezoni kama Mkoa wa Kagera; kwa sababu sasa hivi tunazungumzia masuala ya kibiashara ya kimataifa; Wizara ina mpango gani wa kutenga maeneo katika Mikoa ya Kigoma na Kagera ambayo inaweza kuwa kama *Bonded Warehouse* ama *EPZ* au *SEZ* kusudi nchi hizi ziweze kupata masoko ya sehemu za Magharibi kama DRC, Rwanda na Uganda?

(ii) Kama nilivyosema Mkoa wa Kigoma ni kama Mkoa wa Kagera; tuna maeneo ambayo yako mpakani na nchi hizi kama Mtukula kwa upande wa Nkenge kwa Mheshimiwa Kamala na Kata ya Rubafu katika Jimbo la Bukoba Vijijini ambapo sasa hivi kunajengwa Kivuko cha kuunganisha Tanzania na Uganda: Je, kuna mpango gani wa kufikisha umeme kwenye maeneo haya kusudi tuweze kunufaika na biashara ambayo inapatikana nchi za jirani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, changamoto ambazo Mkoa wa Kigoma unazikabili ni sawa na zile za Mkoa wa Kagera na kwa hiyo, umuhimu ambao tunauweka kwa Mkoa wa Kigoma vilevile tunauweka kwa Mkoa wa Kagera. Kuhusu maeneo maalum ambayo anayazungumzia hapa ya *SEZ* na *EPZ*, napenda nimhakikishie kwamba, Wizara yetu kwa kupitia Mamlaka ya Kuhimiza Mauzo Nje,

tumetenga maeneo 14 katika nchi nzima ya Tanzania na eneo mojawapo lipo katika Mkoa wa Kagera.

Endapo atahitaji takwimu zaidi tutampatia ili aweze kufahamu eneo lipi ambalo tumelitenga, changamoto tuliyonayo sasa hivi ni kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza maeneo hayo yote katika Nchi ya Tanzania lakini la Kagera lipo. Kuhusu la umeme, napenda nimwambie Mheshimiwa Karamagi kwamba, tunaona umuhimu wa kuwa na umeme katika maeneo hayo na Serikali imesikia, tutaliwasilisha katika Wizara husika kuhakikisha kwamba, tunapofungua hicho kivuko basi kunakuwa na umeme ili mambo yote yaende sawa sawa kwa pande zote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda tumezidisha. Kwanza kabisa, naomba nijibu barua zilizoletwa kwangu kuhusiana na *Order Paper* ya leo. Kwamba, *Order Paper* ya leo imeelekea upande mmoja tu. Mheshimiwa Spika siku moja alijibu kwamba, aliagiza Ofisi yake ijaribu kuangalia kuhakikisha kwamba maswali yanakuwa *balanced* kwa upande Chama Tawala na Vyama vya Upinzani. Sasa jibu ni lile lile na nitakachokwenda kufanya mimi sasa ni kuangalia isije ikawa kuna *technical problem* katika Ofisi, lakini majibu ya Mheshimiwa Spika ni yale yale.

Napenda kutangaza wageni tulionao hapa. Wapo wageni wa Mheshimiwa Mussa Zungu, ambao ni Ndugu Twaha Mapeni na Ndugu Abdallah Agosi, karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambao ni Ndugu Lauti Mwambalaswa, mwanafunzi wa mwaka wa pili kutoka Taylors University Malaysia; na mwanafunzi wa Kidato cha Sita Marian Secondary School Bagamoyo, yeye ni Isabella Mwambalaswa; watoto wake hao. Tunashukuru, someni kwa bidii.

Halafu tuna wanafunzi 60 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi ya St. Teresa of Lisieuy English Medium iliyopo Temeke. Wote wasimame; karibuni sana na nadhani mtajifunza mambo yaliyoko hapa.

Nina wageni wa Mheshimiwa Monica Mbega, hao ni wanafunzi 12 kutoka Shule ya Iringa International wakiambatana na walimu wao ambao ni Kristeen Chachage, Mwalimu Mkuu, Ndugu Adam Niederpruem, Mwalimu, Ndugu Gilian Hoops, Mjumbe wa Bodi ya Shule. Tunashukuru sana mmetoka Iringa kuja kuangalia shughuli za Bunge; karibuni sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ambaye ni Ndugu Upendo Asely; ni msichana yatima na mkuu wa familia ya watoto wanne. Yaani ni mtoto ambaye amepewa madaraka ya kuwalea watoto wengine nadhani. Yuko wapi Upendo? Pole sana na nafikiri Mbunge atakusaidia.

Nina wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha St. John; wasimame walipo. Ahsanteni sana wenyeji wetu, mkazane kusoma na karibuni sana.

Orodha ya wageni imekwisha. Tuna matangazo ya shughuli za kazi kwa Kamati mbalimbali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika Ukumbi Namba 227, Jengo la Utawala.

Kwa niaba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwamba, kutakuwa na Kikao mara baada ya kuahirishwa Bunge leo mchana katika Chumba Namba 219, Jengo la Utawala.

Katibu shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2009 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011

*(Majadiliano yanaendeleo)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza Siku ya Jumamosi nilipoahirisha Kikao kwamba, kutakuwa na wachangiaji wane; kutakuwepo na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Cynthia Ngoye na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Baada ya hapo, nitataja Mawaziri ambao watajaribu kupitia hoja zao nao watakuwa ni Waziri wa Viwanda, Biashara, Ushirika na Masoko, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hoja ya Bajeti ya Mwaka 2010/2011. Awali ya yote, niseme kwanza siungi mkono hoja hiyo, kwa sababu ukiangalia Bajeti ya mwaka huu kwa kweli haijawatendea haki wananchi hasa ukiangalia gharama za maisha zinaendelea kuwa kubwa, pamoja na sehemu ya uongezwaji wa bei ya leseni wa magari hasa magari makubwa yenye CC 2500 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, magari haya kimsingi yanawachukua walala hoi (wananchi wa kawaida), ambao kwa vyovyote vile kama leseni zitakuwa zimepanda, ina maana wananchi hawa itabidi waongeze gharama za nauli, pamoja na suala zima tunalojua kwamba mafuta yamepanda. Niseme tu kwamba, tusiangalie sana tarakimu, tuangalie vilevile mfumko wa bei. Pamoja na kwamba, Bajeti ya mwaka huu imeongezeka kwa takriban shilingi trilioni mbili ukilinganisha na ile ya mwaka kutoka

trilioni tisa hadi trilioni 11, bado tukiangalia anguko la thamani ya fedha ya Tanzania ni kubwa sana. Nyongeza hii ni kama asilimia 17, lakini tukiangalia mporomoko wa Shilingi ya Tanzania ni kama asilimia 20. Kwa maana hiyo, tarakimu hizo bado hazajikidhi matakwa ya wananchi. Kimsingi na hata ukiangalia maoni ya wananchi wengi wa kawaida, wanaona kwamba, Bajeti ya mwaka huu haina mvuto wala hamsaidii Mtanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kwamba, Watanzania zaidi ya asilimia 80 ni wakulima; pamoja na uwepo wa suala zima la Kilimo Kwanza na suala zima pia la kuleta Mapinduzi ya Kijani *(Green Revolution),* bado tunaona kwamba fedha zilizotengwa katika Bajeti ya Kilimo ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji maalum ya wakulima. Pembejeo za kilimo tunajua kwamba, bei zake zitapanda kutokana na mfumko wa bei.

Tuangalie pia suala zima la vijana. Tukiangalia katika Bajeti hii, vijana bado hawajathaminiwa kabisa. Sote tunajua kwamba, vijana wa nchi hii ni wengi sana na hawajatengewa bajeti ya kutosha. Vilevile tunajua ni jinsi gani vijana wengi wanavyokimbia vijijini kuja mijini kwa sababu hawajaboreshewa maisha yao kule vijijini. Kwa maana hiyo, kama Bajeti hii haitawajali vijana hawa, tunaamini kabisa kwamba, baadae wataleta matatizo au maafa makubwa sana hapa nchini. Tukiangalia suala zima la watoto, sasa hivi ukipita katika miji yote siyo tu miji mikubwa kama Dar es salaam hata ukienda Mwanza, Arusha au Moshi, utakuta makundi ya watoto wadogo wanakuja mijini kwa kasi na wanakuwa na kazi kubwa, gari linapokuwa linatembea unaona wanakuja wanaosha vioo; hili kwa kweli ni tatizo sana. Tunaomba Wizara inayohusika na kwa vyoyote vile ni Wizara, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na miaka yote tunaona kwamba Wizara hii inapewa bajeti ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kwamba, Wizara hii itaboreshewa bajeti yake ili iweze kutimiza mahitaji ya watoto wanaokuja mijini. Sote tunatambua kwamba, watoto hawa ni Taifa la kesho, lakini watoto hawa hawajapatiwa mahitaji yao muhimu kama vile malazi, chakula na mavazi. Hili ni tatizo kubwa sana na mimi ninaamini tusipowashughulikia watoto hawa, baadae tutakuja kujenga Taifa la vijana makomandoo, ambao watakuja kuipindua Serikali. Tumeona katika nchi jirani, jinsi ambavyo kumekuwa na vijana ambao wamekosa ajira na watoto ambao wamelelewa katika mazingira hayo wanakuja kuwa ni watoto ambao hawana maadili na tunaamini kabisa Tanzania ni nchi ambayo inapenda kujenga maadili. Kwa hiyo, tunapenda bajeti hii iwajali watoto ili baadae tuwe na Taifa la watoto wenye nidhamu na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala zima la ukubwa wa Serikali; nakumbuka toka mwaka 2006, bajeti ya mwanzo kabisa upande wa Upinzani, tuliongelea suala la kupunguza ukubwa wa Serikali. Sote tunatambua kwamba, nchi yetu ni maskini. Nchi maskini lakini iliyokaa katika utajiri mkubwa wa rasilimali pamoja na maliasili ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Kinachoshangaza; ni nchi ambayo imekuwa maskini sana. Baba wa Taifa alituambia ili tuendelee tunahitaji mambo makubwa manne; Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni watu tunao wengi na wanaendelea kuwa wengi wakati Baba wa Taifa akisema tulikuwa na watu wachache, sasa hivi tuna watu zaidi ya milioni 40 lakini bado tunakuwa na maskini. Ardhi tunayo na ni kubwa kuliko nchi zingine zote Afrika ya Mashariki ukiziunganisha lakini bado ni maskini. La tatu, aliongelea siasa safi na la nne uongozi bora. Mimi ninaamini kabisa kwamba, bado tuna tatizo kubwa la uongozi bora ambalo ndilo linatupeleka katika suala zima la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja umaskini wa Tanzania, lakini Serikali tuliyonayo ni kubwa sana. Tuna Baraza la Mawaziri kama 27, lakini nchi kama Marekani, ambayo ni kubwa sana, tajiri, Baraza lao la Mawaziri ni 15 tu; kwa nini hatuwezi kusoma kutoka kwao? Nchi kama ya Uingereza ambayo tumerithi mambo mengi kutoka kwao kiutawala, Baraza lao la Mawaziri ni 21 tu; kwa nini Tanzania tunakuwa na Baraza kubwa la Mawaziri ambapo mimi ninaamini kabisa Baraza hili limekuwa likiigharimu sana Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali wenzetu waone umuhimu huo na kuweza kupunguza Bajeti ya Serikali ili wananchi wa kawaida waweze walau kufaidi. Ukiangalia hata katika hali ya uchumi, Watanzania bado wanaendelea kuwa maskini pamoja na ahadi nyingi za Chama cha Mapinduzi kutoka kwenye Ilani yao kwamba, Maisha Bora kwa Kila Mtanzania lakini kwa kweli maisha bora hayo hatuyaoni na siyo kwamba tunasema kama Wapinzani, tunasema kama Wananchi na mimi ninaamini hata wenzangu wa CCM wanayaona machungu ya maisha ya Mtanzania. Tunaomba mlione hilo mtusaidie ili tuweze kuipeleka nchi hii pale ambapo inastahili. Mimi ninaamini kabisa uwezo huo tunao na tunaweza kabisa kuibadilisha nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee la mwisho ambalo ni suala zima la elimu. Inashangaza na inasikitisha sana kuona kwamba, pamoja na elimu kupewa kipaumbele mwaka jana hata mwaka huu iko ndani ya vipaumbele vya Serikali, lakini bado walimu ambao ndiyo kipaumbele katika elimu, ndiyo wadau wakubwa katika elimu, wameachwa solemba. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba, pamoja na wakuu wa nchi hii au Serikali kuwa na magari mengi, lakini bado mwalimu wa kawaida akitaka kuhamishwa inabidi wanafunzi ndiyo wambebee mizigo; inakuwa kama tunarudi katika enzi za utumwa! Mimi nimeona mwenyewe watoto wanamhamisha kwa kumbebea mwalimu vitu kichwani; kwa kweli hii inasikitisha.

**NAIBU SPIKA:** Walimbebea mpaka wapi?

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanambebea kutoka shule moja mpaka karibu na shule nyingine, halafu wale wa shule nyingine wanavifikisha anakokwenda. Suala hili linatia aibu sana. Siyo hilo tu, juzi kwenye gazeti nimeona Morogoro Vijijini, mwalimu mkuu wa shule moja ya sekondari yuko peke yake, anafundisha kidato cha kwanza mpaka cha nne. Kibaya zaidi, kutokana na kuwa peke yake inabidi watoto wale wasiende likizo; sasa mimi sijui huu ni utaratibu wa wapi kwa sababu ni lazima watoto waende likizo ili kupumzisha akili? Sasa kama watoto watabaki mwaka mzima shule kwa sababu eti wana mwalimu mmoja; hivi Serikali iko wapi;

Wizara ya Elimu iko wapi? Shule ya Sekondari ya Kata mwalimu mmoja; mimi kwa kweli nashindwa kuelewa!

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ambazo zinatolewa: nasema hili kwa uchungu kwa sababu wakati Waziri wa Elimu anatoa Ripoti ya Wizara yake katika Kamati yangu mwisho wa mwezi uliopita ilionesha dhahiri kwamba, fedha walizopewa hata zile za ndani mpaka mwaka unaisha wametumia nusu tu. Sasa ninajiuliza; hata hizi trilioni 11 ambazo tutazipitisha leo kweli zipo au ni kudanganya kwa tarakimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha za ndani hazijatumika na anasema kwamba, Wizara ya Fedha haijampatia, hili ni jambo la kusikitisha sana; tunawapeleka wapi watoto wetu halafu tunasema Kidumu Chama cha Mapinduzi? Ninachotaka kusema, tusiwapotoshe Wananchi; kama kweli ni Kidumu Chama cha Mapinduzi kionekane kinadumu kwa kutekeleza mambo ambayo wameyasema katika Ilani. Vilevile wawe wabunifu kuhakikisha kwamba, Wananchi wanaishi maisha bora na siyo bora maisha, wananchi wengi hawajui watakula nini. *(Kicheko)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, nichukue nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kwa kunipa ushirikiano mkubwa na hata kuweza kutekeleza kwa umakini na kwa kiasi kikubwa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ni *process;* tunajua tumetoka wapi na hivi sasa tuko wapi. Tukiondoa maneno ya kisiasa, nadhani kila Mtanzania atakubali kwamba, tumepiga hatua kubwa katika nchi yetu; maendeleo siyo kitu *automatic* tu kwamba unalala unaamka tayari una maendeleo. Tujiulize tumepata Uhuru lini na tuna miaka mingapi ya Uhuru; kwa miaka hii tuliyoyafanya ni makubwa ukilinganisha na nchi zilizoendelea. Kubwa hapa ni kukubaliana na changamoto zilizopo mbele yetu na changamoto ni sehemu tu ya chachu inayokupelekea ufikirie nini kifanyike baada ya kuwa umefikia hatua fulani ya mafanikio.

Ninazungumza hili nikiwa nina uhakika na nichukulie mfano wa Jimbo langu la Kibakwe, ambalo kwa hakika Watanzania wa Kibakwe wanakubaliana na mimi na tunakwenda kwa pamoja hasa katika maendeleo mazima tuliyofikia katika masuala ya miundombinu hivi sasa kila barabra ya kijijini kwangu inapitika. Uwezekano wa kupita kutoka kijiji kimoja kwenda kingine umefikia 95%, nyumba za walimu wa shule za msingi zimeongezeka kwa kiasi kikubwa karibu kila mwalimu ana nyumba kasoro upungufu uko karibia 15%, takwimu hizi ni kubwa kimsingi kulingana na hatua tulizopiga kuwa tulikuwa wapi na sasa tuko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yamesemwa hapa suala zima la upungufu wa walimu ni changamoto zilizopo. Tulikuwa hatuna sekondari kabisa katika Jimbo la Kibakwe, lakini leo tuna sekondari 12; ni hatua kubwa na wanafunzi wanasoma. Tumeweza kupeleka *form five* kwa Shule zetu za Sekondari za Kata ambazo zinasemwa na wenzetu hawa karibu wanafunzi 80 katika mwaka uliopita ni kiasi kikubwa maana hao

tusingekuwa nao. Niliwahi kusema kwamba, Jimboni kwangu wasomi wenye shahada tulikuwa tunahesabika, leo hii tumekuwa na idadi kubwa; ni kiasi kikubwa ambacho tumekifikia kwa muda huu mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kuna kubezana ni changamoto ambazo tuzipokee kwamba idadi ya walimu ni lazima tuifikirie na bajeti hii ime-*reflect* katika eneo hilo na imetenga fedha ya kutosha kwenye elimu. Ni imani yangu kwamba, itakwenda kuongeza na kupunguza tatizo la upungufu wa walimu na nyumba za walimu. Katika bajeti kuna sehemu kubwa mbili; kuna sehemu ya kukusanya mapato na kuna sehemu pia ya namna ya kutumia mapato hayo. Niende kwenye namna tunavyotumia mapato hasa katika Halmashauri za Wilaya. Halmashauri zinapewa fedha nyingi sana katika bajeti na ndiyo wanaotekeleza miradi inayogusa watu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Halmashauri hizi pamoja na kupewa fedha hizo lakini kubwa katika mambo yanayosababisha kuleta matatizo makubwa ni pamoja na Sheria yetu ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi ni jini linalokula watoto. Sisi kama nchi ni vizuri tukafikiria kuifanyia marekebisho Sheria hii ya Manunuzi. Mambo mengi katika Halmashauri za Wilaya yanabanwa na Sheria ya Manunuzi na ukiingalia Sheria ile na ilivyokaa na urasimu wa Sheria yenyewe si kwamba inachochea maendeleo au ina-*contro*l kitu fulani, bali inapunguza kasi na inatumia gharama kubwa katika kufuata *process* yenyewe kuliko kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeiomba sana Serikali tufikirie sana kuiangalia na kuibadilisha Sheria hii ili angalau iende sambamba na hali ya uwezo wetu. Inawezekana kabisa Sheria hii inafaa kwa wenzetu wa nchi zilizoendelea, lakini kwetu sisi kulingana na hali ya mazingira yetu na umaskini tulionano siyo vizuri tukatumia Sheria ile kama ilivyo ni vyema tukaifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la Miradi inayofadhiliwa na wahisani na hasa Miradi ya Maji katika Halmashauri za Wilaya. Hivi majuzi tu nilikuwa ninaongoza Ujumbe wa Kamati Ndogo ya Serikali za Mitaa, tulipita Mikoa ya Arusha na Manyara; tulipofika pale Kiteto, utekelezaji wa Miradi ya Maji kwa hakika ulikuwa hauridhishi kwa kiasi kikubwa, hali ambayo ilipelekea Kamati kuomba taarifa kamili. Taarifa ilipoletwa tatizo kubwa ni kwamba, fedha za wafadhili zina masharti mengi na masharti haya pengine Wizara nao watusaidie kwamba, wakati mwingine si jambo la busara kuhodhi fedha nyingi kubakia Wizarani, kuweka utaratibu ambao hauendi kule chini kwenye Halmashauri bali mchakato mzima wa manunuzi unafanyika Wizarani. Huu ndiyo mgogoro mkubwa ambao uko katika utekelezaji wa Miradi hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka makubwa kuwa, Miradi 10 ya *World Bank* kila Wilaya inaweza ikakutwa na tatizo hilo hilo. Kwani mchakato mkubwa wa utekelezaji wa miradi unafanyika Wizarani badala ya kuachiwa Serikali za Mitaa zenyewe zisimamie. Serikali za Mitaa ni *Government per se,* kwa mujibu wa Katiba zinatambulika; kwa nini hazipewi nafasi hiyo badala yake mchakato mzima ufanyike Wizarani; Mkandarasi atafutwe Wizarani halafu Wilayani wanafanya kazi gani na huku tuna Muhandisi na kila kitu na pia kuna wataalamu? Ninadhani huu ni upungufu mkubwa, ambao Serikali iuangalie sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la misamaha ya kodi. Katika bajeti hii, Mheshimiwa Waziri alipoisoma sikufurahishwa na kitendo cha misamaha ya kodi hasa katika madini; misamaha ya kodi kwa mfano ya mafuta ya petroli. Mafuta ya petroli kwenye migodi ya madini ndiyo ambayo tungekusanya pesa nyingi sana kuliko kuendelea kukusanya kwenye sigara na bia. Kila siku kuongeza kwenye eneo hilo, mimi ninadhani Serikali hapa pamoja na mikataba ambayo ipo, pamoja na ugumu inaoupata, lakini iangalie namna yoyote kuhakikisha kwamba, katika chanzo hiki ni chanzo muhimu ambacho tungeweza kukusanya pesa nyingi sana, maana hata pato lenyewe la madini hatupati la kutosha, basi tukusanye kutoka kwenye vyanzo kama hivi vya petroli wanavyotumia hawa wenye migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine, kwa mfano, hivi karibuni yametokea mapinduzi ya usafiri rahisi wa pikipiki za Kichina. Pikipiki hizi zina bei nzuri ambayo hata mtu wa kijijini anaweza ku-*afford* kununua, lakini kama tunaanza kuwekea kodi kwa maana hapa naona imeongezeka kutoka 30,000 ya usajili mpaka 45,000, tunataka zianze kupanda bei. Sasa hawa wananchi wa vijijini walishaanza ku-*enjoy* huu usafiri na maisha kule vijijini yamekuwa mazuri kwa sababu unaweza ukatembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kirahisi kwa sababu ya usafiri wa pikipiki. Mimi ninadhani imekuwa ni mapema mno, mngeacha kidogo Watanzania hawa nao wafurahie, watafune nchi yao kidogo wakati Serikali inatafuta vyanzo vingine. Chanzo hiki kwa hakika kitadumaza na kuzuia ile hali ya usafiri ambao ulikuwa ni rahisi na unasaidia sana kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Kibakwe; ni matumaini yangu kwamba, kwa yale ambayo tumeyafanya na ambayo tunatarajia kuyafanya kwa hakika tutaweza kuyafikia kwa ushirikiano kama walionipa na kama wataendelea kunipa ushirikiano mwingine ili wanichague kwa kipindi kinachofuata. Imani yangu ni kwamba, yale tuliyobakiza tunaweza kuyatekeleza. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2010/2011. Nitajielekeza zaidi katika kuchangia suala la kilimo, viwanda, Pato la Taifa na Pato la Mwananchi kwa ujumla. Ninapenda sana nipongeze juhudi ya Serikali kwa kuanzisha Benki ya Wanawake, ambayo ilifunguliwa rasmi mwaka 2009 na Mheshimiwa Rais. Vilevile naomba niipongeze Serikali kwa tamko lake rasmi la kutaka kuanzisha Benki ya Wakulima katika kipindi hiki cha mwaka 2010 na 2011. Mimi nafikiri kutokana na uanzishwaji wa benki hizi, zitaweza kutoa changamoto kubwa na zitaweza kuanzisha na kuongezeka kwa rasilimali katika Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, ninaomba kutoa rai katika mambo mawili yafuatayo:-

Benki zote hizi mbili zikiwekewa utaratibu mzuri zitaweza kutoa mchango mzuri hasa katika suala la mikopo kwa wananchi na hasa wakulima na hapa nawaangalia sana wakulima wanawake ambao ni 70% katika nchi hii ndiyo ambao wanajihusisha sana katika kilimo. Kilimo chao kimekuwa duni, hakiendelezwi ipasavyo kwa sababu siyo rahisi kupata mikopo. Ninaamini kwa kuanzisha benki hizi mbili ambazo sasa zitakuwa

ni benki kwa ajili ya wananchi, zitaweza kusaidia sana katika suala la mikopo kwa wanawake ambao ni asilimia kubwa sana ya wakulima walioko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vilevile nitoe changamoto nyingine katika suala la uanzishwaji wa hizi benki. Kwamba, sasa hivi kwa mfano Benki ya Wanawake iko Dar es Salaam ambako ni Makao Makuu ya Nchi, lakini kama nilivyosema wakulima wengi wako Mikoani, ukisema kwamba utawasaidia wanawake kupitia Benki ya Wanawake ambayo iko Dar es Salaam bila kupeleka matawi katika Mikoa, kwa kweli hapa hatuna *seriousness* ndani yake. Kwa hiyo, naomba Serikali ihakikishe kuanzia kipindi hiki cha mwaka huu wa 2010/2011, iamue kwa uhakika kabisa kuanzisha au kufungua Matawi ya Benki ya Wanawake katika Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri sasa waanze na Mikoa ambayo iko makini katika uzalishaji au inazalisha kwa wingi; kwa mfano, Mkoa wa Mbeya. Naomba tuanzie pale kwa sababu wakulima ni wengi na wanazalisha kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile benki hizi zitoe mikopo ya muda mrefu ambayo haina riba kubwa, unapozungumzia suala la Kilimo Kwanza maana yake ni kwamba lazima uhakikishe mikopo inakuwa ni mikopo rahisi ambayo riba yake inaweza kuwa nafuu kwa wakulima ambao wanazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uzalishaji naamini sasa utaongezeka endapo Benki ya Wakulima itaanzishwa, naomba Serikali ijizatiti katika kuhakikisha kwamba masoko yanapatikana kwa urahisi, masoko ya mazao yamekuwa ni tatizo hasa pale ambapo Serikali inaingilia kati uhuru wa kuuza kwa mfano, mahindi yanapokuwa yamezalishwa kwa wingi, Serikali inaingilia katika kuhakikisha kwamba, mkulima anakuwa huru katika kuuza mahindi yake nje ya nchi. Pale naona unambana mkulima, je, mkulima ambaye amezalisha kwa wingi sana, amezalisha kiwango kikubwa na ndani ya nchi hununui yote, nani atafidia hiyo hasara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima hapa Serikali iseme, je, itakuwa tayari kufidia hasara ambayo itatokea endapo mkulima hatauza mazao yake yote, naomba hili lisimamiwe kwa uangalifu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linahusu suala la kilimo linaendana na suala la viwanda. Viwanda vingi ambavyo tulianzisha hapa nchini, viwanda ambavyo vingechangia sana katika sekta ya kilimo, kwa mfano, viwanda vya magunia, majembe, korosho, vingi vimesimama na vingine wamepewa wawekezaji, lakini ukiangalia kwa undani wawekezaji hao hawaviendelezi kwa makusudi tuliyoyaweka, sasa hali hiyo itaendelea hadi lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vya Magunia mpaka sasa havizalishi, ZZK pale Mbeya amepewa mwekezaji hazalishi majembe, sasa majembe ndiyo yanayohitajika

pamoja na kwamba tume-*introduce* uzalishaji kupitia matrekta lakini kilimo cha majembe bado kinatumika, kiwanda kimesimama, nani atakuwa mwajibikaji sasa. Kwa muda mrefu na miaka mingi inapita tunazungumza hapa Bungeni, wananchi wanalia, tunaomba hivi viwanda vifufuliwe ili wakulima waweze kufaidika kutokana na mazao yanayozalishwa na viwanda hivyo, ni lini sasa hatua hiyo itachukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Mwekezaji ameshindwa na miaka kumi na tano imepita, kwanini isifike hatua sasa Serikali iamue kuwanyang'anya hao wote ambao waliwekeza katika viwanda hivyo ili tuweze kuanza ukurasa mpya. Hapo ndio tutaona jinsi Mkulima au Serikali inavyoweza kupata faida kutokana na viwanda vyetu ambavyo vinatia huruma na uchungu na wale waliowekeza hawana uchungu navyo, vimetengenezwa kuwa magodauni au ni viwanda ambavyo huwezi kuona sura yake ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni tulipitisha Sheria ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko mwaka jana. Hivi sasa wakulima kutokana na suala zima la kuondokana na umaskini wanazalisha mazao mchanganyiko mengi sana, ile sheria itaanza kutekelezeka lini? Mbona sioni kabisa Serikali ikichangamka kuona kwamba ile bodi inafanya kazi ili mkulima awe na uhakika wa kila zao analolilima linapata soko mara moja, naomba ile sheria ianze kufanya kazi haraka iwezekanavyo la sivyo sheria hiyo ambayo madhumuni yake yalikuwa mazuri sana na yanamlenga sana mkulima na yanalenga kumwendeleza mkulima ili aweze kuzalisha kwa wingi, sasa naona dira hiyo inaanza kupotea kwa sababu sheria ile haifanyi kazi. Naomba hili litiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za Vijijini, naomba barabara zetu ziimarishwe na hasa barabara zinazosafirisha mazao ambayo ni ya kila siku, kwa mfano, zao la chai. Katika Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe, wakulima wanazalisha sana chai, lakini barabara zake ambazo zinasafirisha chai hiyo kupeleka katika viwanda ni mbovu na duni. Hapa nataka kuzungumzia juu ya fedha inayotengwa kwa ajili ya barabara hizo, naomba Serikali iangalie hasa ile barabara ya Rungwe ambayo kiwango cha mvua ni kikubwa sana ukilinganisha na Wilaya nyingine katika nchi hii. Kiwango cha mvua katika Wilaya ya Rungwe kinaweza kufikia milimita hata mia mbili au mia mbili hamsini kwa mwaka kwa kiwango cha juu, barabara zake zinapokuwa mbovu mazao kama ya chai ambayo kila siku yanasafirishwa hushindwa kufika katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pamoja na ile barabara ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi, barabara ya lami ambayo inaanzia Katumba mpaka Tukuyu na njia inayopitia sehemu za Luangwa, naomba sasa kwa sababu mchanganuo wake umeshakamilika, fedha itafutwe ya kutosha ili barabara ile iweze kujengwa na usafirishaji wa zao la chai uweze kuwa ni wa uhakika. Naomba hili liangaliwe kwa umakini zaidi ikiwa ni pamoja na barabara nyingine ambazo zinasafirisha mazao kila siku katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya hivyo utakuwa umemsaidia mkulima, utakuwa umeongeza pato la nchi, utakuwa umeongeza pato la Taifa kwa ujumla na hivyo basi tutaweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nilikuwa na haya machache ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha. Ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama mpaka kipindi hiki, lakini pia niseme kwamba kwa kuwa ni bajeti yetu ya mwisho, nawashukuru sana wadau wote ambao walishirikiana nami katika kufanya kazi vizuri hususan Serikali yenyewe, wananchi kwa ujumla bila kuwasahau waandishi wa habari ambao wamekuwa bega kwa bega na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu wakati wakiwa wanachangia na kwa kweli yote ni mazuri kwa pande zote mbili japo kwa kuwa hiki ni kipindi ambacho ni nyeti hali kadhalika na mambo ya kuzungumzia unakotoka yapo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ni kipindi cha kwenda kujibu yale waliyotutuma wananchi, tutavuna tulichopanda muda umefika, katika kipindi chote cha miaka minne, Wabunge tuliwajibika kwanza ndani ya vyama vyetu, mbili hapa Bungeni tukiwa katika Bunge, na tatu katika maeneo yetu ya uwakilishi. Hata michango inayoendelea inategemeana ni kwa jinsi gani tuliwajibika katika maeneo hayo yote matatu, hakuna mchawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri ni kwamba Uchaguzi huu si wa Kitaifa, kwamba sasa ni Taifa linakuchagua wewe Mbunge, unakwenda kujibu pale ulipotoka kwa yale ambayo uliyafuatilia na ukayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi hii nampongeza sana Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania lakini pia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, uongozi siyo kitu rahisi, uongozi unahitaji uvumilivu na unahitaji ku-*balance* mambo, Mheshimiwa Kikwete ameweza katika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati tulipokuwa tunafuatilia sana Serikali yetu ifanye vizuri, tulikuwa tunatoa changamoto za aina mbalimbali, yote hiyo tulijua wana-CCM mwisho wa yote tutakwenda kujibu kwa wananchi wetu, kwa hiyo tulikuwa tunatoa changamoto za aina mbalimbali na Serikali ilikuwa makini kutusikiliza na kuyafanyia kazi. Leo najivunia kifua mbele kwenda kuinadi Serikali yangu imetekeleza wajibu wake hasa katika maeneo ninayotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi mwoga hapendi kuona wenzake wanaomfuatia wakiwa na uelewa au wakiwa na nguvu, anataka aongoze watu ambao hawana upeo mkubwa ili wasimuulize wala wasimhoji, lakini Serikali hii iliona hayo ikaona kwanza iwaelimishe watu wote ndiyo maana tukajitoa kwa hali na mali kwa kushirikiana na wananchi kujenga shule katika kila Kata, kujenga Chuo Kikuu na hivi

sasa tunajivunia kwamba vijiwe vya kuvuta bangi vimeishiwa wateja, watoto wote wapo mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili niseme tu wazi kwamba pamoja na kwamba shule zetu bado hazijafikia kiwango cha utoshelezi kwa upande wa Walimu na maslahi ya Walimu na vifaa vya kufundishia, lakini wale watoto siku zote walikuwa wapo mitaani, ndiyo waliokuwa wanafanya kazi wakiwa na umri mdogo, ndiyo hao waliokuwa wanafanya kazi bila tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika takwimu inaonesha kwamba Tanzania tuna watoto wengi, tunao watu wenye umri chini ya miaka 30 wengi kuliko watu wazima, kwa hiyo tumeokoa Taifa kwa sababu sasa tutakuwa na Taifa lenye tija kwa kazi hii ambayo imefanyika katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika hata kama ukiwa na elimu bado unahitaji kula, ndiyo maana tukasema kwamba kilimo kipewe uzito na kilimo kimepewa uzito. Ukiangalia kitakwimu utaona kwamba kilimo kimeshuka kidogo katika uzalishaji kwa sababu waliokuwa wanazalisha wengi walikuwa watoto na sasa tutakuwa na wazalishaji wazuri wenye elimu, nina uhakika Tanzania tutakimbia kwa sababu tumewekeza mtaji katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine pengine watu wanazungumza hasa kuhusiana na masuala ya uwajibikaji, Serikali imesimamia vizuri sana suala la uwajibikaji kiasi kwamba usimamizi umeongezeka, sasa hivi wananchi wote wanajua kufuatilia jinsi utendaji unavyojitokeza katika maeneo yao na katika hili tunatofautiana kidogo, wengine wanasema inatakiwa kuchukua hatua zote mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikakumbuka mfano wa mama yangu mzazi, yeye ni kiongozi, kuna siku mdogo wangu alikuwa ameacha mbuzi wakaingia kwenye shamba la mzungu mmoja ambaye ni Bruda. Wakati anampa adhabu ya kumpiga viboko ili asirudie tena kuwaachia mbuzi. Yule Bruda baada ya kuona mtoto anapigwa viboko akasema, hapana piga kichwani utosini, mama akasema wewe unataka niue mtoto sasa, akaacha. Kwa hiyo, mambo yote yanakwenda kwa kiasi na kwa mipango maalum, kwamba nini unafanya na unataka ufike wapi. Nasema Serikali kwa upande wa uwajibikaji imetimiza wajibu wake.

Pamoja na hayo kwa upande wangu wa Ruvuma, tunashukuru hivi karibuni tulipata swali la kwamba Serikali haijatimiza mipango yake ya kufikisha umeme kwenye maeneo, kwa kweli angezungumzia Wilaya ya Mbinga labda pengine wangempiga viboko, kwa sababu tuna umeme wa uhakika ambao umetokana na awamu hii. Hali kadhalika umeme wa gridi ya Taifa kama tulivyosema kwamba sehemu kubwa inategemeana na msaada wa wahisani umefikia hatua nzuri kiasi kwamba tunaamini kadri ilivyo kwenye ratiba kufikia 2013 hali itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yangu ni kwamba kesho wana Ruvuma pengine watakuwa hawana taarifa Wakandarasi tayari wako *site* kwenye kikao chao cha kwanza. Nashukuru kazi imefanyika vizuri na Chama kitashinda.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunashukuru Ilani imetekelezwa kwa uhakika.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na hasa kwa kuwa imezingatia kwa kiasi kikubwa malengo ya Milenia kwenye huduma za Jamii, Elimu na Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bajeti imezingatia kwa kiwango kikubwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Pamoja na hayo nina angalizo kwenye maeneo mawili ambayo ni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni msamaha wa *VAT*. Eneo hili litawasaidia sana Wafugaji na Wakulima Wakubwa. Serikali inapaswa kusamehe Zana za Wakulima wa kawaida. Sijaona kama trekta zitakazosomba mazao ya kawaida ya wananchi kama Mahindi, Alizeti, Maharage na kadhalika zimesamehewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia trekta hizo zinatozwa Bima. Vipuri vya Zana za Kilimo kama Sahani za Majembe ya trekta, Spana na kadhalika zinatozwa *VAT* hata hizi trekta za *Power Tillers* tunazoona zitawasaidia wakulima spea zake zitatozwa *VAT* na hivyo nyingi hazitafanya kazi baadaye.

Pili, Bei za *Power Tillers* ni kubwa sana Millioni 8-9 wakati zinanunuliwa na wafanyabiashara kwa Dola 1000 – 1500 tu sawa na shilingi milioni mbili. Kilimo Kwanza hakiwezi kufanikiwa kwa mtindo huu.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa Hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

- Uk. 60 Hotuba ya Hali ya Uchumi. Dhahabu imetajwa kuchangia asilimia 40.9 za *exports*. *Net income* kutokana na dhahabu ni kiasi gani kwa mwaka?

- Uk. 61 inaonekana uagizaji wa mafuta humeza asilimia 22.9 za *imports*. Mwelekeo wa kupatikana mafuta ndani ya mipaka yetu unatupa matumaini gani?

- Baraza la Wawakilishi wanadai mgao wa asilimia 4.5 wanaopata kutokana na faida za Benki Kuu, si stahiki. Serikali inatoa maelezo gani kuhusu hoja hiyo?

- Wizara haioni kwamba kutoza kodi ya majengo kwa msingi wa *"Built – Up – Area"* kungekuwa rahisi na haki kwa wote ikilinganishwa na utaratibu wa sasa?
- Bakaa ya Mfuko wa Jimbo imetumwa lini Majimboni?

- Je, Serikali haioni umuhimu wa kufuta kabisa ada za Sekondari ili wazazi wasikwepe kuwaandikisha watoto wa kidato cha kwanza kwa kisingizio cha kukosa fedha za ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima iliyohusika na uandaaji wa bajeti. Mheshimiwa Waziri nampongeza kwa uwasilishaji pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Kwanza. Inaridhisha kwamba bajeti imeweka msisitizo mkubwa katika kilimo, pia imejibu tatizo la *"Qul-growers"* wa kilimo cha miwa huko Kilombero na Mtibwa, tatizo ambalo ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mifugo. Ni muhimu pia kwamba mazao ya mifugo yamekumbukwa. Lakini nashauri Mheshimiwa Waziri atambue na kukumbuka kuwa tatizo kubwa kwa mfugaji kimatumizi ni madawa hasa ya kuogeshea mifugo na chanjo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Mkuu wa Mipango na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Nawapongeza sana kwa Bajeti nzuri na yenye mwelekeo wa kumkomboa kila Mtanzania kuondokana na umaskini na pia kuifanya nchi yetu kwenda mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii imelenga kuongeza kasi ya Kilimo Kwanza, Miundombinu, Afya, Elimu na kadhalika. Hii itasaidia sana kutuondoa toka kwenye umaskini na kwenda kwenye neema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wakulima wetu wameamua kulima kilimo chenye tija lakini sasa hivi bado wanakwamishwa na uhaba wa pembejeo (Mbolea, Mbegu bora na kadhalika) zana za kilimo matrekta, *Power tillers*, zana za kutumiwa na wanyamakazi, tatizo kubwa linalowasumbua sana Wakulima wetu ni soko la kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iramba Mashariki ni wakulima wazuri sana wa vitunguu maji, alizeti, katani, ngano, giligilani, dengu na kadhalika lakini sasa hivi hakuna uhakika kama ni msimu wa Vitunguu, walanguzi wanatoka Kenya, Burundi, Rwanda na kwingineko kuja kuwalangua wakulima wetu. Napenda kuuliza baada ya kupitisha Sheria ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa nini chombo hiki ambacho ndio kitakuwa mkombozi wa wakulima hakianzi kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wanapenda sana kujenga nyumba za kisasa, tatizo linalowakwamisha ni bei kubwa za bati, saruji na vifaa vingine vya ujenzi, kwa nini Serikali haipunguzi kodi kwa vifaa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwaendeleza wananchi wetu ni lazima tuwasaidie kusindika mazao yao na pia wawe na uwezo wa kupeleka mazao yao kwenye masoko. Nashauri Bajeti hii ilenge kumalizia miradi ya zamani ya Barabara kama Barabara ya Dar es Salaam – Mtwara eneo la Somanga, Dodoma – Singida eneo la Manyoni, Singida – Arusha na pia Daraja la Mto Sibiti, Iramba Mashariki na pia Serikali ilipandisha baadhi ya barabara hapa nchini toka Halmashauri za Wilaya na kuwa Barabara za Mkoa ambazo zinatengenezwa na Serikali kwa mfano Barabara ya Kiomboi – Kidaru, Ibapa - Mkalama, Matongo - Kwito, Mwangeza - Dominiki hadi Kidarata, barabara hizi zilitengwa wakati tayari Bajeti ilishatengenezwa mwaka 2009/2010. Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kutenga fedha mwaka huu wa fedha kwa ajili ya matengenezo. Napongeza sana kwa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kugundua kwamba kuna baadhi ya Halmashauri za Wilaya hazitumii fedha zote za maendeleo zinazotolewa na Serikali. Naunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuzichukua fedha hizo na pia napendekeza wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu maana hawatekelezi majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado napendekeza Wakaguzi wa Ndani wote ikiwa wa Serikali kwa pamoja na wa Halmashauri za Wilaya wawe chini ya Kurugenzi moja itakayosimamiwa na mlipaji Mkuu wa Serikali.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Bajeti kwa ujumla wake imejikita zaidi kwa wananchi na hasa katika sekta za barabara, umeme, elimu, maji na kilimo. Juhudi zielekezwe zaidi katika kusimamia vizuri rasilimali watu na fedha ili zitumike kama Bajeti inavyolenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa ya matumizi ya fedha za umma yapo katika Wizara na Halmashauri za Wilaya nyingi ni lazima sasa usimamizi uende sambamba na kutoa adhabu kali kwa wale wote wanaofuja rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya Taifa vilivyoainishwa katika Bajeti ni sahihi. Hata hivyo, mwaka huu wa fedha juhudi za pekee zielekezwe katika kufufua na kuimarisha Reli ya Kati ili kwanza kunusuru uhai wa barabara zilizopo ambazo zinaharibika sasa kwa sababu ya ubebaji mizigo mikubwa na mizito *(Bulky and Heavy*).

Pili, *Corridor* hiyo ni muhimu sana kiuchumi ikiwa ni pamoja na kufanya biashara nzuri na nchi ambazo ni "*Land locked*" *namely* DRC, Uganda, Burundi, Zambia *and* Rwanda. Mapato yatokanayo na biashara hii yatasaidia sana kuimarisha mfumo wetu wa kibajeti. Jambo hili tumelisema sana, sioni jinsi tunavyoweza kukuza uchumi wetu bila Reli ya Kati. *We are loosing business and big business.*

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo hoja ni pesa tukakope *WB, ADB* na hata Mabenki ya nje ili tuimarishe Reli ya Kati. Tukope ili tuwekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nidhamu ya matumizi makubwa na wakati mwingine yasiyo ya lazima kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika tujue kabisa sisi ni nchi maskini tena maskini kweli. Hivi kwa nini Serikali isizuie safari zote za nje kwa Maofisa wake? Safari nyingi ni *Ceremonial* tu, hazina tija hata kidogo, safari muhimu za viongozi wakuu tu ndiyo zifanyike. Zipo nchi hapa Afrika zimefuta kabisa safari za nje ambazo ni za mikutano ambazo hazina tija, mfano ni nchi ya Ushelisheli. Safari zote za nje zimezuiliwa kwa muda wa mwaka 1-2 tangu 2008. Tanzania, safari nyingi za nje za Mikutano, Makongamano ya Kimataifa hazina tija kabisa, mbali ya manufaa binafsi kwa Maofisa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia magari ya kifahari yote VX8 zote zibaki ni kwa Viongozi Wakuu tu kama vile, Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri tu. Wengine wote watumie magari ya nafuu kama vile *Prado Land Cruiser, Grand Suzuki, Land Lover 110 et cetera*.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari yote ya *GX, Range lover* yote yauzwe tena yauzwe kwa mnada wa hadhara. Fedha itakayopatikana ipelekwe kuimarisha Elimu ya Sekondari hasa Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ashauriwe vizuri ili aione hoja hii. Haiwezekani Wakurugenzi, Mameneja wa Mashirika ya Umma yaliyopo watumie magari ya kifahari kama VX8. Huu ni udhaifu mkubwa katika kusimamia rasilimali zetu za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vipya vya kodi. Wakati umefika, Hazina au Wizara ya Fedha kuangalia vyanzo vipya, vipo vingi, mfano, tuwekeze katika kufikisha gesi yetu Dar es Salaam, magari yaanze kutumia gesi, yote haya yatasaidia sana kupata vyanzo vipya. Kusimamia vilivyo sekta binafsi na *informal sector*, sekta hizi hazilipi kodi vizuri.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa misingi na shabaha ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ni pamoja na suala la kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida tunafahamu umuhimu wa kuendesha sensa ya watu na makazi. Shughuli hii ina umuhimu wake katika kupanga shughuli za kimaendeleo katika nchi. Mipango yote ya nchi inayopangwa iwe ya elimu, afya, ulinzi na usalama wa nchi, upigaji wa kura kuchagua viongozi mbalimbali wa nchi, shughuli za kiuchumi na nyingi nyinginezo hutegemea sana kuwepo kwa takwimu sahihi za watu na mgawanyiko au mtawanyiko wake katika maeneo mbalimbali. Kwa kujua hayo ndio pale nchi inapoweza kupeleka huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa raia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyo umuhimu wa kujua idadi ya watu nchini, ni hivyo hivyo ni muhimu sana kujua idadi ya mifugo nchini. Kwa muda mrefu sana sensa ya mifugo hapa nchini haijafanyika. Takwimu za mifugo zilizopo zinatokana na mkokotoo wa *data sampling* kwenye *household survey* zinazofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa yaliyopelekea matokeo ya ukame na mafuriko yaliyoikumba nchi yetu, mifugo mingi imekufa lakini kila mwaka tunaambiwa idadi ya mifugo inaongezeka. Nina mashaka makubwa na takwimu za mifugo ambazo tunapewa siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kwamba, sambamba na kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya sensa ya watu, ni vyema basi zikatengwa fedha kwa ajili ya sensa ya mifugo (*Head Count*) nchi nzima. Tukiweza kuifanya sensa hiyo na tukajua idadi halisi ya mifugo tuliyonayo Serikali itaweza kupanga mikakati madhubuti ya kuiendeleza sekta ya mifugo nchini, ikaweza kuchangia zaidi katika kutoa ajira kwa wananchi na mchango wake kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni za kugombea Urais, Ubunge na Udiwani akiwa Mgombea mwenza kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi aliahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne itapoingia madarakani itajenga vyuo vya ufundi katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwaandaa vijana kuweza kujipatia ajira halali, ahadi hii ni muhimu sana, kama ingetekelezwa ipasavyo. Lakini la kushangaza ni kwamba tunakaribia kumaliza kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, bado ahadi hii haijatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha. Taarifa tuliyonayo ni kwamba ujenzi wa vyuo hivyo havifiki hata 10 na baya zaidi hakuna hata Wilaya moja katika Wilaya 10 za Tanzania Zanzibar waliojengewa chuo cha ufundi kutokana na ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna uwezekano wa ahadi hii katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ikajirudia mwaka huu wa Uchaguzi, ni vyema basi kama chama hicho

kitapewa ridhaa na wananchi kuiongoza nchi hii hatua madhubuti zichukuliwe kuhakikisha kwamba na Wilaya za Tanzania Zanzibar nazo pia zinaingizwa katika mpango huo ili vijana wa Zanzibar nao wapate fursa ya kupata Elimu ya Ufundi ili waweze kupata ajira za halali.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Makatibu na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara, Wakurugenzi kwa kuandaa hotuba kwa umakini na ya kueleweka vizuri sana kwa wananchi wa kada mbalimbali nchini. Hata hivyo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ingawa katika bajeti ya 2009/10, Serikali ilijitahidi kudhibiti uchanganyaji wa petroli na mafuta ya taa, lakini tatizo hili bado lipo licha ya baadhi ya vituo vya kuuzia dizeli kufungiwa kuuza mafuta hayo. Hii bado ni changamoto na wananchi wanaharibikiwa magari yao ovyo ovyo tu. Ni lazima hatua kali zaidi zichukuliwe na Mamlaka husika.

Pili, naipongeza Serikali kwa kuanza kutenga fedha za sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2012 ila nashauri katika zoezi hilo suala la kuwabaini watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali ndani ya familia litenge rasilimali za kutosha ili nao waweze kuhesabiwa kwa usahihi ili waweze kujumuishwa ipasavyo katika Mipango ya Taifa.

Tatu, makubaliano na Serikali katika jitihada zake za kudhibiti matumizi yake kwa kupunguza posho zisizo na tija. Kuweka luku za matumizi ya umeme na simu katika idara zake, kuratibu ununuzi wa magari ya Serikali na aina za magari husika kwa lengo la kupunguza gharama. Ni kweli Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi bila sababu huku nchi ikiendelea kulalamika kuwa ni maskini. Tanzania si nchi maskini, umaskini wetu huongezwa kutokana na matumizi mabaya ya rasilimali tulizonazo. Hivyo naipongeza Serikali kwa kuwa wazi na kuonyesha dhamira thabiti ya kukomesha ufujaji wa mapato yake na hatua hizo zitasaidia kuonyesha jamii kuwa sasa Serikali imeamua kubana matumizi katika maeneo ambayo hayana tija kwa wananchi.

Nne, ufujaji wa mapato ya Serikali uko pia katika viwango vya majengo ya Serikali ambayo mengi hayakidhi ubora kutokana na ukosefu wa usimamizi thabiti pale ujenzi unapoendelea na tabia ya udokozi wa vifaa vya ujenzi ambayo imejikita kwa baadhi ya wafanyakazi wakati wa ujenzi husika. Hivyo kwa Serikali kuunda chombo cha kusimamia eneo hili itaokoa fedha nyingi za walipa kodi nchini. Natoa pongezi kwa hilo.

Tano, pamoja na kodi nyingi kufutwa au kupunguzwa katika bajeti hii, nashauri ushuru wa vinywaji baridi upunguzwe kutoka shs. 58 kwa lita hadi shs. 60 kwa lita kwa vile hivi ndivyo vinywaji vinavyotumiwa na watoto wagonjwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, nitaomba maelezo ya sababu za makampuni ya uchimbaji madini kuendelea kupewa msamaha wa kodi katika maeneo fulani fulani

ingawa yanapata faida ya madini yanayouzwa kwa mfano, dhahabu. Isitoshe ni kwa nini dhahabu ya nchi isihifadhiwe na Benki Kuu ili isaidie kuimarisha fedha zetu na kuzuia kuyumba kwake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti hii imedhamiria kufufua viwanda, kuongeza thamani katika mazao ya shambani na mifugo kwa kusindika mazao hayo. Hivyo haya yakifanyika wakulima, wafugaji na wavuvi maisha yao yataboreka kwa kuongezeka kipato chao. La msingi ni kujitahidi kutekeleza kwa vitendo hayo mazuri yaliyoandikwa na Serikali. Baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Muumba kwa kunijaalia siku ya leo kuamka nikiwa salama na kuweza kuishika kalamu na kutoa mchango wangu katika Bajeti hii iliyo mbele yetu ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo utafahamu kwamba hotuba hii imepata wataalam wa kuiandaa pia na msomaji hotuba alivyoisoma hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sina budi kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge lako kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa napenda nielekee kutoa mchango wangu katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali kumng’oa mwananchi katika dimbwi la umaskini. Bajeti yote imemgusa mwananchi ila shida kubwa kwa Serikali ni utekelezaji. Bajeti imezungumzia maendeleo. Tujiulize iko siku ambayo Serikali haijahubiri neno maendeleo? Tunazungumzia viwanda ama umwagiliaji maji. Tulidhani bajeti yetu itatueleza idadi ya viwanda vilivyoongezeka hapa nchini, pia wakulima walivyofaidika kwa njia ya umwagiliaji. Mambo haya imekuwa kila leo husemwa lakini bado utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za maendeleo za Halmashauri za Wilaya kutokana na maelezo ya Serikali imethibitisha kuwepo kwa bakaa katika akaunti za Halmashauri zetu. Kama kuna bakaa, je, ni kusema hakuna matatizo katika Halmashauri zetu? Hii ni alama kwamba kuna doa kubwa huko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mbolea Watanzania walo wengi ni wakulima, tukimtaka mkulima ni lazima twende vijijini. Huduma inayotolewa na Serikali kumfikia mkulima kama vile mbolea ni vigumu sana. Kumsaidia mkulima ndio kukuza uchumi pia kumng’oa mkulima katika kilimo kisicho na tija. Je, Serikali katika hili imejipangaje

kumpa huduma hii mkulima huko vijijini kwa wakati muafaka huku tukiangalia miundombinu yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vya mapato. Kuna vitu vingi katika eneo hili ambavyo nchi yetu ina uwezo navyo, lakini mara nyingi huingizwa nchini badala ya Serikali kutoa nchini. Hii ni ishara mbaya kwa nchi yetu kimaendeleo. Kuna mambo mengi katika nchi yetu yanazorotesha uchumi wetu kukua, kwa mfano, ushukaji wa fedha zetu siku hadi siku jambo hili hutuathiri sana pale Serikali inapokuwa na mikopo. Nia ni kukuza uchumi bali riba inakuwa kubwa sana. Ni vyema Watanzania tusimamie tunayosema kwa kuyatekeleza, tuachane na maandiko. Tanzania inawezekana kukopwa badala ya kukopa. Tukiwa wakweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/2011 kiasi cha shs. Trilioni 11.6 zitatumika, katika hizo matumizi ya kawaida ni shs. trilioni 7.8. Kwa kawaida asilimia 70% ya fedha hizi huenda kwenye manunuzi na shs. trilioni 3.8 zitakwenda kwenye maendeleo. Asilimia 100 za hizi ni manunuzi. Ina maana karibu fedha zote zinakwenda kwenye manunuzi. Naiomba Serikali kuweka mkazo kwenye taaluma ya ununuzi kama inavyofanya kwenye taaluma ya uhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 Serikali iliajiri na kufundisha Wahasibu. Mwaka huu pia Serikali imeajiri na kufundisha Wahasibu. Je, taaluma ya ununuzi itapewa kipaumbele lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Kwanza. Naipongeza sana Serikali kwa mpango wa kukipa kipaumbele Kilimo. Mwaka jana Serikali ilitenga fedha kwa Halmashauri kununua matrekta makubwa na yale ya Kubota. Matrekta ya Kubota bei yake madukani haizidi milioni 10 na kule nchini China bei yake mpaka bandarini Dar es Salaam haizidi milioni tano za Kitanzania. Sasa Halmashauri zetu zimenunua matrekta hayo kwa zaidi ya milioni 20 kwa moja. Naiomba Serikali iagize matrekta hayo kwa pamoja ili kupata bei nafuu na halafu kuzigawia Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera ya magari. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa Bungeni kuwa Serikali inaandaa sera ya Magari. Naiomba, Serikali iharakishe sera hiyo ili Serikali ijayo ianze na Sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya bajeti imejaa changamoto zaidi kuliko mapitio ya utekelezaji wa kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kiuchumi dunia, utendaji wa Serikali na mpango ya kimaendeleo imekuwa ikibadilika kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nashauri yafuatayo:-

Kwanza, kuwe na mfumo sahihi wa kufuatilia na kuzingatia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na endapo baadhi ya miradi haikutekelezwa, basi ichanganuliwe na ipewe kipaumbele cha kutekelezwa bajeti inayofuatia.

Pili, kuwe na mkakati mahususi wa kutumia kile tulicho na uwezo nacho badala ya kuwa na bajeti kubwa ambayo haiendani na uhalisi wa mapato. Matumizi yasiyo ya lazima yapunguzwe na yaepukwe kabisa.

Tatu, kuwe na vipaumbele vichache sambamba na kupunguza ghrama kubwa za uendeshaji wa Serikali kwa matumizi ya kawaida.

Nne, kuwe na uamuzi mahususi wa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya sekta ya uzalishaji zaidi pamoja na uboreshaji wa miundombinu.

Tano, kuwe na utaratibu wa kutenga fedha za uchaguzi kila mwaka ili kuepuka kuweka fedha nyingi wakati wa bajeti ya mwaka wa uchaguzi (*To create a sink fund for election*).

Sita, kuwe na mfumo unaoongeza na kupanua wigo wa kodi (*Tax base*) ili kila mwananchi aweze kuchangia na kulipa kodi na kwamba kuwe pia na usimamizi mzuri wa kukusanya na kusimamia mfumo huu.

Saba, bajeti ijibu zaidi changamoto za wananchi badala ya hoja chache zisizo na msukumo na maslahi ya Taifa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Manaibu Katibu Wakuu na Wataalam wote wa Wizara na wengine wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti ya mwaka 2010/2011. Baada ya pongezi hizo, napenda kutoa mchango wangu mdogo wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitabu cha Hali ya uchumi nizungumzie kuhusu kushuka kwa thamani ya shilingi jambo moja ambalo ningependa kupata ufafanuzi au maelezo kuhusu namna shilingi yetu inavyoshuka thamani (*value*) dhidi ya dola ya Marekani. Nataka kujua ni sababu gani zinazosababisha thamani ya shilingi yetu kushuka hivyo. Mwaka jana 2009 thamani ya shilingi ilikuwa shilingi 1200 – 1300/= kwa dola moja ya Marekani; leo Dola moja ya Marekani ni kati ya shilingi 1400/= mpaka 1500/=. Hali hii siyo nzuri kwa uchumi wa nchi yetu. Nataka kujua Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa shilingi yetu haiendelei kushuka thamani hovyo hovyo kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, riba ya mikopo. Viwango vya riba za mikopo bado viko juu sana pamoja na ukweli kwamba viwango hivyo vilipungua kutoka asilimia 16.05 Desemba 2008 kufikia asilimia 14.38 Desemba 2009. Aidha, ongezeko la riba kwenye amana za akiba bado liko chini asilimia 2.83 ukilinganisha na riba za mikopo asilimia

14.38. Bado mwananchi hafaidiki kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa benki hizo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikalli iendelee kuzungumza na benki hizo ili ziendelee kushusha riba kwenye mikoa angalau kufikia asilimia 10. Aidha, Serikali iendelee kuzungumza na benki hizo ili angalau riba zinazotolewa na benki kwenye amana zifikie angalau asilimia 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba zinazotolewa na taasisi nyingine za fedha zisizo za Kiserikali kama vile *Finca Tanzania, Pride, Bayport financial services, Blue financial service* na kadhalika ni kubwa sana. Riba za mikopo kwenye taasisi hizo zinafikia hadi asilimia 200. Hali hii kwa ujumla hailengi kumkomboa mwananchi maskini wa Tanzania kinyume chake inamdidimiza na kumfanya awe maskini zaidi. Serikali inaombwa itunge sheria itakayozibana taasisi hizo ambazo zimewageuza Watanzania kuwa shamba la kuchuma. Naomba maelezo ya serikali katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu Bandari, Reli, Barabara na Viwanja vya Ndege. Hili ni eneo la msingi sana katika uchumi wa nchi yetu. Ili nchi yetu iweze kupata maendeleo ya dhati na ya kweli, tunahitaji kuweka mkazo mkubwa katika sekta nilizozitaja. Zipo jitihada za wazi zinazoonekana katika sekta ya barabara na ile ya viwanja vya ndege, katika hili naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo sekta ya bandari na ile ya reli bado hazijapewa umuhimu wa kutosha. Kwa mfano, reli zote mbili *TAZARA* na ile ya kati, *TRC* inasemekana zinasafirisha wastani wa asilimia saba tu ya mizigo yote inayopita bandarini hii siyo nzuri hata kidogo. Barabara zinalazimika kubeba mzigo mikubwa sana na hivyo kuharibika mara kwa mara hali hii hulazimisha Serikali kutumia pesa nyingi kwa matengenezo ya barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji pia kuimarisha bandari zetu nchini ili zitoe mchango unaostahili katika uchumi wetu. Tukumbuke nchi za Kenya na Msumbiji zinaendelea kuimarisha bandari zao za Mombasa na Beira, sawa ili zichangie uchumi wa nchi zao. Tusipochukua hatua mapema wafanyabiashara wa meli watapunguza au kuacha kabisa kuleta meli zao katika bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bajeti ya mwaka 2010 -2011, vipaumbele vya Serikali Ukurasa wa 41. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi anisaidie hivi kati ya maeneo saba, yaliyotajwa ya vipaumbele, kipi kipaumbele cha kwanza? Nauliza hivyo kwa sababu nilitegemea kilimo kiwe cha kwanza ili tuendane na dhana ya kilimo kwanza. Aidha, nakumbuka tulishauri Serikali ikipe kilimo kipaumbele cha kwanza. Ninachokiona hapa ni kilimo kubakia katika kipaumbele cha nne kama ilivyokuwa kwenye bajeti ya 2009/2010. Mabadiliko yako wapi? Naomba maelezo ya Serikali kwa manufaa ya wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa za utafiti shilingi 30 bilioni, zipo katika ukurasa wa 42(vii). Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewahi kuagiza kwamba asilima moja ya bajeti ya Serikali itengwe kwa ajili ya shughuli za utafiti. Hii ilikuwa pia kutekeleza Azimio la Addis Ababa la mwaka 2008

la Wakuu wa Nchi za Afrika (*AU*). Nataka kujua je, shilingi bilioni 30, ni asilimia ngapi ya bajeti ya Taifa? Pili, je, ni kwa kiasi gani maagizo ya viongozi wetu yanazingatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msamaha wa ushuru wa bidhaa za petroli. Sielewi ni kwanini Serikali imeendelea kutoa msamaha huu? Hakuna sababu zozote za msingi zinazotolewa na Serikali. Naamini kabisa kwamba hakuna mkataba ambao hauwezi kupitiwa. Hivi kama tulifanya makosa bado tuendelee kufanya makosa! Izingatiwe kwamba makampni haya yanapata faida kubwa sana katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itafakari zaidi uamuzi wake huo. Maana kwa kuacha kutoza kodi hiyo tunapoteza pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti. Hii ni pamoja na kutoa pongezi kwa hotuba iliyotolewa na msemaji wa upinzani ambayo kama serikali ikitumia mawazo yake vizuri inaweza kusaidia kuondoa utegemezi wa wafadhili katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei. Hivi karibu tumeona jinsi thamani ya shilingi yetu ilivyozidi kuporomoka dhidi ya dola za Kimarekani. Hii inatokana na nchi yetu kutoza baadhi ya malipo kwa dola, kwa mfano, nchi zetu za jirani za Afrika Mashariki hawaruhusu malipo yoyote kufanyika kwa kutumia fedha za kigeni hata kama ni malipo hotelini. Hoteli husika itamwelekeza mhusika aende katika maduka ya kubadlisha fedha ili alipe deni hilo kwa fedha ya nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu ni tofauti kabisa mfano, malipo yote ya Hifadhi hapa nchini na baadhi ya huduma nyingine kama hoteli nna kadhalika hulipwa kwa kutumia dola, ni wakati muafaka sasa kutumia fedha zetu kwa kutoa tena TAMKO kwamba, malipo yote lazima yafanyike kwa shilingi za Kitanzania hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwango vya riba. Hili bado limekuwa ni tatizo kubwa kwa watu wa kipato cha chini au wakulima wadogo wanashindwa kukopa katika taasisi zetu za benki kwa sababu ya kutozwa riba kubwa sana. Wengi wao mpaka sasa hivi hawana dhamana kwa ajili ya mikopo. Serikali iwatumie wataalam kwa kushirikiana na *BOT* waangalie ni jinsi gani ya kupunguza riba katika taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha kushangaza, kukopa Benki riba ni kati ya asilimia 17% mpaka 25%, lakini ukiwa na *saving Account bank* wanampa mteja riba ndogo sana haifiki hata 5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya Serikali. Hili bado ni tatizo kubwa kwa Serikali kuwa na matumizi yanayozidi mapato. Nashukuru Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametueleza watakuwa na magari *specific* kwa ajili ya wafanyakazi wa

Serikali na Taasisi zake. Serikali inatakiwa pia kuhakikisha samani zote za ofisi za Serikali ziwe ni zile zilizotengenezwa nchini, Jeshi la kujenga Taifa linatengeneza samani nzuri sana. Pia magari ya Serikali yawe ni yale yasiyohitaji *spear* na *service* za bei ghali. Magari yaendane na hali ya sehemu husika. Kwa mfano, hivi Dar es Salaam Serikali za Mtaa zinahitaji Mercedez Benz? Wakipewa Vitara, Suzuki inatosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA lengo lilikuwa kupunguza umaskini kwa kuongeza kazi, bado lengo la MKUKUTA wa kwanza halijafikiwa. Ushauri wangu, itabidi kwanza kuangalia malengo mangapi ya MKUKUTA (I) yalitimizwa kabla ya kwenda kwenye MKUKUTA II.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa wananchi. Pamoja na Serikali kuwajengea wajasiriamali sehemu ya kufanyia biashara pale Dar es Salaam pale Machinga *Complex* ni nzuri ingefanya hivyo kwa mikoa yote Tanzania ili kuzuia vijana wengi kukimbilia Dar es Salaam wabaki katika maeneo yao. Serikali ihakikishe inatenga maeneo hayo katika kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, bajeti hii haijamsaidia kabisa yule mkulima aliyepo kijijini ambaye hawezi kula milo mitatu kwa siku pamoja na kuongeza bajeti ya kilimo lakini watakaofaidika ni wakulima wakubwa.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kuandaa bajeti ya 2010/2011 yenye kujali wanyonge, ni bajeti ya wanyonge hasa Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wafanyakazi. Hongera sana kwa kuwa bajeti hii ndiyo itajenga imani kwa Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya uongozi thabiti wa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa Uchaguzi Mkuu 2010. Napenda kutoa maoni au ushauri kwa maeneo yafuatayo kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa, mchango wa baadhi ya sekta za kiuchumi katika pato la Taifa. Uvuvi ukurasa wa 13, kifungu 27, kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uvuvi kwa asilimia 2.7, mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2005 na kusababishwa tu na matumizi duni na uharibifu wa mazalia ya samaki bali ilichangiwa na mambo yafuatayo:-

Wavuvi wadogo hawana uwezo wa kupata mikopo kwa ajili ya kununua zana za kisasa. Ushauri wangu ni kwamba, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara Mama ianzishe Mfuko Maalum wa Mikopo kwa wavuvi na mfuko huu ulenge wavuvi ambao wameanzisha vikundi. Kwa mfano, katika Wilaya ya Rorya kuna vikundi 36 vya wavuvi ambavyo vikiwezeshwa kwa kupatiwa nyezo na vifaa vinaweza kuchangia kwa asilimia kubwa pato la Taifa. Naomba ushauri huu uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi. Ukurasa 38(iii) kuimarisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili kufikia azma ya kilimo kwanza. Ushauri wangu ni kwamba, tathmini ya haraka pamoja na utafiti ufanyike kuhusu mabwawa yaliyoko nchini ili kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara na mifereji ya maji mashambani na Serikali iunde kanda za maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 41, aya ya 50(ii) kilimo kimetengewa shilingi 903.8 milioni sawa na ongezeko la asilimia 35.5. Ushauri wangu ni kwamba, katika fedha zilizotengwa asilimia 25 ziende kwa kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuimarisha mabwawa yaliyomo na mabwawa mapya. Naomba ushauri uzingatiwe katika Wilaya ya Rorya kuna mabwawa manne na mapya yanayoendelea kujengwa ni matatu. Hivyo, iwapo Serikali itatoa fedha za kutosha mabwawa saba yatazalisha tani 6,733 za mpunga kwa mwaka badala ya tani 861 za sasa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali haijafanya maamuzi ya kuangalia vyanzo vipya vya mapato, inasikitisha kuona bado kwa kila mwaka tunategemea wavuta sigara na wanywao vilevi kwa kuongeza kodi kwenye sigara na vilevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi bora kwa kuwa na maliasili nyingi ambazo hazitumiki ipasavyo kuliongezea Taifa kipato. Serikali iangalie inatumiaje rasilimali zetu kuongeza pato la Taifa, bila kusahau matumizi mazuri ya rasilimali watu na rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu matumizi ya Serikali. Serikali bado haijaweza kudhibiti matumizi yake, bado Serikali imeshindwa kudhibiti *ghost workers*, mishahara inalipwa wafanyakazi hewa. Serikali haijaweza kudhibiti safari za nje za viongozi hasa zile za nje si zote zenye tija. Misafara ni mikubwa mno, ipunguzwe na safari zisizo na tija nazo zipunguzwe. Ununuzi wa magari ya kifahari, bado ni tatizo kwani Serikali yetu ni maskini lakini tajiri wa anasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari ya anasa ni mengi na uendeshaji wake ni mkubwa na vipuri na mafuta vinaigharimu sana Serikali. Juhudi ziongezwe za kupunguza magari ya anasa. Vilevile uwepo utaratibu wa kununua magari kwa *ranks* za viongozi na magari ya Serikali yatambulike ni ya aina gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa samani kila mwaka Serikali inanunua samani nje na sababu kubwa ni ununuzi wa samani dhaifu kutoka nchi za China, Singapore na Indonesia ambapo huharibika kwa urahisi kwa nini Serikali isitumie samani zinazotengezwa nchini? Zina ubora na tutaongeza pato letu na ajira kwa Watanzania, tuache kuongeza ajira na pato la nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misamaha ya kodi. Serikali imelieleza Bunge kuwa imesamehe kodi ya shilingi 324.14 bilioni kwa mwaka uliopita peke yake kwa

kipindi cha miezi sita tu. Ripoti ya *CAG* inaonyesha msamaha wa Tsh 725 bilioni kwa mwaka 2009/2010. Hizi ni fedha nyingi na wengi wanaosamehewa ni wawekezaji kwenye madini. Hebu tuangalie upya jinsi gani misamaha hiyo itapunguzwa ili tuongeze pato tu nchini ili tupunguze au tuache kukopa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe ufafanuzi wa utata wa bajeti ya 2010/2011 ambapo mapato ya ndani yatakayokusanywa ni Tsh 6.003 trilioni lakini matumizi ya kawaida yaani (*recurrent budget*) ni Tsh. 7,790 trilioni sasa ziada ya 1.787 trilioni itatoka wapi? Au Serikali itakopa kwa ajili ya matumizi ya ndani? Je, hii inamaanisha kuwa matumizi yote ya maendeleo tutategemea mikopo na michango ya wahisani maana makusanyo yatakuwa 6,003 trilioni matumizi yaliyopangwa ni 7,790 trilioni yaani tuna upungufu wa trilioni 1.787 vipi kuhusu matumizi ya maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa mtazamo wangu *budget* hii haitaleta unafuu wa maisha ya Mtanzania wa kawaida wa kipato cha chini. Ukizingatia shilingi yetu imeshuka na itazidi kushuka huku mafuta ya petroli na diseli yakiendelea kupanda ambapo yana athari sana katika maisha yetu ya kila siku.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 79(c), ukurasa wa 43 - Taarifa ya Hali ya Uchumi: Naipongeza Serikali kwa kuwa sikivu na kukipa hadhi kubwa zaidi Kipaumbele cha Maendeleo ya Ardhi na Makazi hususan utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa ya Matumizi ya Ardhi ikijumlisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Katika Wilaya na Programu nyingine. Hata hivyo, kipaumbele hiki kilitakiwa kuinuliwa zaidi kwa kupangiwa fedha nyingi zaidi. Hii ni muhimu ili kuwezesha hata vipaumbele vya kilimo na maendeleo ya mifugo, haviwezi kuwa na tija na endelevu bila ya kupanga matumizi ya ardhi yetu ili kila shughuli ifanyike katika maeneo yaliyopangwa na kulengwa.

Kifungu cha 81(f)(ii), ukurasa wa 45 - Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa: Nashukuru kwa kipaumbele cha Viwanda hususan Viwanda Mama vya Chuma (Ligonga) na Makaa ya Mawe (Mchuchuma) kuzingatiwa. Kutokana na miradi mikubwa sana inayotarajiwa ni vyema Ardhi ya Ludewa ikapimwa na kupangiwa matumizi bora ya ardhi pamoja na kufanya tathmini ya Kimkakati ya Mazingira *(SEA)* ili kujihami na kujiandaa mapema kabla ya athari kutokea.

Kifungu cha 86(xi), ukurasa wa 51: Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa: Suala la kuendeleza ukanda mpya wa kilimo wa eneo linalounganishwa na Reli ya Uhuru (ikihusisha Ludewa), yaani TAZARA na Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mbeya na Rukwa ni ubunifu wa hali ya juu na wa kimaendeleo. Hata hivyo, shughuli husika zipangwe kwa umakini kwa kuzingatia matumizi bora ya ardhi na tathmini ya kimkakati ya athari ya mazingira *(SEA)* ili mpango uwe na tija na endelevu.

Kifungu cha 50(vii), ukurasa wa 42 - Makadirio ya mapato a matumizi ya Serikali: Naunga mkono hoja ya kuandaa *a*genda ya kitaifa yenye kuonesha maeneo ya

kimkakati katika utafiti kwa vile hakuna nchi iliyoendelea bila utafiti. Utafiti unahitahiji uwekezaji mkubwa wa wataalamu, vifaa na fedha kwa vile kwa nchi maskini kama Tanzania hususan inapokuwa ni kweli kwamba utafiti hautoi matokeo haraka na matokeo yake siyo *tangible*, inawezekana ikaonekana kama matumizi haya ya fedha ni *Luxury*, lakini si kweli kwani ni uwekezaji wa muda mrefu. Nitahadharishe kuwa, pamoja na kutenga fedha ni vyema kuwa makini katika kuteua timu ya watafiti wanaoweza kufanya utafiti huo kwa umakini na tija.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti hii na kuileta hapa Bungeni tuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti kwa ujumla wake haikuangalia namna gani ya kutoa unafuu wa nishati ya kupitia majimboni ili kuokoa mazingira yetu yanayoteketea kutokana na matumizi makubwa sana ya mkaa.

Zaidi ya 80% ya nishati inayotumika mjini na hata vijjijini ni mkaa. Kitendo cha kusamehe kodi kwenye gesi pekee yake huku mafuta ya taa na umeme haivishikiki ni hatari. Watanzania wanotumia gesi ni wachache sana. Makaa ya mawe bado hayajaenea sokoni. Misitu yetu itakwisha, tujiandae kwa ukame na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda kwa ajili ya mazao ya kilimo na mifugo bado ni tatizo. Tumepunguza ushuru kwa vifaa vya maziwa na kilimo lakini bila kuhakikisha mkulima huyu anawezeshwa kuanzia kulima, kusafirisha na masoko imara, bado wakulima wafugaji hawa hawawezi kujikomboa na umaskini. Ni muda sasa serikali kuhakikisha viwanda vya nyama, maziwa na kusindika matunda maeneo yote ambayo mazao haya yanapatikana vinajengwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti haijagusa vyanzo vipya vya mapato, kwa miaka yote tunategemea mapato ya serikali kwa kuongeza kodi kwenye bidhaa zilezile; pombe, soda, sigara na kadhalika.

Hata hivyo, pato tunalopata huko ni dogo sana, maeneo ambayo tungepata pato kubwa tumeyaacha. Hadi leo Sekta ya Madini ambayo ingeweza kuinua uchumi kwa kiasi kikubwa na kupunguza umaskini wanaonufaika ni wawekezaji. Samaki walioko baharini na kwenye maziwa yanayayotuzunguka wanaonufaika ni watu kutoka nje huko ugaibuni. Hatuna bandari ya samaki, ulinzi wa bahari yetu bado ni dhaifu sana. Kila leo samaki wanakamatwa wa mabilioni ya fedha, meli zinazovua na kuondoka bila kulipa popote ni nyingi. Ni aibu pato la uvuvi limeshuka kutoka asilimia tano mwaka 2008 hadi asilimia 2.7 mwaka 2009. Tunakwenda wapi? Tutaweza kweli kupata pato la kuleta maendeleo kwa Watanzania? Elimu ya ufugaji wa samaki bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna mianya mingi ya upotevu wa Pato la Taifa kutokana na *system* tunazotumia kukusanya fedha maeneo mbalimbali. Utaratibu wa kutumia vitabu vya risiti kukusanya mapato/ushuru mbalimbali umepitwa na wakati. Watumishi wasio waaminifu wanatengeneza vitabu vyao vya risiti kwa siri. Wanachukua fedha nyingi kwa njia ya wizi mtupu. Serikali ianze utaratibu mpya wa kutumia risiti za *computer* kwa kukusanya fedha za walipa kodi ili kuokoa fedha zinazopotea zilete maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa nyumba bora kwa kila mwananchi ni la msingi sana. Serikali imepunguza ushuru kwa viwanda vya *cement* lakini vifaa vingine vya ujenzi vimeachwa. Hili linasababisha vifaa hivyo kuzidi kupanda bei kila kukicha. Wafanyabiashara wanaangalia Bajeti ya Serikali wakiona chochote ambacho kimeachwa kuzugumzwa wao moja kwa moja wanachukulia fursa hiyo kupandisha bei watakayo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam na Morogoro mfuko wa cement ni Tsh.12,500; cha ajabu ikifika Singida, Tabora, Mwanza bei haishikiki; bei Tsh.18,000 - 22,000; kwa mwendo huo nani atakayeweza kumudu kujenga nyumba bora? Hivyo hivyo na kwa vifaa vingine vya ujenzi. Serikali itupie jicho eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti imeonesha kukua kwa kiwango cha misitu na uwindaji kutoka asilimia 3.46% mwaka 2008 hadi 3.5% mwaka 2009. Kwanza, ongezeko hilo ni dogo sana kulinganisha na rasilimali tuliyonayo kwenye misitu yetu na hifadhi zetu.

Usafirishaji wa mazao ya misitu umechangia kipato kwa Taifa, lakini hakuna uchunguzi uliofanyika kuona ni jinsi gani misitu yetu inavyoteketea. Ukataji wa mbao na magogo unaendelea kwa kasi kubwa kwenye misitu ya asili huku kukiwa na hakuna juhudi za nguvu za kukata mti panda mti.

Suala la doria ni muhimu sana nguvu ikaongezwa kwenye hifadhi zetu. Serikali inategemea wawindaji wa kitalii walipie kwa ajili ya kufanya doria kwenye hifadhi/mapori ya akiba; hii ni hatari sana kwa usalama wa rasilimali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapopunguza/kuondoa kodi kwenye bidhaa nia ni kumsaidia Mtanzania maskini. Msamaha wa kodi uliotolewa kwa watu wanaounganisha magari *(car assemble)*, usafirishaji wa maua kwenda nje; hapa Mtanzania maskini anafaidikaje na misamaha hii kama siyo kuwapa ulaji wafanyabiashara wakubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha bidhaa zote zilizopunguzwa/kuondolewa kodi, unafuu huo unakwenda kumfikia mwananchi kule kijijini na siyo kufaidisha wafanyabiashara wenye pesa zao.

Nashukuru sana, siungi mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii haijamgusa sana mwanachi wa kawaida ambapo ni dhahiri bei za petroli na dieseli bado zinaendelea kuongezeka na ni ukweli kupanda kwa bei za mafuta kunakwenda sambamba na kuongezeka kwa bidhaa nyingine zote zilizosalia.

Bajeti haioneshi kupungua kwa bei za bidhaa muhimu ambazo zinalenga dhana nzima ya MKUKUTA, zinazomgusa mwananchi katika maisha ya kila siku, mfano, bei ya saruji bado inaendelea kukua, bei za mabati, sukari, sembe na mchele zinapanda na haionekani serikali ina mpango gani wa kudhibiti bei hizi zisipande kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha Bajeti ya 2010/2011 kuwa makusanyo ya ndani TRA ni shilingi bilion 390 kwa mwezi; ni jambo jema sana lakini wasiwasi uliopo ni kwamba, ni jinsi gani fedha hizo zitatumika vizuri kuwafikia wananchi kuleta maendeleo ya kweli kwenye Halmashauri ambapo inaonekana kuna ubadhirifu, ufisadi na upotevu mkubwa wa fedha na mali (vifaa) kwenye Serikali Kuu na Halmashauri; na Serikali bado haijachukua hatua muafaka wa kudhibiti ubadhirifu wa fedha na mali huku ikitilia mkazo kwenye makusanyo ya fedha kuwaachia wanaozitumia vibaya? Ninashauri kuwa ni vyema serikali sasa iendane na ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuondokana na upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dhana ya Kilimo Kwanza ni vyema serikali ifanye kazi kwa vitendo kwa kujenga viwanda vya mazao ya kilimo ili kuandaa mazingira ya soko la uhakika kwa mkulima ili kuweza kuongeza ajira na kuendelea kwa uhakika wa kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana barabara zetu zinazotengenezwa na makampuni mbalimbali nchini haziko katika ubora unaotakiwa; hivyo, hatupunguzi tatizo bali tunaongeza tatizo, kwani makampuni hayo wanaangalia faida yao kuliko faida ya serikali; ni vyema Serikali iwe makini kwa makandarasi.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongeza nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Taasisi zilizoko

chini yake, kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii muhimu kwa taifa letu. Baada ya pongezi hizo, naomba na mimi nitoe mchango wangu mdogo kama ifuatavyo na niunge mkono hoja kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na mambo mengine, bado Bajeti yetu ni tegemezi kwa maana asilimia 93 ya fedha za Miradi ya Maendeleo zinategemea wahisani (ukurasa wa 20 - 21 wa Kitabu cha Hotuba). Aidha, katika kutumia wigo wa mapato kwa ajili ya kupata fedha za ndani, serikali bado inaendelea na vyanzo vilevile. Hivi ni kweli serikali imeshindwa kubuni vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato; kutegemea ushuru wa magari, vinywaji na vile vilivyoainishwa kwenye Hotuba ya Waziri? Baya zaidi, kuviondolea ushuru baadhi ya vyanzo vinavyochangia pato la ndani kama vile makampuni yanayochimba madini kwa kuondolewa ushuru wa petrol, malighafi ya utengenezaji wa kodi za simu ni hatua inayozidisha kuwa na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka wa bajeti, ushuru kwa vinywaji na sigara umekuwa ukipanda. Kwa nini serikali haiamui kupandisha ushuru wa bidhaa hiyo kiasi kwamba angalau kwa vipindi viwili vya bajeti ushuru kwa bidhaa hizo usipande kuliko ilivyo sasa ambapo kila mtu huamini kuwa, ushuru wa vinywaji na sigara ni lazima upande wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama serikali itategemea vyanzo hivyo vichache bila kupanua wigo wake kwa kuanzisha vyanzo vipya; ni dhahiri kuwa nchi yetu itaendelea kutegemea fedha za nje na kama wahisani wanapandisha kuchangia kwa wakati ahadi zao au kutochangia kabisa, matokeo yake ni kushindwa kuendelea na miradi ya maendeleo iliyopangwa au kuwa na limbikizo la madeni kwa makandarasi kama ilivyo kwa Wizara ya Miundombinu ambayo inadaiwa kiasi cha shilingi 259,255,651,327 kutokana na madai ya hati ya wakandarasi (shilingi 48,015,081,327), malipo ya awali *(advance payment)* shilingi 135,983,000,000 na fidia ya miradi ya barabara shilingi 75,257,570,000. Pamoja na kwamba, serikali inafanya mipango ya kulipa madeni hayo, hata hivyo, pamoja na juhudi hizo bado kutakuwa na upungufu wa shilingi bilioni 123.8 ambazo serikali haijaeleza ni wapi itazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadiri ya madeni haya kukaa bila ya kulipia, riba yake nayo inazidi kuongezeka na hivyo kuifanya serikali kushindwa kuanzisha miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko wapi ule utaratibu uliojiwekea serikali miaka kumi iliyopita ambapo kila mwezi ilikuwa ikitenga fedha zake za ndani kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara, ambapo barabara kadhaa zilijengwa kwa mpango huo bila kutegemea wahisani. Ninashauri serikali iufikirie tena utaratibu huo ili angalau tupunguze utegemezi wa fedha za nje ambazo wakati mwingine zina masharti ya unyanyasaji kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kurundikana kwa fedha za maendeleo kwenye akaunti za halmashauri wakati kwa upande mwingine serikali inadaiwa mabilioni ya fedha, sioni kuna mantiki ya kuendelea kuzipelekea halmashauri fedha nyingi ambazo zinakaa kwenye akaunti tu tena kwa muda mrefu bila kutumika. Huu si mpango mzuri wa matumizi ya rasilimali chache tuliyonayo. Naishauri serikali wakati inafanya marekebisho kwa halmashauri zetu, fedha hizo zipelekwe kwnye miradi mingine ya maendeleo hasa ya ujenzi wa barabara, kwa sababu kukamilika kwa miradi hiyo wananchi wengi watafaidika na barabara hizo; hivyo hakuna kitakachoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuwa imechelewa kuchukua maagizo ya kudhibiti matumizi yasiyokuwa na tija kwa umma, ambayo yalikuwa yakisababisha gharama kubwa na kuwa mzigo mkubwa kwa serikali kupunguza ununuzi wa magari (idadi ya magari), ni moja ya hatua ambayo serikali imeona ianze nayo. Hata hivyo, isiwe kupunguza idadi tu ya magari bali ni lazima serikali iweke utaratibu wa ujazo wa magari utakaotumika kwa watumishi wa serikali, hatua ambayo Kenya ilishaichukua ambapo gari lenye ujazo usiozidi CC 2,000 ndilo waliloamua litumike kwa Watumishi wa Serikali wakiwemo Mawaziri wenyewe.

Aidha, matumizi mabaya ya magari ya umma, serikali haina budi kuyasimamia kwa dhati hasa matumizi binafsi ya Watumishi wa Serikali, sambamba na kuwa na utaratibu mzuri wa kuleta magari ya umma kwenye meneo ya usalama, badala ya kuachiwa dereva au afisa kwenda na gari nyumbani kwake na kulilaza anapoona yeye panafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri pia serikali iimarishe karakana za serikali ili matengenezo yote ya magari ya serikali na taasisi zake, yafanyike kwnye karakana hizo badala ya zile za binafsi kama ilivyo sasa, kitu ambacho huigharimu serikali fedha nyingi.

Serikali ipitie upya mafao ya watumishi hasa wanapostaafu pasiwe na tofauti kubwa kati ya wastaafu wa serikali na wale wa taasisi za umma, sambamba na mishahara wanayolipwa. Ni kitu cha ajabu kwa mtumishi anayestaafu kama mtaalamu na msomi mwenye elimu nzuri tena aliyeitumikia serikali kwa muda mrefu baada ya kustaafu malipo yake yawe sawa na mtumishi mwenye elimu ya chini aliyetumikia kwa muda huo huo lakini aliajiriwa na taasisi au shirika akapata mafao mara nne zaidi ya yule mstaafu wa serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili pamoja na mambo mengine, ndilo hasa wanalolilalamikia watumishi wetu baada ya kuwaona wenzao wanaostaafu kuambulia mafao duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi amependekeza kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa makampuni ya

madini kuanzia mikataba iliyosainiwa Julai, 2009 ambapo makampuni hayo yamesamehewa kulipia VAT kwa bidhaa ya petroli. Hatua hii ya kusamehe ushuru huo utaipunguzia serikali kupata mapato yake ya zaidi ya shilingi 27 bilioni; sioni sababu zipi za msingi za kutoa msamaha huo kwa makampuni hayo yaliyosaini mikataba yake kwa kipindi alichokitaja Mheshimiwa Waziri. Kwa nini msamaha huo usingepewa makampuni yaliyosaini mikataba miaka ya 2006?

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo mimi huu ni udhaifu mkubwa na woga wa kuwaogopa wenye makampuni hayo ambao wamekuwa wakishindwa kuisaidia jamii inayowazunguka kwenye migodi yao kwa kuwapatia huduma za maji, barabara, afya, elimu, shule na kadhalika, kwani serikali nayo ikiwalazimisha wenye makampuni hayo kutoa huduma za jamii nilizozitaja katika viwango vitakavyoamuliwa na serikali au kuwalazimisha kutoa kwa maana ya kulipia ushuru wa petroli angalau kwa asilimia 50; serikali inahofia nini? Wataalamu kutochimba madini serikali itapoteza kiasi gani cha pato lake na kwa nini serikali haichukui hatua za makusudi za kuwaandaa wataalamu wake na kusimamisha uchimbaji mpya wa madini kwa maeneo mapya yanayogunduliwa hadi pale nchi itakapokuwa na wataalamu wake wa kutosha ambao wataweza kusimamia vizuri rasilimali hiyo inayotoweka bila kuwa na manufaa makubwa kwa nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha wa ushuru wa forodha kwa mabasi yotakayoingizwa nchini ni jambo jema. Hata hivyo ni vyema pia serikali ikaangalia na upande mwingine wa kutoa msamaha huo kwa wenye mabasi hasa yaendayo mikoani na yale yanayotoa huduma ya kuchukua abiria kwenye miji yetu.

Aidha, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ukarabati na upanuzi wa barabara unaoendelea kama alivyodai; unaendelea maeneo gani na hali ikoje kwa sasa?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Wafanyakazi wote, kwa bajeti nzuri ya kumsaidia Mtanzania wa hali ya chini.

Pili, naomba Benki ya Wanawake iendelee kupewa uwezo wa kusambaa nchi nzima. Tatu, katika kupanga mipango ya Wizara zote, usawa wa kijinsia uzingatiwe ili wanawake na wanaume wote wafaidike na rasilimali za nchi hii.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha ukuaji katika sekta za kiuchumi kimepungua hasa kilimo kutokana na ukame, lakini zipo sehemu nyeti ambazo mvua zinaendelea. Hatujaweka mkazo katika kilimo cha umwagiliaji kwenye mito na maziwa ambayo yanatuzunguka, bado tunaendelea na kilimo cha kutumia jembe la mkono, uhaba wa pembejeo na mbolea. Hivi sasa serikali ijielekeze zaidi katika kilimo pamoja na hatua za kuongeza *budget* katika kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Budget* hii imelenga zaidi katika Uchaguzi Mkuu wa Novemba, 2010 pamoja na mambo mengine lakini uchaguzi unaeleweka, ipo haja ya kupanga mapema kwani jambo hili linaeleweka; ni vyema sasa mipango yetu ioneshe vipi mwenendo wa bajeti kwenye masuala muhimu ambayo yatajitokeza na siyo kuyafikiria wakati yanapofika na kukaribia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato bado ni hivyo hivyo ambavyo vinajirudia rudia kila mwaka; ipo haja sasa ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato kama vile vya uvuvi, rasilimali za misitu, magogo na wanyama pori na kuachana na vyanzo vya vinywaji, leseni za magari na sigara, ambavyo vinaleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa za mafuta ya petrol na diseli zinaendelea kupanda; hivyo, zinazidisha mfumko wa bei na kupanda kwa gharama za maisha, jambo ambalo ni kero kwa mwananchi na zinasababisha ukali na ukata wa maisha na hivyo mwananchi haelewi kupanda kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali katika azma yake ya kuongeza mapambano dhidi ya rushwa, kesi 15 zimefunguliwa mahakamani. Je, katika kesi hizi ni ngapi zimehukumiwa na ngapi zimebakia pamoja na hatua nyingine zilizochukuliwa kwa watenda rushwa hao? Ahsante.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Tanga kuna miundombinu ya reli, bandari, anga na barabara. Reli ya Tanga imekufa kabisa kiasi kwamba, reli yenyewe imefunikwa na majani. Reli hii ilikuwa ina umuhimu sana kwa ajili ya kurahisisha usafiri ambao ungeanzia Tanga, Moshi, Arusha – Kenya kwa mizigo vilevile na abiria. Serikali haioni kuwa reli hii ingefanya kazi ingeweza kupunguza wingi wa magari ya mizigo yanayotumia barabara zetu ambazo zinaharibiwa sana na magari yanayobeba mizigo mizito?

Kuhusu bandari, serikali ilikuwa na mpango wa kuipanua Bandari ya Tanga eneo la Mwambani na wananchi walifidiwa ili kupisha ujenzi huu, lakini hadi sasa bandari hii haijajengwa na serikali ilisema kuwa bado haijapata mwekezaji; hivi hawa wakezaji zaidi wana nia ya kuwekeza katika madini tu lakini kwenye bandari hawataki?

Hivi sasa yale maeneo yaliyotengwa kwa ujenzi wa bandari baadhi ya wananchi wameanza kujenga makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa sana lakini lawama inawashukia pale wanapoamua kuchukua sheria kwa mtuhumiwa kabla tuhuma yenyewe haijathibitishwa na hii ndiyo inapelekea hasira kwa wananchi hatimaye kusababisha vurugu kati ya Jeshi na raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu kiasi ambacho inabidi aombe rushwa; hii inatokana na kucheleweshewa baadhi ya staili zao. Jeshi la Polisi huwa kila tarehe 15 ya mwezi wanalipwa posho ya kujikimu, lakini posho hii inacheleweshwa hadi tarehe 25 hawajapata. Serikali iliangalie Jeshi hili kwa jicho la huruma ili askari wetu waweze kufanya kazi zao kwa umakini na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ndivyo vinavyofanya kuwepo kwa mzunguko kwa fedha ambao utatoa ajira sehemu mbalimbali; mfano, mfanyakazi itabidi ale kwa hiyo mkulima atanufaika itabidi avae, apate fanicha. Mfanyabiashara na fundi seremala watanufaika. Hiki ndiyo chanzo cha ajira, iwapo viwanda vimefungwa mfano katika Jiji la Tanga, mzunguko wa fedha utakuwa haupo na hatimaye umaskini huongezeka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa matumizi ya simu na umeme; naipongeza Wizara kwa kubuni utaratibu wa kuweka LUKU katika Ofisi za Idara za Serikali. Serikali inapata hasara sana katika suala zima la simu kutokana na simu zinazopigwa ambazo siyo za kiofisi. Mfanyakazi au mtendaji anaweza kutumia simu kuzungumza na jamaa yake ambaye yuko nje ya nchi, tena kwa muda mrefu bila kujali kuwa anachofanya ni kosa. Pia umeme unatumika vibaya hata muda ambao siyo wa kazi, utakuta mafeni yanazunguka, yaani saa 24 hayazimwi kwa vile muhusika hana hasara anayopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hudhibiti matumizi ya magari, magari ya serikali yanatumika vibaya sana na wale wanaoyatumia, pia hawana uangalifu nayo. Gari linaweza likaharibika chombo kidogo tu, lakini linaripotiwa halifai ili gari lile liuzwe linunuliwe na wao wenyewe. Idara zihimizwe kutunza magari yao na matengenezo yafanywe kwenye gereji zinazoeleweka siyo gereji za chini ya miti ambazo baadhi ya vifaa vinaibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa SACCOS; wananchi wengi wanapenda kukopa na SACCOS ndiyo mkombozi lakini wananchi hao walio wengi hawana kipato cha kuwawezesha kujiunga na SACCOS. Sasa mwananchi huyu atasaidiwaje ili apate mkopo iwapo hata ule uwezo wa kujiunga na SACCOS hana? Itafutwe pia njia mbadala ya kuwawezesha wananchi kuwa wajasiriamali ili kujikwamua katika dimbwi hili la umaskini.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii, kwanza, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi ngumu wanayokabiliana nayo wakati wakiandaa mazingira halisi yanayowezesha Taifa hili kusonga mbele ama vinginevyo namwomba Mwenyezi Mungu awasaidie.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji wa Wizara hii, kwa upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ni chombo muhimu sana katika kutoa na kusimamia haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu ambalo limetengwa kwa Wizara ya Katiba na Sheria haliwezi kupata fungu linaloweza kukidhi mahitaji ya utendaji wa mahakama zetu na hivyo kukifanya chombo hiki kuwa dhaifu sana, jambo ambalo linapelekea watu wengi kukosa haki zao na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzingatie sana suala la kutoa kipaumbele kwa elimu. Ili tupate elimu bora lazima tuboreshe mazingira ya elimu, ikiwa ni pamoja na makazi ya walimu ili kumwezesha mwalimu kuipenda kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, unampelekaje mwalimu kijijini kwenda kufundisha wakati hujamtayarishia mazingira ya kazi? Ninaomba sana tuweke mkakati wa kujenga nyumba za walimu. Pia naomba tuwawekee heshima na hadhi walimu wetu ili wasihujumiwe ovyo, kwani kitendo cha kupigwa walimu na wanakijiji kwa kisingizio cha kwamba eti mifugo iliingizwa kwenye eneo la shule na mifugo hiyo kuondolewa na wanafunzi ni kitendo cha aibu na cha kuwadhalilisha walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii ambayo mosi imeendelea kutoa kipaumbele katika kilimo na pili imeanza kujenga dhamira ya kujitegemea badala ya kuwa bajeti tegemezi.

Jambo la kushangaza na linalosikitisha ni la bajeti hii kuisahau kabisa Sekta ya Uvuvi. Kwa mfano, wakati bajeti imetoa msamaha kwa pembejeo za kilimo na mifugo hadi ya kuku, hakuna msamaha wowote kwa zana za kilimo.

Jamii ya wavuvi nchini mwetu imeitikia wito wa kuzisalimisha nyavu zenye macho madogo. Wizara husika inaendelea kulisimamia zoezi hili kwa nguvu kubwa. Hatua hizi zinasaidia kupunguza uharibifu wa mazalio ya samaki na kuwalinda samaki wachanga. Ili dhamira hii ya serikali yetu iwe ni yenye mafanikio, tulitaraji basi bajeti ingetilia maanani kupunguza au kuondosha ushuru kwa zana za uvuvi kama vile nyavu na mashine za boti.

Nitalazimika kusimama japo kwa shingo upande wakati wa Kamati ya Matumizi iwapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha hatatoa maelezo juu ya namna ya kutukwamua wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya bajeti yake na kutoa kipaumbele kikubwa katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti kutoa kipaumbele katika kilimo, lakini natoa rai kuwa ni lazima serikali ichukue tahadhari kubwa kwenye eneo la *Export Levy*.

Uzoefu unaonesha wanunuzi wa korosho mara zote hutengeneza *curtail* kwa nia ya kuwaibia wakulima; hivyo, kwa kuongeza ushuru huo kutoka 10% hadi 15%, upo uwezekano wa wao kujipanga na kununua korosho kwa bei ndogo. Ni vyema mkakati uwekwe ili kuhakikisha bei ya korosho haishuki kwa kisingizio cha kupanda kwa ushuru huu, kutokana na mipango haramu ya *curtail*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa serikali inahimiza ujenzi wa zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila kata. Ninatoa rai kuwa ni vyema jitihada ziwekwe ili watumishi wa kutosheleza wapatikane. Serikali izalishe wataalamu wengi ili kukabiliana na zahanati na vituo vya afya vilivyopo na vitakavyokuwepo. Hali ya sasa ya uhaba ya walimu kwa shule za sekondari haivutii, walimu ni wachache na pia vifaa havitoshelezi; ni vyema basi hali hii isijitokeze kwa sekta yetu ya afya chini ya mpango wa zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ni kichocheo cha uchumi, ni vyema bajeti ikazingatia sana kuendeleza Bandari zetu nchini kwa ajili ya kuchochea mapato yetu na pia kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu, pia sitamsahau Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara. Nawapongeza kwa kuandaa bajeti nzuri ya kisasa na inayoeleweka, kwani maeneo muhimu mmeongeza fedha na kusamehe kodi baadhi ya maeneo kwa manufaa ya Watanzania na hata kuwavutia wawekezaji.

Ninayo mambo mawili, matatu hivi:-

Kwanza, tunaposema vifaa vya kilimo havina kodi ni jambo jema kwa wananchi lakini waagizaji wanapoagiza bidhaa, bidhaa hiyo inapofika bandarini, TRA wanasema hata zile tella za *power tiller* zina kodi na hulazimika kulipia. Mimi nina ushahidi, ningependa ufafanuzi wa maandishi.

Pili, ninaipongeza Wizara kwa kuwa na wazo la kuanzisha Benki ya Kilimo. Wazo hili ni zuri na tumechelewa, nchi nyingi zina benki za namna hii kama China na kadhalika. Benki kama hizi ni vyema zikalenga kwa wakulima moja kwa moja.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi kwa Waziri wa Fedha na Uchumi na Wataalamu wake wote, kwa matayarisho mazuri ya Bajeti ya Mwaka 2010/2011, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mgao wa *Skill Development Levy (SDL)* unahitaji kuangaliwa upya. Kwa sasa Serikali inakusanya *SDL* ya 6% na inagawia VETA 2%; 4% inayosalia inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Napendekeza serikali iongeze mgao wa *SDL* kwa VETA mpaka angalau 3% ili kuiwezesha kumudu majukumu ya kuendeleza Elimu ya Ufundi katika Wilaya zote kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Aidha, napendekeza pia Serikali itenge 3% inayosalia kwa ajili ya *Tanzania Education Authority (TEA)* ili kuiwezesha kuendeleza Sekta ya Ualimu.

Mpaka sasa Twiga Bancorp ambayo inamilikiwa na Serikalli kwa 100%, ina mtaji *(core capital)* wa shilingi 4.5 bilioni. Mtaji huu ni mdogo kiasi kwamba, Benki hii haijapata leseni ya kufanya biashara kama Benki kamili. Ili iweze kupata leseni ya Benki kamili, inahitajika kuongeza mtaji wake mpaka shilingi 5.0 bilioni. Benki yenye mtaji wa shilingi 5.0 bilioni tu ipo katika hatari ya kuanguka na kunyang'anywa leseni ikiwa itapata hasara ya aina yoyote.

Kwa hiyo, ninapendekeza wenye hisa katika Benki hii (Hazina), aongeze mtaji wa Benki mpaka kufikia angalau shilingi 7.0 bilioni kwa kuongeza shilingi 2.5 bilioni mwaka huu wa fedha juu ya *core capital* iliyopo ya shilingi 4.5 bilioni.

Mtaji ukiongezeka kama nilivyopendekeza hapo juu, Benki Kuu itaweza kuipatia Benki ya Twiga leseni kamili ya kufanya Biashara za Kibenki kamili na hivyo kuiwezesha Benki kuongeza faida kutokana na ongezeko la mikopo itakayoweza kuitoa kwa wateja wake. Aidha, Benki hii imekuwa inakusanya amana nyingi *(deposit)* ambazo imeshindwa kuzibadilisha kuwa mikopo kwa sababu ya udogo wa mtaji wake. Tuiwezeshe Benki hii kukuza biashara ya mikopo kwa kuiongezea mtaji.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa ajili ya bajeti nzuri.

Bajeti hii ni nzuri, inatia matumaini kwani inaonekana kuwajali Watanzania wengi wa kawaida. Pamoja na misukosuko iliyopo ya kiuchumi iliyotokana na misukosuko ya uchumi kwenye nchi zilizoendelea, bado uchumi wa taifa letu uliendelea kukua kwa asilimia 6.0 (mwaka 2009). Pili, pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka 628,259 (mwaka 2009) kufikia 693,185 (mwaka 2009). Bajeti hii ni ya matumizi kwani sekta zilizoainishwa kuwa ni vipaumbele vya Taifa vilevile zimepangiwa fedha nyingi; hii inadhihirisha kuwa serikali iko *serious.* Sekta za Miundombinu, Kilimo,

Elimu, Afya, Maji, Nishati na Madini, zote mwaka huu zimetengewa fedha nyingi zaidi ya mwaka (2009/2010).

Tatizo lililopo ni kuwa keki yenyewe ndiyo ndogo. Matatizo yaliyoko kwenye sekta hizi ni makubwa; kwa hiyo, fedha hizi zilizotengwa hazitoshi. Ninaishauri serikali iendelee kupanua wigo wa kukusanya mapato ili Bajeti ya Taifa iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi umeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi. Wananchi wajasiriamali 66,559 wamefikiwa na mikopo; kati yao wanawake ni 23,708 na wanaume ni 42,851.

Je, ni kitu gani kimepelekea wajasiriamali wanawake wawe wachache waliopata mikopo? Ninatambua kuwa, wanawake ndiyo wazalishaji wakuu, ndiyo wajasiriamali wadogo wadogo, wanaopata kipato kidogo na kukitumia kutunza familia. Je, serikali katika bajeti hii imeweka mikakati gani ya kumlenga mwanamke na kuhakikisha Mfuko huu unamfikia?

Mikopo mingi haikurejeshwa kwa muda, kwa sababu watu walipewa mikopo bila kupewa elimu ya kutosha juu ya mikopo na juu ya ujasiriamali. Je, bajeti hii itahakikisha kuwa elimu ya kutosha inatolewa kwa wakopaji kabla mikopo haijatolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake pamoja na wizara nzima kwa jumla la maandalizi mazuri ya hotuba iliyowasilishwa bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika wizara mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ni vema serikali itoe kipaumbele kwa kumalizia viporo vya miradi iliyopo na ile inayoendelea badala ya kuanzisha mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo, dhana ya kilimo kwanza ipewe mkazo zaidi kwa wakulima wadogo kwani hawa ndio wengi nchini. Kufanikisha hili ni vema kuzingatia yafuatayo:-

- Kuwe na urahisi wa upatikanaji wa zana ndogo ndogo na pembejeo kwa bei nafuu.

- Ni vizuri kuwe na punguzo la bei ya mafuta kwa zana za kilimo, hili linawezekana kwani hufanyika katika baadhi ya nchi za Ulaya na Marekani.

- Uimarishaji na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji upewe kipaumbele.

- Ujenzi wa masoko ya bidhaa za kilimo uimarishwe kumrahisishia mkulima mdogo kupata eneo la kuuza mazao yake. Ujenzi wa masoko hayo uambatane na uboreshaji wa barabara za vijijini kumwezesha mkulima kufikisha mazao yake sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maji, juhudi za serikali zinaonekana wazi katika sekta hii. Mifano hai ipo miji midogo ya Mombo na Hale katika Jimbo la Korogwe Vijijini, kwani shida ya maji safi imepungua kwa kiasi kikubwa na kazi ya kubadilisha bomba chakavu katika miji hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingi vinafaidika kwa maji safi kutokana na huduma ya visima vifupi na pampu za mkono. Haya ni mfanikio makubwa ya serikali ya awamu ya nne hususan kwa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu, lengo la Taifa kuwa kila Kata iwe na shule ya Sekondari japo moja limekamilika kwa asili mia moja (100%). Ni ukweli usio na ubishi haya yote ni mafanikio ya serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa sasa ni kuongeza juhudi kuziboresha sekondari zetu kwa kuzipatia walimu wa kutosha, maabara, maktaba, mabweni hususan kwa wasichana na nyumba za walimu ili iwe kama motisha kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miundombinu, Barabara. Miundombinu ya barabara katika Jimbo la Korogwe Vijijini imeboreshwa, takribani kiwa asilimia 85 ya barabara hizi hupitika kwa nyakati zote. Hii ni historia katika jimbo hili. Vile vile kumekuwepo na matengenezo ya barabara mpya kabisa ambazo hazikuwepo awali. Haya ni mapinduzi katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Reli, wakati umefika reli ya Tanga/Arusha ifufuliwe. Usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli unaokoa sana barabara zetu kupitisha magari mazito ya mizigo. Pia umaarufu wa *stations* za Mnyuzi, Korogwe na Mombo utarejea na kuongeza uchumi kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura nianze kwa kusema kwamba Bajeti hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja (100%).

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii ni Bajeti ya kawaida kwa maana kwamba si nzuri wala si mbaya bali ni Bajeti ya kuelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye bajeti hii pia ni wa kawaida kwa maana ya kujaribu kunyoosha maeneo machache yenye kuhitaji marekebisho ili angalau inyooke. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Suala la kodi kwenye mafuta ya taa. Eneo hili litakumbukwa nilimeliongelea takribani mara zote nilipokuwa nachangia Bajeti. Eneo hili linahitaji uangalifu mkubwa na mbinu ili kutowaumiza walalahoi na pia kutotoa mwanya kwa wachache wanaotumia mwanya wa msamaha kwa kujitajirisha. Ushauri wangu ni kwamba mafuta ya taa yawekewe kodi ili kuwaokoa wenye vyombo vya moto na matatizo ya uchakachuaji ambao unawabebesha gharama kubwa ya matengenezo wenye vyombo vya moto kutokana na mchezo mchafu wa kuchanganya mafuta ya taa na diseli. Ifahamike pia kwamba ukiwekea kodi kwenye mafuta ya taa watu hawa watakimbilia kwenye mafuta ya ndege *(Jet A-1)*, lakini na huko pia iwekwe kodi lakini wensye ndege wote watakaokuwa wanaweka mafuta wapewe rejesho la kodi *(Tax returns*) kwa mafuta watakayokuwa wamenunua kwa kuweka kwenye ndege zao. Hii itaondoa kimbilio la pili la wachakachuaji.

Eneo hili kama litasimamiwa kwa makini basi litaongeza kodi kwa serikali lakini pia litasaidia sana wenye vyombo vya moto kwa kuwaokoa na matengenezo yasiyo ya Lazima. Baada ya hapo itafutwe njia mbadala ya kuuza mafuta ya taa vijijini ili kuandaa mizigo kwa mlalahoi pia.

2. Maeneo mengine ni maeneo ya mikopo. Tumekuwa waoga wa kukopa lakini pia tunapokopa tumekuwa ni wasimamizi wabaya wa mikopo *(Debt management).* Mikopo ikopwe lakini si kwa ajili ya kulipana mishahara bali kuimarisha miundombinu yetu. Hiyo itasaidia kwa sababu ujenzi wa miundombinu ni muhimu hasa ukizingatia kwamba gharama zake zinakuwa kubwa kila kukicha.

3. Maeneo mengine ni maeneo ya madini na mafuta. Hayo ni pia ambayo usimamizi wake utahitaji uangalifu na jicho la karibu *(Hands on eyes on approach).* Haya ni maeneo ambayo baadhi ya mataifa tunayoyaona yamepiga hatua basi kwa kweli maeneo haya yamechangia kwa kiasi kikubwa.

4. Kilimo cha chakula na cha biashara. Nilitembelea Kigoma hivi karibuni nikabahatika kwenda kutembelea kilimo cha kahawa. Kahawa ile ni ya *grade* ya juu sana kiasi cha wakulima wake kupata bei kubwa sana kwa kila kilomoja wanayouza. La kusikitisha ni kwamba mashamba yao ni madogo madogo mno, sasa ninachoshauri kwa maeneo kama haya, ni serikali kuwaelimisha wakulima na kuwawezesha kupata mikopo ili waweze kujinunulia angalau *Power Tillers* ili mazao yao aina hii yaweze kulimwa kwa kiwango cha kuridhisha. Tuwasaidieni wakulima wetu kwa kuwarahisishia njia za kufikia mikopo yenye unafuu kwa urahisi.

5.	Utalii nao ni eneo jingine linalohitaji usimamizi wa karibu kwani na mchango mzuri kwa Taifa pamoja na wananchi kwa ujumla.

6.	Maeneo ni mengi lakini nimalizie kulitaja tu eneo la uimarishaji wa viwanda vidogo vidogo (SDO) na viwanda vikubwa. Huu nao ni msingi kwenye maendeleo yetu. Sio tusigeuke wazalishaji wa malighafi na nchi yetu kugeuzwa soko la bidhaa zinazotoka nje kwa bei ya juu kwa malighafi yetu tuliyouza bei chee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema naunga mkono lakini umakini uwepo katika maeneo yote niliyojaribu kuyaainisha hapo juu. Sote kwa pamoja basi, tumshuru Mwezi Mungu kwa hatua hii aliyotufikisha.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa lakini kwa jinsi alivyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa pamoja na urefu wa taarifa ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya napenda kuwapongeza Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, Mkurugenzi na makamishna na wote waliohusika na uandaaji wa Bajeti, ambayo ni nzuri na yenye vipaumbele muhimu saana sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujikita katika kilimo, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu, ili tupate mafanikio ni lazima tujikite kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji, kutumia mbolea na madawa ya kuua wadudu, kuuwa majani kama magugu. Kuhusu umwagiliaji ni lazima tutenge maeneo machache kwanza ambako yapo maji ya kutosha ili miradi itakayoanzishwa iweze kumalizika ili ilete tija kwa serikali na baadaye tunasogea hatua kwa hatua. Lakini tukianzisha miradi mingi (katika Mikoa mbali mbali) miradi hiyo itashindwa kumalizika badala yake tunapata hasara ya kupoteza fedha zetu bila mantiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Pembejeo, naishauri serikali kuondoa ushuru katika madawa ya kuuwa wadudu na magugu ili wananachi wengi waweze kumudu. Kununua madawa hayo ili yawanufaishe katika kuzalisha mazao ya kutosha, ili kutimiza lengo la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Matrekta, ninaishauri serikali kujiondoa katika kusimamia matrekta hayo, badala yake matrekta haya yamilikiwe na vikundi vidogo vidogo (ushirika) *SACCOS* au watu binafsi wenye uwezo wakopeshwe, kwa kufanya hivyo matrekta haya yatatunzwa vizuri sana hivyo kuwa na ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tatizo, urasimu umekuwa mkubwa mno kiasi kwamba vikundi au watu binafsi huchukua muda mrefu mno hadi miaka na wakati mwingine hukosa kabisa pamoja na kutimiza masharti yote, hii kero kubwa mno kiasi cha kulirudisha Taifa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuchanganya mafuta (chakachua), ushauri, *EWURA* wafanye utafiti kuona ni kampuni ngapi zinanunua mafuta aya taa na mafuta ya *Jet A* ili kuona wanayapeleka wapi?

2. Kuhusu vituo holela vinavyojengrwa sehemu mbalimbali, hasa Mkoa wa Pwani eneo la Kibaha inatisha. Hizi ndizo sehemu za kufanyia chakachua, serikali itupie jicho kwa nguvu zote.

3. Sheria, kuhusu adhabu ya uchanganyaji mafuta (chakachua) mara gari linapokamatwa anaehukumiwa ni mwenye gari pekee na wala sio *driver.* Hivyo ushauri wangu adhabu kali apewe dereva maana kwa namna moja au nyingine dereva anajua, kinachoendelea. Ushauri mwingine *EWURA* waweke mashine za kutambua sehemu ya depo lakini pia wapewe wenye vituo vya kuuza mafuta ili mafuta yakiwa machafu wasiyapokee.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa ushirikiano hadi kufikia kuwasilishwa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze serikali kwa kuongeza fedha katika maeneo ya vipaumbele ambayo yameainishwa katika Bajeti hii hasa tukiangalia kwamba kipindi hiki ni kigumu mbele yetu, kuhusiana na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa serikali uliolikabili Taifa letu. Sote tunafahamu kuwa uchaguzi ni gharama kubwa na unahitaji fedha mpaka kukamilika kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba serikali imekusudia kuwaendeleza wananchi kiuchumi kwa mantiki ya kumwendeleza mkulima yule wa kipato cha chini. Ndiyo maana ikawekwa sera ya kilimo kwanza. Lakini pamoja na mambo mengine suala la benki ya wakulima lipewe nguvu ya juu sana kwani bila mikopo mkulima hawezi kuendelea ipasavyo na kufikia hatua ya kilimo kwanza kama tulivyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi suala la mikopo kwa wakulima limekuwa likisua sua na hatimae muendelezo wa mapato yanayotokana na kilimo kuwa madogo tofauti na tulivyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo iwalenge wakulima wakubwa na wadogo bila kujali jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo kwra njia ya ruzuku uendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya utafiti zitumike kama zilizyopangwa

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji uwepo wa kutosha na kadhalika. Wataalamu wa kilimo wawajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza serikali kwa kuangalia umuhimu wa suala la kuwepo utafiti nchini na kuweza kutenga fedha kwa ajili hiyo, kwani bila tafiti hatuwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza serikali kwa kuliona suala utumiaji mbaya wa fedha za serikali au mlundikano bila matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linawakosesha wananchi huduma bora katika miradi ya maendeleo katika muda mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali iendelee kufanya udhibiti zaidi wa fedha za serikali zinazotengwa ziwe zimetumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fedha zilizotengwa katika sekta ya elimu, naomba serikali kuongeza ajira za walimu zaidi nchini ili wanafunzi waweze kusoma vizuri na kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za walimu ziongezwe ili wanaopangwa katika mashule ya vijijini wasilete vikwazo vya kukosa makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa maabara uendelezwe kwa kutiliwa mkazo katika shule za sekondari nchini. Naipongeza serikali kwa kuweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005/2010, katika nyanja mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba serikali endelee na utekelezaji wake huo kwa ufanisi zaidi ili wananchi waweze kuendelea kuwa na imani kubwa kwa serikali yao ambao ipo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la miundombinu ya barabara. Tutakumbuka kuwa sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam kunakuwepo na msongamano mkubwa wa magari hasa ufikapo wakati wa mvua kutokana na miundombinu ya barabara iliyopo mjini hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yaliyotuama, matope, uchafu wa takataka unachangia katika baadhi ya vichochoro zilizopo mjini hapo. Naiomba serikali kuhimiza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuweza kutimiza wajibu wake katika hatua ya matengenezo ya barabara za chochoroni na mifereji ya maji taka ili kuondoa kero zinazokuwepo mjini hapo. Pia serikali nayo kutenga fedha maalum kwa ajili ya matengenezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi.

- Serikali iendelee kutoa elimu kwa wajasiriamali wakubwa na wadogo.

- Waliopata mikopo waendelee kuhimizwa urejeshaji wa fedha hizo ili waweze kukopeshwa wenzao wasiobahatika katika kipindi kilichopita.

- Seikali iweke usimamizi maalum, kwa maana ya kuondoa ubinafsi unaoweza kutokea katika hatua za upatikanaji wa fedha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wafanayakazi wote wa wizara yake kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni. Hotuba hii ni nzuri kwani imeangalia mishahara ya wafanyakazi, imeondoa au kupunguza kodi kwa vifaa na mashine zinazotumika kwa sekta ya mifugo hasa viwanda vya maziwa na kilimo. Hii itawasaidia wafugaji na wakulima kujipatia kipato na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya sasa napenda kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja (100%).

Mheshimiwa Spika, ni lazima ikumbukwe kuwa fedha za serikali zinapatikana kutokana na kukusanya kodi. Hivyo ni muhimu kuwa kuna haja ya kupanua wigo wa kukusanya kodi. Kuna watu wengi wanakipato kizuri hasa wafanyabiashara wadogo ambao hawalipi kodi. Tunaomba mikakati iandaliwe kuhakikisha kuwa watu wote wenyekipato wanalipa kodi. Hii itafanikiwa kama tutaharakisha utaratibu wa kutoa vitambulisho vya kitaifa, ili kila raia aweze kujaza *Tax Return form* ambapo kila mtu ataijaza na kuonyesha kiasi cha kipato anachiopata na hii itakuwa rahisi TRA kumdai kodi anayostahili kupata. Bila *National Identification card TRA* itakuwa na kazi ngumu kuhakikisha kuwa kila mtu analipa kodi.

Mheshimiwa Spika, serikali lazima ibane mianya ya matumizi mabaya ya fedha za serikali. Hivyo posho zisizo za lazima lazima ziondolewe, pesa kama za hospitali

katika maofisi sio za lazima kabisa zinaweza kuondolewa au kupunguzwa kwa kiasi kikubwa. Vile vile posho za wafanyakazi wanazolipwa baada ya kufanya kikao mahali pa kazi, lazima zifutwe kwani hivis vikao vinahusu kazi zao za kila siku, sasa kwa nini mfanyakazi alipwe posho na mshahara kwa kufanya kazi moja.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya magari ya serikali lazima yathibitiwe. Magari ya kifahari yapunguzwe na utumiaji wa mafuta uonyeshwe katika log books ili kuhakiki kuwa madereva hawali njama na wenye vituo vya mafuta kuibia serikali.

Mheshimiwa Spika, wale wote wanaoiba fedha za serikali lazima wachukuliwe hatua za kisheria, ili kuhakikisha kuwa fedha za serikali zinatumika vizuri na sio kunufaisha mafisadi.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake kwa kuandaa Bajeti yenye kuleta matumaini mema kwa wananchi hivyo basi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Marisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge hili Tukufu la Tanzania. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kutoa ushauri kwa serikali kuhusu uchomaji mkaa ambao umekithiri hapa nchini, na ambao hautamaliza ili utapungua. Asilimia kubwa ya wananchi wetu hapa nchini wanatumia mkaa hasa mjini. Na kuacha nchi inabakia kuwa jangwa pamoja na elimu inayotolewa kila siku.

Mheshimiwa Spika, wakati serikali inapofikiria maisha bora kwa kila Mtanzania na inawezekana kabisa ni pamoja na makaazi. Hili tatizo la utumiaji wa makaa liishe kabisa, ningeshauri Shirika la Nyumba linapojenga nyumba nchi nzima kwa ajili ya kupangisha wananchi/wafanyakazi wake, wajenge mabomba ya kupitishia gesi kama wanavyojenga nyaya za umeme.

Mheshimiwa Spika, itakuwa rahisi kutumia majiko ya gesi kwani tayari wananchi wamekwisha anza kutumia majiko hayo. Pia ulipaji wake ni rahisi kwani utakuwa unanunuua gesi kama unavyo nunua umeme wa luku ili tuiokoe nchi yetu inayonyemelewa na ukame pia nchi kubakia jangwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. DR. CHARLES OGESA MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wakuu wa wizara na taasisi chini ya Wizara kwa kazi nzuri. Pongezi kwa Bajeti yenye vipaumbele sahihi yaani elimu, miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna suala la maendeleo ya viwanda ambayo tunahitaji sana kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi. Maendeleo ya viwanda pamoja na mambo mengine, yanategemea upatikanaji wa mitaji mikubwa kutoka katika mabenki, hususan Benki za Maendeleo zinazotoa mikopo mikubwa, ya muda mrefu na masharti nafuu. Kwetu sisi Benki ya Rasilimali *(TIB)* ndiyo stahili katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, lakini ninavyofahamu *TIB* bado ina sheria na muundo wa Benki ya Biashara pamoja na kuwa na mtaji mdogo. Mheshimiwa Spika, swali langu:-

1. Lini sheria ya *TIB* itabadilishwa au muundo wake kubadilishwa ili iwe kweli Benki ya |Maendeleo na yenye fursa zaidi za mikopo kama vile *Equity Financing* na kadhalika?

2. Lini *TIB* itaongezewa mtaji ili kuipa uwezo zaidi wa kutoa mikopo ya miradi mikubwa ya maendeleo. Au, lini TIB itapewa mwanya wa kukopa kwinginepo ili kukuza mtaji wake. *TIB* ingeweza kukopa *PTA, EADB, ABSA* na kadhalika. Kama marekebisho ya sheria yake yangefanywa ili kuipa uwezo huo, lakini sasa haiwezi.

Mheshimiwa Spika, bila ya kuifanya *TIB* kuwa Benki ya Maendeleo katika ukamilifu stahili, itakuwa ni vigumu sana kupatas nyenzo stahili (mikopo) ya kuchochea maendeleo ya viwanda nchini. Hivyo uamuzi wa kuiwezesha *TIB* unatakiwa ufanyike sasa. Hili ni ombi langu mahususi.

Mheshimiwa Spika, narudia kupongeza kwa kazi nzuri ya wizara.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Mzee kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yote hayo yasingewezekana bila uongozi mahiri wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na ushirikiano na wadau wetu, likiwemo Bunge chini ya Mheshimniwa Spika wetu Samuel Sitta, wa kasi na viwango na Naibu Spika Mheshimiwa Anna Makinda (MB).

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefurahishwa kutenga pesa za kutosha kwa ajili ya uchaguzi ili kuwezesha uchaguzi huru na wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuona kuwa tumeweka vipaumbele katika mambo makuu ya miundombinu, kilimo, elimu, umeme, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli ni vema ufuatiliaji uwe wa karibu ili kuona kuwa angalau mambo hayo ya reli ya kati, na barabara kuwa yanakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme wa gridi Makambako – Songea, hiyo 20% ya mkopo mmeshakubalina? Tatizo ni nini tena? Mimi nafikiri hiyo ni fursa nzuri kwetu, kwani inasemekana *SIDA* wapo tayari kutoa asilimia (80%)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa makumbusho ya majimaji kuwa makumbusho ya Taifa na imekuwa kichocheo kikubwa cha uchumi mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru umeme wa Mbinga. Tunashukuru mbolea ya ruzuku, imesaidia kuimarisha chakula Ruvuma na kwa majirani zetu, nchini na hata baadaye kuuza nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ya Mkoa wa Ruvuma imeborekea (Songea). Hongera kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, na Shule za Kata, vijiwe vya bangi vimeishiwa wateja, wote wapo shuleni. Chama cha Mapinduzi kidumu, kimetekeleza wajibu wake, tena kwa mazingira magumu ya ukame, na mtikisiko wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa misaada ya wafadhili ni kutufundisha kusimama wenyewe kiuchumi.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Bajeti ni nzuri mno. Napenda kushauri maeneo yote ya kukusanyia kodi yawe ya ki-eletroni ili kupunguza kupokea fedha taslimu ambpo hicho ni kichocheo cha kuiba au kufanya ubadhirifu katika makusanyo. Aidha, ninashauri adhabu zinazolipiwa fedha zilipwe kwa hundi. Kwa kufanya hivyo kutawezesha makusanyo kuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ninaomba dawa za mboga na virutubisho nazo zipunguzwe bei ili kutoa nafasi kwa wakulima wadogo kujiendeleza na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ni nzuri sana naunga mkono. Nampongeza Waziri wa Fedha kwa kukataza serikali kununua samani kutoka nje ya nchi kwa matumizi yake. Utaratibu huu utongeza ajira na kuimarisha viwanda vya (fenicha) samani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waziri aseme kabisa hapa bungeni ya kuwa samani toka nje kwa ajili ya serikali ni marufuku. Pia naomba waziri aseme pia ya kuwa watakaogiza mabasi kwa ajili ya kutumia wanafunzi tu watasamehewa ushuru ikiwa ni

pamoja na ule mradi wa *CRDB* wa mabasi ya wanafunzi kama alivyokwisha kusema Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii kwa maandishi. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo wake kwetu sote na pia naendelea kuomba neema zake kwa kipindi cha uchaguzi mkuu atubariki sote ili nchi yetu iendelee kuwa ya amani. Nichukue nafasi hii kuishukuru na kuipongeza serikali kwa kukamilisha ujenzi wa daraja la umoja ambalo litakuwa ufunguo kwa uchumi wa mikoa ya Kusini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake kwa kuandaa bajeti Ya serikali katika mazingira magumu yanayolikabili Taifa letu pia kwa kuwa wazi katika kuelezea hali halisi ya uchumi wa Taifa kwa mwaka, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha *"Poverty and Human Development Report"* inaonekana kwamba bado juhudi za ziada zinahitajika katika utekelezaji wa mkukuta. Vile vile katika kitabu cha hotuba ya hali ya uchumi wa Taifa 2009, imeelezwa katika ukuruasa wa 35 kwamba tathimini ya mshauri elekezi ilibainisha kuwa dhana ya dira ya Taifa ya maendeleo 2025 inatekelezeka na kutaongezwa msukumo katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia suala la elimu changamoto ya utoaji wa elimu bora sina wasiwasi sana kwani inatia moyo kuona idadi kubwa ya walimu wanapatiwa mafunzo vyuoni na pia mkakati wa kutenga maabara utasaidia.

Tatizo langu ni kuhusu tatizo la watoto waliotoka katika familia maskini kushindwa kwenda shule/kupata elimu ya ngazi mbali mbali.

Pia watoto wenye ulemavu ni asilimia 40% tu wanaokwenda shule za msingi. Ina mkakati gani kwa makundi haya kwani kitabu cha mpango wa maendeleo wa mwaka 2010/2011 hakisemi lolote juu ya kuwawezesha watoto hawa kupata walao elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine katika elimu ni kuhusu mgogoro wa ardhi baina ya *Tanzania Building Agency (TBA)* na halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ambao umesababisha ujenzi wa shule kusimama kwa kipindi cha zaidi ya miezi tisa.

Vile vile kuna pesa za kujenga maabara kwa hiyo shule ya sekondari ya reli shilingi milioni 40 hazijatumika kwa kazi hiyo kwa miezi sita sasa, bado zipo benki kutokana na huo mgogoro. *TBA* inataka kujenga nyumba za kuuza na Manispaa inajenga "*High School* katika eneo hilo".

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBA* kwa upande mwingine imekataa kupewa eneo jingine kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Ningependa kupata ufafanuzi ni kwa nini ugomvi baina ya Mamlaka za Serikali ambao unapelekea kukwamisha maendeleo kupitia kipaumbele cha elimu. Kutokana na hili ninashawishika kupiga kura ya hapana kama sitapata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya naipongeza serikali kwa jitihada za kupunguza vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano pia maambukizi ya UKIMWI ambazo zimeonesha mafanikio. Pamoja na hayo vifo vya uzazi bado havijapungua lakini mpango wa maendeleo 2010/2011 haujaonesha mkakati mahsusi kuhusiana na kukabiliana na tatizo la vifo vya uzazi.

Nikizungumzia Mkoa wa Mtwara, kwa sasa hospitali ya Mkoa ya Ligula imepata wodi mpya ya wazazi lakini tunahitaji mashine ya *ULTRA SOUND* kwani ile iliyopo haitoshelezi kwa sababu ipo mbali na wadi na inahudumia wagonjwa wa aina zote, hivyo kuna msongamano. Vile vile wauguzi ni wachache ambapo wanashindwa kumudu kuwapeleka wajawazito kwenye vipimo wakati huo huo kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wizara ipeleke *ULTRA – SOUND* katika wodi ya wazazi ili kunusuru maisha ya wazazi. *Report* 2009 inaeleza kwamba kaya masikini zinatumia sehemu kubwa ya kipato katika kupata maji ikilinganishwa na kaya zenye uwezo mkubwa wa kifedha.

Naishauri serikali iliangalie eneo hili kwa umakini zaidi ili kulinda kipato cha wananchi wenye kipato cha chini kiwasaidie katika matumizi mengine badala ya kuishia kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. DEVOTA MKUWA LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono Bajeti.

Nashauri serikali itoe mwamko hamasa na ushawishi zaidi katika msukumo wa Ushiriki wa wananchi katika kutekeleza na kuongeza kasi katika kukuza uchumi ili kujiletea maendeleo. Kila mwananchi akishiriki katika kuzalisha, nchi yetu itaendelea kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Waziri,Manaibu Waziri, wataalam wa Bajeti hii yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Spika Ahsante sana.

**MHE. ANDREW JOHN CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, pamoja na Naibu Mawaziri wa Wizara yake na wataalam kwa kuandaa hotuba ya Bajeti nzuri inayotoa matumaini kwa wananchi, napenda kuanza kwa kusema ninaiunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii imejibu hoja nyingi ambazo zimekuwa zikitolewa na wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge hasa katika maeneo ya kilimo na uendelezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yaliyojikita katika Bajeti ya Serikali ya mwaka ujao wa fedha yapo maeneo ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa makini. Eneo la kwanza ni lile la ongezeko kunwa na la kila mwaka la matumizi ya kawaidia na ongezeko la matumizi ya maendeleo. Si busara hata kidogo kuendelea na hali hii, nashauri tuangalie uwezekano wa kuweka kiwango cha juu *(Cap)* cha matumizi kwa kuweka vipaumbele vyenye tija na ufanisi. Matumizi ya ziada *Over the capped amount*, yatokana tu na ongezeko ya mapato ya ndani.

Pili, mapato ya ndani yanatokana na kodi na yasiyotokana na kodi *as a percentage of GAP* bado yako chini mno kuwezesha uchumi wetu kukua kwa uendelevu. Jitihada mathubuti lazima zifanyike ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato yatakayotozwa kodi.

Tutafanikiwa iwapo serikali itatoa kipaumbele katika kukuza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo mifugo na uvuvi ili kuongeza mchango wa sekta hii kwenye pato la taifa. Aidha ni vema serikali iboreshe zaidi mazingira ya kufanya biashara nchini, ugumu wa kufanya biashara hapa nchini kunazorotesha uwekezaji na moja kwa moja kutoka nje *(FDI).*

Tatu, Serikali ifanye uamuzi wa haraka na wa makusudi ili kuboresha miundombinu hasa ya reli na bandari serikali iangalie uwezekano wa kupata misaada na mikopo kwa masharti nafuu kwa madhumuni hayo hasa kutoka nchi za China na India. Tukiendelea kutegemea *traditional services of funding* hatutafika. Lazima tujifunze kwa haraka namna ya ku-*access credits* kutoka China na India.

Nne, Serikali ilinde na kuendeleza mafanikio, yaliyopatikana kutokana na mageuzi ya kiuchumi. Serikali isiwe na kigeugeu katika kusimamia na kuendeleza *reforms,* nachelea kusema kwamba mara nyingi sisi Watanzania tunatumika bila

kujielewa kuacha kutekeleza mambo ya msingi tuliyoyaanzisha ili hao wanatukwaza wao wayatekeleze.

Ipo mifano mingi ambapo serikali imeyumba kwa kufuta vivutio vilivyotolewa kwa wawekezji na baadaye kurejesha vivutio hivyo. Ili tuweze kuvutia wawekezaji wa nje na wa ndani sera zetu lazima ziwe za uhakika na zitaribike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naishauri Serikali iwe sikivu kwa ushauri wa mapendekezo yanayotolewa mara kwa mara na sekta binafsi yenye lengo la kukuza uchumi wan chi yetu. Mapendekezo ya sekta hiyo ya namna ya kupunguza na kama siyo kufuta uvujaji wa mapato ya Serikali kwenye sekta ndogio ya bidhaa za mafuta ya *petrol* yafanyiwe kazi kwa haraka ili kunusuru mapatao halali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kama nilivyoanza kwa kuishukuru serikali kwa kuwasilisha Bajeti nzuri na yenye mtumaini na nitamke kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Bajeti ya 2010/2011 lakini yapo mambo machache ambayo naiomba serikali iyatazame.

Suala la kwanza ni uchanganyaji wa mafuta ya magari unaofanya na wauzaji wa mafuta. Tatizo hili limefikia kuvuka mipaka yetu kutokana na mafuta yanayopelekwa nchi za jirani kuchafuliwa kwa kutiwa mafuta ya taa. Uchafuzi huu wa mafuta unaharibu jina la nchi yetu na biashara ya mafuta. Aidha magari yana yotumia mafuta hayo yanaathiri vibaya sana.

Upunguzaji wa kodi kwenye mafuta ya taa ndiko kunako hamasisha wafanyabiashara ya mafuta kuchanganya na mafuta ya taa, kama bei ya mafuta ya taa ingekaribia bei ya diesel, hakungekuwepo kianzishi cha "kuchakua".

Lengo la kuweka bei ndogo ya mafuta ya taa lilikuwa kuwapa wananchi nishati kwa bei nafuu. Ukweli ni kwamba wananchi wanaofaidika na utaratibu huu ni wachache sana. Wanaofaidika na utaratibu huo ni wafanyabiashara wa mafuta kwa madhara makubwa sana kwa uchumi wa nchi.

Kuondoa athari hizi, Serikali ipandishe bei ya mafuta ya taa ilingane na ile ya *diesel* na tatizo hili litamalizika. Serikali itafute njia tofauti ya kuwasaidia wananchi kupata nishatai ya bei nafuu ikizingatia kwamba wananchi wengi wanatumia kuni namkaa na sio mafuta ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Viwanda vya kilimo ni kwamba tufufue viwanda vyetu vya zana za killimo. Wapo Wachina wanataka kuanzisha viwanda vya mashine za kilimo hapa nchini wasaidiwe ili azma yao ifanikiwe.

· Kwa kutumia gesi ya Mkuranga Songo Songo na Mtwara na phosphate za Minyingu Mbeya na Mpanda, tuanzishe viwanda vya mbolea kwa matumizi ya nchi yetu na kuuza nje ya nchi.

· Tufufue viwanda vinavyosindika mazao ya kilimo na kuanzisha viwanda vipya vya kusindika mazao ambayo hayana viwanda hivi sasa.

· Tutilie mkazo kilimo cha mazao mapya ya kuuzwa nje ya kwa matumizi yetu.

· Muhimu zaidi, tuongeze sana vitendo, tupunguze maneno. Tunajua matatizo yetu na ufumbuzi wake. Tatizo kubwa hatukuchui hatua hizo tunazozijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyemwezesha Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuiongoza vyema nchi yetu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi chote cha miaka yote mitano vizuri, nami pamoja na wapiga kura wangu wa jimbo la Kwimba tunamtakia yeye pamoja na Serikali atakayoiunda kipindi kingine cha miaka mitano akiwa na afya njema na kwa utulivu wote ili nchi yetu ipate fursa nyingine ya maendeleo.

Aidha napenda nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa yote iliyotuchangia katika maendeleo ya sekta mbalimbali. Mfano dhahiri ni katika maendeleo ya elimu, miundombinu,afya, maji, kilimo na kadhalika. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake nzima kwa hotuba waliyotufikishia Bungeni. Pamoja na mazingira magumu yanayoizunguka mipango na Bajeti nzima ni vizuri. Naipongeza Wizarai na Serikali kwa jumla naipongeza kwa kuendeleza kuiona elimu kama kipaumbele chetu na kukiongeza fedha. Vipaumbele hiki ikiwa na vilivyotajwa jama miundombinu, kilimo, afya, maji na nishati ni vizuri sana na nashauri elimu iendelee kupewa fedha za kutosha hatimaye elimu bora itoe wataalamu wazalendo wenye uzalendo na uwezo, weledi wa kutosha kuendeleza sekta zote za msingi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Ushauri wangu ni kuwa ni vyema Serikali pamoja na kuviainisha vipaumbele nilivyovitaja hapo juu ni vyema ikiongozwa na weledi wa kizalendo ikabainisha vyema vipaumbele ndani ya vipaumbele hivyo. Si vyema sekta ikaanishwa kama kipaumbele na ikatengewa fedha nyingi na fedha hiyo ikaishia katika shughuli ambazo si za manufaa kwa wengi. Si vyema Wizara ikapewa fedha na fedha hiyo sehemu yake kubwa ikatumika kwa ustawi wa wachache hapo Wizarani tu. Ni mara ngapi viongozi mbalimballi wa Wizara moja wanasafari kwenda nje ya nchi wakichukuana wao kwa wao bila kuchukua watu kutoka mikoani? Ni viongozi wangapi Wizarani wanakwenda nje ya nchi kwa safari za *shopping* na kurudi na vitu idadi lukuki kwa manufaa yao na kuziacha Wizara na watumishi wengine katika hali duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara kuwa kuliona hili japo si moja kwa moja na kutamka kuwa kutakuwa na udhibiti mkubwa wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo kwanza mimi ninaamini kuwa kama bado kunahitajika semina ni chache sana, lakini ninaamini kitakachotokea mara baada ya fedha kuanza kutolewa semina zitaanza makongamano yataendeshwa kama kwamba maafisa ugani hawako kabisa au hawajui lolote. Ushauri wangu ni kuwa maafisa ugani waajiriwe kwa mikataba na wapimwe kwa maendeleo ya majukumu yao katika maeneo wanayosimamia. Naamini kuwa maafisa ugani tulionao wakiamua kufanya kazi kwa ubunifu wao wote, nguvu na kwa moyo, vyote hivi havipatikani kwa semina na makongamano, tubadilike kwa kuwabadilishia mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mazingira mazuri ya kuendelea lakini hatuna budi kubadilika na ni kwa namna moja tu kwa kuamua tufanye kazi tena kwa upendo kwa nchi yetu na kujituma. Tukiamua nina amini na Mwenyezi Mungu atatuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iijenge upya reli ya kati, magari makubwa yanayosafirisha mizigo kutoka bandarini kwenda nchi jirani za Kongo *(DRC)*, Rwanda, Burundi na Uganda yanachangia sana kuharibu barabara zetu zinazojengwa na hivyo kuzifanya zijengwe kila mara shughuli ya kusafirisha mizigo ingefanywa kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Miundombinu ni kubwa sana imeelemewa na kazi nyingi, napendekeza iundwe Wizara ya Reli na Bandari kutokana na Wizara hii ili kuleta ufanisi zaidi katika kujenga reli na bandari zetu na pia Wizara ijue itakavyoshughulikia ujenzi wa barabara sekta zingine.

Kuhusu kilimo, nasisitiza kuwa ukombozi pekee utatokana na kilimo cha wanyamakazi na *plau* wengi wa watu wetu ni maskini bado hawana uwezo wa kumiliki na kuendesha matrekta makubwa na madogo, shida ni uwezo wao mdogo wa kununua au kupata vipuli, nyenzo hizi ni nzuri lakini tatizo ni uwezo wa kuyaendesha maksai na *plau* havina gharama za kuyaendesha havihitaji mafuta (dizeli).

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa mkoa wa Rukwa wanazalisha mazao kwa wingi kwa kutumia wanyamakazi. Nashauri vituo vya kusambaza nyenzo za kilimo vitumike pia kusambaza *plau* kwa wingi wa wananchi wapatiwe wanyamakazi ambao ni gharama nafuu kuliko matrekta. Matrekta yaachwe kwa matajiri au wenye uwezo wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 30 zilizotengwa kwa utafiti kazi itasaidia sana kuleta tija, tafiti nyingi sana zimefanyika nchi hii tokea Uhuru na makabrasha, majarida mengi yameandikwa yako makabatini bila kufanyiwa kazi. Tafiti mbalimbali zinafanyika.

Napendekeza fedha hizi zitengwe kujenga barabara ya Manyoni – Itigi - Chaya - Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti labda uangaliwe jinsi ya kutumia madini ya *uranium* ambayo yamepatikana kwa wingi ukanda wa kati mpaka eneo la Jimbo la Manyoni.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii ya kwanza kumpongeza Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya Bajeti katika kipindi hiki kigumu kinachokumbana na mtikisiko wa hali ngumu ya uchumi duniani, pamoja na hilo naona maandalizi yamekuwa mazuri na ya kutiliwa mfano, naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni budi zikapata majibu ya uhakika ili kila aliyesikia apate ukweli wa hali halisi kuliko kupotoshwa maana mengi yaliyosemwa yasipopata majibu yatatumika wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu. Tunajiandaa kwa kutoa maelezo ya wananchi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya maeneo ambayo lazima yapewe malengo ya kutosha ni madai ya makandarasi wa barabara kudai shilingi bilioni 305 kiasi ambacho kinawafanya baadhi waache hata kuendelea na kazi. Pia suala la ahadi za Mheshimiwa Rais zote zipitiwe na kuagiza wakuu wa mikoa watoe ukweli wa ahadi hizo na tuone namna ya kuzitekeleza angalau kwa kutoa fedha za kuonyesha nia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amefanya mengi sana katika kujenga demokrasia katika nyanja zote na kulifanya Taifa letu liwe la amani na utulivu. Lakini nashauri mambo yafuatayo yazingatiwe:-

1. Kasi ya ongezeko la watu ni kubwa sana haiwezi kutuwezesha kupunguza umaskini. Ni bora sasa tuwekeze katika suala la afya ya uzazi na ya mtoto. Elimu ipewe umuhimu wa kwanza, Bajeti lazima ilione hili.

2. Hali chakula mwaka huu wa uchaguzi lipewe kipaumbele kwa sasa kuwa zaidi ya tani 20,000 Sumbawanga kwenye ghala la Taifa hali ambayo inafanya mazao ya msimu huu kutonunuliwa, kwa nini Serikali isinunue na kuyasambaza sehemu ambazo zina upungufu ili msimu wa mvua ukianza kila sehemu iwe na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri atumie nafasi hii kuiomba Serikali ya China itoe fedha nyingi kwa ajili ya kilimo na hasa ukizingatia kuwa mwaka juzi tulichelewa kupeleka maombi kupata fedha zao toka "*Concession Loan*" yao, na kufanya wenzetu wa Uganda na Kenya kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nadhani Serikali inaweza kuona namna ya kupunguza *OC's* za Wizara kwa asilimia mbili tu na tukazipeleka kwenye kulipa madeni, mbalimbali ili tujenge heshima kwa wadai wetu kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Wizara iliomba itoe hesabu ya kiasi kinachotengwa kwa ajili ya Tume ya Sayansi ili mfuko huo utumike kuendeleza taaluma ya Sayansi na Teknolojia. Nashauri Mheshimiwa Waziri atoe maelezo bayana kwa kushirikisha taasisi na maeneo yote yanayopewa fedha za utafiti. Hili ni muhimu maana naona fedha hizo ambazo zimetawanywa zinaweza zikaonekana kama kuwa hakuna lolote linalotengwa kwa shughuli kama hizo wakati fedha zimetengwa ila kwa kusambazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti pamoja na kuwa na uzuri lakini bila kuwa na watendaji waaaminifu na watendaji wenye nia na ari kubwa ya kusimamia maagizo ya Serikali kama yalivyowekwa ndani ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kheri na mafanikio mengi ya uchaguzi ujao. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu MaWaziri wote wawili, pia niwapongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi na kukamilisha Bajeti ya mwaka huu 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali chini ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kudhibiti na kuongeza makusanyo ya kodi mwaka hadi mwaka ongezeko la Bajeti linasaidia katika utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Serikali kuzingatia mambo muhimu ambayo ni ya Kitaifa kwa mwaka huu wa fedha, kwanza, kukamilisha kazi ya vitambulisho vya Taifa, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na nyongeza ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya ni nyeti na yamechukua sehemu kubwa ya Bajeti ya Taifa, lakini pamoja na mambo hayo muhimu bado Bajeti imezingatia fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo kwanza miundombinu ya umwagiliaaji ipewe kipaumbele katika Mikoa ya Kati (Jimbo la Iramba Magharibi), kuweka mabwawa ili kutunza maji kwa ajili ya umwagiliaji wa mazao mara mvua za masika zinapokwisha.

Nyongeza ya maafisa ugani ili kutoa elimu kwa kilimo cha kisasa, zana bora za kilimo, bado mfuko wa pembejeo unachelewesha kutoa mikopo kwa wakulima wenye sifa kwa ajili ya matrekta mfano wakulima wa Jimbo la Iramba Magharibi, Nicodemus Napegwe (milimoduu) (Kijiji cha Misigiri), John Tutu (Kijiji cha Ulemo) na George wa Manipanta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu waidhinishiwe kupatiwa mikopo ya trekta mwaka 2008 hadi sasa hawajapatiwa mkopo huo pamoja na kukamilisha sifa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Fedha itoe elimu ya kutosha ili kuzijengea uwezo wa makusanyo ya ndani Halmashauri za Wilaya kwani kuna mapato mengi lakini yamepotea bure. Makusanyo haya yataongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini na nishati, bado sekta hii inachangia kiwango kidogo Pato la Taifa mikakati na mbinu zitazamwe upya ili kuona namna sekta hii itakavyonufaisha Taifa kimapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hazina kupeleke fedha sehemu mbalimbali katika utekelezaji wa sekta za maendeleo, bado kuna udhaifu mkubwa kuhakikisha fedha zinapelekwa kwa wakati sehemu mbalimbali, naomba Hazina ijitahidi kuwasilisha fedha kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze kwa kuiopongeza *TRA* kwa jitihada zake za kukusanya mapato. Kupanda kwa kiwango cha makusanyo ya kila mwezi ni ushahidi wa kazi na jinsi inavyofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Serikali iendelee kuisaidia *TRA* ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kwa maamuzi ya kutoa ruzuku kwa wakulima wa mazao ya mahindi na mpunga katika mikoa sita iliyoteuliwa kwa uzalishaji wa chakula. Uamuzi huu wa Serikali umesaidia sana kuongeza uzalishaji wa chakula, hata hivyo, bado usimamizi wa karibu unatakiwa ili kubaini mawakala wachache wa pembejeo ambao si waadilifu na ambao wanasababisha fedha za Serikali kupotea na kurudisha nyuma jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wakulima ni jambo lililo dhahiri kwamba maendeleo ya wananchi zaidi ya asilimia 80 yanategemea kilimo. Mara nyingi tunazungumzia wawekezaji wakubwa katika kilimo kikubwa cha biashara. Maeneo mengi ya uwekezaji katika nchi yetu yameshikwa na wageni. Madini, utaliii na viwanda ni mfano mizuri, nashauri Serikali iwe na dhamira katika eneo la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watanzania kumiliki uchumi katika eneo la kilimo. Naushauri mchakato wa kuanziasha Benki ya Wakulima uendee kwa kasi na Serikali ionyeshe dhamira ya kutoa kipaumbele kwa watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara zote Bajeti inaposomwa, asilimia kubwa ya Watanzania wanajua kuwa kodi ya bia na sigara ni lazima zitapanda. Naishauri Mamlaka ya Mapato kutazama maeneo mengine ya kuweza kupata mapato badala ya kutegemea sigara na bia tu. Wapo baadhi ya watu ambao bia ni sehemu ya chakula. Si busara kuendelea kutegemea bia na sigara tu katika kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimniwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza mapato, hivi sasa mapato yetu ya ndani ni kama shilingi trilioni sita tu, lakini matumizi ni zaidi ya shilingi trilioni 11. Tatizo ni kwamba wigo wa walipa kodi ni finyu hivyo ni lazima tupanue wigo wa walipa kodi ili tuongeze mapato. Njia moja ya kuongeza idadi ya walipa kodi ni kutizama shughuli za sekta isiyorasmi *(informal sector)* tu hii ni sekta kubwa sana na ina fedha nyingi sana ambazo hazitozwi kodi. Serikali ipige tochi sekta hii ili baadhi ya shughuli zitozwe kodi kwa mfano wanaopangisha nyumba zenye kodi kuanzia shilingi 100,000/= kwa mwezi (kima cha chini cha mshahara), wanaofuga ng’ombe kibiashara, kuku, nguruwe na kupata mapato zaidi ya shilingi 100,000/= kwa mwezi. Pia kuna viwanda vidogo *(cottege industrial)* ambavyo ni vingi lakini havilipi kodi, kwa kifupi Wizara ifanye *study* ikishirikiana na MKURABITA kuona shughuli za sekta isyo rasmi zinazoweza kutozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya kuongeza mapato ya Serikali ni kupitia kodi ya ardhi *(land rent),* ili kutoza kodi ya ardhi ni lazima ardhi yetu yote ipimwe *(to be surveyed),* iwekewe mpango wa matumizi *(land use plan)* na imilikishwe *(titling).* Hivi sasa kati ya ukubwa wa eneo letu lote la ardhi (888,000 sq.km), eneo lililopimwa na kumilikishwa ni 2% tu, na tunakusanya kodi ya ardhi ya shilingi bilioni 17 tu. Je, kama tungepima walau 50% ya ardhi mapato si yangekuwa makubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi unahitaji fedha lakini bahati mbaya sana Bajeti zetu katika sekta ya ardhi ni ndogo sana na hivyo upimaji ardhi ni mdogo, kwa kifupi tuiondoe ardhi kutoka kuwa mtaji mfu na tuifanye mtaji hai utakaowaingizia Watanzania mapato makubwa wao binafsi (kupitia hatimiliki zao kutumika kama dhamana ya mikopo) na Serikali yao kupitia kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi Serikali iwe makini kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima hasa udhibiti wa ununuzi wa magari ya bei kubwa, mategenezo ya magari na safari za nje zisizo za lazima. Ahsante.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake, pia niwapongeze Manaibu Waziri wawili, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa mchango wangu kwenye suala zima la kilimo kama tunavyojua kwamba nchi yetu ina ardhi nzuri ya kutosha na inazalisha

matunda kwa wingi. Lakini matunda yanakuwa mengi mpaka yanafikia kuozeana na kutupwa. Ushauri wangu naiomba Serikali ijenge viwanda kwa wingi vya kutengeneza *juice* na *jam* kwa matumizi ya ndani ya nchi na nje ya nchi ili kuongeza mapato ya nchi yetu na pia kuepuka kuletwa *juice* za maboksi kutoka nchi za nje. Pia vijana wanaozurura ovyo mitaani waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uvuvi halikupewa kipaumbele, kama tunavyojua Tanzania ina bahari ya kutosha ambayo Mwenyezi Mungu kajaalia ina samaki wengi sana hata inafikia wavuvi wa nchi za mbali wanakuja kuvua kwenye bahari ya Tanzania. Naiomba Serikali iwasaidie wavuvi wadogo wadogo kuwapa nguvu za kutosha kwa kuwawezesha kuwapa nyenzo ili ziwasasidie katika shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe mkazo katika kuendeleza bandari zetu ili ziweze kutekeleza kazi zake vizuri, kama bandari ya Mtwara ambayo ni ya asili ni vyema ikaendelezwa kwa ajili ya kuchochea uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa niaba ya Serikali kwa Bajeti ambayo kwa kiwango kikubwa imeelekea kuwalenga wakulima na wafugaji ambao ni asilimia kubwa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nauelekeza kwenye eneo la kuwawezesha kiuchumi wananchi. Sasa hivi kuna mifuko mingi sana inayolenga kuwawezesha wajasiriamali wadogo wakati mifuko hiyo ni midogo midogo tu *(under funded)* hivyo *impact* yake haijitokezi wazi wazi. Napendekeza Serikali iunde mifuko mikubwa kama miwili hivi ambayo iko *well funded.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, mfuko mkubwa wa *Micro-finance.* Mfuko huu utaangalia wajasiriamali wadogo wadogo ambao hawajawa na mawasiliano ya moja kwa moja na mabenki *(the un-banked).* Mfuko huu unaweza kuajiri *Fund Managers* ambao wanaweza kuendesha mifuko hii Wilayani kwa ujira wa asilimia ya ufanisi wa mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa pili ninaoupendekeza ni ule ujulikanao kama *Venture Capital.* Huu ni mfuko unaolenga wajasiriamali wataalamu ambao kwa uzoefu wa nchi nyingi ndio hutengeneza *the middle class.* Kwa kuwa na mifuko michache, Serikali itaweza kuwekeza rasilimali kubwa ambayo kwa kusimamiwa na wataalamu itakuwa endelevu na mafanikio yake yataonekana.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote ambao kwa namna moja au nyingine wametoa mchango wao mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi naipongeza Bajeti hii kwa kutilia mkazo mkubwa katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kuinua kilimo pamoja na wakulima wenyewe italeta tija iwapo tu dhana hii itaenda sambamba na kuwepo kwa miundombinu ya uhakika kwa mfano barabara, umeme na kadhalika ili wakulima wetu wawe na uhakika wa kusafirisha mazao yao mara tu wanapoyavuna na kuyapeleka katika masoko.

Mheshsimiwa Spika, wakulima wetu wanajitahidi kuitikia wito wa kilimo kwanza lakini napenda kuiuliza Serikali imejipangaje kuhusiana na suala la masoko ya uhakika ili wakulima wetu wawe na uhakika wa kuuza mazao yao na kwa faida, vinginevyo bila kuwapo na masoko ya uhakika na miundombinu iliyo bora basi wakulima watakata tamaa na ile dhana ya kilimo kwanza haitaleta tija kwa wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshsimiwa Spika, kumalizia, napenda niipongeze Serikali ya awamu ya nne kwa juhudi zake za kuinua uchumi wa nchi na kwa juhudi zake za kujenga barabara za kuweza kuunganisha mikoa yetu na hata nchi za jirani. Lakini napenda kuishauri Serikali ijitahidi kwa nguvu zake zote iweze kuifufua reli ya kati ili irahisishe treni zetu kubeba mizigo iliyo mizito ili kuzinusuru baadhi ya barabara zetu kwani zinaharibika sana kwa kupitiwa na magari mazito ya mizigo na kuzifanya zididimie na hata kusababisha ajali.

Mheshsimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni nyongeza ya maelezo niliyotoa kwa kuzungumza Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu limepewa kipaumbele katika Bajeti hii. Nashauri pesa za kutosha zitengwe katika kujenga nyumba za walimu, bila nyumba za walimu sekondari zetu zitaendelea kukosa walimu. Walimu hawatakuwa tayari kuishi katika nyumba zisizo na ubora wakati tumewajengea vyumba vizuri vya walimu, makazi bora ni siri ya afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile sula la kutoa pesa kwa ajili ya maabara ni muhimu. Nchi haitakwenda, bila kuwa na wataalam hatuwezi kusonga mbele ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri usimamizi mzuri wa fedha zinazokwenda kwenye halmashuri, manispaa, majiji zifuatiliwe kwa karibu ili kuhakikisha zinafanya kazi ile ile tuliyolenga. Kwa hiyo basi, waongezwe wataalam kwenye *council* zote ili wazifuatilie hizo pesa hadi huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yetu iwe katika malengo maalum. Malengo hayo tuyafuatilie ili tuhakikishe yanatekelezwa katika muda tuliopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Serikali ilizingatie suala la wajasiriamali wadogo wadogo, na katika msingi huo narudia kushauri kuwa injini zenye CC 0-2000 zisiongezewe kodi. Kodi ianzie kuongezwa CC 2001 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari/vyombo vya moto vyenye CC 0 - 2000 ni vidogo. Ni vile vinavyochukua hata nafasi ndogo, mfano pikipiki, bajaji, Suzuki, Vitara, Rav 4, Escudo na mengine madogo. Magari/vyombo hivi vina matumizi mazuri ya mafuta, uchafuzi mdogo wa mazingira na nafasi ndogo ya *parking.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi ni vya kusaidia kuharakisha juhudi za wajasiriamali kuendesha shughuli zao za kiuchumi. Hawa waagaliwe na watiwe moyo. Vyombo/magari yenye CC zaidi ya 2000 waongezewe kiasi cha kodi, kwani ni makubwa na hata gharama ya ununuzi ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato ya ndani; Serikali itazame na kupata mapato kutoka vyanzo vipya vya ndani hasa kodi kutoka sekta ya madini, uvunaji magogo ya mbao, utalii, uwindaji, uvuvi, bandari na uchukuzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya Serikali (Kawaida), katika hali ngumu ya kiuchumi kama sasa, kuna matumizi yasiyo ya lazima na Serikali iyaondoshe ama kuyapunguza sana. Kasma za usafiri, posho, warsha na ukarimu ni maeneo ya kutazamwa na kupunguzwa sana. Ununuzi wa magari ya fahari usitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za maendeleo, Serikali ikope fedha na kuinua kiasi cha fedha za maendeleo kufikia 10% ya Bajeti nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgao wa Bajeti uwiane zaidi. Wizara muhimu kama Katiba na Sheira, Maji na Umwagiliaji, Mifugo na Uvuvi, ziongezewe majukumu yake ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgao wa Bajeti Kimkoa utazamwe upya kwani tofauti kati ya mkoa na mkoa ni kubwa sana. Kwa miaka mitatu (3) sasa mfululizo, kuna mikoa nane (8) ambayo imekuwa ikipendelewa sana Kibajeti na kupatiwa fedha nyingi sana ukilinganisha na mingine.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 62 ukurasa wa 33 wa taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa, kasoro kubwa ninayoiona kwenye Bajeti hii ni kwamba iko *anti-environment* kwa vile iko kimya kabisa kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatisha zaidi wakati huu ambapo dunia nzima na hususan Tanzania imekumbwa na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na matokeo yake yako wazi Tanzania na ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kutengwa fedha kwa ajili ya kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi, kwa bahati mbaya gharama za kupambana na athari hizo zimeachiwa wahisani kwa asilimia 100%. Kkatika hali hii usimamizi wa mazingira hauwezi kuwa na tija na haiwezekani kunusuru uchumi na maendeleo ya nchi kama inavyowekwa katika Kifungu cha 62 katika ukurasa wa 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo ya kina suala hili na kasoro hii na jinsi Serikali itakavyorekebisha kasoro hii.

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi bandarini ni aibu ya Taifa. Nilikuwa Zambia, wafanyabiashara wamelalamika sana kuwa bidhaa zao zinaibiwa Bandarini Dar es Salaam, hivyo kulazimika kutumia zaidi Bandari ya Durban na kuikosesha Tanzania mapato. Wizi *TAZARA* ndiyo usiseme, hata wafanyakazi wake wanalalamika kana kwamba wao sio wahusika! Matokeo yake wafanyabiashara wanaikimbia *TAZARA* na mapato ya shirika si mazuri.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna tofauti kubwa baina ya Bajeti iliyopita na Bajeti hii ya sasa kiasi kwamba wananchi wategemee kupata nafuu ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuoni mipango madhubuti ya kutekeleza kilimo kwanza hasa ikiziangatiwa kwamba kilimo ndiyo tegemeo kubwa kwa wananchi walio wengi katika nchi hii. Serikali inapaswa kuweka mazingira bora yatakayowezesha sekta binafsi kuweza kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya mbolea vifufuliwe ili tuweze kuzalisha mbolea ya kutosha badala ya kutegemea zaidi mbolea kutoka nje ambayo ina bei kubwa kiasi kwamba wakulima wadogo wanashindwa kuinunua. Ni muhimu pia kujenga viwanda vya kusindika mazao katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji wa matunda na mazao mengine mbalimbali badala ya kuuza yakiwa malighafi na hivyo kuwapatia kipato kidogo wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii haikuzungumzia lolote kuhusu uvuvi sekta ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa Pato la Taifa, mfano halisi unaothibitisha haya ni ile meli iliyokamatwa na samaki na kupewa jina samaki wa Magufuli. Samaki ni chakula, samaki ni uchumi lakini kwa sasa wanaofaidika na samaki

wetu na wavuvi wa meli za nje wanaokuja kuvua samaki wetu na kuondoka bila nchi yetu kupata faida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wa Morogoro ulitangazwa kuwa ghala la Taifa lakini bado hadi leo hakuna kilichofanyika bali hata huko Morogoro kwenyewe kuna matatizo. Wakulima wa mpunga walizalisha mpunga wa kutosha lakini umeharibika kwa kukosa soko na Serikali kushindwa kuununua. Hii inasikitisha sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutokuwa makini sana na hivyo kutumia zaidi maneno kuliko vitendo na hivyo kuwasababishia hasara wakulima wa mpunga Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo lakini umeme bado ni tatizo katika nchi yetu, Serikali inapaswa kuwa makini zaidi kuhusu suala zima la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uchumi wa nchi yetu uzidi kukua, mawasiliano kwa njia ya barabara na ya anga yanapaswa kuangaliwa kwa uzito wake kwani haya yataifungua nchi katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajielekeze kwenye Sheria ya Ukaguzi, 2008, Kifungu cha 44(3) na Kanuni namba 105 ya 2009 na ahusishe na kitendo cha kukiuka sheria na kanuni alizotunga yeye na kuziidhinisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na Watendaji wake wote, kwa hotuba yake nzuri iliyosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania endapo kutakuwepo na ufuatiliaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri za Wilaya ndio tegemeo kubwa la kuwaletea wananchi maendeleo yao, lakini zipo Halmashauri ambazo zinadhoofisha na kukwamisha maendeleo hayo kwani baadhi ya Watendaji siyo waaminfu katika kutekeleza kazi zao. Pamoja na kwamba mwaka huu wa 2010/2011, Halmashauri zitakusanya jumla ya Shs.172.582 bilioni, fedha hizo zingeleta tija kama zitasimamiwa na kama kutakuwepo ufuatiliaji mzuri. Fedha nyingi zinaliwa na zinafaya kazi za miradi chini ya kiwango. Vilevile ni vema wakaajiriwa Wakaguzi wa Ndani ambao ni waaminifu, kwani wapo baadhi ya Wakaguzi wanaoshirikiana na watendaji wenye dhamana ya kusimamia miradi kufunika fedha zinazoliwa, aidha kazi zilifanywa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na kuunga hoja mkono.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa kazi nzuri ambayo imepelekea kuweza kuwasilisha hoja nzuri ya makadirio ya Bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kuchukuwa nafasi hii, ili nichangie suala la kuimarisha Bandari zetu ambazo ni njia kuu ya uchumi wa nchi yetu. Endapo Bandari pamoja na barabara zetu zitaimarishwa, uchumi utakua sana kwa vile zinaunganisha nchi jirani ambazo hazina Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi nalo lina nafasi yake katika kuinua kipato cha wananchi pamoja na Serikali. Endapo wavuvi watapatiwa elimu sahihi ya uvuvi na vifaa vya kisasa, kuna uhakika kuwa wataongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii iimarishwe na hasa kwa sasa ni muhimu kutoa elimu na kuhimiza utalii wa ndani ambao pia utasaidia kuongeza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara na Taasisi zilizohusika katika kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi na Bajeti kwa mwaka 2010/2011. Pamoja na changamoto nyingi zinazotokana na mdororo wa uchumi Duniani, ukame, mafuriko na kupungua kwa misaada, wameweza kuandaa bajeti ya Taifa kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika kuona hatua za kuendeleza uzalishaji mali, uboreshaji miundombinu pamoja na kubana matumizi zinachukuliwa. Hakika hatua za kusisimua uzalishaji katika kilimo, viwanda, madini, utalii na sekta nyingine za kiuchumi pamoja na uboreshaji wa miundombinu, ndio njia thabiti za kuendeleza uchumi wetu kwa mujibu wa malengo yetu na mazingira magumu yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dhana ya Kilimo Kwanza, hapana budi hatua madhubutu zikuchukuliwe kuweka malengo na utekelezaji wake kusimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa nguzo tisa za Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua njema ya kuondoa kodi kwa pembejeo za kilimo, ingefaa ifikiriwe pia kwa vifaa vya mizani na upimaji na kutoa vivutio kwa wawekezaji wa zana za kilimo pamoja na vifaa vya mizani ili kuondoa kero ya wakulima wadogo wadogo kupunjwa kivipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa uvuvi, haujapata mkazo stahiki katika mipango yetu na bajeti tunayojadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mhimili muhimu katika Kilimo Kwanza, ni pamoja na masoko ya kuaminika. Zaidi ya hatua za kuimarisha ushirika na mfumo wa stakabadhi ghalani, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha magulio na masoko ya msingi. Aidha, baada ya kuzungumza kwa muda mrefu sana, sasa wakati umefika kutekeleza mipango ya ujenzi wa masoko ya kimataifa ya matunda na bidhaa za mboga mboga ya Segera na Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa hatua za kuboresha na kuendeleza miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na miundombinu mingine ya mawasiliano. Ni jambo la faraja kubwa sana, hivi karibuni tumeshudia Mheshimiwa Rais akiweka mawe ya msingi kwa ujenzi wa barabara nyingi ikiwemo barabara ya Tanga – Horohoro na nyinginezo. Pamoja na kushukuru na kufarijika kwa haya, ni muhimu hatua hizi zichukuliwe kwa ukamilifu wake ili kuleta mafanikio yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, barabara ya Tanga – Horohoro, haiwezi kuleta mafanikio tarajiwa iwapo ujenzi wake hautaendana na ujenzi wa Bandari ya Tanga pamoja na reli ya Tanga – Arusha – Musoma vinginevyo ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga – Horohoro inaweza ikawa kwa faida kubwa zaidi kwa bandari ya Mombasa kuliko kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa Bandari zetu za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara pamoja na Reli za Kati, Tanga – Musoma na Mtwara - Ziwa Nyasa, ni mkakati thabiti ambao ungeweza kutuondoa katika lindi la umaskini linalolikabili Taifa letu hivi sasa, tuweke mkazo unaostahili kwa kipaumbele hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu na kutowajibika kwa baadhi ya viongozi na watendaji wetu, ni kasoro zinazokwaza utekelezaji bora wa mipango yetu na maendeleo yetu. Nafarijika kuona kwamba hotuba hii ya bajeti imeweka mkazo juu ya *OPRAS*. Nashauri *Clients Charter* nayo iwekewe mkazo. Wafanyakazi, Wakulima, Wavuvi na viongozi katika ngazi zote, hawana budi kujituma na kuwajibika ipasavyo ili mipango yetu mizuri na bajeti yetu iweze kuzaa matunda yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia kusema kwamba katika jitihada zetu za maendeleo, tutapata kasi kubwa zaidi ya maendeleo endapo tutaweka kipaumbele kwa viwanda kama kichocheo kikubwa kwa Kilimo Kwanza na kwa uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, Serikali kukopa kwa ajili ya matumizi kwa maendeleo, ni suala muafaka lakini si muafaka kwa Serikali kukopa kwa matumizi ya kawaida *(Recurrent).* Naamini tukiendelea kuchukua hatua za kubana matumizi na za kuhamasisha uzalishaji na ulipaji kodi, unaweza ukatusaidia kuepuka kukopa kutoka Benki za Biashara vinginevyo ni afadhali kutumia Nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya changa ya Mkinga bado ina kilio kikubwa cha mgao wa bajeti kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hususani ofisi ya Halmashauri ya Wilaya, maji kwa Makao Makuu na kwingineko, umeme kwa vijiji vya Dahini, Gombero, Kwale, Vuga na Boma. Aidha, Wilaya ya Mkinga bao ina hoja kubwa ya kukamilisha Hospital ya Wilaya, kujenga Zahanati na Vituo vya Afya kwenye Vijiji na Kata mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama zilivyo Wilaya nyingi, Wilaya ya Mkinga ina upungufu mkubwa wa Walimu, maabara, gari za wagonjwa na mawasiliano ya simu. Naamini Serikali itaendelea kuitazamia Wilaya hii changa na ya pembezoni kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali nzima ya Awamu ya Nne, kwa kutekeleza kwa mafanikio makubwa sana Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na kwa mpango na bajeti nzuri kwa mwaka 2010/2011. Ni imani yangu kwamba bajeti hii italinufaisha Taifa na kuiwezesha CCM kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011. Pia ninawapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii, nimefurahishwa sna na mpango wa Serikali wa kuboresha maslahi ya watumishi na kupanua ajira, kipengele cha (xi), katika ukurasa wa 29. Kwa kuwa Serikali imeamua kuweka mpango huu, nitumie nafasi hii, kuiomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wale watumishi walio katika maeneo ya vijijini. Watumishi hawa wana maisha magumu sana mfano Walimu na Wauguzi. Mazingira wanayoishi ni magumu, nyumba za watumishi hakuna, vifaa vya kutolea huduma, hakuna na hii husababisha watumishi wengi wanapopangiwa vijijini hawaendi kuripoti, matokeo yake katika maeneo ya vijijini, shule hazina Walimu, Zahanati hazina Waganga. Hii husababisha matatizo na changamoto kwa wananchi kutopata huduma zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha maisha ya watumishi, ninaomba Serikali katika bajeti ya mwaka 2010/2011, iangalie suala zima la kuboresha huduma kwa watumishi hawa kwa kujenga nyumba za watumishi na kutoa kipaumbele katika kuleta vitendea kazi ili kuboresha mazingira na kutoa motisha kwa watumishi hawa ili wasikate tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninaomba Serikali ione uwezekanao wa kuwapa *Hardship Allowance*, malipo ya ziada ili kuwapa motisha watumishi hawa. Hii italeta motisha na hali ya kuwajibika kwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kupanua ajira, ninaiomba Serikali iangalie uwezekanao wa kuwalipa mishahara viongozi wa vijiji. Hii ni kutokana na kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia shughuli za maendeleo katika vijiji husika. Kwa kuwalipa mshahara, itaongeza uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali zinazoelekezwa katika vijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia kidogo kuhusu bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa mwaka huu wa bajeti, imeweka kipaumbele katika suala zima la Kilimo Kwanza, hili ni jambo zuri sana lakini la kujiuliza, je, ni kwa jinsi gani Serikali imejipanga katika kulitekeleza suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo kiweze kushamiri vizuri nchini, lazima Serikali ijidhatiti vizuri katika kupatikana mbolea kwa wingi na kwa wakati. Si busara wala si kuleta ufanisi pale mbolea inapokuwa haitoshi na hiyo kidogo inayopatikana kutofika inapotakiwa kwa wakati. Hivyo, ni vyema dosari ndogo ndogo kama hizi zikafanyiwa kazi ili kuondokana na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inayo rasilimali nyingi ambazo kama zingetumiwa vizuri pakawepo na uzalendo ambapo wenye dhamana wangejali maslahi ya Taifa basi uchumi wa nchi hii ungekuwa katika hali inayoridhisha na matunda yake kuonekana. Leo hii tunaambiwa kwamba uchumi wetu unakua lakini wananchi wanauliza kama uchumi kweli unakua mbona hali zao za maisha zinazidi kuwa duni kila siku au uchumi unakaa ndani ya vitabu tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi yoyote ile duniani, yanategemea ubora wa miundombinu wa nchi husika, hebu tujiulize, miundombinu ya nchi yetu kama vile barabara, bandari, reli n.k. iko katika hali gani? Kwa kweli hali ya miundombinu yetu hasa niliyoitaja hapo juu, ni duni sana. Pamoja na uduni wa miundombinu hiyo na hasa barabara, bajeti hii haikutoa kipaumbele kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa mwaka wa fedha ujao, inakadiria kukusanya mapatao kwa kiwango kikubwa lakini swali langu ni kuwa katika kiwango hicho kinachokadiriwa kukusanywa, mashirika na taasisi zilizobinafsishwa, zitatoa mchango wa kiasi gani katika pato la Taifa? Je, yale mashirika yaliyobinafsishwa na ambayo hayafanyi vizuri kinyume na madhumuni ya kubinafsishwa kwake, Serikali inayachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kutoa pongezi zangu nyingi kwa Waziri Mkullo, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha, kwa kazi yao nzuri waliyofanya katika kusimamia uchumi wetu hasa katika kipindi kigumu cha uchumi Duniani. Pia kwa jinsi wanavyojitahidi kugawa rasilimali kidogo zilizopo katika maeneo mengi ambayo ni muhimu (vipaumbele) kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa maoni yangu katika sekta maeneo yafuatayo, Serikali inapaswa kusamehe ushuru wa Forodha pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani kama kwenye matairi ya malori, mabasi, matrekta na vipuri vya malori, mabasi, mashine na viwanda na matrekta. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na usafirishaji na hivyo kuinua sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuwalipa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu n.k. pesa taslimu kwa ajili ya kujilipia simu, maji na watumie magari yao ya binafsi kwenda kazini na kurudi majumbani mwao. Kuna matumizi mabaya ya magari ya Serikali simu n.k na hivyo kupelekea gharama kubwa zisizo za lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali itume au izipatie fedha Halmashauri zote kwa wakati mmoja ili kurahisisha "*Oversight*" ya matumizi ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, utafiti wa kina ufanywe kwa lengo la kubaini ni hatua zipi zitasaidia kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kumpongeza Waziri Mkullo, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kukuza na kuboresha uchumi wa nchi yetu.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, hivyo hayajui fika maeneo ambayo Serikali inaweza kuongeza pato kwa kukusanya mapato zaidi? Tuangalie eneo la mafuta, je, Wizara yako kupitia *TRA*, ni kweli hawajui eneo gani linakwepa kodi? Hebu tujiulize, Tanzania ilinunua Rada kwa thamani ya fedha nyingi ambayo ina uwezo (tulivyoambiwa) wa kuona mipaka yetu yote lakini meli zinazokutana baharini na ku-*refuel* baharini, hazijulikani! Ikiwa *TRA* ni kweli hawajui mchezo huu mchafu unaofanywa baharini, je, meli za uvuvi ziko ngapi na wapi wana *refuel*?
Wizara yako imewahi kufuatilia suala hili, kama bado, je, haijui upo umuhimu mkubwa wa kulifuatilia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya uchumi ya *Mtwara Corridor* uko wapi? Mbona bajeti au mipango yetu ya uchumi unaachwa? Kwa nini mwanzoni mwaka 2000 hadi 2008 ilikuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya maswali haya, ahsante.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Pili katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005-2010. Msema kweli ni mpenzi wa Mungu, kweli katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wamefanya mengi, kweli kabisa haijapata kutokea! Hongera sana. Kwa msingi hiyo, naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisemee kidogo yaliyotokea katika Ilani hii ya CCM 2005-2010, naomba nijikite kidogo kwa yaliyotokea Jimboni kwangu, Wilaya yangu, Mkoa hadi Taifa. Kuhusu miundombinu, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, barabara inayotokea Tabora - Nzega kupitia Bukene na barabara ya Nzega – Itobo – Kagongwa – Kahama. Ninafurahi imetengenezwa kwa kiwango cha changarawe, watu wote sasa hata Mawaziri, Spika wakienda Majimboni mwao wanaitumia, ni nzuri na wanatumia muda au dakika ndogo sababu ya uzuri wake. Kinachotakiwa hapa ni kuongeza ule uimara zaidi au magari yenye uzito zaidi yasipite au yasitumie barabara hii ili isiharibike mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni ahadi ya Rais, umeme toka Nzega – Bukene, hongera sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne, wataalamu wapo na mitambo yao wamehifadhi katika bohari mojawapo la Igembenabu, Bukene. Wale Watani zetu wa Jadi wanasema "hii ni danganya toto" na Wanyamwezi husema kwa idhini yako naomba kunukuu "*Kuzunya kwa ngwa thoma, kwiboneleja"* maana yake "Mt. Thomas alipoambiwa Yesu amefufuka, hakuamini mpaka alipomuona mwenyewe kwa macho yake. Kwa lugha nyingine maana yake wataamini pale watakapoona umeme umewaka. Kwa misingi hiyo, basi tuhitimishe umeme uwake Bukene kwani ni kisehemu kidogo tu, kilomita 48 tu. Naiomba sana Serikali ihitimishe ili tufunge kalomo, kalomo ni mdomo, hivyo kufunga midomo yote, naamini inawezekana kabissa kwani Mwalimu Nyerere alisema *"It Can Be Done Play Your Party."*

Mheshimiwa Naibu Spika, la umuhimu na zuri sana ni katika kuwadhamini wakulima katika bajeti ya 2010/2011. Wakulima hapa ni 80% ya wananchi wote wa Tanzania na wakulima maana yake ni wakulima na wafugaji. Naomba kukiri kwamba, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo na mambo mengi waliyotuomba wakulima, wafugaji na wafanyabiashara wenye viwanda vya maziwa n.k., wapunguziwe kodi katika mashine, *packing materials*, pembejeo n.k., yote yamefikiriwa na yamepewa misamaha ya kodi, kweli ni faraja sana kwa wakulima, hongera sana kwa kuwadhamini wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwapongeza katika kilimo cha kisasa yaani umwagiliaji kwa kujenga mabwawa madogo madogo na ninaishukuru Serikali kwa kunipa bwawa kubwa sana, linachukua Kata mbili yaani Kata ya Kahama ya Nhalanga na Kata ya Mogwa. Naamini Kilimo Kwanza kinatekelezeka na naamini baada ya Kilimo Kwanza hasa kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji, naamini umaskini *Bye, bye* na chakula au mazao yatafika kwa urahisi kwenye masoko basi bei ya mazao itakuwa poa, maana yake "*Last Consumer*" yaani ulaji utakuwa bei poa. Hivyo, itatugusa sisi wote, mambo safi tu , hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipopata Jimbo la Bukene, kulikuwa na sekondari *schools* mbili tu sasa tuna shule za sekondari kila Kata, tuna kata 16, shule nilizokuta ni mbili. Kwa misingi hiyo, shule za sekondari kumi na nne (14), nimeshiriki kutoa matofali ya chumba kimoja cha daraja katika Kata zote, na hii imetia hamasa sasa tuna shule za sekondari Kata zote. Kuhusu elimu, hapa hatuna Walimu, kuna shule kama *Kasela Secondary School*, Kata ya Kasela, wana Mwalimu mmoja tu. Hivyo tunaomba Walimu na maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi Serikali imefanya ila naomba tuongezewe vifaa kama pikipiki kwa ajili ya Askari wetu, hivi sasa pikipiki nilizowapa Sungusungu, ndio zinasaidia katika doria Jimboni kwangu katika ulinzi jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kama ilivyo ada, kumshukuru Mwenyezi Mungu na wapiga kura wangu, kwa kuwa na imani kwangu na hasa ushirikiano walionipa. Nawashukuru sana maana kwa ushirikianao wao imewezekana kufanya haya niliyotaja na mengine mengi ambayo tumefanya hadi ushindi wa vijiji, tumepoteza kijiji kimoja tu  kati ya vijiji sitini  na sita (66). Vitongoji 432, tumepoteza vitongoji 12, kwa misingi hii, upinzani haupo, nilishauua. Yote yamebadilika kwa uongozi wangu kwa vitendo, natoa ahadi na kutekeleza mara moja, katika utekelezaji wa Ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mungu akinijalia nikiwa hai, nitatetea Jimbo na naamini Mungu atanishindia kupitia kwa watu kwani sauti ya wengi ni sauti toka kwa Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru wewe mwenyewe na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge letu Tukufu, wote tunawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu hii ni nzuri lakini tuelewe bila elimu hakuna maendeleo katika maisha ya mtu au nchi yoyote ile. Kwa hiyo, naiomba Wizara, bajeti hii itumike kama ilivyopangwa na kuepukana na ubadhirifu ndani ya nchi, isiwe maneno tu vitendo viwe wingi. Kwa hiyo, Serikali itekeleze ikipitishse bajeti tu basi kazi

ya utekelezaji kwa upande wa vifaa na vitendea kazi vya Kilimo Kwanza viwepo na fedha itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya nchi yetu kama vile barabara, umeme au reli, maji n.k. yote hayo bado kwa nchi yetu yako chini, kwa nini? Mheshimiwa Waziri, analifahamu hili, kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia bajeti hii basi suala hili litatuliwe baada ya kupitishwa bajeti na Tanzania iwe mfano kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na wapiga kura wangu, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BAKARI H. MWAPACHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011 – 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu wake Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, Katibu Mkuu Ramadhani Khijjah, Manaibu Katibu wakuu na viongozi ndani ya Wizara na taasisi zake kwa maandalizi ya hotuba zote mbili. Hotuba hizi zimeandaliwa vizuri sana, zimechambua kwa kina hali ya uchumi wetu, tumetoka wapi, tuko wapi na tunatarajia kufanya nini katika siku za usoni. Nasema kwa dhati kubisa kwamba Wizara ina wataalam wazuri na wamejipanga vizuri ndani ya Wizara ambayo ni *well structured* pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote katika kusimamia uchumi wetu kwa ufanisi na tija kubwa wakati wa msukosuko wa uchumi duniani, aidha Gavana wa Benki Kuu amefanya kazi nzuri katika kuongoza *task force* iliyojielekeza katika kudhibiti hali mbaya ya uchumi dhidi ya nchi yetu wakati wa msukosuko huo wa uchumi. Tumeweza kuhimili vizuri hali hiyo na kutuwezesha kuvuka hadi kufikia hapa tulipo sasa hivi, pamoja na athari zizojitokeza mwaka 2009 katika sekta mbalimbali kama alivyozitaja Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo katika hotuba zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kusisitiza masuala machache kuhusu maeneo yafuatayo kutokana na nafasi yangu kuwa Mbunge wa Tanga. Kwanza umuhimu wa kuendeleza sekta ya miundombinu. Tanzania, kwa ujumla wake haiwezi kusonga mbele bila kuimarisha barabara, reli na bandari zake. Kwa upande wa Tanga bila ya kuwekeza katika maeneo haya, Tanga haitafufuka baada ya zao la mkonge kurudi nyuma baada ya kutaifishwa kwa mashamba katika miaka ya 9160 na 1970. Tunashukuru kwa baadhi ya barabara zinazoelekea Tanga kama vile kutoka Mombasa na ile ya Kilosa – Handeni – Korogwe zinajengwa ambazo zitakuwa ni changamoto kwa kukuza uchumi wa Tanga. Lakini tunahitaji barabara ya Bagamoyo – Pangani - Tanga kujengwa ili nayo ichangie ukuwaji wa uchumi wa Tanga. Lakini muhimu zaidi ni ujenzi

wa reli kutoka Musoma – Arusha - Tanga ambayo pia itaendana na ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani katika Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri ametaja vipaumbele vya sekta husika ikiwa ni pamoja na miundombinu, akitaja na barabara, reli, bandari na kadhalika. Lakini Bajeti haizungumzii upatikanaji wa fedha katika maeneo au miradi niliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii niliyoitaja haitakuwa kwa manufaa ya Tanga, bali kwa Taifa zima. Naiomba Serikali ifanye maamuzi ya ujasiri na haraka ili kuchochea kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge wa Tanga, napenda kumshukuru Waziri Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa hatua aliyoichukua safari hii kwa kutoa msamaha wa *VAT* katika vifaa mbalimbali vya mashine na vifaa vya uzalishaji na usindikaji wa maziwa na pia kutoa msamaha huo kwa upande wa vifungashio vya bidhaa za maziwa. Nasema ahsante kwa hili kwa sababu itavifanya viwanda hivyo kupunguza matumizi yake, kama vile *Tanga Fresh* na hivyo kutoa motisha na bei kubwa zaidi kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la uvuvi, Serikali inasema nini, mbona kila mwaka sekta hii inapuuzwa? Lini Serikali itatenga pesa ya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia masauala hayo muhimu kwa upande wa Jimbo langu la Tanga sasa ningependa kuchangia masuala machache kuhusu Bajeti yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti imeandaliwa vizuri sana. Kwa ujumla, nia ya Bajeti ni ku *restore the economy after global financial crisis* na kulenga katika kukuza uchumi, kutoa unafuu wa maisha kwa wafanyakazi na kuboresha maisha kwa wananchi kwa ujumla, changamoto iliyo mbele yetu ni kuweka mikakati thabiti ya kiutekelezaji. Naomba kuelezwa kuna mkakati gani kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumziwa mengi katika maeneo mbalimbali kuhusu mapato na matumizi kwa upande wa Serikali kwa ujumla wake. Mawazo yametolewa namna ya kuimarisha nchi kiuchumi, jinsi ya kusimamia mapato na matumizi ya Serikali, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na taasisi nazo kuwa nyingi na hivyo kuwa mzigo. Haya masuala ambayo yamekuwa yakizungumziwa kila mwaka, hatujakuwa na *big picture* ya maeneo haya mawili muhimu na hasa katika kupunguza matumizi. Kwa hili Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Waziri wa Fedha afikirie kuunda Kamati ambayo itaweza kuchambua suala hili na kutoa mapendekezo ya namna ya kupunguza matumizi ya Serikali, ikiwa ni pamoja na ya kuongeza mapato kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja hii mkono asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuandaa Bajeti hii ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii naomba nijikite sana katika matatizo yanayowakabili wananchi wetu wa mkoa wa Mtwara. Kwanza kabisa ni suala la stakabadhi ghalani kwa wakulima wetu. Hadi sasa mfumo huu wakulima wameukubali, lakini bado wanaomba baadhi ya maeneo yarekebishwe hasa katika suala la malipo ili waweze kulipwa kwa mkupuo kisha wasubiri malipo ya majaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi hivi sasa suala la upatikanaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima wetu bado hazijakidhi haja, hivyo naomba Serikali iongeze Bajeti yake katika kutoa ruzuku na kuagiza dawa kulingana na mahitaji ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya katika mkoa wetu zahanati zimeongezeka kwa kiwango kikubwa lakini bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi hivyo kusababisha huduma finyu kwa wananchi, naiomba Serikali iangalie kuongeza watumishi kwa sekta ya afya kwa hospitali zetu na zahanati za Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hospitali zetu na zahanati zetu zimekuwa na upungufu mkubwa wa dawa hivyo wananchi wetu wanakosa tiba zilizo bora na sahihi kwani wagonjwa wengi wameishia kununua dawa katika maduka ya dawa jambo ambalo linawagharimu fedha nyingi na wengi kupoteza maisha kwa kukosa huduma bora kwani wengi hupata huduma hii wakiwa majumbani bila uangalizi wa daktari. Naishauri Serikali iangalie tatizo hili ili dawa za kutosha zipatikane katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu katika mkoa wetu wa Mtwara pia shule za sekondari zimeongezeka kwa kiwango kikubwa, shule za msingi zipo za kutosha hivyo kwa kiwango kikubwa watoto wetu wanapata elimu ya msingi na ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hii bado mkoa wetu una upungufu mkubwa sana wa walimu, jambo ambalo linadidimiza sana upatikanaji wa elimu iliyo bora kama Serikali haitachukua jitihada za haraka kwa kuleta walimu wa kutosha katika shule zetu. Mkoa wetu wa Mtwara kwa miaka ijayo hatutakuwa na vijana wa kutosha watakaochaguliwa kwenda katika Vyuo Vikuu hivyo mkoa wetu wa Mtwara kwa miaka ijayo hatutakuwa na vijana wa kutosha watakaochaguliwa kwenda katika Vyuo Vikuu, hivyo mkoa huu utakuwa kama umetengwa katika upatikanaji wataalam wanaotoka Mtwara. Pia katika sekta hii ya elimu naiomba Serikali iongeze Bajeti au ruzuku zinazoenda Halmashauri kwa ajili ya MMEM na MESS ili kuweza kujenga madarasa

yaliyo bora ili watoto na walimu wetu waweze kuishi katika nyumba bora na watoto wetu kuwa na pahala pazuri pa kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie katika sekta ya miundombinu. Wananchi wa mkoa wa Mtwara tunashukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuendeleza jitihada za awamu ya tatu kwa kukamilisha Daraja la Umoja linalounganisha nchi yetu na nchi ya Msumbiji hii inatupa matumaini kwamba shughuli zetu za kiuchumi zitaongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili pia linaunganishwa na barabara ya lami kutoka Masasi hadi Mangaka na baadaye daraja hili litaunganishwa na barabara ya lami kutoka Mangaka hadi Mtambaswala, kwa kweli ni hatua kubwa ya maendeleo, ombi langu kubwa kwa Mtambaswala naomba Wizara ya Ardhi waone umuhimu wa haraka kupitia *National Housing* wajenge nyumba katika eneo hili ili watumishi watakokuwa hapo mpakani kama polisi, askari wa uhamiaji, walimu, waganga na kadhalika wapate nyumba bora za kuishi ili kuwapa motisha na ari ya kupenda na kukubali kuishi mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kutoa msisitizo kwa Serikali kusimamia na kuhimiza ukamilishaji wa kilomita 60 zilizobaki kwa barabara ya Kibiti - Lindi, eneo hili bado halijakamilika na limekuwa kero kubwa sana kwa wakazi wa Mikoa ya Kusini ambapo kilomita hizi 60 mkandarasi huyu anahitajika kushauriwa kuongeza kasi kwani magari mengi yamekuwa yakikwama na kusababisha abiria kulala njiani mvua zinaponyesha, hivyo matarajio yangu Serikali itaona umuhimu wa kusimamia suala la kukamilisha eneo hili kwa kasi na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kuchangia katika sekta ya maji. Suala la maji kwa mkoa wetu bado kuna tatizo kwa Wilaya za Newala, Tandahimba, Nanyumbu na Masasi, tunashukuru sana jinsi Serikali ilivyoweka mpango wa kuondoa tatizo la maji kwa Newala na Tandahimba lakini bado naiomba Serikali itoe pesa za kutosha kukamilisha kazi ambayo imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Masasi niliiomba Serikali kukarabati Bwawa la Mchema ili kupunguza tatizo la maji kwa mji wa Masasi na Serikali ilikubali kukarabati bwawa hili na kuchimba bwawa lingine katika Mto Myesi naomba Serikali ituambie kazi hii ya kukarabati Bwawa la Mchema na kuchimba bwawa lingine katika Mto Myesi Serikali imetenga fedha kiasi gani na kazi hii itaanza lini ili kuondoa adha kubwa iliyopo katika mji wa Masasi?

Mwisho naishukuru Serikali kwa kukubali kuanzisha mradi wa maji kupitia *World Bank* katika vijiji vya Nambawala, Mraushi na Lilala ninaomba utekelezaji uwe wa haraka. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba awali ya yote nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi kwa

ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Napenda kuwahakikishia kwamba nitaendelea kushirikiana nao wakati wote katika kukamilisha malengo tuliyojiwekea ambayo kwa kipindi hiki hayakuweza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa namna ya kipekee kabisa nichukue fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa jinsi ilivyowajibika ktika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005 kwa nchi nzima, lakini kwa namna ya pekee katika Jimbo la Mbozi Magharibi. Kwa kifupi kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu, naishaukuru Serikali kwa kuchimba visima vya maji katika vijiji vingi, kuanzisha ujenzi wa miradi ya umwagiliaji, kuanza kuboresha miundombinu ya barabara na usambazaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumshukuru Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kutembelea Jimbo langu kule Kamsamba hapo 31/10/2009, ikiwa ni miaka 28 toka Rais wa kwanza Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipotembelea huko mwaka 1981. Hakika ujio wa Rais Kikwete ulileta faraja kwa wananchi na imani kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Nne bila kusahau kwamba hata mie ilinipa afueni kubwa dhidi ya shinikizo nililokuwa napata kutoka kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi waliipokea Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005 kwa shangwe na furaha kubwa wakiwa na matumaini ya maisha bora, mbele yao hata hivyo pamoja na hayo barabara ya Taifa kutoka Tunduma – Sumbawanga, ambayo waliahidiwa hadi leo haieleweki itaanza kujengwa lini, pamoja na kuambiwa itajengwa na fedha za *Millenium Challenge Cooperation*, barabara ya Mkoa ya Mlowo – Kamsamba kilomita 25 kati ya Itumbula na Kamsamba pamoja na Daraja la Mto Momba ambalo ni kiungo kati ya Mikoa ya Mbeya na Rukwa, haieleweki itajengwa lini, ingawa Mheshimiwa Rais alipotembelea Kamsamba aliahidi kufanikisha ujenzi huu na barabara ya Mkoa ya Izamba – Msangano – Utambalila kipande kati ya Isalalo na Msangano na kipande kati ya Msangano na Trindingoma kupitia vijiji vya Nkala na Chitete pamoja na *box caravates* nne zilizoahidiwa, ijengwe ili kuunganisha Bonde la Ufa la Rukwa lijulikanalo kwa jina la *Msangano Trough*, ambalo ni maarufu kwa kilimo cha mpunga, mahindi, ufuta, karanga, alizeti na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kakozi (Ndalambo) – Kapele – Kasinde – Ilonga inayoungana na barabara ya kwenda Kasanga kule Ziwa Tanganyika ni barabara muhimu sana, nayo inahitaji kupewa hadhi ya Mkoa na kutengenezwa ili kurahisisha msafiri kutoka Tunduma jimboni kwangu hadi Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi ambazo ni sawa na mishipa ya damu katika kuinua uchumi, hazipitiki. Hivyo basi nataka nihakikishiwe kuwa zitalimwa ili zipitike wakati wote wa mwaka kinyume na hali ilivyo sasa. Kama nilivyokwisha kusema, wananchi wa jimbo langu ni wakulima hodari wa mazao niliyoyataja hapo juu, lakini tatizo kubwa ni usafiri na usafirishaji wa mazao yao ambayo wanashindwa kuyafikisha kwenye masoko mikoani na nje ya mkoa. Ni imani yangu kubwa kuwa wananchi wana imani kubwa na Serikali hii na wanaamini kabisa kuwa itapata ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu ujao kama ambavyo wana imani nami. Naomba kilio chao kisikike ili kwa miaka mitano ijayo tukijaliwa tufanye kazi ya kujenga Taifa kwa pamoja.

Kuhusu maji safi na salama, Serikali kwa kupitia mipango mbalimbali ukiwemo ufadhili wa nje na ndani na *TASAF*, vimejitahidi sana kusambaza mipango ya uchimbaji visima vya maji jimboni tatizo kubwa limekuwa mkandarasi huchimba visima visivyoridhisha. Vingine vilitoa maji siku chache tu wakati vingine havikutoa maji kabisa. Naomba kwa visima vinavyotarajiwa kujengwa Serikali isimamie kwa karibu sana wakandarasi hao maana imedhihirika wazi kuwa wengi si waadilifu na pengine si waledi wa fani ya uchimbaji wa visima vya maji.

Kwa upande wa kilimo, tunaishukuru Serikali kwa kutoa ruzuku kwa pembejeo na zana za kilimo. Kwa bahati mbaya kabisa suala la mbolea na mbegu katika Jimbo la Mbozi Magharibi, hususan msimu wa mvua uliopita, liliambatana na udanganyifu mkubwa. Pembejeo hizi hazikuwafikia wakulima kabisa katika baadhi ya vijiji vya Kata za Tunduma, Myunga, Chitete, Chilulumo, Ivuma na Kamsamba. Vocha zimepotea bila kuwafikia walengwa. Kuhusu matrekta hadi sasa yale matrekta 13 *(power tillers)* ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alielezea Mbozi ingeyanunua hayaeleweki ni lini yatanunuliwa. Taarifa za danganya toto zinasema yako bandarini toka Januari, 2010 naomba Serikali ifuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kuipa elimu kipaumbele namba moja katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 kwani maendeleo yote yanategemea uwepo wa Watanzania wenye elimu wanaoweza kupanga mipango sahihi na kuifikisha kwa wananchi kwa utekelezaji sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kuunga mkono hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011. Kwanza napenda kupongeza Serikali pamoja na Wizara ya Fedha kwa hatua waliyofanya katika kuwapa watu chakula wakati wa njaa. Kama Serikali wasingefanya bidii watu wengi kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA) kwa kuwa Serikali inaandaa mkakati wa MKUKUTA awamu ya pili marekebisho yafanyike kutokana na makosa yaliyofanyika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bajeti hii fedha nyingi zimeendelea kwenye kilimo. Lakini ikumbukwe kwamba baadhi ya wananchi wanashughuli nyingine tofauti na kilimo kama mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mifugo wengi wamekufa kwa ajili ya kiangazi tegemeo letu ni msaada wa Serikali kutafuta namna ya kuwasaidia wale ambao wamefiwa na mifugo yote, kama Serikali inavyowasaidia wakulima kwa ajili ya mbegu, matrekta pembejeo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wananchi hawa hawana tegemeo la kuanzisha ufugaji tena, Serikali watafute fedha za kuwapa wafugaji kununua mifugo, fedha za kununua dawa na mifugo. Kuna dawa ya chango kwa ajili ya *E.C.F.*, kwa ajili ya ugonjwa ambao unawapa wafugaji matatizo mengi sana kwa ajili ya vifo vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na suala la Mheshimiwa Waziri wa Fedha kutokana na usimamizi wa fedha za umma katika Wizara na Idara za Serikali Kuu pamoja na matumizi mabaya na udhaifu wa usimamizi wa fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Serikali iangalie matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri. Udhibiti ukifanyika miradi mingi itafanyika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Longido ni miongoni mwa wilaya zilizoko mpakani, wenzetu wa Kenya wanapata mapato mengi kutokana na miundombinu ya biashara, masoko na sheria ambazo zinamwezesha mwananchi kufanya biashara ndani ya Kenya na Tanzania, naomba vikwazo ambavyo vinamnyima mwananchi kufanya biashara ndani na nje ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa thamani ya fedha yetu ni kikwazo kikubwa kwenye ushindani na wenzetu ambao thamani ya fedha zao ni nzuri. Wakenya wametuzidi kwa ajili ya kushuka kwa shilingi yetu. Naomba Serikali iangalie hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Serikali. Nampongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba nzuri Bungeni. Hii Bajeti ni nzuri.

Nawashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Vijijni kwa kunichagua na hatimaye kufanya kazi kwa pamoja kwa ushirikiano mzuri/mkubwa. Tumetekeleza Ilani yetu ya uchaguzi kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Niko tayari tena kuwa Mbunge wao kufuatia uzoefu niliopewa na wao na kwa misingi niliyokwishaweka hadi sasa ili kujenga juu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, naomba niipongeze Serikali kwa jitihada zake kubwa katika kuboresha kilimo nchini. Leo tunazungumzia kauli mbiu ya kilimo kwanza ili kushirikisha maeneo mengine kama barabara na viwanda ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Suala la ruzuku ya pembejeo za kilimo ni hatua mojawapo katika kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la kurekebisha katika kuendeleza kilimo ni vocha za pembejeo ziwafikie wakulima kwa wakati, mkulima apate fursa ya kuchagua anachokihitaji kama ni mbolea au mbegu. Mashamba mengine yanarutuba, mkulima anahitaji mbolea tu apewe. Kumekuwa na matumizi mabaya ya vocha ikiwa ni pamoja na kughushi kwingi na mbegu bandia. Pia udhibiti wa kuuza mazao ya kilimo kwa kutoa vibali ni kikwazo kwa wakulima wa Babati ambao wanatarajia kuvuna vizuri mbaazi na mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ardhi, ardhi ni msingi mmojawapo katika MKUKUTA unaohusu njia kuu za uzalishaji. Katika Jimbo langu la Babati Vijijini kuna migogoro mingi ya ardhi kati ya wakulima wakubwa na wadogo, kati ya wenye *lease* na wanavijiji majirani. Kuna migogoro kati ya Chama cha Ushirika cha *RIVACU* na wananchi wa Dohom, Endasago na Arri. Kuna mgogoro kati ya *Breweries* na wananchi wa Arri.

Kwa ujumla naomba iundwe tume ya kuchunguza migogoro ya muda mrefu ya ardhi jimboni Babati Vijijini. Naipongeza Serikali kwa upande mwingine kumaliza mgogoro wa wananchi wa Mwada na chama cha Ushirika - *RIVACU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya barabara na reli, nasisitiza umuhimu wa kuwa na mtandao mkubwa wa reli nchini kuunganisha makao makuu ya mikoa yetu. Aidha, nasisitiza umuhimu wa barabara katika uchumi na maendeleo ya kijamii, miundombinu hii inategemeana. Pia naishukuru Serikali kwa ujenzi unaoendelea wa barabara ya Minyingu – Babati – Singida na mpango unaoendelea kati ya Babati na Dodoma hadi Iringa.

Kwa upande wa barabara vijijini, Serikali Kuu isaidie katika maeneo ya ujenzi wa madaraja makubwa. Aidha, naomba barabara zifuatazo zipandishwe hadhi kuwa za mkoa ambazo ni Duduje – Sharmo – Riroda – Bonga, Matufa – Mamire – Balapo – Haraa na Dareda – Dohom – Kirusix – Vibao vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifikirie kuwasidia posho/maslahi Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji kwani wanafanya kazi nzuri sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ni nzuri sana na ninaunga mkono asilimia mia moja.

Nimefurahi sana kwa Bajeti hii kuweka kipaumbele kwenye kilimo na miundombinu kwani mazao ya wakulima tatizo kubwa ilikuwa ni jinsi ya kusafirisha mazao hayo kwa sababu barabara ni mbovu na madaraja kwa wakulima wa kawaida mazao yao yalikuwa na bei ya chini sana. Walikuwa wanalanguliwa sana.

Nashukuru sana jimboni kwangu barabara nyingi zimelimwa na kuboreshwa sana hii ni pamoja na ujenzi wa madaraja. Pia ujenzi wa uwanja wa ndege wa Ilembula nao ninashukuru sana kwani uko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA*. Hivyo naomba Serikali iniongezee fedha uwanja huo ukamilike.

Kuna daraja kubwa na Wangutwa/Mzimbazi Njombe lenye thamani shilingi milioni 102 daraja hilo limekamilika, napongeza sana Serikali ila naomba tutengewe Bajeti ya barabara zinazounganisha daraja hilo la wananchi lililokuwa linawatesa na limesaidia vijiji vingi.

Kuna mambo mengi sana naishukuru sana Serikali kwa uboreshaji kwenye sekta za elimu, afya, kilimo, maji, miundombinu na huduma zingine za jamii. Naishukuru sana Serikali pamoja na taasisi za kidini.

Kwa upande wa mambo ya Kitaifa, kwa kuwa tatizo la Dar es Salaam juu ya msongamano linahusu Bajeti ya Serikali, ushauri wangu ni kwamba ili kupunguza msongamano ni vizuri mji wetu huduma za muhimu kama vile mabenki na huduma zingine ziwe nje ya mji na magari makubwa yasiruhusiwe kwenda mjini yaani katikati ya jiji na magari mengine madogo madogo yatozwe ushuru wa barabara na yapangiwe muda maalum na kuwepo magari makubwa ya usafiri wa umma na tuimarishe usafiri wa majini na reli zinazoingia mjini hasa Dar es Salaam.

**MHE. DR. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti ya 2010/2011. Kwanza kabisa, natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Katibu wake, Manaibu wote wawili na Watendaji na viongozi wote ngazi mbalimbali waliowezesha bajeti hii ya 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kufuatana na vipaumbele ambavyo vimelengwa na bajeti hii ya mwaka 2010/2011, imelenga na itamnufanisha mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 75 ya wananchi wanaishi vijijini na wanategemea kilimo. Wananchi hawa ni wazalishaji wakubwa wa mazao yote, mifugo, samaki na nyuki (asali). Uchumi wa Tanzania ili ukue unategemea kilimo na hasa kilimo

cha mapinduzi, Kilimo Kwanza zaidi ya mazao (70%) yanazalishwa na wanawake. Kwa hiyo, kwa kutenga shilingi bilioni 903.8 ongezeko la asilimia 35.5 itasaidia sana kuinua kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba mkakati uwepo wa kufikisha vocha na mbolea kwa wakulima na kwa wakati muafaka. Mikoa mingi kwa sasa wanavuna, hasa Mikoa ya Kusini. Kwanza wananchi wanaishukuru Serikali kwa mbolea ya ruzuku, lakini iwafikie kuanzia mwezi wa Nane. Wakati huu ni wa kuvuna, kwa hiyo, wananchi wanakuwa na hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufanikiwe katika kilimo, utafiti pia umepewa kipaumbele. Hili ni jambo zuri kwa watafiti na kwa wakulima. Pia nasisitiza kwamba licha ya kufanya tafiti nyingi za mbegu bora, pia tafiti ndogo zipewe kipaumbele. Tafiti hizi zifanyike mahali pote kwa wakulima. Wakulima wanapata mavuno kidogo, wakati mwingine kutokana na matatizo ya udongo, uchunguzi wa udongo utasaidia sana kujua ni mbolea gani inatakiwa na kwa kiasi gani na kwa zao gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imelenga kipaumbele cha kuimarisha benki ya wanawake, na kuanzisha Benki ya Wakulima ili kumlenga mwanachi wa kawaida na hasa mwanamke. Naomba mikakati izingatie kuanzisha matawi ya benki Mikoani hadi Wilayani ambapo kuna walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki hizi zitakapokuwa na matawi Mikoani na Wilayani, zitasaidia sana wanawake na wananchi wengine hasa katika kilimo na ujasiriamali, biashara ndogondogo, na uchumi wa nchi yetu utakua kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu, hasa ujenzi na ukarabati wa barabara, kipaumbele hiki ni kizuri muhimu sana kwa wananchi. Ili kuwa na maendeleo au kuleta maendeleo, lazima tuwe na barabara safi na bora. Asilimia kubwa barabara zote zikitengenezwa na kupitika kwa mwaka mzima wananchi watafurahia maendeleo haya na ukweli, bajeti itakuwa imewalenga kikweli. Mikakati iwekwe kutengeneza barabara hasa za kwenda mashambani. Hii itasaidia kukuza uchumi wa nchi yetu na kuinua kipato cha mwananchi hasa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, klilimo, barabara pamoja na masoko ya mazao ya kilimo yaliyo wazi yatasaidia sana kukuza uchumi wetu. Kwa hiyo, kama kipaumbele cha bajeti kilivyo, mikakati iwekwe katika maeneo hayo ili kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia bajeti hii, kwa mfano, barabara ya Ifakara – Mlimba (Morogoro – Kilombero), barabara ya Morogoro (Mjini) - Kisaki (Morogoro vijijini) na Barabara ya Lupiro – Malinyo (Ulanga) zikitengenezwa na kupitika kwa urahisi kwa wakati wote, wananchi wataweza kuinua kipata chao na uchumi wetu utakua. Barabara itasiaidia katika usafirishaji wa mazao na biashara nyingine kwa urahisi kutoka kwa wakulima mpaka sokoni kwa walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi sana kwa upande wa umeme kama kipaumbele kilivyo. Tuzidi kulenga sana katika kupelekea na kueneza umeme vijijini. Hii itasaidia pia katika uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo na hasa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mboga, matunda na maziwa. Jambo la kujali gesi asilia kwa kutoongeza kodi itasaidia hasa kulinda mazingira ambayo binadamu anaharibu sana kwa kutafuta nishati ya kuni.

Mwisho kabisa, natoa shukurani zangu kwa wanawake wa Morogoro walioniwezesha kuwa mmoja wapo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti ya 2010/2011.

**MHE. PROF. PHELEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, niligusia maeneo ambayo kama yatatiliwa mkazo kwa Serikali kuyawezesha yatachangia uchumi wa Taifa kwa asilimia kubwa. Maeneo hayo ni uvuvi na kilimo cha umwagiliaji.

Maeneo haya niliyotolea ushauri namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake wazingatie ushauri niliotoa, nilisahau kutoa tamko la kuunga mkono, sasa natamka rasmi kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampa hongera Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Fedha kwa bajeti ambayo inaonesha mabadiliko makubwa na matumaini mema ya mwelekeo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie juu ya viongozi wenzetu, Wenyeviti wa vitongoji na vijiji. Ni ukweli usiopingika kuwa viongozi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, kwani hawana hata kipato chochote ambacho kinaweza hata kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku. Ingekuwa vyema kama Wizara ingetenga angalau kifungu kidogo tu ili kiwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kuhusu kodi ya vijana wetu wanaotumia pikipiki kwa ajili ya kujiajiri. Ingekuwa jambo la busara kama Serikali ingefuta kodi kabisa ili wajipatie kipato kidogo cha kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu punguzo la kodi ya mfanyakazi. Ni kweli kwamba punguzo hilo lililoongezwa halimsaidii chochote mtumishi huyu kuendesha maisha yake ya kila siku. Naomba Wizara ijaribu kutimiza kwa upya punguzo hili, kwani halikidhi kabisa haja ya mfanyakazi Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kidogo kuhusu Mkoa wa Dar es Salaam. Ni ukweli usiopingika kuwa barabara nyingi za mjini Dar es Salaam ni mbaya kabisa tena hazifai na kwa kuwa ni uso wa nchi yetu, inatia aibu kubwa mno. Hivyo,

naiomba Serikali itengeneze barabara zote ndogo ndogo ili kurahisisha usafiri wa ndani kwa ndani, lakini pia kufanya Mji wa Dar es Salaam kuwa na sura nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme juu ya barabara ya Singida kuelekea Mwanza na Nairobi, imechukua muda mrefu sana kwa matengenezo ya lami. Serikali iweke macho yake mawili ili kuhakikisha barabara hii inakamilika mapema kabla ya uchaguzi.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nami napenda kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Fedha – Mheshimiwa Mkulo pamoja na Manaibu wake, Mheshimiwa Omar Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari kwa utendaji wao makini na kutolewa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu inaonekana ni tatizo, kwani eneo kubwa la mapato tunalipa msamaha mfano kutoa msamaha kwa makampuni ya madini ambayo yalifunga mkataba wao Julai 1, 2009. Kwa maoni yangu, kuwasamehe kodi hawa wachimbaji madini ambao baadhi yao wana mikataba ya miaka mingi hivi hatuoni kama ni kuikosesha mapato nchi yetu, hivyo basi, ni bora kungetoza kodi walau kiasi kuliko kutoa msamaha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa ushauri wangu kuwa tozo la ongezeko la pikipiki sioni kuwa ni vizuri kwani unapoongeza tozo ni ukweli ulio wazi kuwa hizo pikipiki kama zitaongezwa kodi basi mwathirika ni mwananchi ni lazima kodi ya mtumiaji wa mwisho itapanda na watu walio wengi washindwa kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ibuni njia nyingine na sio kila siku kodi yetu kuelekezwa kwenye ushuru wa magari, pombe, soda na sigara. Pia naiomba Serikali ifute ile asilimia tano ya tozo la *TRA* kuwaachia, mimi naona kuwa ni kikwazo kwa wafanyabiashara, kwani sasa imekua ni kutozwa kodi tu hawajali hiki ni nini, hata kama utoe maelezo haisaidii, wanachojali ni kutoza wazidi kiwango ili wapate ile asilimia tano. Naiomba Serikali kufuta hili na pesa yote iingie katika mfuko wa Serikali na wao wapate mgao kama wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii, Serikali imemsahau kabisa mvuvi katika msamaha wa kodi. Mvuvi hayumo kabisa, sio kwa nyavu, injini, wala zana yoyote ya uvuvi. Huu ni ubaguzi ulio wazi, kwani wavuvi nao ni Watanzania, ni haki yao ya msingi kuvua. Tunaomba muwatazame. Pia tunaomba pamoja na kusema mmeboresha huduma ya afya, lakini mtambue kuwa adha ya wahudumu vifaa na dawa ni kubwa sana tena sana, Watanzania hawa ni watu wanyonge na hasa watu wa vijijini, kwani wana majengo bila madaktari wala vitendea kazi. Hii ni kuipa Serikali aibu wanawake kuzalia chini hadi mchangani, njiani. Ni bora bajeti ya mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano itengwe na isichanganywe na bajeti ya Wizara, kwani kuna fununu kuwa

mafungu huhama na kufanya kazi nyingine. Hivyo, ni bora bajeti hii ya wajawazito ingejitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ni kwamba, wingi wa Shule za Kata, sio ubora wa elimu. Hivyo basi, Watanzania tunahitaji elimu bora na sio bora elimu. Hivyo basi, tunaiomba Serikali kuzitazama upya Shule za Kata ambazo zinainua elimu za watoto wa Watanzania wasio na uwezo wa kuwapeleka watoto wao katika shule za kulipia. Ahsante.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa kazi kubwa walizofanya mpaka kukamilika kwa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hotuba kwa kusema kwamba kwa kweli bajeti hii sio nzuri hata kidogo, kwa sababu haijamsaidia mwanachi mwenye kipatao cha chini. Vile vile imekuja wakati mgumu wa kuelekea katika uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini ni sekta kubwa ya uzalishaji, lakini Serikali inapata kipato kidogo sana. Hii inatokana na usimamizi mbovu wa Serikali, faida kubwa wanapata wawekezaji wageni na kupata utajiri na kuwaacha Watanzania kuwa maskini. Kwa hiyo, sasa kuna haja ili tume ya Jaji Bomani iwezeshwe iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameitikia wito wa Kilimo Kwanza. Sasa Serikali iwapatie mikopo na mfuko wa pembejeo ili wapate zana za kilimo, mbolea, pembejeo wataalamu wa kutosha ili waweze kuzalisha mazao kwa wingi; barabara ziboreshwe ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kupeleka kwenye masoko ili wasinyonywe na wajanja na vilevile Benki za Wakulima zianzishwe kwa haraka ili wapate kuhifadhi fedha zao wapate mikopo waondokane na matatizo ya kushambuliwa na majambazi baada ya kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Kama huna afya bora huwezi kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, hospitali zetu, Vituo vya Afya viboreshwe na kupatiwa vitendea kazi, madawa na vilevile Waganga wetu, Wahudumu, Manesi, waangaliwe na waboreshewe maslahi yao ili waepuke kupokea rushwa au kutoa lugha chafu kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bandari zetu ziboreshwe ili uchumi wetu uzidi kukua kwa sababu ukiangalia wafanyabiashara wengi wanatumia Bandari ya Mombasa kwa kukwepa msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam ni ndogo sana, inahitaji ipanuliwe. Bandari ya Tanga inahitaji ijengwe ili uchumi wetu ukue na wafanyabiashara wasipate usumbufu.

Baada ya mchango huu, nawatakia kila la kheri katika utendaji kazi zenu. Amina.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Wizara na Serikali yote kwa juhudi kubwa inayoifanya katika kutekeleza mipango na malengo, Dira ya Taifa na kutekeleza ilani ya CCM 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mapendekezo yangu kwa Wizara kwamba Serikali iibue vyanzo vipya vya mapato zikiwemo kodi ndogo ndogo ambazo haziwezi kuwa kero kwa mwananchi wa kawaida kama kodi za nyumba za kupanga (ambazo mpangaji hulipa kiasi cha Sh. 50,000/= kwa mwaka, tozo iwe Sh. 5,000/= na kodi za maduka ya biashara ambayo hutoza Sh. 100,000/= kwa mwezi, tozo iwe Sh.10,000/= kwa mwaka au kodi nyingine ambazo hutozwa na madalali wa viwanja na nyumba za matumizi mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kupata kiasi kikubwa ambacho kitaweza kutoa huduma mbalimbali za kijamii kwa kuwa madalali wengi hunufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na kutoza tozo la udalali. Naishauri Serikali ijihusishe kwa kutambua eneo hili ambalo lina vyanzo vingi vya mapatao, lakini halipewe umuhimu unaostahili. Kuna maeneo kama ya kuuziana magari, kuuziana mashamba kuuziana viwanja, kukodi nyumba/ vyumba vya biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kodi inayotokana na uharibifu wa mazingira, katika kuboresha mazingira na usafi wa jiji la Dar es Salaam na miji mingine Serikali ingeainisha kodi ambayo itahusu mazingira *(Carborn Tax)* kwa kutoza vyombo kama meli, boti, treni, ndege, magari makubwa na madogo viwanda mashine na mitambo ambayo inatoa moshi kwa kutoza kiasi kidogo sana kama Sh. 50,000/= kwa vyombo vikubwa na kiasi cha Sh.10,000/= kwa magari madogo na mitambo midogo na kiasi hiki kitozwe kwa kila mwaka. Kwa kufanya hivi, Serikali itaweza kupata chanzo kipya cha mapato, kwa takwimu ya magari yote nchini meli kubwa na ndogo zinazoingia hapa nchini, viwanda vyote na mashine na kadhalika. Ni kiasi kikubwa sana ambacho kitabadilisha mazingira, usafi wa majiji yetu na kupanda miti kwa wingi hapa nchini na hasa katika mikusanyiko yenye msongamano wa magari, viwanda ambavyo huzalisha moshi mwingi na kuharibu hali ya hewa.

Kuhusu usalama barabarani, nashauri itungwe sheria mpya ambayo itakuwa kali kwa kutoza faini kubwa ili kunusuru ajali za mara kwa mara na pia madereva wasiojali sheria waache kuharibu miundombinu ya wapitao kwa miguu, *(pavement)* na alama za barabara kung'olewa kwa ajali.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri. Mchango wangu utajikita katika maeneo yenye kuchochea uchumi kwa haraka.

Kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara kwa kuondoa kodi ya *VAT* kwa wakulima wa miwa wanaposafirisha miwa yao kutoka mashambani kwenda katika viwanda. Lakini kuchochea kilimo chini ya mpango wa kilimo kwanza hakuwezi kufanikiwa kwa kusambaza fedha za kuendeleza kilimo kisiasa bila kuzingatia fursa zilizopo katika Mikoa kama Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma na Morogoro. Mikoa hii iwe *breadbasket* ya nchi nzima, siyo suala la upendeleo, ni kwa sababu ya Mikoa hii kuwa na ardhi nzuri, mvua za uhakika, hali ya hewa safi kwa mazao muhimu kama mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma mpango wa maendeleo wa mwaka 2010/2011 katika sekta ya barabara, mtazamo wangu ni kuwa barabara pia zinajengwa kisiasa kuliko kufuata uchumi wa eneo ambalo barabara hizo zinakwenda. Nina uhakika baadhi ya barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami lakini mwisho wa siku kutakuwa hamna bidhaa ya kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hufuata bidhaa. Barabara ya Wilaya yangu ya Kidatu hadi Ifakara hadi Mlimba kiuchumi ni barabara muhimu sana. Kwa siku barabara hii hupitisha malori sio chini ya mia moja kwenda kubeba mazao kama mpunga, mahindi, ndizi na kadhalika.

Serikali iliahidi mwaka 2007 kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, lakini kwa fedha iliyotengwa, ahadi hii haitatekelezeka mwezi Februari. Waziri wa Miundombinu alitamka kwa wanachi wa Kijiji cha Mdugaji kuwa barabara ya Ifakara hadi Mlimba itajengwa kwa kiwango cha lami. Lakini katika mpango wa mwaka 2010/2011 sijaona barabara hii. Je, wananchi wataielewaje Serikali yao? Tayari maeneo hayo yamefunguka kiuchumi kwa kuanzishwa mashamba makubwa ya uwekezaji katika Kijiji cha Mgeta, Merera, Rupia, Ngalimira, Taweta na Uchindila, lakini pamoja na kufunguka huku mazao hayo hayatapata bei nzuri kama haina barabara nzuri za kubebea mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ina vyanzo viwili vya umeme, lakini wakazi wengi wa Wilaya hii wako gizani. Tuna *Kidatu Hydo Electric Power Plant* na *Kihansi Hydro Electric Power Plant*. Pamoja na mgodi wa umeme wa Kihansi kupitisha njia ya umeme kwenda *grid* ya Taifa vijiji ambavyo *pylons* hizi zinapita, viko gizani.

Kwa kweli mimi naona jambo hili siyo *fair* kwa wakazi wa Wilaya ya Kilombero, kwani wamebaki kuwa walinzi tu wa *Pylons* hizi.

Naomba Wizara, kama mpango wa dharura, iwafikirie wananchi wa Vijiji vya Udagaji, Chita, Chika JKT, Ikule, Mkangawalo, Mngeta, Mchombe, Njage, Mkingu, Namwawala, Mofu Idete, Ihanga, ifikiriwe kupata umeme ambao unazalishwa katika Wilaya yao.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa kuwasilisha Hotuba yao ya Bajeti ya mwaka huu 2010 kwa umakini kabisa na kuongeza matumaini makubwa kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Awamu ya Pili ya mradi wa ukombozi wa wanyonge, yaani MKUKUTA. Naiomba Wizara hii izingatie zaidi zile sehemu zote ambazo bado hazijafaidika na awamu ya kwanza ya MKUKUTA ili nao waweze kufaidikia na rasilimali hii ilioko nchini katika awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo kwanza ni sera ya Taifa. Ni vizuri kuelekeza nguvu zote kwenye sera hii kwani wakulima wetu wengi wanajaribu kulima bila uelewa, bali wanatumia uzoefu walionao tu. Naishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima wetu ili waendane na karne hii na kuweza kuwapatia zana za kisasa za kilimo na kuondokana na kilimo cha zamani ambacho ukweli hakijaleta manufaa ya kumkomboa mkulima huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi yetu ya Bandari hayaridhishi kukidhi haja na matumizi sahihi ya Bandari zetu na kama tutazitumia vizuri ni njia mojawapo ya kutuongezea mapato kwani kama tutawaridhisha wateja wetu wakubwa walio kwenye nchi za jirani ni njia moja nzuri na kubwa ya kuongeza mapato hapa nchini ili tuanze kuondokana na matumizi ya Bandari moja, kwani ukiritimba wa Bandari ya Dar es Salaam ni chanzo kikubwa cha kupunguza mapato ambayo tungelitekeleza majukumu yetu kwa ufasaha zaidi, basi tungeondokana na utegemezi katika Bajeti yetu kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** Maeneo ya kutazamwa upya ili serikali ipate kodi ni kama ifuatavyo:-

*Bureau de change eg. western Union Money transfer, money gram* katika benki zetu za biashara na kadhalika. *Eg.* Ukiwapelekea *dollar* wanazibadilisha kwa shilingi na baadaye kuzipeleka kwa dola, huu ni unyonyaji wa wazi na hawaulizwi wanatoza tozo kubwa sana sina hakika iwapo *WF* inapata chochote.

(i) Biashara za kuzuri *(Beauty Saloon)* wanatoza fedha nyingi kwa usukaji, uoshaji nywele, upambaji maharusi hawaguswi. Hii ni kiasi gani serikali inapata kwa *saloon* zote nchini? Wawekewe hata *token.*

*(ii)* *Restaurants* nyingi zinafanya biashara za malaki kwa siku. Je Serikali/Halmashauri wanapata nini?

*(iii)* *Consulting forms* zichambuliwe mapato yao watoe kodi.

Naelewa kodi zozote zitakazotolewa katika i, ii, iii.

Zitawafikia wananchi wanaotumia bali naona nao waonwe katika kuchangia katika kodi.

2. Idara ya Uvuvi iangaliwe kwa huruma sana hii haisaidiwi hawapati nafuu yoyote si ya kupunguziana kodi, vipuri, *engine* na nyavu ili waweze kuvua vizuri na kuongeza mapato na hatimae kodi itaboreka.

3.Umuhimu wa kuipa kipaumbele reli yetu ili iweze kusaidia kuchangia uchumi wetu.

Hata mara moja haijatokezea sekta ikapewa fedha za kutosha za kufanya *overhaul* ya miundombinu yake, kuimarika kwa reli ndio unafuu na *survival* ya barabara zetu. Barabara inayojengwa kwa mamilioni ya shilingi baada ya miaka miwili ni lazima ifanyiwe *resurfacing* na kuziaba mashimo. Hivyo tutaendelea kuwa *donor-dependant.* Reli inapojengwa mara moja tu itachukua miaka kadha kabla ya kufanyiwa marekebisho, *unless* kuwe na ajali.

Mheshimiwa Spika, tutajikomboa kama tutawekeza katika reli.

4. Sasa bahari yetu itumike ipasavyo. *Deep sea fishing* ianze na serikali isikatae kuwa na hisa kwa makampuni makubwa ya Uvuvi. Wengi wanavua wanaharibu maliasili zetu, wana *process* samaki baharini na kuuza nje bila hata Serikali kujua. Lazima Serikali au chombo chake kifanye *monitoring* juu ya zile meli za Kigiriki zinazovua.

5. *Compressor* za samaki nazo zisitozwe ushuru kwani zinasaidia kutengeneza barafu na kuhifadhi samaki wavuvi nao waonwe!

6. Bado sijaona *efforts* za viongozi wanaosimamia mfuko wa JK na AK katika kumsaidia mnyonge. Mikopo mingi iliyotokana na mifuko hiyo kule Pemba haikuwasaidia walegwa. Fanyeni utafiti imetolewa kiupendeleo. Ni kwa kiasi gani tutamsaidia Mtanzania aweze kumiliki uchumi wa nchi yake, *efforts* za makusudi

zifanywe waweze kufanya kampeni ndogondogo na kubwa na waweze kumiliki hisa katika makampuni hayo.

Naelewa Serikali imejitahidi sana kuona namna bora ya kumsaidia Mtanzania ila umasikini wetu ndio uliotufanya tusipige hatua sana. Sasa tupate jibu kwa kusimamia vyema maliasili zetu za madini, misitu na bahari ili navyo vichangie uchumi wetu.

**MHE. MWINCHOUM ABDULRAHMAN MSOMI:** Mhe Spika, Awali ya yote naipongeza Wizara hii chini ya usimamizi wa Waziri wao Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Naibu Mawaziri wao kwa kazi kubwa waliyoifanya ya uchambuzi na hatimaye kufika kuwasilisha taarifa hii / hotuba hii Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na maamuzi yaliyochukuliwa na Serikali katika kuamua hatua zifuatazo:-

1. Kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba wanazoishi wazee wenye umri zaidi ya miaka sitini ambao hali zao za kiuchumi haziwawezeshi kulipa kodi hiyo baada ya kuthibitishwa katika serikali za mitaa kuwa kweli hana uwezo wa kulipia kodi husika.

Mheshimiwa Spika, Jambo niliwahi kuiomba Serikali kuliangalia kama walivyotoa upendeleo maalum kwa wenye umri wa miaka sitini katika sekta ya Afya. Nimefarijika kwa Serikali kuliona kwamba ni jambo muhimu na kulitolea maamuzi katika Bajeti hii ya serikali ya mwaka 2010/2011.

Vile vile niliwahi kutoa rai kwa serikali katika michango yangu hapa Bungeni kwamba tuazimie kubadilisha/kusitisha kwa muda ulipaji kodi kwa mabasi yote makubwa yatakayoingia kutoka nje ya nchi Jijini Dar es salaam.

Naipoingeza Serikali pia kwa kuliona hili na kuamua sasa kutoa misamaha hiyo kwa muda ili kulikomboa Jiji kiusafiri na kuondosha msongamano wa mabasi ya Daladala *(Hiace).*

Mheshimiwa Spika, Suala la umuhimu ambalo Serikali haina budi kilitupia jicho la huruma ni juu ya misamaha ya kodi ya zana za uvuvi ikiwa ni pamoja na mashine za boti za uvuvi, nyavu, mishipi na vyombo vyenyewe vya uvuvi leseni zote zinazohusiana na uvuvi. Aidha hatuna budi kushajiisha/kuhamasisha wawekezaji wa sekta ya uvuvi kujenga viwanda vya kusindika samaki katika ukanda wa Mtwara – Dar es salaam ili kuwawezesha wavuvi kupata soko la uhakika katika ukanda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvuvi wa kamba wadogo*(Prawns)* una tija sana hivyo serikali haina budi kutoa kipaumbele katika uvuvi wa aina hii kwa kutenga fedha za kutosha zitakazotumika kuwekeza ufugaji wa samaki kamba hao kwa kuweka miundo mbinu kutoa elimu na mafunzo kwa vitendo hasa kataka maeneo ya wilaya ya Rufiji na

Mafia. Kamba hawa *(Prawns)* kimataifa wana soko kubwa sana. Tusipuuzie hilo (Mkakati uwekwe).

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Daraja la Kigamboni lipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) hivyo ni mpango wa kitaifa. Serikali haitoi msukumo wa kutosha ni vyema tukalishughulikia kwa wakati unaostahili ili mradi huo uendane na mradi wa ujenzi wa mji mpya wa kigamboni.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia ili kuisadia sekta ya uvuvi ni busara hatua zichukuliwe kuanzishwa Bodi ya Uvuvi ambayo naamini kama watateuliwa Wajumbe wenye ujuzi na uzoefu wa sekta hii na kufanya kazi ipasavyo sekta ya uvuvi italeta tija kubwa nchini. Wizara imejikita sana katika shughuli za mifugo hivyo kuathiri uvuvi.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa la kutwaa Ardhi ambazo zimemilikiwa na wanachi bila ya kujiandaa kulipa fidia za Ardhi hizo. Hili ni tatizo sugu sana katika jamii yetu ya Tanzania naiomba Serikali kuweka msimamo na maamuzi thabiti kwamba ardhi isichukuliwe bila ya kuwepo malipo ya fidia. Hii inalitukanisha Taifa. Viongozi wetu suala hili tulipatie ufumbuzi wa kudumu na kiongozi atakaeenda kinyume na maelekezo haya atachukuliwa hatua kali za kinidhamu. Ni kero hivyo miradi yote itakayopangwa iende sambamba na wajibu wa kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA OMAR KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kupongeza sana tena sana kwa hotuba nzuri. Kabla sijatoa mchango wangu naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, mimi nina machache ya kushauri na pia kuomba na kukumbusha.

Kwanza ni juu ya Bodi ya mazao mchanganyiko. Hii Bodi naomba sana ianze haraka sana ili na wakulima wa mazao hayo wafaidike wakiwemo wakulima wa nazi, muhogo, mahindi na kadhalika.

Pili kwenye suala la kilimo kwanza Serikali iandae pia soko la uhakika lakini pia kuwahamasisha wawekezji kufungua viwanda vya mazao yetu. Kwa mfano viwanda vya matunda, muhogo, nazi na hata mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, nashauri kukamilisha barabara kuu na hasa zile zilizokwisha anzwa lakini pia tuangalie sana barabara moja muhimu ya ufukweni maana yangu ni Bagamoyo –Saadani – Pangani hadi Tanga.

Hii barabara ni muhimu sana kwani barabara hii itaunganisha Dar es salaam na Mombasa na ni muhimu kwa ajili ya shughuli za utalii wa ufukweni.

Jambo jingine ambalo naishauri serikali kuhakikisha Gati la Mafia na kiwanja cha ndege cha Mafia navyo vinakamilika, sio tu kwa huduma za wananchi wa mafia, lakini pia kuendeleza utalii ule ule wa fukwe zetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kuna vitu vidogo vidogo tunavisahau nami naona ni vizuri tukumbuke kuna vituo vya Afya na Zahanati bado vinahitaji wataalam. Kwa kweli baadhi ya majengo haya yanafikia kuchakaa haina wahudumu kabisa au wapo wachache. Wananchi wamefanya kazi nzuri wakishirikiana na serikali yao kujenga majengo haya.

Mheshimiwa Spika, juu ya umeme sio tu *LUKU* kwenye idara na Wizara za Serikali, mimi nashauri *LUKU* itufanyie haraka kwa watumiaji wote wa umeme. Ni muhimu sana kuondoa usumbufu kwa *TANESCO* na WATEJA.

Mheshimwa Spika, Mwisho kweli miradi ya *TASAF* mingi hairidhishi hata kidogo kuanzia kwenye ujenzi lakini hata ya jamii (Ufugaji, Uvuvi Na kadhalika. Miradi mingi inaonekana *value for money* haipo.

Nashukuru itoshe nakusema nakutakia kila la kheri kwenye utekelezaji wa Bajeti hii pia kukutakia kheri kwenye uchaguzi ujao. Mwenyezi mungu akujalie urudi au turudi sote, *AMEN.*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE . Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, asilimia 41% ya kodi zote zitakazokusanywa 2010/2011 zinatokea *Large Tax Payers Department* wakati huo huo gharama za kufanya biashara zinaongezeka na hivyo kuathiri shughuli za uchumi kwa 23% ya Bajeti ya kawaida itafuatiliwa na misaada / mikopo. Sio kweli kuwa hatutakopa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hii sio ishara nzuri. Serikalini iache mawazo ya kukopa katika mabenki badala yake:-

Punguza matumizi ya kawaida kwa kiwango kikubwa.

Kopa katika soko la Hisa ili ku-*finace Transimision lines za umeme issue infrastructure Bond.*

Makubaliano na suala la *Eurobond* lakini iwe ni kwa ajili ya Barabara na reli peke yake.

Miradi ya kuzalisha (Kufua) umeme iundiwe *Pension Funds.*

Serikali iuze hisa 25% za *zain* ili kupata mapatao mengine.

2. Misamaha ya kodi za mafuta kwa kampuni za madini itaua fungamanisho la sekta ya madini na sekta ya umeme na ile ya ujenzi. Hii inatokana na kuwa na mafuta haya

yanatumiwa kuzalisha umeme na kwa kuwa misamaha hii haifikii *contractors* wa ndani kupelekea makampuni ya madini kufanya *"owner minig" "Owner mining* inapoteza sana mapato ya serikali kwani kampuni hazitozwi kodi ya zuio*(withholding taxes on technical services)* hatua zifuatazo zichukuliwe:-

i. Tofauti katika *MDA, MINE development* na *commercial operations.*

*ii. Extend 15 Withholding Tax (WHT) on Technical Services to companies doing owner mining.* Hili ni muhimu sana ili kufungamanisha *sector* ya madini na sekta ya kujenzi na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.

3. *Controller and Auditor-General (CAG) shall audit 2009/2010 stimulus package.*

4. *One point two percent (1.2%) growth of mining sector is alarming.* Serikali ieleze wazi sababu za sekta hii kutoendeshwa inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina fedha za kutosha imetenga Bajeti ya 327 bilion kwenda Wizara ya Nishati na Madini.
Wizara ilitanganza *tender* ya kununua mitambo ya umeme *100MW* kwa Dar es Salaam na *60MW* kwa Mwanza kwa mradi huu pekee zitahitajika jumla ya T.sh.220 bilion ambazo Serikali haina. Kamati ya Bunge ya *POAC* iliagiza mifuko ya Hifadhi kuwekeza kwenye kufua umeme. Mifuko imekubali kuwekeza huko. Hii zabuni waichukue mifuko ya Hifadhi baada ya Serikali kutoa pesa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 95. Utekelezaji huu umesaidia Watanzania kupata huduma nyingi muhimu. Mfano, Maji safi, Barabara, Elimu Huduma ya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi hii nzuri aliyofanya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wetu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania naomba Watanzania wote tumlipe mema kwa kumpa kura za kishindo katika Uchaguzi Mkuu ujao wa tarehe 30 Oktoba, 2010 pamoja na wabunge na madiwani wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitawapongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Waziri Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii ambayo imejikita kumjali Mtanzania wa chini.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu Elimu ya Sekondari kutolewa bure. Napenda kuwapongeza wananchi wote wakiwemo wanawake kwa kushirikiana na Serikali yao na kujenga shule za Sekondari kwa kila Kata na Vijiji baadhi ili wanafunzi wengi waweze kupata elimu ya sekondari tofauti na miaka iliyopita. Wanafunzi walifaulu wengi bali nafasi zilikuwa chache kwa sababu shule za sekondari zilikuwa chache sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri serikali kupitia Bajeti hii kuwa elimu ya sekondari ianze kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu kujiunga na kidato cha kwanza waweze kwenda shule. Hii itasaidia shule nyingi zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikana na serikali kwani bado kuna kikwazo cha wanafunzi wengi kutokwenda shule kwa ajili ya wazazi kutokuwa na uwezo au kutukuwa na mwamko wa elimu.

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa kuwa elimu ya Sekondari ikitolewa bure shule nyingi zilizojengwa zitatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kudhibiti bei ya mafuta nchini. Napenda kutoa maoni yangu kuwa bado kuna tatizo kwa suala la mafuta *dizel*, *petrol* na kadhalika. kwani kuondoa kodi katika kusafirisha mazao kutoka shambani hadi kiwandani ni kumpa nafuu mkulima mkubwa na wawekezaji wakubwa bado wakulima wadogo wadogo ama wafanyabiashara wadogowadogo hawajanufaika kwani mafuta bei iko juu na saa hivi matumizi ya magari ni ya kawaida kabisa wala sio starehe ndio miundombinu ya Watanzania wengi.

Ninaishauri serikali kuwa sasa ni wakati muafaka biashara ya mafuta kuchukuliwa na serikali ili tuweze kudhibiti bei kwani watu binafsi hupandisha bei kila siku kwa kisingizio cha *VAT* (Serikali iwekeze kwenye mafuta) mbona serikali iliweza kuchukua shule za Mashirika ya Dini na hospotali na majengo ya watu binafsi kwa ajili ya maslahi na nchi yetu na serikali ilifanikiwa na kwa sasa nchi ina wasomi na wataalam wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kupanda kwa mishahara ya Wafanyakazi. ninapenda kuipongeza serikali kwa kupandisha mishahara ya wafanyakazi ingawa Mheshimiwa Waziri hakutaja kima cha chini ni shilingi ngapi au asilimia ngapi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, wakati anafanya majumuisho ataje kima cha chini ili wafanyakazi wafahamu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sasa ni riba kubwa kwa Mashirika na Benki zinazokopesha. Ninaipongeza serikali mabenki na Mashirika ambayo yamekuwa mstari wa mbele katika kuwakopesha wananchi wanaojitahidi kupambana na umasikini, bali kuna tatizo la riba iko juu sana katika taasisi zote zinazokopesha utaratibu ambao unampa uzito mwananchi kuomba mikopo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali kupunguza riba katika mikopo inayotolewa kwa wananchi ili wanajitahidi kuondokana na umasikini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Madiwani kupewa Mishahara, napenda kuipongeza serikali kwa kuwa tayari kushauriwa ni ukweli isiofichika kuwa waheshimiwa madiwani wamekuwa wadau wakubwa wa kuibua miradi ya maendeleo, kusimamia na kuchangia fedha na mali katika kutekeleza miradi ya maendeleo ingawa hawana posho nono ya mishahara na wapiga kura wao hawajui haya.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali sasa kuona umuhimu wa kuwapa madiwani mishahara na posho zilizo nono ili pale wnapoombwa kuchangia shughuli za maendeleo wasishindwe, kitendo ambacho huwa kinawadhalilisha sana kwa wapiga kura wao.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu matumizi ya umeme kwa watendaji wa Serikali na simu. Ninaipongeza serikali kwa kutambua matumizi ya simu na umeme na kutafuta njia ya kupunguza matumizi hayo kuwa ni kulipa kabla ya kutumia. Mimi ninaona kuwa hiyo sio dawa, ninaishauri serikali kuwa bora kuweka lengo la matumizi ni kiwango gani ili kila taasisi kutekeleza kiwango hicho sio zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho nirudie kuipongeza serikali kwa kazi kubwa iliyofanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, hususani sekta ya Elimu ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na kadhalika. Nashauri kuweka nembo yake Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumwenzi daima vizazi na vizazi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge orodha ya Waheshimiwa Wabunge tumeimaliza, sasa tunaingia orodha ya Mawaziri ambao pia wanapewa dakika kumi kwa sababu wanachangia tu, mwenye haki ya kujibu peke yake ni Waziri wa Fedha, naomba mjipange yale mambo mazito myajibu mapema. Nitaanza na Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko Mheshimiwa Mary Nagu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii baada ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi na ukanipa nafasi ya kwanza kabisa nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu wote wawili na watendaji wote kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuweza kuweka Hazina yetu vizuri na kuweka sera za kodi ambazo zimesaidia sana katika kujenga viwanda vyetu na zinaendelea kujenga viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa sababu mwaka huu ni mwaka ambao tunafikia tamati na niwashukuru wananchi, Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hanang’ kwa ushirikiano wa karibu sana walionipa katika kutekeleza Ilani ya uchaguzi. Wilaya yangu ambayo ni Jimbo langu, wananchi wote na viongozi wote na Chama cha Mapinduzi tunashirikiana kwa pamoja na kwa kutumia bajeti hii ya Serikali tumeweza kutekeleza mambo mengi ndani ya ilani na wananchi wa Wilaya ya Hanang’ ni mashahidi kwamba ilani imetekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba kutoa majibu ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge zilizohusu sekta ya viwanda biashara na masoko wakichangia hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda hautaniruhusu kujibu hoja zote hapa, hoja zitakazobakia zitajibiwa wakati Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko atakapowasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza inahusu kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kupunguza gharama za kufanya biashara na uwekezaji katika nchi yetu, vile vile Serikali irekebishe maeneo ya Sheria ya Ardhi, upatikanaji wa leseni ambapo Wizara yangu inahusika na upatikanaji wa leseni. Mazingira ya kufanya biashara si rahisi, gharama ni kubwa, pamoja na msukosuko wa uchumi duniani, ugumu wa kufanya biashara katika nchi yetu ni jambo ambalo limesababisha kuteremka kwa uwekezaji kutoka nje toka dola milioni mia saba arobaini na nne mwaka 2008 hadi dola milioni mia sita hamsini mwaka 2009 sawa na upungufu wa asilimia 14.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni Serikali yetu imekuwa ikitoa ahadi za kurekebisha hali hiyo lakini kila kukicha hali inazidi kuwa mbaya. Kupata leseni ya biashara Rwanda inachukua siku tatu, Tanzania katika makaratasi inatamkwa isizidi siku tano lakini hali halisi ni kuwa hata kujibiwa barua yako inaweza kuchukua mwezi na hii ni hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Damas Nakei Mbunge wa Babati Vijijini na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja ya kwanza, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba Wizara imeendelea na juhudi za kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kukamilisha taratibu za utekelezaji wa sheria mpya ya shughuli za usajili wa biashara. Ningependa wananchi wajue hapa katika Sheria mpya na hata pale sheria ilipokuwa ya zamani ilirekebishwa kwa wale wafanyabiashara wanaofanya biashara chini ya milioni 20, leseni inapatikana bure. Nina hakika hii ni hatua madhubuti ya kuweza kuwahamasisha Watanzania wafanye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia Wizara imeanza na uhamasishaji jamii juu ya utekelezaji wa sheria hiyo katika Halmashauri 16 kwa sababu tusingeweza kujitawanya na tukawa tumefanya kazi ipasavyo katika Wilaya zote za Tanzania. Kwa hiyo, tumeanza na Wilaya 16 ikiwemo Wilaya ya Tanga, Babati, Arusha, Moshi, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Temeke, Kinondoni, Ilala na Singida na kubakiwa na Halmashauri nane za Lindi, Mtwara – Mikindani, Pwani, Mbeya, Sumbawanga, Njombe, Iringa na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili linatarajiwa kutoa fursa ya kuainisha mafanikio na maendeleo yatakayohitaji maboresho na elimu kwa wafanyabiashara inatolewa kupitia Shirika letu la *SIDO* ambalo kwa kweli limefanyakazi kubwa sana kwa wajasiriamali wadogo na naamini kwamba *SIDO* imekuwa mkombozi wa Watanzania wanyonge na kwa hiyo, kuanzisha viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo.

Aidha, Wizara imekuwa ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI katika kufanya tathmini ya kutambua uwezo wa Halmashauri zilizoteuliwa ili kujenga uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na kukosekana kwa mfumo imara wa ufuatiliaji wa wawekezaji na wafanyabiashara wanaopewa leseni za uwekezaji pamoja na leseni za biashara. Vile vile ufinyu wa bajeti kwa ofisi za biashara za Halmashauri za Manispaa umeathiri uwezo wa kutoa elimu. Kwa hiyo, kutokana na hii bajeti finyu inakuwa inatoa elimu hiyo kwa kusuasua. Hata hivyo, kupitia bajeti ya mwaka huu ambayo ndiyo itaelekea kumalizia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi nina hakika tutaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara hasa kwa wafanyabiashara wetu wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa nijielekeze ni kwamba, Serikali iweke umuhimu mkubwa katika kuendeleza siyo tu elimu ya sayansi na teknolojia bali vile vile elimu ya biashara na ujasiriamali. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Kulingana na matamko ya sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo tayari vyuo mbalimbali vikiwemo hata Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Elimu ya Biashara, ambacho kiko chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara Masoko vimejumuisha kozi ya biashara na ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, *CBE* kwa kutumia mitaala yake mipya imeingiza somo la ujasiriamali katika ngazi zote za mafunzo ili kuwajengea wahitimu wake uwezo wa ujasiriamali na kuwapa mbinu mbalimbali za biashara. Tumeongeza idadi ya wanafunzi, nina hakika wanapohitimu hawatakwenda kufanyakazi maofisini bali watakuwa wajasiriamali wazuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, nitaendelea katika bajeti yangu kujibu hizi hoja ambazo sijazijibu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naomba Waheshimiwa Mawaziri kuhusu kushukuru wananchi wa Majimbo yenu, mtashukuru kwenye hotuba zenu. Hapa muingie kabisa kwenye biashara mliyoulizwa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo na hoja kadhaa ambazo ziligusa Wizara yangu katika mjadala. Sasa napenda kutumia nafasi hii kujibu zitakazobaki zitajibiwa wakati wa mjadala wa Wizara yangu.

Kulikuwa kuna hoja kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing)* ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Waheshimiwa Wabunge wengine. Katika kuzijibu nitajibu kwa pamoja sasa hivi Shirika la Taifa la Nyumba tunalifanyia mabadiliko makubwa ili litoke kuwa Shirika ambalo linajihusisha na kupangisha nyumba na kukusanya kodi kama ndiyo shughuli yenyewe ya shirika. Tunataka Shirika la Nyumba sasa liwe ni chombo cha kujenga nyumba nyingi kwa Watanzania hasa wa kipato cha chini na kipato cha kati na kuziuza ili Watanzania waweze kupata nyumba bora. Uwezo wanao, tunachotaka kufanya ni mabadiliko ili uwezo huo utumike kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumekwishapata Mkurugenzi Mkuu Mpya kama alivyosema Lucy Mayenga tumemtoa katika sekta binafsi ili tuchanganye uzoefu wa Serikali na uzoefu wa sekta binafsi tuweze kupata shirika ambalo litakuwa na uongozi thabiti. Vile vile tumepata Bodi mpya ya Wakurugenzi ambayo nayo tumechanganya watu kutoka Serikalini na pia sekta binafsi. Sasa hivi Muundo wa Shirika unatazamwa upya, Bodi inatazama muundo mpya wa Shirika ili likae kibiashara kuliko kukaa kama mpangishaji. Kwa hiyo, zile nafasi za Wakurugenzi wa Mikoa ambao walikuwa wanaitwa Wakurugenzi wa Matawi sasa watakuwa ni *original managers,* watakuwa na madaraka ya kubuni miradi ya ujenzi kuitafutia fedha na kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya wakurugenzi kuanzia Mkurugenzi Mkuu ni wakurugenzi wanaomsaidia, hazitakuwa ajira za kudumu zitakuwa za mkataba. Akifanya vizuri tutaongeza mkataba. Kama asipofanya vizuri basi tutatafuta Mtanzania mwingine mwenye uwezo. Kwa hiyo, hakuna mtu mwenye uhakika wa kazi ya kudumu, Mkurugenzi pale katika Shirika la Nyumba. Hili tumeweka ili wapate msukumo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi wakijua kwamba wakifanya vizuri tutaongeza mkataba. Wakifanya vibaya tutatafuta Mtanzania mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti inayokuja mwaka huu tutaona kwamba, wataanza sasa kujielekeza katika kujenga nyumba katika miji na katika Mikoa na kadri tunavyoendelea watajenga uwezo kwa kukopa katika vyombo vya fedha, watajenga na kuwauzia nyumba Watanzania. Kwa hiyo, Watanzania nataka niwahakikishie kwamba tuwe na subira, tuone jinsi shirika letu ambavyo litajibadilisha kutujengea nyumba nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba, je, wataanza kuuza lini nyumba zao, swali hili liliulizwa na Mheshimiwa Zungu. Kwanza niseme kwamba hawatauza nyumba zao zote, nyumba ambazo ziko katika maeneo mazuri kibiashara, zile baadhi watabaki nazo ili wazitumie kama dhamana ya mikopo na wapate fedha na kutujengea nyumba. Zingine watazibomoa wajenge kubwa zaidi zitakazowahudumia Watanzania wengi zaidi na kuwapatia mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyumba ambazo ziko katika maeneo ambapo kwa kweli hawapati faida. Yaani gharama za kuziendesha zile nyumba ni kubwa kuliko kile wanachokipata. Kwa hiyo, zile ndizo tunasema kwamba, wanaweza wakaziuza na

wanaziuza kwa mikopo na kabla ya kuziuza lazima kuna maandalizi ya kufanya, kwanza kuwajua hawa ni akina nani ,uwezo wa kulipwa ukoje, ni benki gani ziko tayari kuwakopesha ili waweze kununua hizo nyumba. Kwa hiyo, maandalizi hayo ndiyo yanayofanyika hivi sasa. Yakishakamilika basi nyumba za aina hiyo, zitauzwa kama Serikali tulivyoahidi mwaka jana. Hiyo ilikuwa ni kuhusu *National Housing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa ardhi, kuipangia matumizi bora na kumilikisha ardhi kwa wananchi ni hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Hamad Rashid na wengine. Ardhi tuliyonayo ukiondoa ile ardhi yenye maji ni kilomita za mraba karibu 888,000. Katika ardhi yote hiyo ambayo imeshapimwa ikapangiwa matumizi na kumilikishwa ni asilimia mbili, nyingine yote bado haijapimwa wala kupangiwa matumizi wala kumilikishwa na ndio moja ya chanzo cha migogoro ya ardhi hapa nchini kwa sababu ardhi yetu kubwa hatujaipima, hatujaipangia matumizi bora ya ardhi, hatujaimilikisha. Ndio changamoto kubwa katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu hasa katika Hotuba ya Waziri wa Fedha ya Hali ya Uchumi, alipokuwa anataja maeneo ya kipaumbele katika bajeti hii na sekta ya ardhi ilitajwa kwamba ni eneo la kipaumbele. Hili kwa mara ya kwanza tangu tupate uhuru kuiweka sekta ya ardhi kama moja ya sekta za kipaumbele. Huko nyuma tulikuwa tunaona ardhi ni sekta ambayo ipo tu kama haiwezi kuwekewa bajeti. Nashukuru sasa kwamba tumetambua hali hii na mwaka huu wa fedha tutakaposoma bajeti mtaona kuna ongezeko la bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakachofanya mwaka huu wa fedha ni kujiandaa kufanya maandalizi ya kupima ardhi yetu. Kufanya maandalizi hayo kwanza ni kwa kupata watalaam. Katika sekta ambayo ina watalaam wachache sana katika Halmashauri ni sekta ya ardhi. Kuna upungufu karibu asilimia 70 ya watalaam hawapo. Mtapimaje ardhi kama hakuna watalaam wa kupima. Kwa hiyo, tunajiandaa katika bajeti hii tuhakikishe katika Halmashauri zetu watalaam wanakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Wizara hii tunajiandaa kwa vifaa vya kupimia ardhi. Utapimaje ardhi kama vifaa vyenyewe hakuna? Hizi *GPS, total session* kama hazipo. Ni bajeti ya kuandaa kuweka mazingira ya kuanza kupima ardhi. Kwa hiyo, watalaam wataajiriwa katika Halmashauri, nadhani TAMISEMI na Halmashauri za Wilaya na Miji tumeshazungumza nao, wameshaona umuhimu huu, watatoa ajira, tutaanza kununua vifaa vya kupima ili bajeti zinazokuja sasa tuanze kupima kwa kasi kabisa vijijini ili wanavijiji na wenyewe mashamba yao yapimwe wapate hati miliki, wazitumie kama dhamana kupata mikopo. Vile vile na mijini ili Miji yetu iweze ikajengwa kwa mpangilio ulio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bajeti zinazofuata na katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tutakwenda kuinadi mwezi Oktoba, jambo moja kubwa litakaloonekana mle ni kuwahakikishia Watanzania kwamba kama CCM itaendelea kuwa madarakani moja ya mipango yao sasa ni kupima ardhi, kuwamilikisha, kuwaondoa kwenye misingi kupitia ardhi ambayo Mwenyezi Mungu ametupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la kurekebisha Sheria za Ardhi ili ziambatane na hali ya sasa hasa tunapoingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hili nalo tutalifanya, ile mianya ambayo inaweza ikafanya wageni wakapata ardhi yetu kwa urahisi tuweze kuiziba na Watanzania wanufaike na ardhi yao kuliko wageni ambao wanaweza wakapata ardhi kinyemela kwa sababu sheria yetu bado haijakaza sawasawa. Sasa hivi inasema tu kila mgeni mwekezaji atapata ardhi. Sasa mwekezaji anaweza kuja wala haisemi hata ukomo, mwekezaji atapata zaidi. Kwa hiyo, hii ni mianya ambayo iko katika sheria zetu tutazirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante nashukuru. Kama nilivyosema Waheshimiwa Mawaziri muingie moja kwa moja kwenye hoja. Salam zingine mtatoa kwenye hotuba zenu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Pili, naomba nikubaliane na mwongozo wako kwamba nitawashukuru wananchi wa Rungwe Mashariki baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Umeshawashukuru tayari.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naomba niende moja kwa moja katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza wakati wa mjadala wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha zinazonihusu sasa. Ni mbili nazo zimeulizwa na Mheshimiwa Philemon Mikol Sarungi, Mbunge wa Rorya na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed Mbunge wa Chonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi ameisisitizia Serikali kwamba katika sekta ya kilimo, fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo, anasema angalau asilimia 25 ziende kwenye sekta ndogo ya mwagiliaji. Sasa naomba nimtaarifu Mheshimiwa Sarungi na Waheshimiwa Wabunge kwamba asilimia 75 ya fedha zote za *program* ya kuendeleza sekta ya kilimo *(ASDP) Agricultural Sector Development Programme* ambazo ni trilioni 2.4 kwa miaka saba kuanzia mwaka 2005/2006 mpaka 2012/2013, asilimia 75 ya fedha zote zinakwenda kwenye sekta ya umwagiliaji. Fedha zote ni trilioni 2.4 kwa miaka saba. Kwa hiyo, asilimia 75 ya zote hizi ni fedha zinatengwa kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, naomba vile vile kumtaarifu kwamba ili zifike kwa wakulima na kwa kiwango kikubwa, mbali na fedha zinazotengwa kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya *DADPs* ambapo huwa wanaandaa miradi ambayo baada ya kuandaliwa miradi inaweza ikatengewa fedha za ziada kutoka kwenye Mfuko wa Kitaifa ambao ni Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji wa Wilaya, Serikali imeona kiwango ilichokiweka kwa *scheme* moja kupata fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji wa Wilaya kilikuwa

chini, kilikuwa ni shilingi milioni 500. Kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali imeongeza kiwango hicho sasa kitakuwa milioni 800 kwa *scheme* moja. Hili ni ongezeko kubwa ambalo lote linalenga katika kusaidia wakulima katika ngazi ya Wilaya kwenye maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kauli mbiu ya Kitaifa sasa ni Kilimo Kwanza. Lakini hakuna kilimo bila maji unaweza kuwa na kilimo bila mbolea lakini huwezi kuwa na kilimo bila maji. Kwa hiyo, nasema kauli mbiu ni kilimo kwanza, lakini kwanza kabisa ni maji. Nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni lile ambalo tumeombwa na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed tuelezee mkulima ananufaika vipi na kilimo cha umwagiliaji? Faida ni nyingi lakini kubwa zaidi ni ongezeko la uzalishaji. Kwa mfano, ukilima kilimo cha umwagiliaji mpunga unaweza ukaongeza uzalishaji kutoka tani 1.8 kwa hekta moja mpaka kufika zaidi ya tani 5. Hili ni ongezeko kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitunguu unaweza ukaongeza kutoka tani 13 kwa hekta mpaka tani 26, nyanya tani tano mpaka tani 18, mahindi unaweza ukaongeza kutoka tani moja mpaka nne. Nasema kilimo cha umwagiliaji ni mkombozi wa Mtanzania, ni mkombozi wa mwananchi. Lakini kuna faida nyingine vile vile ongezeko la kipato cha mkulima. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote kipato kimeongezeka sana katika *scheme* za umwagiliaji. Inabidi uende *scheme* yoyote tu, chagua uende utembelee *scheme* yoyote. Mimi nachagua *scheme* moja ya Igomelo ambao wale mnaopita kwenda Mbeya mnaweza mkafika Igawa pale mnachepuka kidogo tu dakika tano mnafika kwenye *scheme* ya Igomelo. Pale mtaona maajabu, *scheme* ile imesaidia sana katika kukuza Mji wa Igawa, utajiri na maendeleo unayaona yako wazi, hukuti nyumba za nyasi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia *power tiller* kama vile ni kitu kipya, lakini kwa maeneo ya Igomelo miaka mitatu iliyopita *power tiller* ilikuwa pale, ukifika katika ile *scheme* hicho ni kitu cha kawaida. Zote hizi ni *power tillers* za wakulima, wananchi bila msaada wowote ule. Sasa unaweza kutaja maeneo mengine. Wale ambao mmepita *lower Moshi Scheme, scheme* ya Itumbiko huko Kibondo, kila mahali, penye umwagiliaji nasema kilimo cha Umwagiliaji kitakuwa ndiyo mkombozi wa Watanzania kwa maana ya kuipatia nchi chakula cha kutosha na kwa usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia matumizi ya mbolea yameongezeka kwa sababu sasa unaweza ukapeleka huduma kwa wakulima ambao wanalima pamoja katika *scheme* kwa urahisi zaidi, unaweza kutoa ushauri kwa urahisi, ushauri wa kilimo. Unaweza ukafanya majaribio ya utafiti wa mbegu bora katika eneo kama hilo, ndio maana kwa kweli mambo yamekuwa mazuri katika hizo *scheme* na fedha nyingi hata katika bajeti ya

sasa kama nitakavyoeleza katika bajeti yangu ni kwamba zimewekezwa katika umwagiliaji na itakuwa bora kuliko ilivyokuwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mawili mengine mengi yalizungumzwa kuhusu kero ya maji, hilo nitalipatia nafasi maalum nitakapojibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati nitakapokuwa nawasilisha hoja yangu. Nakushukuru sana. Ahsante sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii kwa kutoa maelezo mafupi juu ya hoja ambazo zimezungumzwa hapa. Nitapenda kutoa majibu haya kwa jumla isipokuwa pale ambapo nitalazimika kutaja aliyesema. Kwa upande mmoja kumekuwa na mjadala wa jumla juu ya ukuaji wa uchumi au ukuaji wa sekta ya kilimo kwamba inakuwa kidogo. Kwa mfano, kwa mwaka huu tunaoumaliza kwa taarifa ya uchumi, kilimo kimekuwa kwa asilimia 3.2 na takwimu hiyo ikachukuliwa ikawa *amplified* ikaonekana kwamba ndio jibu la wastani la kukuwa kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema tu kwamba kilimo kimekuwa kwa asilimia ndogo kwa sababu ya matatizo mengi ambayo yametokea ingawa sisi binaadam mara nyingi huwa tunasahau sana kwa muda mfupi lakini kilimo hiki kimekuwa kwa asilimia ndogo kwa sababu ya majanga yaliyotokea. Mwaka jana ndio ilikuwa mwaka ambao kilimo kilipata mtikisiko mkubwa sana kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani na bei za mazao karibu yote zilianguka. Bei ya pamba ilianguka sana mpaka Serikali tukalazimika kutumia fedha kumpatia mkulima ili aweze kutoka pale alipokuwa amefikishwa na soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo huwezi kutegemea ukuaji uwe wa ajabu sana. Kwa hiyo, mtikisiko wa uchumi duniani ulituathiri kwa kiwango kikubwa, lakini vile vile nchi yetu ilikabiliwa na ukame katika Mikoa mingi sana. Mikoa yote ya kaskazini ilibidi tuipatie chakula ambalo sio jambo la kawaida kwa Mikoa ya Kaskazini, lakini ilibidi tutumie zaidi ya tani laki moja na ishirini elfu na kitu kwa ajili ya kuwalisha watu sio kwa sababu hawataki kulima lakini mvua ilikuwa hamna. Kama alivyosema Profesa Mwandosya pembejeo namba moja ya kilimo ni maji, sasa kama maji unayoyategemea yanatoka juu na hayakuja, matokeo yake ni kwamba hakuna mazao yanayopatikana na katika mazingira haya huwezi kutegemea sekta ikue kwa asilimia nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka vile vile niseme kwamba nimesema mara nyingi kwamba kukua kwa sekta ya kilimo inategemea uwekezaji, sasa hivi tunategemea uwekezaji kutoka kwenye bajeti ya Serikali basi, ambapo hakuna nchi yoyote ambayo imekuza uzalishaji katika sekta hii ya kilimo kwa kutegemea bajeti ya Serikali peke yake na hili tumelijua ndio maana dhana ya kilimo kwanza, sasa tunazungumza juu ya kuanzisha benki ya kilimo. Kwa sababu nchi zote ambazo zimefanikiwa katika kukuza kilimo zimekuwa na *agricultural credit*, nenda nchi yoyote. Uende Vietnam, uende India lazima kuwepo na mfumo wa kukopesha ambao unamwezesha mkulima huyu aweze

kuondokana na ile *vicious circle* ili aweze kupata mtaji wa kuweza kuwekeza, anunue zana mpya, anunue pembejeo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu *advances* hizo hazipo ndio maana Serikali inalazimika kuingia na kuingiza mfumo ule wa ruzuku ya pembejeo. Kwa kweli tungeweza tukasema mkulima akope tu na anunue pembejeo anazohitaji. Lakini kwa sababu na mfumo wenyewe wa kukopesha nao haujawa tayari, basi unategemea bajeti ya Serikali na wengine wamesema bajeti hii bado haikidhi, jibu langu ni rahisi hakuna bajeti itakayokidhi, kwa sababu *resources* ni *limited* na matatizo yetu ni mengi tu, sasa tutafanyaje? Lazima watagawana kilichopo na kwa kuwa kwa mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 35 basi ndio tunashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwakani hatutakuwa na uchaguzi tena pengine mazingira ya mwakani yatakuwa tofauti na mwaka huu na tunategemea kwamba kunaweza kuwepo na ongezeko zuri zaidi kuliko tulilopata ili tuelekeze kufikia azimio la mapato la asilimia 10 ya bajeti ya Serikali. Nilitaka kulitolea maelezo ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed wa Chonga, ni kwamba miundombinu sio mizuri sana, kwa hiyo, ufikishaji wa pembejeo unakuwa na matatizo. Nakubaliana nae na juhudi zinafanyika kuendeleza miundombinu. Bodi ya Mazao Mchanganyiko imekwishapatiwa viongozi na sasa wanafanya kazi ya kuiunda upya ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea na ruzuku tutaendelea kuitoa kama tulivyokuwa tunaitoa miaka iliyopita na rafiki yangu Mheshimiwa Cheyo jana alikuwa anaisema sana hii kwamba ni wizi mtupu na akawa anaisema huku ananiangalia. Nataka kukubaliana naye kwamba kuna matatizo ya hapa na pale ambayo yatarekebishwa lakini mfumo ni safi, unamfikishia mkulima mahitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila hakuna mfumo ambao ni *perfect* duniani, yote ina matatizo, inarekebishwa tu. Serikali iwapatie wakulima mikopo ya Mfuko wa Pembejeo, tunaendelea kufanya hivyo kama ambavyo tunafanya wakati wote. Juu ya biashara ya ufuta ambayo ilisemwa na rafiki yangu Mheshimiwa Hamisi, watu wa Lindi wameamua kuingia kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani na huu mfumo unasimamiwa na sheria iliyotungwa na Bunge na wameshaona ukombozi wake kupitia biashara ya korosho. Sasa kama kuna mtu anataka kwenda kununua ufuta kule, aende tu anunue tu kwa njia ya mnada kupitia vyombo vya ushirika ambavyo vipo kule na vinafanya kazi yake, tunachotaka wote ni bei nzuri kwa mkulima. Mwisho wa yote ni hilo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri mambo mengine tutayatolea maelezo katika hotuba ya Wizara ambapo tutajibu mengine ambayo yamebakia kama yale ya kusema bajeti ya ulaji tu. Wizara yangu itaeleza kila senti itamfikiaje mkulima kwa njia ya huduma. Kwa sababu nusu ya bajeti ya Wizara ya Kilimo inapeleka mbolea kwa

mkulima mpaka kijijini kwake. Sasa kama huo nao ni ulaji sasa uwekezaji utakuwa upi na ulaji ni upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa hii nafasi na pili napenda niwashukuru sana Wabunge wengi ambao wamechangia hoja ya elimu katika hoja hii ya Waziri wa Fedha. Nitajitahidi kutoa maelezo katika maeneo matatu ambayo ni kupanua elimu katika ngazi zote, kuangalia upya ada za sekondari kama ilivyopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge wachache na *speed* ya ujenzi na ukamilishaji wa vyuo vya *VETA* katika Wilaya na Mikoa mbalimbali. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa elimu katika ngazi zote umefanyika kwa juhudi kubwa na ni vizuri Watanzania wote tukajivunia upanuzi huu kama ambavyo nitaueleza kwa kifupi katika mawasilisho haya. Katika ngazi ya elimu ya msingi, ukiangalia kigezo cha idadi ya wanafunzi ambao sasa wako shuleni, mwaka 2005 tulifikia idadi ya wanafunzi milioni sita na nusu waliokuwa wamesajiliwa katika shule za msingi. Hivi leo waliosajiliwa katika shule za msingi ni milioni nane mia nne arobaini na moja elfu na mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika,aidha katika elimu ya sekondari tulikuwa na shule za sekondari za umma na binafsi shule elfu moja mia saba ishirini na tano na hivi leo shule hizo zinafika elfu nne mia mbili hamsini na saba. Aidha, uandikishaji wa shule unaendelea kwa nguvu kabisa. Idadi ya wanafunzi wanaofaidika na elimu ya sekondari sasa imeongezeka kutoka laki tano ishirini na nne elfu mwaka 2005 na kufikia milioni moja mia nne sitini na tano elfu. Watu wengi wanaziona shule hizi ambazo zimeongezeka hasa hizi shule za Kata kama vile ni shule hohehahe sana ambazo mchango wake ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba katika mtihani wa kidato cha nne uliofanywa mwaka 2009, idadi ya vijana wote ambao walifaulu mtihani huo kwa kiwango cha daraja la kwanza mpaka la tatu na hivyo kustahili kuendelea na masomo katika ngazi ya kidato cha tano, asilimia 50.15 wametoka kwenye shule za Kata. Haya ni mafanikio makubwa sana ukilinganisha na ukweli kwamba asilimia 10 pekee ndio wametoka kwenye zile shule za zamani za Serikali na asilimia 38.9 wametoka kwenye shule za watu binafsi. Hakuna mtu ambaye hawezi kuona mchango huu mkubwa uliofanywa na upanuzi mkubwa wa elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu ya ufundi stadi, idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kusoma huko, waliongezeka kutoka sabini na nane elfu mia tano themanini na sita mwaka 2005 na kufikia laki moja ishirini na tano elfu mia tano thelathini na tisa mwaka 2009. Maelezo ya ujenzi katika vyuo hivi yatafuata hivi punde. Vyuo vikuu vyetu hapa nchini vilikuwa ishirini na nne mwaka 2005, hivi leo vyuo hivyo vimeongezeka na kufikia thelathini na nne. Wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo, wameongezeka

kuanzia hamsini na tano elfu mia tano ishirini na tisa na kufikia laki moja na kumi na saba elfu na sitini na nane mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ni vizuri nikataja na kulieleza Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa ujumla kwamba, katika kipindi hiki tumejenga na kukamilisha Chuo Kikuu kikubwa kuliko vyote katika Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara ambacho ni Chuo Kikuu cha Dodoma. Hivi leo chuo hicho kina wanafunzi kumi na saba elfu. Sambamba na upanuzi huu, changamoto nyingi zimetajwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini Serikali imezichukulia hatua changamoto hizi kwa kiasi kikubwa sana. Kwanza tumeongeza vyuo vya ualimu kutoka thelathini na nne vilivyokuwepo 2005 kufikia Vyuo vya Ualimu sabini na saba na wanafunzi wanaosomea ualimu katika vyuo hivyo wameongezeka kutoka kumi na nne elfu mpaka thelathini na tano elfu mia tisa tisini na nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa kila mwaka tunao uwezo wa kupeleka walimu watano katika kila shule ya sekondariya umma hapa nchini. Matatizo ambayo tunayo sasa ni makazi ya walimu wanapopelekwa katika shule hizo na tatizo hili tunalishughulikia katika kipindi hiki cha mwaka 2010/2011. Kwanza tunaanza utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari awamu ya pili kuanzia Julai 2010 ambao utahudumia mengi ya matatizo ambayo yamejitokeza katika ngazi hiyo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako hivi leo Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema kuwa, shule ya Kibungo haina walimu, kule Morogoro tulipelekea walimu sita katika mwaka huu wa fedha unaoisha. Lakini walimu wote wale waliondoka katika shule ile. Kwa sababu hiyo, tumechukua hatua nyingine ya kutengeneza barabara ya Kibungo Juu ili shule ile iweze kufikika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Watanzania wote kwamba tujitahidi na tujiandae kuwangoja walimu wapya ambao watakuja katika kila shule mwaka huu ili waweze kubaki katika maeneo yao. Kwa upande wa Serikali, kila hatua imechukuliwa ili kuhakikisha kwamba walimu wanabaki mashuleni ikiwa ni pamoja na kuwalipia stahili zao za ajira, pamoja na mishahara ya kwanza kuifikisha kule kabla walimu hawajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilitolewa pia pendekezo kwamba ada za shule za sekondari ziondolewe kwa sababu kuna wananchi wengi hawawezi kulipa shilingi elfu ishirini kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada hizi na mahitaji ya shule ni makubwa sana, kwa hivyo, kwa jinsi ambavyo uwezo wa Serikali unaongezeka tutaziangalia hatua kwa hatua na kuendelea kuangalia zile familia na watoto wanaotoka kwenye familia ambazo zina uwezo mdogo ili kuwasaidia na kuhakikisha kwamba mtoto wa Kitanzania anapata elimu ya sekondari kama ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imelenga. Aidha, katika 2010/2011, Serikali imeondoa ada za mitihani katika kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita kwa shule zote za umma. Muda ni mdogo na mengi ya ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge zitatolewa katika hoja yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa kifupi kwamba kuhusu *VETA*, Serikali imechukua hatua kubwa sana ya kupanua, kuboresha miundombinu na kuhakikisha kwamba kila Mkoa unapata chuo kikubwa au *centre* kubwa ya *VETA* hapa nchini. Katika kipindi hiki cha 2005 mpaka 2010, vyuo hivyo vimepanuliwa, vimewekewa vifaa vipya na kuongezewa walimu wa kutosha katika Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Tabora, katika eneo la Bulianghulu, katika Wilaya ya Mpanda, katika Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Singida.

Aidha, Serikali imejenga Chuo cha Hoteli na ukarimu katika Mlima wa Njiro pale Arusha. Tumeboresha na kuweka vifaa vipya katika *VETA* Mkoa wa Mtwara na Sumbawanga na chuo kipya cha *VETA* kimejengwa Oljoro, Songea na Chuo cha Mikumi kimeboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vyuo vipya vimejengwa Songea kama nilivyosema, Njiro kule Arusha, Sumbawanga na Singida. Nitaendelea kufafanua na kutoa maelezo juu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge katika hoja yangu tarehe 10 Julai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hoja iliyojitokeza ya kwanza ilikuwa ya Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum ambaye amesema kwamba vitendea kazi katika hospitali na vituo vya afya viongezwe ili adha ya akinamama kujifungua mchangani isiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama wanaodhuria kliniki, ni asilimia 95 na wanaojifungua kwa kweli sasa hivi ni asilimia 52 tu kwa saababu ya changamoto mbalimbali. Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2010/2011, kupitia Bohari ya Madawa, itanunua na kusambaza vifaa kwa ajili ya akina mama wajawazito kujifungua yaani *delivery packs.* Vifaa hivyo watapewa akina mama wajawazito watakapohudhuria kliniki ya mwisho kabla ya kujifungua ili waende navyo katika vituo vya kutolea huduma za afya wakati wa kujifungua pale ambapo hakuna *delivery kits.* Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa wameagizwa na wanatakiwa kuhakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya, vina *delivery kits* na *delivery packs* kwa ajili ya akina mama wajawazito kujifungua. Hivyo, Waganga Wakuu wote tumewakumbusha na wanatakiwa kulitekeleza suala hili na tunachokisema hapa ni kwamba akina mama sasa waende kliniki ili waweze kupatiwa hivi vifaa ili waweze kupata huduma nzuri watakapokuwa wanajifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imechangiwa na Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na Mheshimiwa Dunstan Mkapa, ni kwamba Vituo vya Afya na Zahanati havina watalaam wa kutosha na majengo yanachakaa kwa maana hiyo Serikali ilikumbuke suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inaendelea kupanga Watalaam wa Afya kulingana na vibali ambavyo vinatolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kila Halmashauri na Taasisi zenye mahitaji hayo. Hili linaenda sambamba na kuongeza udahili kama tulivyokuwa tukisema katika Vituo vya kufundishia vya Afya ili kuongeza wahitimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika suala ujenzi wa majengo mapya na ukarabati wa majengo yaliyochakaa ya vituo vya huduma ya afya, unaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha katika Mpango mzima wa Maendeleo ya Afya na Msingi lakini pia fedha za maendeleo zinaenda katika Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Mheshimiwa Mgana Msindai ambaye alizungumzia kwamba kila Zahanati Waganga wapatikane ili waweze kutoa huduma. Kama nilivyosema, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inaendelea na utekelezaji wake wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi ambao ulianza mwaka 2007 mpaka mwaka 2017 ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na Zahanati na kila Kata inakuwa na Kituo cha Afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa watalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imejitokeza ni ya Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum ambaye amesema kwamba *CCBRT* haifanyi kazi kama hospitali ya Mkoa, ijengwe hospitali inayofanana na Muhimbili. Aidha, wagonjwa hupewa ahadi yaani *appointment* kwa muda mrefu ili kumwona Daktari Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mzima wa kuimarisha huduma za afya na kuongeza wataalam katika hospitali za Manispaa za Dar es Salaam, utapunguza msongamano na ahadi za muda mrefu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kwa hiyo, tutakapoboresha, ikawa na wataalam wengi, suala la *appointment* au ahadi zitakuwa fupi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile hospitali ya *CCRBT* huwa imepangwa na inatengewa fedha katika mpango mzima katika kuimarisha hospitali zote ili iweze kuwa Hospitali ya Rufaa kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, suala la kuitaka Hospitali ya *CCRBT* kujengwa ili iwe kama Muhimbili, haitawezekana. Kwa sababu Muhimbili yenyewe ni hospitali ya Rufaa ya Taifa, kwa hiyo, hatuwezi tukaijenga *CCRBT* ikafanana na Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, alisema kwamba vyandarua vyenye viatilifu vitolewe bure kwa akina mama wanaojifungua. Serikali inatoa vyandarua bila malipo kwa watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano. Aidha, vyandarua vinatolewa kwa Mfumo wa Hati Punguzo ambapo wanalipa shilingi 500 kwa akina mama wajawazito. Ni kweli nakubaliana naye, kadri tunavyoendelea tutaboresha ili tuweze kuona kwamba hata hao wanaolipa shilingi 500 hawalipi. Lakini vile vile kupitia pesa ya *Global Fund*, sasa hivi tunao mpango ambapo kila kaya watapata vyandarua.

Nashauri akina mama waende kujifungulia hospitali lakini pia waende kliniki ili waweze kupatiwa vyandarua lakini pia na watoto wao waweze kupatiwa vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho iliyojitokeza ni ya Mheshimiwa Mussa Azan Zungu ambaye alisema kwamba Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam kupewa hadhi ya Hospitali za Mikoa hasa katika mgao wa dawa. Ni kweli kabisa kutokana na idadi ya watu wanaohudumiwa katika Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam, Wizara imekuwa ikiliangalia hili ili kama ilivyo kwa wenzetu Polisi kuwa na Ofisi za Mkoa katika Manispaa hizi na sisi tunaangalia utaratibu wa kuweza kuwa na Ofisi za Kimkoa kwa upande wa Afya katika kila Manispaa za Dar es Salaam. Lakini vile vile tutakapokuwa tunafanya hivi basi tutahakikisha dawa za kutosheleza katika ngazi ya Kimkoa zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo yaliyokuwa yamejitokeza, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naungana na wenzangu kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu Mawaziri pamoja na timu yake kwa ujumla, kwa hotuba yao ambayo inatupa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kuchangia katika kuunga mkono hoja hii baadhi ya masuala ambayo yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini kama walivyosema wenzangu, maelezo ya kina yatatolewa tutakapokuwa tunawasilisha makadirio ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi, tunauzingatia kuhusu Sekta za Nishati na Madini. La pili, ni hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani, hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, napenda kutoa ufafanuzi kwanza wa ujumla kuhusu uimarishaji wa huduma ya umeme nchini kwa maana ya suala la uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Lakini pia Kambi ya Upinzani ilitoa changamoto kwa nini leo tunavyoongea ni asilimia 14 tu ya Watanzania ndiyo wamefikia huduma hii ya umeme badala ya kuwa zaidi ya hapo. Napenda tu kusema kwamba juhudi zimefanyika na yako mengi yanaendelea lakini kikubwa ni kwamba katika kipindi hiki tumebadilisha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 ambayo sasa inatoa fursa kwa sekta binafsi kusaidiana na juhudi za Serikali katika kuongeza huduma ya umeme kwa maana ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Lakini pia kwa kipindi hiki kuanzia mwaka 2005 mpaka sasa, tunafahamu Mamlaka ya Udhibiti wa masuala ya Maji na Nishati *(EWURA)* ilianzishwa ambayo inasimamia masuala ya nishati na maji. Lakini pia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* ni chombo chetu ambacho nacho kilianzishwa na kimekuwa kikifanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilishangazwa na kutoona juhudi za Serikali, kwa nini Serikali haijihusishi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuzihamasisha kuweza kuwekeza katika Sekta ya Nishati. Sipendi kusema kwa hisia lakini naamini kwamba Mheshimiwa wakati anawasilisha taarifa yake kwa niaba ya Kambi ya Upinzani alikuwa anafahamu kinachoendelea Serikalini kwamba kati ya mambo ambayo Serikali imekuwa ikiyafanya kwa kushirikiana na Taasisi nyingine ni kuishirikisha hii mifuko na mazungumzo yanaendelea, stadi zimeshaanza kufanywa. Tungekuwa tunafanya mtihani, tungesema kwamba Mheshimiwa Muwasilishaji kwa niaba ya Kambi ya Upinzani alikuwa na taarifa ambazo zili-*leak* upande wa Serikali, lakini nasema ni jambo ambalo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine ambalo napenda kulitolea ufafanuzi. Kuna hoja ilitolewa kwamba Mkuranga gesi nyingi imepatikana lakini Serikali inajielekeza zaidi katika Mkoa Mtwara kujenga kiwanda cha mbolea. Sina hakika na hili lakini ninachotaka kusema ni kwamba ni suala la uelewa. Namheshimu sana Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa jinsi alivyo makini na utafiti lakini katika hili, angeongeza juhudi kidogo tu akapata taarifa za sasa Serikalini ili kuboresha hii taarifa, ingekuwa jambo jema sana. Angefahamu kwamba Mkuranga gesi iliyopatikana haijathibitishwa kuweza kuchimbwa kibiashara, kwa sasa inahitaji tathmini na uchorongaji wa visima zaidi ili kujiridhisha kama gesi iliyopatikana kweli inatosha kuchimbwa kwa manufaa ya biashara lakini kurudisha pia gharama za wachimbaji ama wawekezaji katika eneo hilo. Kinachofanyika sasa hivi ndiyo juhudi hiyo inaendelea, mwekezaji anaendelea, Kampuni ya Merodi Prom ya Ufaransa, kujiridhisha zaidi na hicho kilichopatikana kama kuna *reserve* zaidi ya hiyo iliyopatikana ambayo sasa itathibitisha kwamba uchimbaji ama uchorongaji kwa ajili ya kupata gesi zaidi unaweza kufanywa na hivyo kufungua fursa za uwekezaji mwingine kama viwanda vya mbolea na kadhalika. Kwa hiyo, hili suala lilikuwa ni suala la uelewa na tuko tayari kuendelea kutoa taarifa kupitia Bunge lako Tukufu, lakini pia kubadilishana mawazo zaidi na Kambi ya Upinzani kwa juhudi zinazoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umeme, kumekuwa na changamoto imetolewa, mawazo binafsi, hoja za Wabunge kwa niaba ya wananchi, tuongeze juhudi za kufikisha huduma za umeme katika sehemu mbalimbali. Katika hili, tuna mipango ya muda mfupi, tumekuwa tukisema tuna mipango ya muda mrefu, lakini pia tuna mpango wa muda wa kati. Kwa haraka haraka, katika mpango wa muda mfupi, tumekuwa tukisema kwamba sisi kati ya sasa mpaka mwaka 2012/2013 mpango wa muda mfupi, tunatarajia kuongeza kwenye gridi ya Taifa, megawati 900 na zinapatikanaje? Kiwira tunazalisha megawati 200 na utaratibu unaendelea wa kuhakikisha kwamba uwekezaji katika huu mradi unaendelea. Kinyerezi tuna megawati 240, Gesi ya Mnazi Bay kule Mtwara tuna megawati 300 lakini pia sasa hivi tunakamilisha ununuzi wa megawati 160 kwa ajili ya Dar es Salaam, megawati 100, Mwanza megawati 90. Sasa tunasema katika mpango wa muda mfupi, tutaongeza kwenye gridi ya Taifa, megawati 900. Hii ni habari ya kweli kwa sababu maandalizi yameshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, ni hivi karibuni tu tutatoa taarifa rasmi hapa, kuhusu utekelezaji wa miradi zaidi ya 40 katika

Mikoa 16 ya Tanzania ambayo sasa Wakandarasi wameshapatikana na taratibu zingine zinakamilishwa za kusainishiana mikataba ili waanze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema niliyoyasema hapa mwaka jana, wananchi watulie, waamini Serikali muda wote imekuwa inafanya juhudi za kuhakikisha kwamba huduma hizi zinawafikia. Tutatoa taarifa rasmi kwa kila kijiji, kwa kila Mkoa, kwa kila Wilaya, ni miradi gani itakayotekelezwa katika hiyo Mikoa 16, miradi zaidi 40. Waheshimiwa wengi hapa watanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *MCC* zabuni zimeshatangazwa, zinafunguliwa tarehe 1 mwezi wa saba, zilikuwa zifunguliwe mwezi wa sita lakini Makandarasi walioonyesha nia, waombaji wa hiyo kazi, baada ya kuzungukia Mikoa ambako itatekelezwa wakasema waongezewe mwezi mmoja wa kufanya tathmini ili wawasilishe taarifa zao. Kwa hiyo, nakubaliana kwamba miradi ya *MCC* Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Tanga na Mbeya, zabuni hiyo inafunguliwa mwezi wa saba ili sasa tuwapate Wakandarasi watakaokwenda kusogeza huduma zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala limeulizwa kuhusu viumbe ambavyo vinaonekana vinakwaza, vinachelewesha utekelezaji wa mradi wa Malagarasi. Tunasema sisi tunatekeleza miradi hii kwa kuzingatia itifaki zingine na makubaliano mengine ya Kimataifa. Limejitokeza jambo ambalo linakwaza kwa sasa kuanzisha mradi wa uzalishaji wa umeme pale kwenye maporomoko ya maji pale Malagarasi. Lakini tumekwishaongea na *MCC*, tunaangalia namna nyingine ya kufanya mradi huo utekelezwe bila kuathiri upatikanaji kwa umeme katika Mkoa wa Kigoma na hasa kwa kuzingatia jibu ambalo limetolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ambalo tunaamini kwamba Watanzania wamelipokea vizuri kupitia Bunge lako Tukufu kwamba Mkoa wa Kigoma sasa ahadi ya kufikisha umeme wa uhakika imeshakamilika na sasa tunapoongea hakuna mgawo wa umeme katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, nafahamu Wilaya ya Bukombe, uchungu ni mkubwa sana lakini tunafahamu katika baadhi ya sehemu za Mkoa wa Mwanza pamoja na Mkoa wa Arusha, tumeshakamilisha taratibu, tunadhani kati ya sasa na mwezi wa nane kutakuwa na hatua kubwa itakayofikiwa. Nitatoa taarifa wakati wa bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Makambako – Songea, tumeshamaliza kile ambacho kimetusumbua kwa muda mrefu mpaka Rudewa tumeshakamilisha hilo zoezi na tutawapa taarifa kwenye mradi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Songea Mjini, Mheshimiwa Dr. Nchimbi simwoni, Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pale tumesema kwa sababu mahitaji ya umeme Mkoa wa Ruvuma, hasa Mkoa wa Ruvuma, Mji wa Songea yanaongezeka kwa kasi, tumekubaliana kwamba tununue jenereta pale, zoezi la ununuzi linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakachuaji, juhudi zinaendelea. Maoni na ushauri wa Wabunge tunaupokea. Lakini juhudi zinazoendelea sasa hivi ni kwamba kuanzia mwezi wa nane, Mamlaka ya Udhibiti na Maji, wataanza kutumia vyombo vinavyoitwa mabaara zinazotembea, katika juhudi za kudhibiti uchakachuaji, lakini pia uagizaji mafuta ya pamoja tunatarajia utaanza mwezi wa tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya kodi imesemewa sana. Nafahamu Mheshimiwa Waziri wa Fedha atalisemea zaidi lakini hili lilikuwa la kiutaratibu. Tumerudisha ule utaratibu mwaka huu katika kujielekeza kwa hela ambayo tumekubali sisi kama nchi inayozingatia miongozo ya kisheria kwamba tuheshimu makubaliano tuliyonayo lakini bila kuathiri kile ambacho tunakikusudia. Kwa hivi utaratibu huu umerudishwa kwa makampuni ambayo yalikuwa na mikataba na mikataba ile imelindwa. Yale makubaliano ambayo tuliyafanya, sasa tukazungumze, tueleweshane kwamba ile mikataba ilipotolewa kipindi kile mazingira yale yanaendelea kutumika kwa sasa badala ya kuonekana kama ni Serikali inayolazimisha, tukasema tufuate utaratibu wa kuzingatia uongozi wa kisheria. Kwa hiyo, tunakwenda kujadili sasa. Haina maana kwamba hilo jambo limefungwa, hapana, hili tutakwenda kulijadili, tuone kama mazingira yameshabadilika na tunaamini kwamba katika maeneo fulani yameshabadilika, tutakuwa tunatoa moja baada ya lingine. Kwa hivyo, ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. Lakini pia tuwe na imani, Sheria mpya hii imetujengea mazingira ya kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Sanya, ametutahadharisha kwamba tusiingie katika suala la *uranium* bila kujiandaa. Kwa niaba ya Serikali, naomba nikuhakikishie kwamba Serikali hii imejiandaa vizuri katika kuwezesha uwezo wa ndani ya nchi lakini pia tunashirikiana na Taasisi za Kimataifa pamoja na chombo chetu Mheshimiwa Profesa Msola yupo hapa, ile Tume ya Mionzi Serikali ni kubwa tunajiandaa kuhakikisha kwamba uzalishaji wa madini ya *uranium* utakapoanza mwaka 2012 na sisi tusichelewe kuanzia hapo kuweza kunufaika mojawapo ni kuzalisha umeme. Ni jambo tunalolifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la transfoma, Mheshimiwa Dr. Mwakyembe tumezingatia. Ni taratibu zinafuatwa tu lakini tunafahamu kasi iliyokuwepo lakini tunalizingatia na wenzetu wa Miundombinu wanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme Lindi na Mtwara, Mheshimiwa Raynald Mrope, umeongelea kwa uchungu sana. Tunafahamu, lakini kikubwa ni kwamba lilikuwa ni suala la taratibu, *EWURA* wanakamilisha masuala ya kimsingi na wapo hatua za mwisho kabisa. Sitaki kusema ya ndani kwa sababu kwenye Wizara yangu yatasemwa lakini ni kwamba vile vikwazo ambavyo vilikuwepo, si vikwazo ilikuwa changamoto na tumefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu, wananchi wa Msimbati kule kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia, wananchi wa Newala na Nanyumbu pamoja na Tandahimba, wataanza kutumia umeme wa gesi asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Watanzania wana imani, umeme utawafikia kwa viwango vikubwa sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Pia nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa uwasilishaji nzuri wa hoja yake na pia Waheshimiwa Manaibu Waziri na Wataalam wa Wizara wote, Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kumwezesha Waziri wa Fedha kuwasilisha hoja hiyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba pia kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wale ambao katika kuchangia hoja hiyo, waligusia masuala ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa ufafanuzi wa ujumla katika maeneo yale ambayo yamegusiwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja hii katika masuala yanayohusiana na Wizara yangu ya Miundombinu na maeneo haya ni maeneo ya barabara, bandari, reli na viwanja vya ndege. Nitafanya kwa muhtasari kwa muda ule ambao nimepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la barabara, suala kubwa lilikuwa kwamba Serikali iboreshe miundombinu ya barabara nchini. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Hemed Mohamed, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Mgana Msindai pamoja na wengine kama nimewasahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, inatekeleza Programu ya miaka 10 ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi *(TSIP).* Mpango huu umeanza kutekelezwa mwaka 2007/2008 na utaendelea mpaka 2016/2017. Lengo la programu hii, ni kuimarisha miundombinu yote ya usafirishaji ikiwa ni barabara kuu, barabara za Mikoa, bandari, reli na viwanja vya ndege. Vile vile Serikali kupitia TAMISEMI, inaimarisha mtandao wa barabara za Wilaya kupitia mpango wake wa *Local Government Transport Programme (LGTP)* ili barabara hizi ziweze kupitika kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, *LGTP* imeanza kutekelezwa mwaka 2007 kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ya barabara za Dar-es-Salaam kwamba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba inatengeneza au inapanua mtandao wa zile barabara. Kwa hili niseme tu kwamba Serikali imeanzisha mradi wa kuboresha barabara za Jiji la Dar-es-Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Mradi huu umeanza mwaka wa fedha 2008/2009; kwa kuanzia, barabara zenye urefu wa kilometa 58 zitaboreshwa pamoja na ukarabati wa mtaro mkubwa wa maji kuanzia barabara ya Nyerere hadi barabara ya Uhuru. Kazi ya ujenzi imeanza katika barabara tatu ambazo ni *Jet Corner* hadi Vituka yenye urefu wa kilometa 12, *Ubungo Bus Terminal* - Maziwa -

Kigogo *Round About,* yenye urefu wa kilometa 6.4 na Kigogo *Round About* - Jangwani - Barabara ya Twiga, yenye urefu wa kilometa 2.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Meryce alihoji pia kuhusu barabara ya Singida - Mwanza na akasema kwamba imechukua mkuda mrefu sana. Naomba niseme kwamba barabara ya Singida – Mwanza, ni sehemu ya Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati. Ujenzi wa kiwango cha lami hivi sasa unaendelea katika sehemu ya Manyoni – Isuna, yenye urefu wa kilometa 54 na 34 zimeshamalizika, sasa hivi tunaendelea kumalizia kilometa 20. Ukamilishwaji huu tunategemea itakapofika mwezi Disemba mwaka 2010, sehemu hiyo ya Manyoni – Isuna itakuwa imekamilika. Kwa hivyo, Ukanda wote wa Kati, utakuwa umejengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Dar-es-Salaam kupitia hapa Dodoma kwenda Singida hadi kufikia Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara ya Mwanza – Singida – Babati – Arusha - Namanga, ujenzi wa ukanda wa Kaskazini Magharibi, upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Barabara kutoka Mwanza – Singida, sehemu hii yote imejengwa kwa kiwango cha lami. Sehemu ya Singida – Babati – Minjingu, yenye urefu wa kilometa 223, inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2012 na ujenzi wa sehemu ya Arusha – Namanga, yenye urefu wa kilometa 105, unaendelea na kazi inatarajiwa kukamilika mapema mwezi Julai mwakani 2011. Tunatarajia kazi zitakamilika kama ambavyo mikataba imeainisha na kusimamiwa na Wakala wa Ujenzi wa Barabara *(TANROADS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, amehoji sana kwamba barabara hizi zinakwenda kwenye maeneo muhimu ya kiuchumi hasa katika Jimbo lake, barabara ile ya Kidatu – Ifakara – Mlimba ni kwa nini haipati msukumo? Niseme tu kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hiyo kuu ya Kidatu – Mlimba na imechukua hatua mbalimbali za kuboresha barabara hii. Kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi, Serikali inaendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara kwa kiwango cha lami nyepesi kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, kupitia vifungu vya Barabara za Mikoa, Serikali imetenga fedha ili sehemu ya Ifakara - Mlimba ifanyiwe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Masuala mengine ya barabara nitayachanganua katika hoja yangu nitakapowasilisha ili iweze kujibu yale ambayo pia yameulizwa katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninapenda kulizungumzia katika hoja hii, ni bandari. Eneo hili limechangiwa na Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy na Mheshimiwa Herbert Mntangi na hoja kubwa ilikuwa ni kwamba bandari zetu ziboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, sasa imekamilisha Mpango Madhubuti wa Uendelezaji wa Bandari *(Port Master Plan),* kama hatua muhimu katika kubainisha mahitaji ya bandari zetu na namna ya kuziendeleza, ikiwemo bandari ya Dar-es-Salaam kuwa kivutio kwa wawekezaji na wasafirishaji wa mizigo. Mpango huu umeainisha miradi

itakayotekelezwa katika kipindi cha muda mfupi, kwa maana ya 2009 – 2011, muda wa kati kuanzia 2012 – 2018 na kipindi cha muda mrefu kuanzia 2019 na kuendelea hadi 2028 kwa bandari zote nchini katika mwambao wa bahari na zile zilizo katika maziwa. Kupitia mpango huu, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, imeshaanza utekelezaji wa upanuzi wa bandari ya Dar-es-Salaam, ikiwemo ujenzi wa magati mapya, gati namba 13 na 14 kwa ajili ya uchukuzi wa shehena za kontena. Usanifu wa magati haya mapya umekamilika na fedha kwa ajili ya ujenzi zimepatikana. Kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni uongezaji wa kina katika njia ya kuingilia bandarini, ili kuwezesha meli kubwa kuingia. Ujenzi wa kituo cha kupakulia mafuta na kuboresha magati namba 1 - 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Tanga, bandari hii haina uwezo wa kuhudumia meli kubwa kutokana na kina chake kuwa kifupi, kwa hiyo mpango uliopo ni wa kujenga bandari mpya eneo la Mwambani na hatua zimeshaanza kuchukuliwa kwa maana ya kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeshanunua eneo la ekari 180 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari mpya pale Mwambani. Ujenzi wa bandari hii, unalenga kwenda sambamba na kuendeleza Maeneo Muhimu ya Uchumi *(Export Processing Zone)*, ambapo mradi huu utaendana pamoja na *EPZ* ili kuweza kuhakikisha kwamba bandari hiyo tunaweza tukaitumia kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni reli. Katika eneo hili suala kubwa ni kwamba miundombinu yetu ya reli iboreshwe na kwamba bandari hizi ili ziweze kufanya kazi ni lazima miundombinu ya reli iwe ni ile ambayo inakidhi mahitaji makubwa ya kusafirisha bidhaa. Ni kweli kwamba ipo haja ya kuimarisha reli, kwa kuwa Tanzania inategemea kilimo kama uti wa mgongo, basi mali zake nyingine kama vile madini, zinahitaji usafiri wa reli na kwamba pato la nchi litaongezeka kwa kuhudumia nchi za jirani ambazo hazina bahari. Kwa kutambua umuhimu huo, tayari nimeshatayarisha mpango kabambe ambao unaoanisha nchi zote za Afrika Mashariki, kwa mtandao wa reli. Serikali ya Tanzania kwa upande wake, kwa kuanzia itatekeleza miradi miwili muhimu; moja ni ujenzi wa ile reli ya kuanzia Dar-es-Salaam – Isaka – Kigali na kutoka Keza (Tanzania) – Msombati (Burundi). Mpango huu upo katika ngazi ya mbali ya utekelezaji; upembuzi yakinifu umeshafanywa na sasa hivi Serikali hizi tatu zinajiandaa kwa mkakati wa usanifu ili kuweza kuijenga reli hii mapema iwezekanavyo. Lakini pia wakati huo huo kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda, Serikali hizi mbili zinafanya majadiliano kwa ajili ya kuandaa mradi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma, ambayo itaunganisha bandari hiyo ya Mwambani na Bandari ya Kampala kwa ajili ya kuhudumia nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni hoja kuhusu viwanja vya ndege. Hapa hoja iliyotolewa mahususi ni ya Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, kwa maana ya kiwanja cha ndege cha Mwanza. Labda niseme tu kwamba Serikali imejipanga vizuri kama vile katika *Port Master Plan,* kwa ajili ya bandari lakini pia kwa viwanja vya ndege. Hiki ambacho Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella amekizungumzia ni kimoja tu, lakini niseme kwamba vyote tunavishughulikia kwa ukamilifu wake ili kuhakikisha kwamba miundombinu ya usafiri wa anga inakuwa ni miundombinu ambayo

inakidhi haja ya usafiri. Serikali inatekeleza na inaendelea na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Katika mwaka huu wa fedha, zimetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo, maegesho ya ndege za mizigo, njia za viungo, barabara za ndani na mfumo wa maji safi na maji ya mvua, zimepangwa kuanza kwenye mwezi Oktoba mwaka huu 2010. Kazi hizo zitagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya *BADEA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema hoja nyingine nitazifafanua nitakapowasilisha hoja yangu, naomba kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mbili ambazo zinahusu Wizara ya Maliasili na Utalii. Hoja ya kwanza imetoka kwa Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru, ambayo inahusu Serikali idhibiti wanyama waharibifu, hasa ndovu. Naomba nitoe maelezo yafutayo. Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283, (iliyorekebishwa mwaka 2002), inaruhusu hatua zichukuliwe kwa wanyamapori wakali au waharibifu pindi watakapofanya uharibifu katika mali au kutishia maisha ya binadamu na hali kama ni mbaya pia sheria inaruhusu wauwawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa tatizo hili ni kubwa, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la wanyamapori nchini kote, kwa nia ya kuwaondolea kero wananchi na athari za wanyamapori. Baadhi ya hatua zinazochukuliwa ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pale taarifa inapotolewa tu kwenye vituo husika, Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori, hushiriki katika zoezi la kudhibiti wanyama hao wakali na waharibifu, kwa utendaji wa kawaida. Kazi hii hufanywa kwa kushirikiana kati ya Halmashauri za Wilaya na Wizara yangu, kwa kupitia Kanda za Kikosi Dhidi ya Ujangili, ambapo kanda hizi tunazo sehemu mbalimbali. Kwa upande wa Kusini mwa Tanzania, ikiwemo Tunduru, kuna ofisi ya Kikosi Dhidi ya Ujangili, Kanda ya Kusini Songea, ambapo ni mojawapo ya jukumu lao pamoja na kudhibiti wanyama waharibifu na wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni Halmashauri za Wilaya, zinapewa msaada wa kukabiliana na wanyama waharibifu na wanyama wakali kwa kugawiwa silaha na risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, elimu ya kutumia njia mbadala ya kuzuwia wanyamapori wanaovamia mashamba, kama vile kutumia vinyesi vya tembo vilivyochanganywa na pilipili, ambavyo huchomwa moto na moshi wake hutumika kuwafukuza wanyamapori, hususan ndovu. Mbinu hii imetumika na kuonesha mafanikio katika Wilaya za Kilwa, Liwale, Bunda na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana au kupunguza kero hizi za wanyapamapori waharibifu, kwa sasa Serikali inashirikiana na wadau wa kuhifadhi wanyama kutoka nchi mbalimbali kufanya utafiti kwa ajili ya kuangalia tuchukue hatua gani zaidi au njia ambazo zitakuwa ni za maana zaidi katika kukabiliana na tatizo hili.

Kwa hivi sasa, tunafanya utafiti katika mapori mawili kwenye vijiji ambavyo viko pembezoni mwa Pori la Akiba la *Selou*, lakini pia katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na mipakani katika hifadhi ya Amboseli kule Kenya. Tafiti hizi zitakapomalizika na zikigunduliwa kwamba zitafaa, tutazitawanya sehemu mbalimbali ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumefanya mkutano na wadau mbalimbali wanaohusika na uhifadhi katika kuangalia upya uhifadhi wa tembo. Mkutano huu tumeufanya mwaka huu 2010 na sasa tunaandaa mkakati mpya wa jinsi ya kuhifadhi tembo na kuangalia upya udhibiti wake utakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, hoja ilikuwa imetoka kwa Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza na lenyewe lilikuwa linasema kwamba Sekta ya Utalii haijatumika vizuri; kwa mfano maeneo ya zamani ya vivutio yafufuliwe. Wizara yangu, kwa kupitia Bodi ya Utalii, ilikuwa ikitangaza utalii kwa mpango mkakati ambao ulianzia mwaka 2006 na utaisha mwaka 2011 na kwa sababu mkakati huo unaisha mwaka 2011, sasa hivi tumejipanga upya, tunauangalia tena mkakati huu ili tuweze kuainisha mambo mapya zaidi ya kuweka katika mkakati mpya utakaokuwa ni wa 2011 mpaka 2016 pamoja na mambo mbalimbali mapya ya jinsi ya kutangaza utalii yataongezwa humo. Sasa hivi tayari mapendekezo yapo kwenye Bodi ya Utalii ili kuweza kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kupitia mpango huo ambao tukishauainisha, Wizara yangu itaendelea na kazi ya kuainisha na kufanya tathmini ya maeneo ya zamani yanayoweza kufufuliwa kama vivutio vya utalii. Kwa hivi sasa kuna baadhi ya maeneo ya zamani tayari tumeshaanza kuyafanyia kazi na matunda yake yanaonekana na mengine yako njiani karibu kumalizika, ikiwemo njia ya utumwa na njia ambayo ilikuwa ikitumika kwa ajili ya biashara ya ndovu enzi hizo za utumwa, hii tunaifufua. Lakini pia Boma la Wajerumani la Bagamoyo, tumeshaanza kulijenga na kulikarabati. Pia Ngome ya vita ya Majimaji, ipo tayari na tumeifanya ni mojawapo ya makumbusho na vivutio vingine vingi ndivyo hivyo ambavyo sasa vitaainishwa na tuweze kuviwekea mkakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia swali la mwisho lilikuwa linahusu vipepeo wa Muheza ambao Mheshimiwa Mntangi na lenyewe aliliongelea. Tumekubaliana na hilo wazo lake na nitatuma wataalamu ambao watakwenda Muheza kuwaona hawa vipepeo. Sambamba na hilo pia katika Sheria mpya ya Wanyamapori, Na.5 ya 2009, tutaitumia hiyo kuchukua hatua zitakazostahili kwa ajili ya hawa vipepeo wa Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale tuliotaka waweze kuanza kujibu hoja ya Waziri wa Fedha na Uchumi, wametosha. Kwa hiyo, mchana tunapenda Naibu Waziri na Waziri wa Fedha, waingie moja kwa moja kujibu hoja zile ambazo mmetoa na wakati huo huo, ninawasihi Waheshimiwa Wabunge wote, tuwepo saa 11.00 jioni, haya ni matakwa ya Kanuni zetu na pia ni matakwa ya Katiba.

Kanuni yetu ya 98(1) na (2), kwa sababu ya faida yetu sisi wenyewe, tuisome Kanuni hiyo. Kanuni ya 98 (1) inasema hivi:-

*"Mjadala juu ya Hotuba ya Bajeti utakapomalizika, Spika, atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 90(2)(b) yaKatiba."*

Kanuni ya 98(2) inasema:-

*"Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura za wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja,"*

Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba inasema hivyo, sasa msiniambie ninawatisha, ndio utaratibu wenyewe. Maana mtu anasema Naibu Spika, aliamua kututisha, sio kuwatisha, Ibara ya 90(2)(b) inasema:-

*"Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote, isipokuwa tu-*

*(a) ....*

*(b) Kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali."*

Sasa ndio maana tukifika katika kiwango hiki, ndio zile *Part Caucas* zinafanya kazi. Kwa mfano, hawa Wapinzani wamealikana saa 7.00, tukifika hapa watakubaliana wote wa-*walk out*, wata-*walk out,* wanaweza kukubaliana hivyo na nyie wa CCM, vivyo hivyo kama mnataka kuitetea Bajeti yenu ambayo ndio inahitimisha Ilani, ni lazima wote muwepo hapa. Kwa hiyo, ndio hicho tunachokisema. Hapa kwa ku-*walk out* kwa Wapinzani, sio tatizo na nyie wenyewe wa CCM mkitaka kuiangusha Serikali yenu, msiwepo hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndio maana saa 11.00 jioni kila Mbunge anapaswa, tena sio kwa kusema "nafikiri waliosema ndio wameshinda", aah! Kama Spika atakaa hapa, yeye atatoa uamuzi wa mwisho kama tumegongana, lakini suala la kugongana halipo. Kwa hiyo, ninawasihi Waheshimiwa Wabunge wa vyama vyote, saa 11.00 jioni tuje hapa tuweze kudhihirisha tumekubali bajeti au tumekataa kwa kupiga kura. Kwa hiyo, Mbunge yeyote asikosekane isipokuwa yule aliyeko hospitali.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sina matangazo mengine, tunamuachia Waziri wa Fedha na Uchumi, akaendelee kuboresha majibu yake. Lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote waliopata nafasi kuanza kujibu hoja zinazowahusu, kwa sababu mmemsaidia Waziri wa Fedha, aingie kwenye Sera ya Bajeti zaidi kuliko kuingia kwenye mambo ya sekta ambayo Waheshimiwa Mawaziri wamejibu na wakati wa Wizara zao tena wanaweza kuimarisha pale wanapofikiria kwamba hawakuimarisha vizuri.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.20 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Spika, alipositisha shughuli za Bunge mchana, tulikuwa tumemaliza kuwasikiliza Waheshimiwa Mawaziri, kwa hiyo, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hatimaye mtoa hoja. Kwa hiyo, sijui wamejipangaje lakini kwa pamoja wana dakika 70. Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, ana dakika zake 20 halafu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja dakika 50. Kwa utaratibu huo, basi naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aendelee.

**WABUNGE FULANI:** Dakika 60.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri nifafanue tu, uwe hapo hapo, kuna watu wanapiga kelele sijui sitini, arobaini, ni hivi, mtoa hoja ana dakika zake 60, mwingine yeyote ana dakika zake kumi kwa jinsi tulivyotengua, jumla ni 70. Nimewasiliana na Mheshimiwa Waziri Mtoa hoja, amechukua zake kumi, kampa Mheshimiwa Naibu Waziri ili ziwe hamsini, kwa hiyo, yeye kabaki na hamsini, ndiyo hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha mchana wa leo kuwa hapa pamoja nanyi ili kutekeleza majukumu ya Kitaifa ambayo tumewekewa. Lakini vilevile napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara mbili nyeti katika kipindi changu cha miaka mitano, namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wangu wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkullo, kwa kunilea na hadi hii leo tunahitimisha kipindi chetu cha miaka mitano, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mkullo, amekuwa ni mvumilivu, amekuwa ni muongozaji na hadi leo tumekuwa wachapaji kazi wazuri ndani ya Wizara ya Fedha, kwa msimamo wa Mheshimiwa Mkullo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, kwa kushirikiana nami katika kipindi chote cha miaka mitano, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na nawaomba tuendelee kushirikiania katika kipindi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiembe Samaki, kwa kuniteua na kunipa kura nyingi sana na hatimaye kuingia katika Bunge hili. Wamenivumilia kipindi chote ambacho niko Bungeni na sasa natarajia watanisaidia kuniwezesha tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia shukrani zangu, kwa kumshukuru mke wangu, Narman na watoto wangu wote, kwa msaada walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawaambia nawapenda sana na nitaendelea kuwapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, pia namuomba Mwenyezi Mungu, Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Sumari apone, aweze kurejea nchini ili aweze kuwatumikia vyema wapiga kura wake wa Jimbo la Meru na ninawaomba wapiga kura wa Jimbo la Meru, wamsaidie, wamuombee dua Mheshimiwa Sumari na wampe kura zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, nataka niseme tu kwamba, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, zilikuwa ni nyingi na kwa dakika ishirini ambazo nimepatiwa, nitajaribu kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja na hatimaye Waziri wangu, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, atamalizia zile hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wametutaka tutoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme, Serikali ni ile inayosikiliza maoni na ushauri kutoka kwa wananchi wake. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na imesikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Maoni yenu Waheshimiwa Wabunge yameshakuja, mengine tumeshayafanyia kazi, mengine mtayaona katika bajeti hii na mengi mtayaona katika bajeti zijazo, nalowaombeni Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono bajeti yetu, nchi ni yetu sote, tunataka maendeleo ndani ya nchi yetu. Maendeleo hayaji siku moja, ni mchakato hatimaye nchi yetu tutapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, nakuja sasa katika hoja ambazo Wabunge mbalimbali wametaka tuzitolee ufafanuzi. Hoja ya kwanza ambayo nataka kuitolea ufafanuzi, ni ile ambayo Wabunge wengi walitaka kuelewa uwiano uliopo sasa baina ya ukuaji uchumi na idadi ya watu na hatimaye Serikali tunafanyaje. Nataka niseme, watu ni rasilimali muhimu sana katika ukuaji wa uchumi lakini kwa hatua hii ambayo Watanzania tunakuza idadi ya watu, kwa kweli hatutapiga hatua katika miaka ya hivi karibuni, lazima Watanzania tuangalie idadi ya watu inavyokua. Leo hii, idadi ya watu ni kubwa. Mwaka jana nimeeleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ina nafasi yake katika ukuaji wa uchumi lakini mwananchi mmoja mmoja naye ana nafasi yake katika ukuaji wa uchumi hasa katika suala zima la idadi ya watu. Leo familia moja ina watoto watano mpaka sita, lazima ukuaji wetu wa uchumi hautaenda sambamba na idadi ya watu tulionao.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ni mingi katika eneo hili na nitajaribu kuitaja baadhi tu ya mikakati. Moja ambalo Serikali yetu inafanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunatoa msukumo zaidi katika elimu na hasa elimu ya sekondari kwa wasichana ili hatimaye wasichana waweze kusoma na wachelewe kuolewa na hatimaye wajue nafasi yao na idadi ya watoto ambao anaweza kuwazaa katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha familia ambayo *education level* yao iko juu zaidi, idadi ya watoto inakuwa ndogo na hasa unapokuja kutazama *education* ya mama. Kwa misingi hiyo, Serikali hii itahakikisha kwamba inatilia mkazo *education* ya wasichana ili hatimaye ongezeko la idadi ya watu liweze kwenda sambamba na idadi ya ukuaji wa uchumi. Vilevile mkakati mwingine wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunatoa elimu ya uzazi kwa umma au kwa vijana kuhusiana na *family planning* ili hatimaye tuweze kuzaa idadi ya watoto ambao tunaweza kuwahudumia. Leo hii Watanzania wengi tunazaa watoto ambao hatuwezi kuwahudumia na hatimaye tunakuwa na hili wimbi la umaskini ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambazo Serikali inazichukua, ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji hasa katika sekta ya kilimo na kuyaongezea thamani na hatimaye kuweza kusafirisha nje. Hii itatusaidia zaidi kuweza kukuza uchumi wetu kwa sababu asilimia 70 ya Watanzania wanajishughulisha na sekta ya kilimo. Vilevile mikakati ni kujenga miundombinu ambayo itarahisisha upatikanaji wa mazao kutoka katika sehemu ya uzalishaji hadi kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa idadi ya watu katika familia ni mzigo kwa familia yenyewe na kwa Taifa ndiyo maana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamepiga kelele kwamba bajeti yetu ya kawaida ni kubwa kuliko bajeti ya maendeleo. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, bajeti yetu ya kawaida itaendelea kuwa kubwa kwa misingi kwamba *population* yetu nayo ni kubwa, tukifikia hatua tukiweza kuidhibiti *population* yetu bajeti yetu ya kawaida inaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tulitakiwa kulifafanua, ni suala la kuwaelimisha wakulima juu ya upatikanaji wa mikopo na hasa wakulima wale wadogo wadogo. Nataka niseme tu kwamba asilimia 70 ya wananchi wetu wanategemea kilimo na sehemu kubwa ni wakulima wadogo wadogo. Suala la kuwaelimisha wakulima wadogo wadogo, ni muhimu sana kwa nchi yetu. Serikali imeanzisha Dirisha la Kilimo na lengo ni kuelekea katika kuwa na Benki ya Kilimo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema tuko mbioni katika kipindi kifupi nchi yetu itaanza kuwa na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa, Serikali imetenga fedha kwa mipango ufuatao na naomba Waheshimiwa Wabunge na wakulima waweze kunifahamu, asilimia 30 ya fedha ambazo ziko katika Dirisha la Kilimo, zimetengwa kwa ajili ya taasisi

zinazotoa mikopo midogo midogo yaani Benki za Jamii. Hii mikopo midogo midogo, itakwenda kwa wakulima wadogo lakini zimetengewa Benki za Jamii *(Community Bank)* ili ziweze kuwapa mikopo wakulima wadogo. Lakini vilevile asilimia 30 nyingine zimetengwa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika, *SACCOS*, vikundi vya wakulima wadogo wadogo vilivyosajiliwa, hii vilevile inakwenda kwa wakulima wadogo wadogo. Kwa maana nyingine tunaweza kusema kwamba asilimia 60 ya fedha zilizotengwa, zimetengwa kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo kupitia maeneo mbalimbali ya ukopeshaji. Lakini zote hizi ni katika kumsaidia mkulima, tunapomsaidia mkulima mdogo tunaweza tukazalisha kwa wingi na hatimaye tukaweza kusafirisha bidhaa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, riba tumesema haitazidi asilimia nane, ni kati ya asilimia tano mpaka asilimia nane, tofauti na mabenki ya biashara ambayo riba inaanza asilimia 16 mpaka asilimia 24 lengo letu ni kumsaidia mkulima mdogo mdogo. Majukumu yetu Waheshimiwa Wabunge ni kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wakulima wadogo wadogo katika maeneo yetu ili wachangamkie fursa hizi.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita, niliulizwa swali kutoka Mbozi, ninaimani kwamba wakulima wa Mbozi wakishirikiana na Mbunge wao, sasa watakuwa wamenifahamu jinsi ya kupata mikopo hii kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Dirisha hili liko wazi na sasa fedha zinaanza kutoka, tuchangamkie Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo iliulizwa na Waheshimiwa Wabunge, ni uwiano wa fedha za matumizi ya maendeleo umezidi kushuka dhidi ya fedha za matumizi ya kawaida. Nataka niseme tu, tunapotekeleza hii miradi ya maendeleo kwa wingi, narudia, tunapoitekeleza miradi yetu ya maendeleo kwa wingi, mfano mzuri *University of* Dodoma, utapokamilika mradi ule, lazima uingie kwenye shughuli za kawaida. Kwa hiyo, huu uwiano usitupe shida Waheshimiwa Wabunge, ndiyo hoja ya msingi ambayo inayotuonyesha kwamba tunatekeleza miradi mingi ya maendeleo, ikishamalizika, miradi mingi ya maendeleo inaingia ili iweze kuhudumiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo nataka nisema kwamba kitu muhimu cha kulinganisha na kukichunguza, bajeti yetu ya maendeleo ukilinganisha na pato letu la Taifa linakua au haikuwi? Hiki ndiyo kitu cha kuangalia sio kutazama maendeleo *vis-à-vis* kawaida huwezi kupata kitu unapotazama vitu hivyo viwili lakini tutazame bajeti yetu ya maendeleo *vis-à-vis our capital, GDP* inakuwa haikuwi. Ninataka nikupeni takwimu tu, mnamo mwaka 2007/2008, bajeti yetu ya maendeleo ilikuwa ni asilimia 7.6 ya *GDP*, mwaka 2009/2010 bajeti yetu ya maendeleo ilikuwa ni asilimia 9.1 ya *GDP*, mwaka huu wa bajeti, tunaouongelea sasa, bajeti yetu ya maendeleo ni asilimia 11, hii inaonyesha dhahiri kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba bajeti ya maendeleo inaongezeka kila mwaka ukilinganisha na *GDP* yetu. Hili tunalifanya na ndiyo maana nikasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi jamani ni Serikali makini, inaelewa nini inachokifanya na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge tunasema nyie poeni, mtusikilize sisi Mawaziri tunawaletea vitu kidogo kidogo, vingine kwenye vichwa vyenu baadaye muende kuwaelimisha wananchi wote, hawa wananchi ni wetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge walitaka ufafanuzi, ni Serikali ibuni vyanzo vipya vya mapato ili kupanua wingo. *This is a very complicated issue,* nataka niieleze kidogo Waheshimiwa Wabunge ili tufahamiane. Katika miaka ya nyuma, tulikuwa tuna kodi nyingi sana hapa. Sote kwa umoja wetu tukasema kwamba hizi kodi zinakwenda kwa mwananchi, tunamkomoa mwananchi, kwa hiyo, kodi zile tukazifuta, nyingine tukaziunganisha. Suala la kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, hapa halina msingi, hivi vyanzo ambavyo tunavyo, tumevi-*exhaust* kiasi gani? Huo ndio msingi.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na semina ya vitambulisho, wenzetu wakatuahidi kwamba vitaweza kutusaidia kwa kiwango kikubwa sana kukusanya mapato. Leo tunaolipa kodi ndani ya nchi hii, ni watu milioni moja na nusu, wakati wanaostahili ni watu milioni 14, ndio kusema Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekwenda haraka sana katika mchakato wa kuanzisha utaratibu huu**,** kila anayetakiwa kulipa kodi kwa mujibu wa stahili yake atalipa na kodi hii itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme moja, kuna watu ambao wanaharibu mazingira, hii kodi ya mazingira tunaanza kufikiria kwa kina kabisa mchakato wa kuanzisha kodi ya mazingira, ili wale ambao wanaharibu mazingira, waweze kuchangia katika kuyarudisha mazingira katika hali nzuri. Leo tunayaona magari hapa yanatembea yanatoa moshi, wanaharibu mazingira tu, sasa tunataka tuifikirie sana kodi hii na mchakato wake tumeshauanza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumziwa na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba *TRA* inazuia asilimia tano ya mapato yake ili iwe ni matumizi yake katika kutekeleza majukumu yake. Nataka niseme tu *TRA* hawana utaratibu huo, utaratibu wowote ule unaofanywa na *TRA* ni kwa mujibu wa sheria, ndani ya sheria iliyoanzisha *TRA*, hakuna kifungu hiki. *TRA* ina bajeti yake kama Wizara nyingine, inapeleka kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha ambaye yeye anaitazama akiona kubwa anapunguza, akiona anakubaliana nayo, anaikubali na mahesabu ya *TRA* yanakuwa *audited* na *CAG*. Kwa hiyo, *TRA* katika sheria yake haina kifungu cha asilimia tano, kwa maana hiyo hai-*hold* asilimia tano.

Mheshimiwa Spika, *Zanzibar Revenue Board,* walikuwa na hiyo *clause* kwamba asilimia tano ya mapato wanai-*retain* na mimi nilikuwa mjumbe wa *Zanzibar Revenue Board,* tukaona kwamba hiki kifungu si kizuri tukakifuta. Kwa hiyo, hata *Zanzibar Revenue Board,* hawana kifungu hicho. Kwa hiyo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tusomeni hizi sheria na tuzi-*digest*, *TRA* hawana kifungu hicho, wao ni kama Idara nyingine, wanafanya makisio yao, Waziri mwenye dhamana ya fedha anapitia, baadaye anakubaliana na inakuja hapa inapitishwa na inakaguliwa na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa ni suala la *1.7 trillion shillings* ambazo tuliziweka kwa ajili ya kunusuru uchumi. Hoja hapa ni kwamba fedha zilizotolewa ilikuwa ni 1.*2 trillion shillings:* Je, zilizosalia zimekwenda wapi? Au ndiyo chenchi hiyo?

Nataka niseme kwamba nia yetu katika kunusuru uchumi ilikuwa tupeleke *1.7 trillion*, lakini kwa sababu fedha tulizozipata kutokana na vyanzo vyetu vyote ilikuwa ni 1.2 ndiyo fedha hizo tulizozipeleka na hakuna fedha nyingine ambayo tumeipeleka huko. Lakini nataka niseme taarifa ya utekelezaji inaandaliwa na itakapokuwa tayari, basi Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kuweza kuiona. Hakuna *extra* iliyopatikana kwani iliyopatikana ni 1.2 na ndiyo hiyo tuliyoipeleka kwa ndugu zetu ili kuweza kunusuru uchumi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu kusimamia kwa karibu zaidi matumizi ya fedha za umma hasa katika Halmashauri zetu. Nataka niseme kwamba fedha za umma ni fedha ambazo walipa kodi wamelipa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, sisi kama Wizara ya fedha wenye dhamana ya kusimamia masuala yote ya fedha, suala hili tunalifanyia kazi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nataka niseme kwamba kuanzishwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutasaidia sana kuweza kudhibiti haya matumizi ya hovyo hovyo hasa katika Halmashauri zetu. Nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika hili kwa sababu sisi sote tunatoka katika Halmashauri ili tuweze kuona kwamba ile fedha ambayo imepelekwa kwenye Halmashauri itumike kwa mujibu wa mipango ambayo imewekwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge, sote sisi ni Wabunge, sote sisi tunataka maendeleo, sote tunapenda nchi yetu, hakuna hata mtu mmoja asiyependa nchi yake, nawaomba sana muiunge mkono bajeti yenu ili tuweze kutekeleza majukumu ambayo tumepewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi kwa maelezo yaliyo fasaha kabisa.  Sasa ni zamu ya mtoa hoja - Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, unazo dakika hamsini.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nikushukuru wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuongoza vyema mjadala wa hotuba kuhusu taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2009 na mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge yanasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka ujao. Tunawashukuru wote.

Mheshimiwa Spika, hotuba zangu mbili zimechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 64 waliochangia kwa kuzungumza. Napenda kuwatambua Wabunge waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamad R. Mohammed - Mbunge wa Wawi na Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Athuman Said Janguo - Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Juma H. Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharabi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai - Mbunge wa Iramba Mashariki na Mheshimiwa Dr. Christant M. Mzinakaya - Mbunge wa Kwela. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura - Mbunge wa Tunduru, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ahmed A. Salum - Mbunge wa Solwa, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella - Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Herbert James Mntangi - Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa - Viti Maalum, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Raynald A. Mrope - Mbunge wa Masasi na Mheshimiwa Musa A. Zungu - Mbunge wa Ilala. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif - Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama - Mbunge wa Lushoto, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Damas P. Nakei - Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe - Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia - Mbunge wa Rufiji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed - Mbunge wa Kojani, Mheshimiwa John M. Cheyo - Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa - Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa - Mbunge wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa - Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Charles N. Keenja - Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati na Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya -Mbunge wa Lulindi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi - Mbunge wa Kasulu Magharibi, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya - Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis - Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka - Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Lucy T. Manyenga - Viti Maalum, Mheshimiwa Oscar R. Mukasa - Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mbunge wa Muleba Kusini, Mheshimiwa Thomas Abson Mwang’onda - Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe - Mbunge wa Kyela na Mheshimiwa Joseph J. Mungai - Mbunge wa Mufindi Kaskazini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya - Mbunge wa Mji Mkongwe, Mheshimiwa Maria I. Hewa - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha - Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga - Mbunge Viti Maalum,

Mheshimiwa Mariam S. Mfaki - Viti Maalum, Mheshimiwa Basil P. Mramba - Mbunge wa Rombo na Mheshimiwa Dr. Anthony M. Diallo - Mbunge wa Ilemela. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Sussan A. J. Lyimo - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa George B. Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Eng. Stellah M. Manyanya - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mary Michael Nagu - Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Aisha O. Kigoda Naibu - Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa William M. Ngeleja – Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa - Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga - Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Omar Y. Mzee - Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 83 wamechangia kwa maandishi naomba niwatambue na wenyewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' - Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama - Mbunge wa Lushoto, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira - Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai - Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko - Mbunge wa Kasulu Mashariki na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha - Mbunge wa Wete. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga - Viti Maalum, Mheshimiwa Hemed M. Hemed Mbunge - Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni - Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi -Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Lucy F. Owenya - Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Philemon N. Sarungi - Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya - Viti Maalum, Mheshimiwa Maua A. Daftari - Viti Maalum, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi - Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Khalima O. Kimbau - Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto -Mbunge wa Kigoma Kaskazini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma - Viti Maalum, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel - Viti Maalum, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga - Viti Maalum, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika - Viti Maalum, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi - Viti Maalum, Mheshimiwa Castor R. Ligallama - Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud - Mbunge wa Jang'ombe, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi - Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya - Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim - Mbunge wa Mtambile na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa - Mbunge wa Bububu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta - Viti Maalum, Mheshimiwa Omar A. Mzee -Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil - Viti Maalum, Mheshimiwa Riziki O. Juma - Viti Maalum, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir - Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Juma A. Njwayo - Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Samuel Mchele Chitalilo - Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Benadetha K. Mushashu - Viti Maalum, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila - Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa John P. Lwanji - Mbunge wa Manyoni Magharibi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Paul P. Kimiti - Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Mheshimiwa Juma H. Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Mohammed Abdi Abdulaziz - Mbunge wa Lindi Mjini, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati - Mbunge wa Manyoni Mashariki, Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhani - Viti Maalum, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi - Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Ali Juma Haji - Mbunge wa Chaani, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Benedict N. Ole Nangoro - Mbunge wa Kiteto na Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi - Mbunge wa Ludewa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami - Mbunge wa Moshi Vijijini, Mheshimiwa Juma S. Omar - Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa Michael L. Laizer - Mbunge wa Longido, Mheshimira Harith B. Mwapachu - Mbunge wa Tanga, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe - Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame - Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Damas P. Nakei - Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa Yono S. Kevela - Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya - Mbunge Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Zaynab M. Vullu - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro - Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Lolesia J.M Bukwimba - Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki - Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege - Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Eng. Mohammed Habib Mnyaa - Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu - Mbunge wa Bukene, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis - Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Laus Omar Mhina - Mbunge wa Korogwe Vijijini, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Mbunge wa Kwamtipura na Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka - Mbunge wa Morogoro Mjini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah - Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha - Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi - Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Eng. Stellah M. Manyanya - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza - Viti Maalum, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro - Mbunge wa Vunjo na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Devotha M. Likokola - Viti Maalum, Mheshimiwa John. M. Cheyo - Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mheshimiwa Charles N. Keenja - Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Andrew John Chenge - Mbunge wa Bariadi Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, nafarijika kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nitatoa majibu kwa muhtasari kwa hoja zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi imetoa mapendekezo mazuri ambayo Serikali imeyakubali na inaahidi kuyafanyia kazi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kupanua wigo wa kuongeza mapato, kuangalia eneo la sera na uendeshaji wa taratibu za kukusanya kodi, kuimarisha mpango mkakati wa *TRA* wa kuboresha ukusanyaji kodi, kuangalia upya utaratibu wa kuanzisha Mamlaka na Wakala wa Serikali ambao sasa wanainyima Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika kuhusu misamaha ya kodi katika tasnia ya Madini, Serikali imeingia mikataba na kampuni za Madini, yaani *Mining Development Agreements* ambayo imeainisha vivutio vya kodi. Aidha, kila kampuni ina mkataba wake tofauti na Serikali. Katika hotuba yangu ya bajeti nimefafanua kwamba Serikali itatoa unafuu maalum wa kodi ya ongezeko la thamani na msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za petroli kwa kampuni zilizosaini mkataba na Serikali. Msamaha utatolewa kulingana na masharti yaliyopo kwenye mikataba iliyosainiwa kati ya Serikali na kampuni za Madini kabla ya tarehe 01 Julai, 2009. Kwa mantiki hiyo, kampuni zote ambazo ziliingia mikataba baada ya Julai 01, 2009 na ambazo hazina mikataba hazihusiki na msamaha huo.

Kwa kuwa, mikataba ya kabla ya Julai, 2009 iliingiwa kati ya Serikali na kampuni hizo ni vigumu kisheria kwa Serikali kuamua peke yake kufanya marekebisho ya vivutio vya kodi kwa lengo la kuzipunguzia bila kuzihusisha kampuni husika. Serikali itaendelea na mazungumzo na kampuni za Madini ili kurejea mikataba hiyo kwa lengo la kuweka uwiano sawa katika kugawana mapato yanayotokana na raslimali za madini. Kazi hii ilishaanza kwa baadhi ya kampuni na mwelekeo ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Kamati imesisitiza umuhimu wa Serikali kuainisha matumizi yake na uwezo wa kuamsha mapato. Serikali ichunguze matumizi yake na kuhakikisha kuwa ni ya kimkakati. Aidha, Kamati imeishauri Serikali ije na mkakati wa makusudi wa kupunguza matumizi yake yasiyo ya lazima, yaani *cross cutting measures.*

Mheshimiwa Spika, wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011 nilieleza kuwa hatua mbalimbali zitachukuliwa na Serikali kupunguza matumizi. Napenda nirudie baadhi ya hatua nilizozipendekeza na hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kudhibiti matumizi ya simu na umeme;

(ii) Kudhibiti matumizi ya magari;

(iii) Kuhakikisha kwamba Serikali inalipa posho za nyumba kutokana na uwezo wa bajeti;

(iv) Fedha zilizopangwa kwa ajili ya posho mbalimbali katika Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri zitapunguzwa na kudhibitiwa;

(v) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani juu ya uandaaji wa hesabu katika viwango vya kimataifa, yaani *IPSAS*;

(vi) Kuanzia mwaka 2010/2011 Halmashauri zinatakiwa kuonyesha bakaa katika akaunti ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha ili zijumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata kama chanzo cha mapato;

(vii) Serikali itatumia utaratibu wa malipo unaosimamiwa na Benki Kuu, yaani *Tanzania Inter Bank Settlement System* kwa kifupi *TISS* kwa malipo yatakayofanywa na Wizara zote zilizopo Dar es Salaam na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

(viii) Kudhibiti utoaji wa dhamana za Serikali kwa vyombo mbalimbali vya umma ili kuepuka ongezeko lisilohimilika na deni la taifa; na

(ix) Serikali itakuwa na chombo maalum kitakachosimamia ujenzi na viwango vya majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba bajeti ya mwaka 2010/2011 itatekelezwa kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa ili yaweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya biashara ningependa kufafanua kwamba Serikali inategemea kukopa mikopo ya biashara ya kiasi cha shilingi trilioni 1,331.2 bilioni kutoka ndani na nje ya nchi. Bado mikopo ya kibiashara itazingatia masharti nafuu ikiwa ni pamoja na muda wa kurejesha mikopo usiopungua miaka mitano na zaidi pamoja na riba nafuu. Mikopo ya ndani itatokana na uuzaji wa hati fungani za Serikali za muda mrefu. Aidha, Serikali itahakikisha mikopo hiyo haiathiri hali ya utulivu wa kiuchumi na kutokukosesha sekta binafsi mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukikopa mikopo ya ndani yenye masharti ya namna hii hadi sasa. Kwa hiyo, siyo jambo geni. Vilevile napenda kusisitiza kwamba mikopo hii itatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo tu, sababu za Serikali kuanza kukopa mikopo ya kibiashawa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni upungufu wa mapato ya ndani na mikopo na misaada ya wahisani katika kuongeza kasi ya utekelezaji MKUKUTA na dira ya maendeleo ya 2025 hasa katika maeneo ya miundombinu, yaani barabara, reli, nishati, maji, bandari na madaraja, kilimo hasa cha umwagiliaji na viwanda vya msingi. Ni muhimu kuongeza uwekezaji katika maeneo haya ili kuwezesha uchumi kukua kwa haraka zaidi na hivyo kuongeza kasi ya kupunguza umasikini nchini. Kutumia mikopo kibiashara kwa miradi ya maendeleo ni utaratibu unaokubalika dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, Kamati imeishauri Serikali kupunguza urasimu na kuharakisha mchakato wa utoaji maamuzi, kuboresha utoaji wa utaratibu wa utoaji leseni na kuwa na mfumo wa bodi unaovutia uwekezaji. Serikali imekubaliana na ushauri huu na hatua za kufanikisha hii zitaendelea kuchukuliwa.

Aidha, katika hotuba yangu nilipowasilisha taarifa ya hali ya uchumi baadhi ya hatua katika eneo hili nilizielezea. Namshukuru pia Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye asubuhi alijaribu pia kuelezea eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa awali, Kamati imetoa mapendekezo mengi ambayo Serikali imeyakubali na itaendelea kuyafanyia kazi. Nachukua fursa hii kuishukuru tena Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya 2010/2011. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Dr. Abdallah Kigoda kwa umahiri wake na kwa msaada kwa Wizara yetu ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imetoa ushauri na mapendekezo mengi ikiwa ni pamoja na bajeti mbadala. Mapendekezo hayo ni pamoja na kuitaka Serikali kuziwezesha asasi ndogo ndogo za fedha kupata mikopo nafuu na kuingia nazo ubia ili kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa riba nafuu inayolipika, kuhakikisha kwamba nchi ina umeme wa uhakika, Serikali kutumia teknolojia ya *maping* ili kujua raslimali zote zilizopo nchini na namna tunavyoweza kuzitumia kuzipa uwezo wa kijiendesha *NDC* na *STAMICO* ili ziweze kumiliki maeneo ya *industrial, minerals* na kuingia ubia na makampuni ya nje bila kudhulumiwa na Serikali iendelee kupima ardhi ili kuwezesha wananchi kumiliki ardhi hasa kutokana na nchi kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali inayaafiki mapendekezo hayo na itaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri mzuri uliotolewa na Kambi ya Upinzani, pia imetoa bajeti mbadala kwa Serikali kuichambua. Serikali imeangalia bajeti mbadala na kubaini kuwa mapendekezo mengi ni mazuri.

Hata hivyo, Serikali inashauri kwamba katika suala la vyanzo vya mapato ni vyema kwa miaka ijayo mapendekezo haya yakawasilishwa Serikalini mapema ili yajumuishwe katika mchakato wa bajeti. *(Makofi)*

Kwa kawaida, mchakato wa bajeti huanza mwezi Novemba na kumalizika mwezi Februari, ili kuhakikisha kwamba maamuzi muhimu yanachukuliwa kati ya mwezi Machi na mwezi Mei. Kama mapendekezo yaliyopo katika bajeti mbadala yangewasilishwa mapema Serikalini, wataalam wangeyachambua kwa kina na nina hakika yangeweza kujumuishwa katika bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msukosuko wa fedha na uchumi duniani, Serikali iliandaa mpango wa kunusuru uchumi na athari za msukosuko, yaani *rescue*

*package*. Naibu Waziri alizungumzia hili lakini kwa sababu ya umuhimu wake, nitapenda kulirudia. Mpango wa dharura wa muda mfupi uliandaliwa na gharama zake zilikadiriwa kufikia Sh. 1, 700,000,000,000/=, Serikali iilitarajia kupata fedha hizi kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wafadhili na kukopa kutoka katika masoko ya ndani.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Sh. 1,298,000,000,000/= zimekwishapatikana na zimetumika kama ifuatavyo:-

(a) Kuziba pengo la bajeti lililotokana na upungufu wa mapato ya ndani. Jumla ya shilingi bilioni 663.3 zilikopwa kupitia dhamana za Serikali ikilinganishwa na shilingi bilioni 828 zilizotarajiwa.

(b) Kuhusu kuziba pengo la akiba ya fedha za kigeni, Benki kuu imeishapokea kiasi cha shilingi bilioni 411.2 kutoka Shirika la Fedha Duniani chini ya utaratibu wa *Exogenous shop facility* ukilinganisha na shilingi bilioni 436.2 zilizotarajiwa ili kuongeza akiba ya fedha za kigeni.

(c) Kuhusu kulinda ajira na vipato, kiasi cha shilingi bilioni 19.2 kimeshalipwa kama fidia ya hasara *(loss compensation)* kwa makampuni na wafanyabiashara binafsi waliopata hasara ya moja kwa moja kutokana na kuporomoka kwa bei za kahawa na pamba ukilinganisha na shilingi bilioni 21.9 zilizokadiriwa awali.

Kwa upande mwingine jumla ya shilingi bilioni 15 zimetengwa kwa ajili ya kudhamini mikopo (*loan rescheduling with government guarantee*) kwa makampuni na wafanyabiashara binafsi wa sekta mbalimbali walioshindwa kurudisha mikopo yao kwa wakati uliotakiwa kutokana na kushindwa kufikia malengo ya mapato. Chini ya mpango huu, shilingi bilioni 45 zilikadiriwa kutumika. Lengo la hatua hizi ni kuwawezesha wakopaji kupata mikopo mipya kwa ajili ya shughuli za ununuzi wa mazao kwa msimu wa mwaka 2009/2010.

Vilevile kiasi cha shilingi bilioni 20 kilitolewa chini ya mpango huo ikiwa ni ruzuku kwa bei ya zao la pamba. Serikali pia ilitoa kiasi cha shilingi bilioni nane kwa lengo la kupanua mifuko ya dhamana ya *export credit guarantee scheme* na *small and medium enterprises.*

(d) Serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 10 ili kuongeza akiba ya chakula kwa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Chakula. Aidha, Serikali imeishatoa shilingi bilioni 20 kwa ajili ya mikopo ya bembejeo za kilimo na Benki ya Raslimali. Benki ya Raslimali imeishapokea kiasi cha shilingi bilioni 19 kwa ajili ya kuwezesha kutoa mikopo ya kilimo.

(e) Kulinda uwekezaji muhimu hususani miundombinu. Serikali imeishatoa kiasi cha bilioni 10 kama mikopo kupitia Benki ya Raslimali kwa ajili ya kugharamia uwekezaji katika sekta ya nishati ukanda wa kusini.

Hivyo basi fedha zote zilizopatikana zimetumika kama ilivyoanishwa hapa juu. Serikali bado inaendelea na juhudi za kutafuta kiasi cha takribani shilingi bilioni 400

zinazohitajika ili kuufanikisha mpango wote. Hata hivyo, matumizi katika baadhi ya vifungu yatapungua ukilinganisha na mpango wa awali. Mafungu makubwa ni kama haya yafuatayo:-

(a) Kuhusu mikopo ya masharti nafuu, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 80, kiasi hiki hakitahitajika tena kwa sababu Serikali ilishakitoa.

(b) Katika kusaidia Shirika la Reli Tanzania, kiasi cha shilingi bilioni 110.4 kingehitajika. Kiasi hiki hakitahitajika tena baada ya mkataba baina ya *TRL* na Serikali kusitishwa.

(c) Katika dhamana kwa mikopo, kiasi cha shilingi bilioni 30 hakitatumika kwa sababu mikopo iliyokidhi masharti ilihitaji kiasi cha bilioni 15 tu. Serikali inaandaa taarifa kamili ya utekelezaji wa mpango mzima na mara taarifa itakapokamilika itakuwa ndiyo msingi wa ukaguzi wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na ule wa Kambi ya Upinzani, pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliotoa michango yao ya maoni na ushauri utasaidia katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011.

Baadhi ya mapendekezo yalihusisha maeneo yafuatayo:-

Kupunguza riba za kukopa na kuongeza riba za amana, vyanzo vipya vya mapato, kuimarisha miundombinu ya reli na barabara, kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuboresha sekta za jamii, mgawanyo wa mapato ya muungano, kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi walioko pembezoni mwa nchi, kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima, kurahisisha masharti ya dirisha la kilimo la *TIB*, kuimarisha sarafu ya nchi yetu, kuongeza fursa za ajira, kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya uchaguzi mkuu, kuhakikisha Serikali inafanya tathimini na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru uchumi na Serikali na kupunguza utegemezi kwa misaada kutoka nje. Tunachukua ushauri huu na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu baadhi ya hoja hizo kama ifuatavyo:- Kuhusu riba za mabenki, kulingana na Sheria ya Mabenki na Vyombo vya Fedha ya mwaka 1961 pamoja na ile iliyorekebishwa mwaka 2006, benki za biashara zimeruhusiwa kupanga riba kulingana na ushindani katika soko. Kwa hiyo, katika kupanga viwango vya riba, benki za biashara huzingatia ushindani katika soko la fedha na mitaji, gharama za upatikanaji wa fedha, gharama za uendeshaji na sifa za mkopaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa riba hutegemea sifa alizonazo mkopaji. Kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji na kutokuwepo kwa taasisi ya kuhakiki ukweli wa taarifa za waombaji mikopo nchini vimechangia kwa kiasi kikubwa viwango vya riba za mikopo kuwa juu. Mchakato wa kuanzisha vyombo vya kuhifadhia taarifa za wakopaji umekwishaanza na upo katika hatua nzuri. Kuwepo kwa vitambulisho vya Taifa pia kutasaidia kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo mapya ya kutoza kodi hasa maduka ya fedha kigeni, saluni na migahawa ni kwamba, kulingana na Sheria za kodi zilizopo biashara za maduka ya fedha za kigeni, saluni na migahawa hutozwa kodi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, kodi ya ongezeko la thamani inatozwa kwa biashara ya migahawa na saluni kama biashara husika imefikia kiwango cha usajili wa *VAT* ambacho ni shilingi milioni 40 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuboresha sekta ndogo ya uvuvi, kuondoa kodi kwenye vipuli na injini, napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba injini na nyavu za uvuvi tayari zimeshasamehewa kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, injini za boti za uvuvi na nyuzi za kutengenezea nyavu za uvuvi hazitozwi ushuru wa forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kugawana mapato kutokana na vyanzo vya Muungano, nasema kwa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za Muungano yamekuwa yakifanyiwa kazi na Serikali zetu mbili, ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kila upande umeishaandaa mapendekezo yake ambayo yamepangwa kujadiliwa kwenye vikao vya pamoja chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira kwani masuala haya yanahitaji mashauriano ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuboresha mazingira ya kazi na maeneo ya pembezoni, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ili kuwavutia Watumishi katika maeneo haya. Kwa mwaka 2010/2011 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 66.85 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, yaani Maboma ya Halmashauri, nyumba za watumishi, zahanati na vituo vya afya, miradi ya maji, madaraja vijijini, hosteli za wanafunzi wa kike katika shule za Sekondari na ununuzi wa boti na magari. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Spika, katika miezi ya hivi karibuni, thamani ya shilingi ya kitanzania dhidi ya Dola ya kimarekani imekuwa ikipungua. Kwa kipindi cha mwaka ulioishia Aprili, 2010, Shilingi ya kitanzania ilipoteza thamani dhidi ya Dola ya kimarekani kwa asilimia 1.2. Kupungua huku kwa thamani kumetokana na kuimarika kwa Dola ya kimarekani kufuatia kuzorota kwa sarafu ya *Euro*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wawekezaji wanaiona Dola ya kimarekani kama sarafu iliyo bora zaidi duniani hasa katika kipindi hiki ambacho nchi za Ulaya zinajaribu kujikwamua na tatizo la madeni sugu ya nchi ya Ugiriki ambayo yamesababisha sarafu ya Ulaya hususani *Euro* kuanguka kwa kiasi kikubwa. Hata sarafu ambazo zimekuwa na historia ya uimara kama Dola za Australia na Canada zimeanguka dhidi ya Dola ya Kimarekani. Hapa Afrika Mashariki, kati ya tarehe 6 - 20 Machi, 2010 wakati Shilingi ya Tanzania imeanguka kwa asilimia 0.7 Shilingi ya Kenya imeanguka kwa asilimia 1.3 na ya Uganda ilianguka kwa asilimia 2.5.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili ni ongezeko la manunuzi ya Dola na mabenki hapa nchini kwa ajili ya kuongeza akiba zao za fedha za kigeni. Ongezeko hili limetokana na kupungua kwa kasi ya utoaji mikopo kutoka mabenki kufuatia msukosuko wa uchumi duniani. Katika kipindi hiki mabenki yamekuwa makini zaidi katika kutoa mikopo na hivyo kuongeza zaidi uwekaji wa akiba katika raslimali za fedha za kigeni badala ya kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kuwa kushuka kwa thamani ya Shilingi kunazorotesha uchumi ni kwamba, kwa upande mmoja kupungua kwa thamani ya Shilingi kunaongeza bei ya bidhaa tunazoagiza kutoka nje hususani mafuta ya petroli na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji. Kwa upande mwingine kupungua kwa thamani ya Shilingi kunaboresha ushindani wa bidhaa na huduma zetu tunazouza nje na kuongeza kipato cha Watanzania wanaouza bidhaa nje, hususani wakulima wetu wa pamba, kahawa, korosho na kadhalika.

Changamoto yetu ni kuhakikisha kuwa wauzaji wa bidhaa nje wanaitumia vyema fursa kama hii mara inapotokea kwa kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu fedha zilizopungua za kusaidia bajeti (*general budget support*) kutoka kwa wahisani katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa misaada na mikopo ya kibajeti kunatokana na baadhi ya wafadhili kutoa fedha zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kutolewa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ili kusaidia Serikali kupambana na athari za msukosuko wa kiuchumi kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti.

Hivyo, ni dhahiri kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya fedha 2009/2010, 2010/2011 tutakuwa tumepata fedha zote za *GBS* kwa kupindi hicho kama ilivyotarajiwa.

Aidha kiasi cha Sh. 2,452, 908, 000,000/= kinatakiwa kupatikana kutokana na misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na Kamati ya Uchumi na Fedha, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nieleze kwa muhtasari tu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne, hadi sasa.

Kama nilivyoeleza katika hotuba zangu mbili, ya hali ya Uchumi na ile ya Bajeti, Serikali ya Awamu ya Nne imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali. Katika eneo la ukuaji wa uchumi kati ya mwaka 2005 - 2009 ukuaji wa uchumi umeendelea kuwa imara licha ya athari za msukosuko wa kiuchumi duniani, kupanda kwa bei ya mafuta kwenye Soko la Dunia na uhaba wa mvua uliotokea katika miaka 2005/2006 na 2008/2009.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge minong'ono imekuwa siyo minong'ono ni mazungumzo kabisa. Sasa ni vizuri tuendelee kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha za Uchumi, tuseme kwa staha ndivyo inavyotakiwa, ahsante sana!

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Katika kipindi hicho, wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 kwa mwaka, kiwango ambacho kilikuwa ndani ya lengo la MKUKUTA la ukuaji wa uchumi wa kati ya asilimia sita na asilimia nane ifikapo mwaka 2010.
Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 2948.3 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 4,693.6 mwaka 2009. Aidha, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 2,048.4 mwaka 2005 sawa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi 4.8 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 3,551.3 mwaka 2009 sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa takribani miezi sita.

Mheshimiwa Spika, malengo ya uchumi kwa mwaka 2010 ni pamoja na haya yafuatayo:-

Moja, ukuaji wa pato halisi la Taifa kwa mwaka 2010 inatarajiwa utakuwa asilimia saba ukilinganisha na asilimia sita ya mwaka 2009.

Pili, juhudi za kukusanya mapato ya ndani *(revenue effort)* zinategemea kufikia uwiano wa pato la Taifa wa asilimia 17.3 mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na asilimia 16.4 mwaka 2009/2010.

Tatu, kasi ya upandaji bei inakadiriwa kupungua kufikia asilimia nane mwezi Juni, 2010 ikilinganishwa na asilimia 10.7 mwezi Juni, 2009. Aidha, kasi ya upandaji bei inategemewa kushuka zaidi na kufikia asilimia tano ifikapo mwezo Juni, 2011. Nne, hatua zinachukuliwa kuboreshwa mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara.

Tano, kuwa na akiba ya fedha za kigeni za kutosha kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyoanishwa katika hotuba ya hali ya uchumi vimepangwa kulingana na maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi. Kilimo ikiwa ni pamoja na Mifugo na Uvuvi vimepewa uzito wa kipekee. Bajeti iliyotengwa na Serikali itasaidia katika kuwezesha maeneo ambayo sekta binafsi imekuwa ikikumbana na kikazo katika kuwekeza. Hivyo, bajeti hiyo ni mchango wa Serikali na mchango mwingine mkubwa utatoka kwa sekta binafsi. Vipaumbele vingine ni miundombinu, uendelezaji wa ardhi na makazi, vitambulisho vya Taifa, nishati, viwanda na sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele vilivyoelezwa hapo juu, napenda kutaja baadhi ya maeneo muhimu yaliyomo katika bajeti ya 2010/2011. Moja, bajeti inalenga kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 kwa kutenga fedha za kutosha za kuhakikisha Uchaguzi Mkuu unafanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

Pili, sekta ya elimu imetengewa Sh. 2,045,300,000,000/= ikilinganishwa na Sh. 1,743,900,000,000/= mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote kuanzia Elimu ya Msingi hadi Elimu ya

Juu ikijumuishwa watoto wa masikini wanapata elimu. Serikali itaendelea kuboresha sekta ya elimu hatua kwa hatua kulingana na uwezo wake pamoja na michango ya sekta binafsi na asasi nyingine.

Tatu, Bajeti imetenga fedha kwa ajili ya mchakato wa kutengeneza vitambulisho vya Taifa ili Watanzania tutambuane. Vitambulisho vya Taifa vitasaidia kuwarahisishia wananchi kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Nne, Bajeti ya maji imeongezeka kwa asilimia 14.5 ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi mijini na vijijini. Hatua hii ni kwa manufaa ya jamii.

Tano, kuongeza bajeti ya kilimo ili kuimarisha huduma za ugavi, kufanya tafiti katika uzalishaji wa mbegu na mifugo bora na kuongeza ruzuku za madawa na mbolea.

Sita, kupanua na kukarabati miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na hivyo kuongeza bajeti ya miundombinu kwa asilimia 37.3. Sote tunakubaliana kuhusu umuhimu wa kuboresha na kupanua miundombinu yetu.

Saba, kuboresha sekta ya afya kwa kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na hospitali na ukarabati wa hospitali za Mikoa na ununuzi wa madawa kwa kuongeza bajeti kwa asilimia 25.2. Serikali inafahamu umuhimu wa kuboresha afya kwa jamii.

Nane, kuboresha maslahi ya watumishi; sote tunafahamu umuhimu wa maslahi ya watumishi katika kuongeza ari, juhudi na ufanisi kazini.

Tisa, Bajeti hii imelenga kuongeza mtaji wa Benki ya Wanawake nchini kwa shilingi bilioni mbili kila mwaka ili huduma zake ziwafikie wanawake wengi zaidi. Kuwawezesha wanawake katika shughuli zao kwa kuwapatia vyanzo vya mikopo nafuu. Ni jambo jema kwa jamii yote kwani akinamama wanabeba jukumu zito katika familia.

Kumi, kuanzisha dirisha la kilimo na kuanzisha Benki ya Kilimo ili kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wakiwemo wakulima wadogowadogo. Hii ni hatua muhimu katika kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza.

Mwisho, kuboresha sekta ya fedha kwa kuanzisha Benki ya Kilimo, kuimarisha Benki ya Rasilimali, kuharakisha utekelezaji wa kutoa huduma ya kukodisha zana za kilimo na ujenzi (*financial leasing*) na kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya fedha ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi juu uwekaji akiba katika Mabenki.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua kubwa zinazochukuliwa na Serikali ni kuboresha kilimo kupitia bajeti hii na kuweka misingi na mazingira na upatikanaji wa mikopo kwa masharti nafuu kwa sekta hiyo. Ikumbukwe kuwa upatikanaji wa fedha na kugharamia kilimo ni moja ya nguzo kumi za kilimo kwanza na utekelezaji wake umepangwa kwa kuainisha na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu ni dhahiri kuwa bajeti ya mwaka huu ni ya kipekee na ambayo inazingatia mahitaji ya wananchi katika ngazi mbalimbali ikiwemo wananchi wa vipato vidogo mijini na vijijini. Ni ukweli usiopingika kuwa kwa azma hii ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi CCM ina nafasi kubwa ya kuendelea kuongoza na kuwatetea Watanzania maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti mwaka 2010/2011 ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya MKUKUTA malengo ya Maendeleo ya Milenia na hatimaye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hata hivyo, ili kufikia malengo yetu mapema zaidi kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwa kuzalisha mali na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, ushiriki katika uzalishaji kwa mwananchi mmoja mmoja au katika vikundi ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Aidha, sekta za kilimo, mifugo, uvuvi zikiboreshwa na kutilia mkazo usindikaji wa mazao ya kilimo zina nafasi kubwa ya kuchangia Pato la Taifa na kukuza ajira. Bajeti hii pia inalenga kuongeza jitihada za Serikali za kuendeleza ardhi na kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2010/2011 imeandaliwa katika mazingira magumu kufuatia msukosuko wa kiuchumi ulioikumba nchi yetu na mabadiliko ya tabia nchi iliyosababisha ukame na njaa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Aidha, bajeti hii imeandaliwa katika mazingira ambayo bei ya mafuta ya petroli imeendelea kuongezeka. Vile vile ni kipindi ambacho misaada na mikopo ya kibajeti imepungua ukilinganisha na mwaka unaomalizika wa 2009/2010.

Pamoja na changamoto hizo Serikali imeweza kubuni vyanzo mbadala vya mapato ambavyo vimewezesha Serikali kuongeza mgao wa matumizi kwa sekta za kilimo, miundombinu, elimu, afya na maji. Ni matumaini ya Serikali kwamba utekelezaji wa bajeti hii utasaidia sana kusukuma maendeleo kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni bajeti rafiki na imelenga mwananchi wa kawaida. Bajeti pia imetoa fursa kwa sekta binafsi kupitia utaratibu wa *Public Private Partnerships.* Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuiunge mkono bajeti hii ili kutimiza azma ya kuwaletea maendeleo wananchi na hivyo kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na kwa kunipa mimi Mustafa Mkulo heshima ya kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa nusu ya pili ya kipindi chake cha kwanza cha Awamu ya Nne. (*Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein - Makamu wa Rais kwa uongozi wake na hasa katika kutatua kero za Muungano. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanda Peter Pinda - Waziri Mkuu kwa kusimamia vyema

shughuli za Serikali Bungeni na kwa ushirikiano na maelekezo mbalimbali aliyokuwa akinipa yaliyonisaidia kutekeleza kazi zangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha Bunge letu kwa viwango vya hali ya juu vya Kimataifa. Nawashukuru na Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge, Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mlionipa wakati wote nilipokuwa natengeneza majumuisho yangu kama Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Fedha na Uchumi, napenda tena kuwashukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, namshukuru sana Katibu Mkuu Alhaj Ramadhani Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu John Haule, Laston Msongole na Dr. Servacius Likwelile pamoja na Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Dr. Phillip Mpango.

Napenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Prof. Beno Ndugu na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndugu Harry Kitilya kwa ushirikiano mzuri walionipa wakati wote nikiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kilosa kwa kunipa ridhaa ya kuwa Mbunge wao na kwamba naamini sikuwaangusha na kwamba watanipa tena nafasi mwezi Oktoba. Mwisho, kama nilivyosema mwanzo, napenda kuishukuru familia yangu mke wangu, wanangu, wajukuu zangu kwa uvumilivu wao wakati nikiwa Dodoma kwa kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Fasili 68(7), Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri amekiuka ibara ya 44 fasili ndogo ya tatu na pia kanuni 105 ambayo inamtaka baada ya Kamati yako kukubaliana na Waziri wa Fedha na Uchumi juu ya bajeti ya *(CAG)* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Waziri kwa kanuni ambayo ameiwekea sahihi yeye mwenyewe amesema hiyo bajeti haitageuzwa na mtu yoyote na italetwa Bungeni.

Hazina imekata shilingi bilioni nane za kazi ambayo ndiyo kusema kwa bajeti kubwa kama hii itakuwa ni vigumu kufanya hiyo na tumemwongezea kazi na matumizi ya Waheshimiwa Wabunge. Mimi naomba utupe mwongozo ili Bunge lako lisije likavunja sheria ambayo imetunga lenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ni mpya na imenifikia wakati huu. Mwongozo wangu ni kwamba kukubali jumla ya bajeti hakuathiri kitu chochote kwa sababu hoja anayoitoa Mheshimiwa John Cheyo inaweza kuzungumzwa kipekee na marekebisho yanayohitajika yakafanyika badala ya kuzuia kabisa kupitisha bajeti kwa sababu ninavyoelewa hata tutakavyofika kwenye *appropriation bill* ile jumla inayoidhinishwa ndiyo ya maana.

Kwa hiyo, kama kuna hoja kwamba *CAG* amepunguziwa fedha katika kasma yake inaweza hoja hiyo ikaamuliwa bila kuharibu utaratibu tunaoingia sasa wa Kikatiba ambao kama hatuwezi kuuamua sasa tunaingia kwenye mgogoro mwingine wa Katiba kwamba Bunge litakuwa halikupitisha bajeti, jambo ambalo litasimamisha kabisa Serikali na kuleta athari kubwa kwa wananchi.

Kwa hiyo, mimi naamua kwamba tutaendelea na hatua zinazofuata, nimwombe Mheshimiwa John Cheyo kwa wakati unaohusika kama tutakavyoshauriana na pia atakavyoshauriana na Serikali tuweze kuliamua hilo kwa wakati wake kwa sababu tukiliamua basi fedha zinaweza kutoka mahali popote zikaweza kuingia katika mfuko huo na tukawa tumekaa vizuri tu. Hatuvunji chochote, hatuvunji Katiba kwa kukubali ujumla wa bajeti yenyewe ambayo ndiyo pendekezo la sasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu zetu, sasa nitaomba *Sergeant at Arm* agonge kengele ili Waheshimiwa Wabunge wote waliopo nje, tunapewa kama dakika tano hivi waweze kuingia kwa sababu kura zitakazopigwa ni kura za jina kwa jina *(roll call vote)* kwa mujibu wa kanuni ya 98(2) kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Spika alipoahirisha leo mchana. Kwa kuendelea tu, itakuwa hatuwatendei haki Wabunge wafuatao walioaga rasmi kwa kusema tu Mtera, Mtera, sio kweli.

Waliopo kwenye matibabu ni Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi yuko India kwa matibabu, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo naye yuko India, Mheshimiwa Stephen Galinoma yuko *Ocean Road* amelazwa Dar es Salaam, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula kama mnavyokumbuka alivamiwa na majambazi kule Bukombe Jimboni kwake na bado yuko Muhimbili anaendelea na matibabu.

Pia wafuatao wameaga rasmi kama utaratibu unavyohitaji, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni yuko *New York* anatuwakilisha kwenye Mkutano ambao ulipangwa toka awali; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa amekwenda Zanzibar kuhudhuria mazishi; Mheshimiwa Nimrod Mkono ana dharura ya kifamilia kule Musoma; Mheshimiwa Janet Kahama amekwenda Arusha kwenye mazishi; Mheshimiwa Felister Bura yuko Musoma kwenye mazishi; Mheshimiwa Elisa D. Mollel kuna msiba kule Arusha Jimboni kwake kwa jamaa wa karibu; Mheshimiwa Margaret Sitta amekwenda Dar es Salaam kikazi na Mheshimiwa Gaudence Kayombo yuko Morocco anahudhuria Mkutano wa Sita wa *Pan African Forum*.

Kwa hiyo, orodha hii nadhani Katibu anayo ili tusiwe tunasema tu Mtera kama vile watu wamekwenda kutembea kule kwa Mzee Malecela.

Katibu naona dakika zetu 5 zimekwishapita, kwa hiyo tutaingia kwenye utaratibu wa kanuni ya 98(2) ili kuweza kupata uamuzi wa Bunge.

**KATIBU:** Upigaji wa kura kwa mujibu wa kanuni 98(2) na kanuni ya 79(1)(8)(10), ili kutimiza masharti ya katiba…

**SPIKA:** Kabla hujaendelea Katibu kuna tangazo muhimu hapa. Serikali baada ya kusikia hoja ya Kamati ya *PAC* inayoongozwa na Mheshimiwa Cheyo kumbe kabla hata ya kusoma majibu, Waziri wamesharejesha kwa bajeti ya *CAG* zote shilingi bilioni nane zilizokuwa Hazina. Ahsante sana na nashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa nyongeza tu, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Ngeleja, amefuatana na Mheshimiwa Rais kwa ziara ya Mkoa wa Kigoma. Ahsante sana.

Kupiga kura Bungeni kwa mujibu wa Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni ya 98(2) na Kanuni ya 79(1)(8)(10) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007.

**NDG. DR. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mhe. Spika, tutapiga kura kwa kuita jina moja baada ya jingine. Mheshimiwa Mbunge ana uhuru wa kuamua Ndiyo au Hapana au Huamui.

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda | - | Ndiyo |
| Mhe. Phillip Sang'ka Marmo | - | Ndiyo |
| Mhe. Muhammed Seif Khatib | - | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Juma Athumani Kapuya | - | Hakuwepo |
| Mhe. Dr. Mary Michael Nagu | - | Ndiyo |
| Mhe. Dr. John Pombe Magufuli | - | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Mark James Mwandosya | - | Ndiyo |
| Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi | - | Ndiyo |
| Mhe. Capt. John Zefania Chiligati | - | Ndiyo |
| Mhe. Margaret Simwanza Sitta | - | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla | - | Ndiyo |
| Mhe. Stephen Masatu Wasira | - | Ndiyo |
| Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa | - | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe | - | Ndiyo |
| Mhe. Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa | - | Ndiyo |
| Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia | - | Ndiyo |
| Mhe. Sophia Mnyambi Simba | - | Hakuwepo |
| Mhe. Dr. Batilda Salha Burian | - | Ndiyo |
| Mhe. Bernard Kamilius Membe | - | Hakuwepo |
| Mhe. Mathias Meinrad Chikawe | - | Ndiyo |
| Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala | - | Ndiyo |
| Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga | - | Ndiyo |
| Mhe. Mustafa Haidi Mkulo | - | Ndiyo |

Mhe. Lawrence Kego Masha - Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja - Hakuwepo
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika - Ndiyo
Mhe. Celina Ompeshi Kombani - Ndiyo
Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema - Ndiyo
Mhe. Anne Semamba Makinda - Ndiyo
Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari - Ndiyo
Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje - Hakuwepo
Mhe. Balozi Seif Ali Iddi - Ndiyo
Mhe. Dr. Emmanuel John Nchimbi - Ndiyo
Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza - Ndiyo
Mhe. Dr. Cyril August Chami - Ndiyo
Mhe. Dr. Aisha Omar Kigoda - Ndiyo
Mhe. Joel Nkaya Bendera - Ndiyo
Mhe. Dr. David Mathayo David - Ndiyo
Mhe. Christopher Kajoro Chiza - Ndiyo
Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka - Ndiyo
Mhe. Jeremiah Solomon Sumari - Hakuwepo
Mhe. Mohamed Aboud Mohamed - Ndiyo
Mhe. Omar Yussuf Mzee - Ndiyo
Mhe. Balozi Hamis Suedi Kagasheki - Ndiyo
Mhe. Lucy Sawere Nkya - Ndiyo
Mhe. Dr. James Mnanka Wanyancha - Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige - Ndiyo
Mhe. Adam Kighoma Malima - Ndiyo
Mhe. Hamad Rashid Mohamed - Hapana
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa - Hakuwepo
Mhe. Dr. Willibrod Peter Slaa - Hapana
Mhe. Halima James Mdee - Hapana
Mhe. Shoka Khamis Juma - Hapana
Mhe. Grace Sindato Kiwelu - Hapana
Mhe. Riziki Omar Juma - Hapana
Mhe. Dr. Ali Tarab Ali - Hapana
Mhe. John Momose Cheyo - Ndiyo
Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo - Hapana
Mhe. Said Amour Arfi - Hapana
Mhe. Kabwe Zuberi Zitto - Hakuwepo
Mhe. Mwanawetu Said Zarafi - Hapana
Mhe. Salim Abdallah Khalfani - Hapana
Mhe. Mhonga Said Ruhwanya - Hapana
Mhe. Salim Hemed Khamis - Hapana
Mhe. Anna Maulidah Komu - Hapana
Mhe. Mwadini Abbas Jecha - Hapana
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya - Hapana
Mhe. Ibrahim Mohamed Sanya - Hapana
Mhe. Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa - Hapana

Mhe. Fatma Mussa Maghimbi - Hapana
Mhe. Masoud Abdallah Salim - Hapana
Mhe. Abubakar Khamis Bakary - Hakuwepo
Mhe. Lucy Fidelis Owenya - Hapana
Mhe. Fatma Abdalhabib Fereji - Hakuwepo
Mhe. Ania Said Chaurembo - Hapana
Mhe. Omar Ali Mzee - Hapana
Mhe. Ali Said Salim - Hakuwepo
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili - Hapana
Mhe. Bakari Shamis Faki - Hapana
Mhe. Mohamed Ali Said - Hapana
Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga - Hapana
Mhe. Juma Said Omar - Hapana
Mhe. Ali Khamis Seif - Hapana
Mhe. Savelina Silvanus Mwijage - Hapana
Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassmy - Hakuwepo
Mhe. Mgeni Jadi Kadika - Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah - Ndiyo
Mhe. Anna Margareth Abdallah - Ndiyo
Mhe. Mohamed Rished Abdallah - Ndiyo
Mhe. Mohammed Abdi Abdulaziz - Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid - Ndiyo
Mhe. Ali Haji Ali - Hakuwepo
Mhe. Fatma Othman Ali - Ndiyo
Mhe. Aziza Sleyum Ally - Ndiyo
Mhe. Ame Pandu Ame - Ndiyo
Mhe. Kheri Khatib Ameir - Ndiyo
Mhe. Ameir Ali Ameir - Ndiyo
Mhe. Idd Mohamed Azzan - Ndiyo
Mhe. Rostam Abdulrasul Azizi - Hakuwepo
Mhe. Faida Mohamed Bakar - Ndiyo
Mhe. Prof. Feetham Filipo Banyikwa - Ndiyo
Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga - Ndiyo
Mhe. Gosbert Begumisa Blandes - Ndiyo
Mhe. Lolensia Jeremiah Maselle Bukwimba - Ndiyo
Mhe. Felister Aloyce Bura - Hakuwepo
Mhe. Pindi Hazara Chana - Ndiyo
Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni - Hakuwepo
Mhe. Andrew John Chenge - Ndiyo
Mhe. Gideon Asimulike Cheyo - Ndiyo
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo - Ndiyo
Mhe. Samuel Mchele Chitalilo - Ndiyo
Mhe. Mohammed Amour Chomboh - Ndiyo
Mhe. Paschal Costantine Degera - Ndiyo
Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji - Ndiyo
Mhe. Mohammed Gulam Dewji - Ndiyo

Mhe. Dr. Anthony Mwandu Diallo - Ndiyo
Mhe. Meryce Mussa Emmanuel - Hapana
Mhe. Col. Saleh Ali Farrah - Hakuwepo
Mhe. Stephen Jones Galinoma - Hakuwepo
Mhe. Dr. Zainab Amir Gama - Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke - Hakuwepo
Mhe. Ali Juma Haji - Ndiyo
Mhe. Zuleikha Yunus Haji - Ndiyo
Mhe. Hemed Mohammed Hemed - Hapana
Mhe. Maria Ibeshi Hewa - Ndiyo
Mhe. Parmukh Singh Hoogan - Ndiyo
Mhe. Dr. Christine Gabriel Ishengoma - Ndiyo
Mhe. Issa Kassim Issa - Ndiyo
Mhe. Yahya Kassim Issa - Ndiyo
Mhe. Athuman Said Janguo - Ndiyo
Mhe. Asha Mshimba Jecha - Ndiyo
Mhe. Rajab Hamad Juma - Ndiyo
Mhe. Siraju Juma Kaboyonga - Ndiyo
Mhe. Janet Bina Kahama - Hakuwepo
Mhe. Charles Muguta Kajege - Ndiyo
Mhe. Nizar Mustafa Karamagi - Ndiyo
Mhe. Teddy Louise Kasella-Bantu - Ndiyo
Mhe. Mariam Reuben Kasembe - Ndiyo
Mhe. Eustace Osler Katagira - Ndiyo
Mhe. Vita Rashid Kawawa - Ndiyo
Mhe. Gaudence Cassian Kayombo - Hakuwepo
Mhe. Charles Ndiliana Ruwa Keenja - Ndiyo
Mhe. Yono Stanley Kevela - Hakuwepo
Mhe. Vuai Abdallah Khamis - Ndiyo
Mhe. Mwajuma Hassan Khamis - Hapana
Mhe. Abdisalaam Issa Khatib - Ndiyo
Mhe. Hassan Rajab Khatib - Ndiyo
Mhe. Abdallah Omar Kigoda - Ndiyo
Mhe. Hassan Chande Kigwalilo - Hakuwepo
Mhe. Felix Ntibenda Kijiko - Hakuwepo
Mhe. Estherina Julio Kilasi - Ndiyo
Mhe. Juma Hassan Killimbah - Ndiyo
Mhe. Aloyce Bent Kimaro - Ndiyo
Mhe. Halima Omar Kimbau - Ndiyo
Mhe. Archt. Fuya Godwid Kimbita - Ndiyo
Mhe. Paul Peter Kimiti - Ndiyo
Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini - Hakuwepo
Mhe. Capt. John Damiano Komba - Hakuwepo
Mhe. Suleiman Omar Kumchaya - Ndiyo
Mhe. William Jonathan Kusila - Ndiyo
Mhe. Omar Shabani Kwaangw’ - Ndiyo

Mhe. Al-Shymaa John Kwegyir - Hakuwepo Mhe.
Florence Essa Kyendesya - Ndiyo
Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Hapana
Mhe. Michael Lekule Laizer - Ndiyo Mhe. James Daudi
Lembeli - Ndiyo
Mhe. Castor Raphael Ligallama - Ndiyo
Mhe. Devota Mkuwa Likokola - Ndiyo
Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu - Hakuwepo
Mhe. Sameer Ismail Lotto - Hakuwepo
Mhe. Edward Ngoyai Lowassa - Ndiyo
Mhe. George Malima Lubeleje - Ndiyo
Mhe. Emmanuel Jumanne Luhahula - Hakuwepo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi - Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida - Ndiyo
Mhe. Anna Richard Lupembe - Ndiyo
Mhe. John Paul Lwanji - Ndiyo
Mhe. Clemence Beatus Lyamba - Ndiyo
Mhe. Ernest Gakeya Mabina - Hakuwepo Mhe. Joyce
Nhamanilo Machimu - Ndiyo
Mhe. Ephraim Nehemia Madeje - Ndiyo
Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge - Ndiyo
Mhe. Yusuf Rajab Makamba - Ndiyo
Mhe. Jackson Muvangila Makwetta - Ndiyo
Mhe. Benito William Malangalila - Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela - Ndiyo
Mhe. John Samwel Malecela - Ndiyo
Mhe. Halima Mohammed Mamuya - Ndiyo
Mhe. Ramadhani Athumani Maneno - Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya - Ndiyo
Mhe. Vedastusi Mathayo Manyinyi - Ndiyo Mhe. Abdul Jabiri
Marombwa - Ndiyo
Mhe. Wilson Mutagaywa Masilingi - Ndiyo
Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa - Ndiyo Mhe. Haroub
Said Masoud - Ndiyo
Mhe. Janeth Mourice Massaburi - Ndiyo
Mhe. Joyce Martin Masunga - Ndiyo
Mhe. Zubeir Ali Maulid - Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga - Ndiyo
Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka - Ndiyo
Mhe. Monica Ngezi Mbega - Ndiyo
Mhe. Janet Zebedayo Mbene - Hakuwepo
Mhe. Mwanne Ismaily Mchemba - Ndiyo
Mhe. Zakia Hamdani Meghji - Hakuwepo
Mhe. Mariam Salum Mfaki - Ndiyo
Mhe. Feteh Saad Mgeni - Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama - Hakuwepo

Mhe. Laus Omar Mhina - Ndiyo
Mhe. Zabein Muhaji Mhita - Ndiyo
Mhe. Fatma Abdallah Mikidadi - Ndiyo
Mhe. Mohamed Hamisi Missanga - Hakuwepo
Mhe. Margreth Agness Mkanga - Hakuwepo
Mhe. Dunstan Daniel Mkapa - Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono - Hakuwepo
Mhe. Rita Louise Mlaki - Ndiyo
Mhe. Martha Mosses Mlata - Ndiyo
Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa - Ndiyo
Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o - Hakuwepo
Mhe. Herbert James Mntangi - Ndiyo
Mhe. Ali Ameir Mohamed - Ndiyo
Mhe. Salim Yussuf Mohamed - Hapana
Mhe. Elisa David Mollel - Hakuwepo
Mhe. Balozi Dr. Getrude I. Mongella - Ndiyo
Mhe. Dr. Samson Ferdinand Mpanda - Hakuwepo
Mhe. Benson Mwailugula Mpesya - Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina - Hakuwepo
Mhe. Kilontsi Muhama Mporogomyi - Ndiyo
Mhe. Basil Pesambili Mramba - Ndiyo
Mhe. Felix Christopher Mrema - Hakuwepo
Mhe. Raynald Alfons Mrope - Ndiyo
Mhe. Dr. Ibrahim Said Msabaha - Ndiyo
Mhe. Ruth Blasio Msafiri - Hakuwepo
Mhe. Manju Salum Omar Msambya - Hakuwepo
Mhe. Dr. James Alex Msekela - Ndiyo
Mhe. Balozi Abdi Hassan Mshangama - Ndiyo
Mhe. Mgana Izumbe Msindai - Ndiyo
Mhe. Mwinchoum Abdulrahman Msomi - Ndiyo
Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu - Ndiyo
Mhe. Prof. Idris Ali Mtulia - Ndiyo
Mhe. Mtutura abdalla Mtutura - Ndiyo
Mhe. Mudhihir Mohamed Mudhihir - Ndiyo
Mhe. Oscar Rwegasira Mukassa - Ndiyo
Mhe. Joseph James Mungai - Hakuwepo
Mhe. James Philipo Musalika - Hakuwepo
Mhe. Omar Sheha Mussa - Hakuwepo
Mhe. Mossy Suleiman Mussa - Ndiyo
Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu - Ndiyo
Mhe. Dorah Herial Mushi - Ndiyo
Mhe. Dr. Harrison George Mwakyembe - Ndiyo
Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi - Ndiyo
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa - Ndiyo
Mhe. Ludovick John Mwananzila - Ndiyo
Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro - Ndiyo

Mhe. Thomas Abson Mwang'onda - Ndiyo
Mhe. Mchungaji Luckson Mwanjale - Hakuwepo Mhe. Harith Bakari Mwapachu - Ndiyo
Mhe. Hamza Abdallah Mwenegoha - Ndiyo
Mhe. Charles Nyanguru Mwera - Hakuwepo
Mhe. Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya- Ndiyo
Mhe. Damas Pascal Nakei - Ndiyo
Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro - Ndiyo
Mhe. Richard Mganga Ndassa - Hakuwepo
Mhe. Philemon Ndesamburo - Hakuwepo
Mhe. Job Yustino Ndugai - Hakuwepo
Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa - Ndiyo
Mhe. Kingunge Ngombale-Mwiru - Ndiyo
Mhe. Cynthia Hilda Ngoye - Ndiyo
Mhe. Hadija Saleh Ngozi - Ndiyo Mhe. Brg.Gen. Hassan Athumani Ngwilizi - Ndiyo
Mhe. Juma Suleiman Nh'unga - Hakuwepo
Mhe. Juma Abdallah Njwayo - Ndiyo
Mhe. Dr. Omari Mzeru Nibuka - Ndiyo
Mhe. Sijapata Fadhili Nkayamba - Ndiyo
Mhe. Said Juma Nkumba - Ndiyo
Mhe. Daniel Nicodem Nsanzugwanko - Hakuwepo
Mhe. Tatu Musa Ntimizi - Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu - Ndiyo
Mhe. Ponsiano Damiano Nyami - Ndiyo
Mhe. Esther Kabadi Nyawazwa - Ndiyo
Mhe. Ussi Ame Pandu - Ndiyo
Mhe. Mwaka Abdulrahaman Ramadhan - Ndiyo
Mhe. Shally Josepha Raymond - Ndiyo
Mhe. Mch. Dr. Getrude P. Rwakatare - Hakuwepo
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq - Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said - Ndiyo
Mhe. Bujiku Philip Sakila - Ndiyo
Mhe. Kidawa Hamid Saleh - Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum - Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum - Ndiyo
Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi - Ndiyo
Mhe. Lucas Lumambo Selelii - Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka - Ndiyo
Mhe. Haji Juma Sereweji - Hakuwepo
Mhe. Peter Joseph Serukamba - Hakuwepo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby - Hakuwepo
Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah - Ndiyo
Mhe. William Hezekia Shellukindo - Ndiyo
Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo - Hakuwepo
Mhe. Jacob Dalali Shibiliti - Ndiyo

Mhe. John Magale Shibuda - Hakuwepo
Mhe. Dr Guido Gorogolio Sigonda - Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene - Hakuwepo
Mhe. Mohamed Said Sinani - Ndiyo
Mhe. Dr. Luka Jelas Siyame - Ndiyo
Mhe. Mohamed Rajabu Soud - Ndiyo
Mhe. Ali Haroon Suleiman - Hakuwepo
Mhe. Abdallah Salum Sumry - Ndiyo
Mhe. Elieta Namdumpe Switi - Ndiyo
Mhe. Hafidh Ali Tahir - Ndiyo
Mhe. Fatma Abdalla Tamim - Ndiyo
Mhe. Kaika Saning'o Telele - Hakuwepo
Mhe. Martha Jachi Umbulla - Ndiyo
Mhe. Zaynab Matitu Vulu - Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura - Ndiyo
Mhe. Godfrey Weston Zambi - Ndiyo
Mhe. Mzee Ngwali Zubeir - Ndiyo
Mhe. Mussa Azan Zungu - Ndiyo

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:**Katibu subiri kidogo Mheshimiwa Janet Kahama ameingia baada ya jina lake kwa *alphabet* kupitwa lakini yuko ndani ya ukumbi kwa hiyo, naomba umhoji.

Mheshimiwa Janet Bina Kahama - Ndiyo

**DR. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Idadi ya waliotakiwa kupiga kura ni 320, kura moja haikupigwa kwa sababu ni kura ya uamuzi ya Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Hesabu ili tupate kura za Ndiyo, za Hapana na zile zisizofungamana na upande wowote. Wakati tunaendelea kusubiri makatibu wasaidizi wawili wakifanya hesabu kwa wale wapenzi wa kandanda ninasikitika kuwafahamisha kwamba hadi sasa Japan moja, Cameroon bila goli limefungwa katika dakika ya 39 na mtu anayeitwa Honda. *( Kicheko)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Kanuni.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Kanuni ya 68.
**SPIKA:** Endelea.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa kuwa Bunge hili limejengwa kisasa kuzingatia maendeleo haya ya *ICT* na

kwa kuwa Spika wetu ni wa viwango, inakuwaje ya kwamba hatukuweza kupiga kura katika mwenendo wa kisasa na sasa tunahitaji kukodisha wahesabu kura?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sababu yake ni rahisi tu, ukumbi wote huu utafumuliwa upya ili Novemba Mosi kutakuwa na ukumbi tofauti kidogo kwa maana hii. Mathalani kwenye *ICT* nyaya zinazopitisha umeme kwenda kwenye vipaza sauti ni hizo hizo zinapitisha nyaya nyingine ambazo zinakwenda kuonyesha kwenye hivi ving'amuzi au tuseme *TV* zilizoko humu kwa hiyo, kuna nyaya tatu kinyume kabisa na utaratibu zimepitishwa katika sehemu ambayo isingepaswa na ndiyo maana kukitokea hitilafu kidogo ya umeme basi hata vipaza sauti haviwezi kutoa tena sauti.

Kwa hiyo, tumeshauriwa kwamba hilo lifanyike, la pili ni kwamba kuna baadhi ya viti na baadhi ya meza mnazotumia kwa sababu havikuwa imara sana vimeanza kuonyesha dalili ya kuchoka. Ya tatu Bunge lijalo linatarajiwa kuwa na Wabunge 360, viti vyote vilivyomo humu ndani kwa jumla ni 340 kwa hiyo, lazima yafayike marekebisho ya kuongeza viti 20 ukichanganya sababu zote hizo kuna mchoro mpya tumekabidhiwa na Kamati ambao baadae nitatoa taarifa katika Mkutano huu na ninamshukuru sana Mhe. *Engineer* Fuya Kimbita kwa kazi kubwa sana aliyoifanya kama *Architect*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wametembelea Bunge la Scotland, Bunge la Australia na Mabunge mengine yanayofanana na haya majirani na wale watakaojaliwa kuwako hapa tarehe Mosi Novemba ukumbi huu utakuwa bora kuliko ulivyo sasa. Lakini pia kila mmoja atakuwa na sijui niite *TV* au *screen* kila kiti mbele yake kwenye *desk* kutakuwa na *screen,* kutawezesha mawasiliano baina ya Serikali pengine na Mbunge na anaweza kujibu humu humu na kura sasa zitapigwa *electronically,* sasa yote hayo yasingeweza kufanyika wakati tuko humu tunasubiriwa tumalize shughuli zetu, tuondoke basi mafundi watavamia hapa na kutengeneza hilo na tutaondokana na adha hii ambayo Mhe. Mbunge amelalamika na hiyo ndiyo hali halisi na kura tayari sasa zimehesabiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, zoezi hili linachukua muda na linafanywa kwa uangalifu kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 90 (2)(b). Moja ya mazingira kati ya matano ambapo Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania anaruhusiwa kulivunja Bunge ni pale ambapo Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali kwa hiyo, ndiyo maana inabidi tuwe waangalifu sana maana yake athari za hilo nadhani wote mnajua nawashangaa kidogo hawa wanaopiga kura wanaosema Hapana, lakini nadhani ndiyo demokrasia yenyewe kwa sababu lingefanikiwa ile ya Hapana athari zake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza mafao yetu yangepungua kwa miezi mitano maana yake tungevunjwa kesho na mambo mengi ya hovyo hovyo. Kuna mambo mengine ambayo Serikali na Spika wameyapanga mazuri tu yote yangenyauka, sasa mimi sijui lakini kwa bahati nzuri sana matokeo ni kama ifuatavyo. *( Makofi)*

*(Hapa Spika wa Bunge alikabidhiwa matokeo ya kura na Katibu wa Bunge na kuanza kusoma)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, matokeo ni kama ifuatavyo, kura zilizopigwa na ambazo pia za wale ambao hawakuwepo jumla yetu ni 320, kura za Hapana ni 37 na wenzetu ambao hawakuwepo ni 63 na kura za Ndiyo ni 220. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa matokeo haya na kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ni kwamba walioafiki ni wengi. Kwa hiyo, kura za Ndiyo ni nyingi na kwa maana hiyo sasa ni kwamba nina wajibu wa kutangaza kwamba Bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2010/2011 leo tarehe 14 Juni, 2010 hapa Dodoma imepitishwa rasmi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye orodha ya shughuli za kesho kutakuwa na Muswada wa Sheria ya Fedha *(The Finance Bill)* na nadhani inaweza ikatuchukua siku nzima kwa hiyo, pengine Mhe. Waziri Mkuu atatoa hotuba yake siku ya Jumatano, kesho kutwa asubuhi.

Baada ya kusema hayo tumekamilisha shughuli zilizopangwa kwa leo nawashukuru wote kwa ushirikiano wenu na ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuwa mtulivu katika hali ambayo ina uchokozi mwingi, lakini ndiyo demokrasia yenyewe na tumepata mtu ambaye anaweza kuhimili mapigo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi hapo kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.47 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 15 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*